*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 13 Mei, 2017

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE (K.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**MWENYEKITI:** Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2016/2017. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sote hapa kuweza kufika siku ya leo na kuweza kushiriki katika Mkutano huu. Kwa namna ya pekee kabisa, naomba nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa ya kulitumikia Taifa letu na kuwatumikia Watanzania katika nafasi hii ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naahidi kuwa nitaendelea

kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi wa hali ya juu na namwomba Mwenyezi Mungu aniongoze na kunisimamia katika kazi zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na wenye mafanikio makubwa kwa Taifa letu. Namshukuru sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa maelekezo yao mazuri na miongozo wanayonipa katika kutekeleza kazi zangu. Aidha, nampongeza Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuongoza vyema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nashukuru na kukupongeza wewe, Wenyeviti wa Bunge na Naibu Spika pamoja na Spika kwa kuliongoza Bunge letu vyema na kwa weledi wa hali ya juu. Natoa pia pongezi za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, kwa kuichambua bajeti ya Wizara yangu na kwa ushauri ambao Kamati hii imeutoa ambao umewezesha na utaendelea kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana, napenda kuungana na Watanzania wenzangu katika maombolezo tuliyonayo kutokana na msiba mkubwa uliolikumba Taifa letu kutokana na ajali iliyotokea Karatu tarehe 6 Mei, 2016 na kusababisha vifo vya wanafunzi 32, Walimu wawili na dereva wa Shule ya Msingi Lucky Vincent iliyopo Arusha. Msiba huu mkubwa umeacha simanzi na majonzi makubwa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine, napenda kutoa pole kwa wazazi, walezi, ndugu, wanafunzi na uongozi wa Shule ya Lucky Vincent na wote waliopoteza

wapendwa wao katika ajali hiyo mbaya iliyolikumba Taifa letu. Hakika Taifa letu limepoteza vijana ambao walikuwa wanajizatiti kielimu ili waweze kulitumikia Taifa lao kwa weledi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

MMheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba tuendelee kuwakumbuka katika sala zetu majeruhi watatu kati ya watu 38 waliokuwa katika basi hilo ambao walisalimika katika ajali hiyo, ili Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka na hatimaye waweze kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msiba huu uliwagusa pia majirani na marafiki zetu ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee kabisa, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Rais wa Kenya, Mheshimiwa Uhuru Kenyatta ambaye alimtuma Waziri wake wa Elimu, Mheshimiwa Dkt. Fred Okengo Matiang', kushiriki katika msiba huu. Serikali yetu ilifarijika sana kwa ushirikiano waliotuonesha katika kipindi hiki kigumu cha majonzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana pia Washirika wetu wa Maendeleo katika Sekta ya Elimu ambao wamekuwa wakitoa pole kwa barua na kwa simu kutokana na msiba uliotokea. Niseme tu kwamba msiba huu umewagusa watu wote na hivyo tunasema ahsante sana kwa watu wote ambao waliungana nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa 2016/2017 na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa 2017/2018. Nitaanza na mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha sh.1,396,929,798,625 ambapo Sh.499,272,251,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh.897,657,547,625 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017, jumla ya sh.979,785,341,945.18 zilikuwa zimetolewa ambapo sh.350,008,368,423.59 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 70.1 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Fedha za maendeleo zilizotolewa zilikuwa ni sh.629,776,772,521.59 ambayo ni sawa na asilimia 70.2 ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha zilizotumika; nazungumzia fedha ambazo zimepokelewa, fedha zilizotumika, hadi kufikia tarehe 30, Aprili, 2017 zilikuwa ni sh.924,821,633,369.42, ambayo ni sawa na asilimia 94.4 ya fedha zote zilizotolewa. Kati ya fedha hizo, sh.345,545,773,733.57 zilitumika kwa matumizi ya kawaida na sh.579,275,859,725.85 zilitumika kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika kazi ambazo zilitekelezwa na Wizara yangu kwa Mwaka 2016/2017. Kama tunavyofahamu, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia na kutekeleza sera, sheria na taratibu katika Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imefanya uchambuzi wa mahitaji bora wa kisheria utakaowezesha kuwepo na usimamizi na uendeshaji fanisi zaidi wa elimu na mafunzo nchini. Kutokana na uchambuzi uliofanyika, imependekezwa kuwepo kwa Sheria moja Kuu ya Elimu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara yangu zitaendelea na utekelezaji wa majukumu chini ya sheria zao mahususi kwa kuzingatia muktadha wa sheria kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie uboreshaji wa miundombinu katika taasisi za elimu. Kama tunavyofahamu, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka kipaumbele katika kuboresha Sekta ya Elimu na imeweka kipaumbele katika kuhakikisha kwamba miundombinu katika Sekta ya Elimu inakuwa ni ambayo inavutia na inaweza ikawezesha wanafunzi kupata elimu iliyo bora. Katika mwaka

2016/2017, Wizara yangu ilifanya shughuli zifuatazo katika kuboresha miundombinu katika taasisi za elimu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuelezea ukarabati wa shule kongwe. Wizara yangu imegharamia ukarabati wa shule kongwe ambazo ni pamoja na Jangwani, Azania, Kibaha, Kigoma Sekondari, Tosamaganga, Songea Wasichana, Malangali, Mirambo, Minaki, Nangwa, Mpwapwa, Musoma Ufundi, Mtwara Ufundi, Ifakara, Kantalamba, Tanga Ufundi, Ifunda Ufundi, Moshi Ufundi, Bwiru Wavulana, Iyunga, Zanaki, Kibiti, Ndanda na Tambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutakumbuka kwamba mwezi Septemba, 2016, ndugu zetu wa Mkoa wa Kagera walipatwa na tetemeko ambalo, pamoja na mambo mengine liliathiri pia miundombinu katika Sekta ya Elimu. Miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Ihungo iliharibika kabisa kutokana na tetemeko la ardhi lililotokea Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa, ilitupatia Pauni za Uingereza milioni 2.23 ambayo ni sawa na takribani shilingi bilioni sita, kwa ajili ya kujenga upya Shule ya Sekondari Ihungo ambapo ujenzi wa shule hiyo unaendelea chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo Tanzania na kwa sasa umefikia hatua ya upauaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukarabati wa Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto. Sambamba na Shule ya Sekondari Ihungo, Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto ambayo inachukua wanafunzi wenye mahitaji maalum nayo iliathirika na tetemeko katika baadhi ya majengo. Ukarabati wa shule hiyo pamoja na ujenzi wa mabweni mapya manne, zahanati na vyoo viwili unaendelea chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba. Tunaishukuru sana *UNICEF* ambao ndio waliotuwezesha kwa upatikanaji wa kiasi cha Dola za Kimakerani 318,000 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Mugeza Mseto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie ukarabati wa vyuo vya ualimu. Wizara yangu imegharamia ukarabati wa miundombinu ya madarasa, maabara, vyoo, mabweni, mifumo ya majitaka na majisafi katika Vyuo vya Ualimu kumi ambavyo ni pamoja na Tabora, Korogwe, Kleruu, Butimba, Morogoro, Tukuyu, Kasulu, Songea, Mpwapwa na Marangu. Lengo ni kufanya mazingira ya kujifunzia kuwa ya kuvutia na kuongeza udahili wa wanachuo wanaosomea Masomo ya Sayansi, Hisabati, TEHAMA na elimu ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Miundombinu Mipya Katika Vyuo vya Ualimu. Sambamba na ukarabati, Wizara yangu inaendelea na kuongeza majengo katika Vyuo vya Ualimu vya Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga. Ujenzi wa miundombinu hiyo mipya ambayo inajumuisha ujenzi wa nyumba za wakufunzi, nyumba ya Mkuu wa Chuo, ujenzi wa madarasa, maktaba, maabara, ukumbi wa mihadhara na mabweni ambayo yana uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 338 kwa kila chuo umefadhiliwa na Serikali ya Canada, lakini vilevile Serikali yetu inachangia. Hatua ya ujenzi iliyofikiwa katika kila chuo imeainishwa katika aya ya 24, ukurasa wa 11 mpaka wa 12 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika mwaka 2016/2017, Serikali imejenga mabweni mapya 20 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mabweni hayo yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 3,840 yatasaidia kuondoa adha kubwa waliyokuwa wanaipata wanafunzi wa vyuo vikuu katika kupanga mitaani. Uwezo wa mabweni hayo ni mkubwa zaidi ikilinganishwa na wanafunzi takribani 2,700 ambao ndio kwa sasa wanalala katika mabweni ambayo yako ndani ya chuo kikuu tangu kilipoanzishwa mwaka 1964.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutekeleza ahadi yake ya kujenga mabweni hayo ndani ya miezi minane tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie ujenzi wa maktaba mpya ya kisasa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao unaendelea na utagharimu Dola za Kimarekani milioni 41 ambayo ni sawa na takribani shilingi bilioni 86.1. Ujenzi huu unafadhiliwa na Serikali ya China na maktaba hii itakuwa ni moja kati ya maktaba kubwa kabisa katika Afrika Mashariki na Kati na itakuwa na uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2,500 kwa mwaka mmoja. Tunategemea kwamba ujenzi wa maktaba hii utakamilika mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie Hospitali ya Kufundishia ya Mloganzila. Serikali imekamilisha ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; na hospitali hii ni ya kisasa kabisa kwa miundombinu na vifaatiba vinavyotumia teknolojia ya kisasa, na hivyo basi, itasaidia kutoa mafunzo ya Udaktari, Ufamasia na Uuguzi wa kiwango cha hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti na hapa naomba niweke msisitizo, kwamba kwa mafunzo ya Udaktari, mgonjwa ndiye kitabu cha Daktari. Ili upate Daktari bora lazima pia awe anafanya mazoezi. Kwa hiyo kuwepo kwa hospitali hii kutawawezesha kutoa mafunzo ambayo yatakuwa ni mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa naomba nizungumzie majengo ambayo yamekamilika katika Chuo Kikuu cha Sokoine. Kituo cha uratibu ya hali ya ukaa ambacho kimejengwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha kilimo kimekamilika na kimeshaanza kufanya kazi ya kuratibu kiwango cha hewa ya ukaa *(National carbon monitoring).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo hicho kina vifaa vya kisasa vinavyotumika kwa ajili ya utafiti na kufundishia kuhusu kiwango cha hewa ya ukaa. Kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho pamoja na kuongeza tija katika kupima hewa ya ukaa iliyopo, lakini pia kimeongeza nafasi za kufundishia wanafunzi 464.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ujenzi wa kituo cha mafunzo ya utafiti wa mzingira na viumbe maji katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo awamu ya kwanza umekamilika. Kituo hiki ni cha kipekee kwa sababu katika eneo la Afrika na Maziwa makuu hakuna kituo cha namna hiyo na kimejikita zaidi katika kutoa elimu ya sayansi ya tiba kwa viumbe maji. Wale wenzangu wanaofuga samaki mkatembelee pale kwa sababu mnaweza mkapata *solution* ya matatizo yenu. Kituo hicho kinatoa mafunzo kwa wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Maabara ya Sayansi Katika Chuo Kikuu cha *SUA*. Ujenzi wa maabara nne za kemia, baiolojia, *micro-biology* na mimea kwa ajili ya kitivo cha sayansi Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ujenzi wake unaendelea na maabara hizo zitakapokamilika zitatoa nafasi ya kuweza kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote inaonesha jitihada ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa namna ambavyo imeweka kipaumbele katika sekta ya elimu kwa kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu. Orodha ya kazi zilizofanyika bado haijakamilika, inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia iliratibu ujenzi wa miundombinu katika shule 274 ambapo shule za msingi ni 142 na za sekondari ni 132 katika Halmashauri 119 kupitia programu ya lipa kulingana na matokeo. Ujenzi huo umehusisha madarasa 1,081, vyoo 2,802, mabweni 200, mabwalo tisa, majengo ya utawala sita, nyumba za Walimu 11 na visima vya maji nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi huu ulitumia njia ya *force account* kupitia Kamati za Shule. Fedha za ujenzi zilikuwa zinapelekwa moja kwa moja shuleni na mfumo huu umesaidia kupunguza sana gharama na muda ambao unatumika katika ujenzi. Aidha, kupitia programu ya afya na maji safi shuleni ambayo inatwa *SWASH*, jumla ya shule 1,116

ambazo zimejumuisha shule za msingi 1,023 na sekondari 93 zilijengewa miundombinu ya vyoo bora na kusambaziwa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza baadhi tu; maana nimeona kutokana na muda mengi yapo kwenye kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza sasa mafanikio katika kuboresha miundombinu, naomba nijielekeze katika ithibati na udhibiti wa elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua kwamba, elimu bora ni muhimu na ina nafasi ya kipekee katika kufanikisha maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Katika mwaka 2016/2017 shule 83 zilisajiliwa baada ya kukidhi vigezo, vibali vya ujenzi kwa shule 95 zisizo za Kiserikali zilizotolewa na wamiliki wa shule 86 walithibitishwa. Aidha, Wizara yangu ilizifunga shule 10 za kutwa zilizoandikisha wanafunzi kabla ya kusajiliwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kutoa wito kwa wamiliki wote wa shule kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kwani Wizara yangu haitasita kuchukua hatua kwa yeyote atayekiuka taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Ubora wa Shule. Hadi kufikia Aprili 2017, Wizara yangu ilikuwa imekagua shule 7,729 sawa na asilimia 71.4 ya shule 10,818 zilizokuwa zimepangwa kukaguliwa. Kutokana na ukaguzi uliofanyika, ushauri ulitolewa kwa Walimu wa masomo ili kuboresha ufundishaji. Aidha, Wizara inaendelea na kazi ya kuandaa kiunzi cha udhibiti ubora wa shule *(quality assurance framework)* pamoja na kuandaa zana za udhibiti ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipambanua kuhakikisha kwamba katika eneo la udhibiti ubora tunaweka miongozo ambayo itakuwa na ufanisi zaidi katika kuhakikisha kwamba shule zetu zinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie suala la upatikanaji wa vitabu shuleni. Wizara yangu imechapisha na kusambaza vitabu shuleni kwa ajili ya elimu msingi na sekondari. Katika kitabu cha hotuba ya bajeti ambacho nimekigawa, nimeweka vielelezo ambavyo vinaonesha mgawanyo wa vitabu hivyo kiwilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia inatambua na kuthamini sana wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo sambamba na vitabu vya wanafunzi vilivyosambazwa lakini vile vile tumechapisha vitabu vyenye maandishi ya nukta nundu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum; na mchanganuo wa mgawanyo wa vitabu hivyo umeoneshwa katika kielelezo namba nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na makofi mazuri na furaha kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini nitumie fursa hii kueleza masikitiko yangu kwamba Wizara yangu imebaini kwamba hivi vitabu ambavyo tumesambaza, ndani ya hivyo vitabu kuna baadhi ya makosa ya kimaudhui, jambo hili ni la kusikitisha sana kwa sababu vijana wetu wanategemea wapate elimu ambayo ni bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kubaini baadhi ya makosa katika vitabu, Wizara inafanya kazi ya kuvichambua vyote vilivyopitishwa mwaka huu, na nakuhakikishia watu wote waliohusika na uzembe wakusababisha makosa katika vitabu hatakuwa na cha mswalie Mtume. Wizara imeshaanza kuchukua hatua dhidi yao na itaendelea kuchukua hatua kali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiweka msisitizo, kama mtakumbuka katika bajeti iliyopita, mimi hapa nilishikiwa shilingi kwa ajili ya vitabu vyenye makosa na tukaweka utaratibu wa kwenda kuvisimamia. Kwa hiyo, kinachojionesha suala si utaratibu, suala inawezekana ni uwezo lakini pia liko ndani ya Serikali yetu na kama watu

hawana uwezo watupishe wakae Watanzania ambao watakuwa wanajali na wataweza kutoa kitu ambacho kinastahili kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kamwe haitaweza kuvumilia watumishi wazembe ambao wamesababisha hasara kutokana na kutokuwa makini katika utendaji wao. Nalihakikishia Bunge lako kwamba, tutaisafisha Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo ndiyo yenye jukumu la kuandaa mihtasari na mitaala ili kuhakikisha kwamba ina watumishi wenye ujuzi stahiki unaoendana na uzito wa majukumu yao na kwamba kila mara lazima wahakikishe kwamba tunapokuwa tunatoa vitabu ambavyo ni kwa jili ya manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye lazima viwe na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie mikakati ya kuimarisha umahiri wa Walimu katika ufundishaji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imetoa mafunzo kwa walimu 32,000 wa darasa la tatu na nne na Walimu 519 wanaofundisha wanafunzi viziwi na wasioona. Kwa hiyo utaona tumeweka uzito kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum tunapotoa mafunzo kwa Walimu na tumeweka utaratibu pia na Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum nao wanapata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tunaendelea kusambaza vifaa vya maabara kwa shule 1,696. Katika hotuba yangu nimeonesha mgawanyo wa shule zipi zitapata vifaa vya maabara; na hapo Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewane vizuri. Tunagawa vifaa vya maabara kwa shule ambazo zimekamilisha ujenzi wa maabara; zote zimepata bila kujali ziko wapi, bila kujali ziko chini ya mmiliki au ni utawala wa chama kipi, zote zimepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, shule ambazo maabara zake hazijakamilika nitumie fursa hii kuzihimiza Halmashauri zihakikishe kwamba zinakamilisha kwa sababu katika mwaka huu tumetenga fedha na kama itatokea shule zimekamilika basi tuweze kuzipatia vifaa. Kama Wizara

tungependa sana shule zote za sekondari ziwe na maabara na kama zikikamilika kama nilivyosema tutagawa vifaa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge katika hili ningeomba pia tusaidiane kuzihamasisha Hamashauri zetu. Kwa wale ambao watakuwa hawajapata vifaa kwa sababu Halmashauri hazijakamilisha Maabara

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie madeni yasiyo ya mishahara. Kupitia mradi wa lipa kulingana na matokeo yaani *(EP4R),* Wizara yangu imelipa madeni ya Walimu yasiyo ya mishahara yenye thamani ya sh.10,505,160,275.00 kwa ajili ya Walimu 22,420 kuanzia Julai, 2016 mpaka Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo tunaipata katika ulipaji wa madeni, kwa sababu Wizara yangu inalipa madeni baada ya kuwa yamehakikiwa na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Yapo madeni mengi ambayo yalikataliwa na yalirudishwa kwenye Halmashauri; kwa hiyo fedha hizi ambazo tumelipa ni kwa ajili ya madeni yale tu ambayo yalihakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu, katika bajeti yetu bado tunazo fedha za kulipa hela za madeni yasiyo ya mishahara. Kwa hiyo, tunahimiza wale ambao madeni yao yalikataliwa au wale ambao walikuwa hawajawasilisha wafanye hivyo kabla ya mwisho wa mwaka ili Walimu ambao wanastahili waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia inaendelea kuratibu utoaji wa motisha kwa Halmashauri na katika mwaka 2016/2017 imetoa kiasi cha sh.22,360,574,170. Nimeweka kielelezo ambacho kinaonyesha kiasi cha shilingi tulichopelekwa kwa kila Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kuhusu mafunzo ya Walimu. Wizara yangu imeendelea kutoa mafunzo ya Walimu wa sayansi 1,946 na kununua *computer* 290 kwa ajili ya vituo 29; haya ni mafunzo kazini na lengo ilikuwa ni kuimarisha ufundishaji wa TEHAMA katika shule za sekondari. Imeandaa kiongozi cha mwalimu wa masomo

ya sayansi kwa wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu ili kuboresha ufundishaji na imeendelea na mafunzo ya Walimu 17,307 katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali 35. Vile vile Kazi nyingine ambazo zimefanywa na Wizara yangu zimeainishwa katika aya ya 53, ukurasa wa 26 – 28 wa kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Katika vitu ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano inavipa kipaumbele katika sekta ya elimu ni pamoja na wanafunzi wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Ili kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum nao wanapata fursa na wanajifunza kwa ufanisi, Wizara yangu imenunua vifaa mbalimbali vya kielimu na visaidizi kwa wanafunzi wenye baki ya usikivu na wasioona. Nimeweka kielelezo ambacho kinaonesha aina ya vifaa tulivyonunua na mgawanyo wake katika Wilaya. Jumla ya sh.6,137,851,600.00 zilitumika kwa ajili ya kuwanunulia wanafunzi vifaa kwa ajili ya mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze katika shughuli zilizofanywa na taasisi na mashirika kwa mwaka 2016/17, nitaanza na Mamlaka ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi *(VETA). VETA* imeendelea na kusimamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Njombe ambacho kinajengwa Wilayani Ludewa pamoja na chuo cha Namtumbo. Vile vile inasimamia ujenzi wa utawala katika cho cha ufundi stadi Kihonda na hapa Dodoma, Chuo cha *VETA* kinajenga Karakana ya kisasa ambayo ni ya useremala na itakuwa inatengeneza samani kwa ajili ya kuuza. Kwa hiyo, itakapokamilika nitawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wakatembelee na watuunge mkono waweze kununua samani za kisasa kutoka kwenye *VETA* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zinazofanywa na *VETA* ni kama ambavyo zimeainishwa katika kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Bodi ya Mikopo. Bodi hiyo imeendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi, na katika mwaka 2016/2017 jumla ya wanafunzi 122,374 walipata mikopo ambapo wanafunzi 28,785 ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza na mikopo yao iligharimu jumla ya sh.104,613,516,187,000.00 na wanafunzi wanaondelea, mikopo yao imegharimu bilioni 379.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ilitoa ruzuku kwa wanafunzi 184 na wanataaluma 44 ambao wanaendelea na masomo yao ya uzamivu nchini Ujerumani. Pia ilitoa mikopo kwa wanafunzi 448 wanaoendelea na masomo katika vyuo vikuu vilivyo nje ya nchi ambapo jumla ya sh.5,362,054,708.00 zilitumika hadi kufikia Aprili, 2017. Bodi ya Mikopo pia imeendelea kuimarisha marejesho ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwasisitiza wanufaika wote wa mikopo ambao hawajaanza kufanya marejesho waanze kutekeleza wajibu wao wa kisheria mara moja ili kuepuka usumbufu na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vyuo vya maendeleo ya wananchi. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imefanya ukarabati wa miundombinu ya madarasa na Karakana pamoja na kutoa vifaa vya kufundishia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Rubondo, Geita, Kisarawe, Sengerema, Bariadi na Kasulu. Imesambaza vifaa vya ufundi ili kuimarisha ufundishaji na imefanya kikao na Wakuu wa Vyuo wote nchini tarehe 3 Machi hapa Dodoma kwa lengo la kubaini changamoto zao na kuangalia mikakati ya namna gani tunaweza tukaboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Baraza la Mitihani. Baraza hili limeendelea na jukumu lake la msingi la kutunga mitihani katika ngazi mbalimbali. Vile vile ili kuimarisha usalama wa mitihani na kurahisisha kazi ya ufungaji limenunua mashine ya kisasa kabisa ambayo itakuwa inahesabu na kufunga karatasi *automatically;* yaani imenunua *Poly Wraping and packaging machine.* Vile vile

Baraza la mitihani lilifanya uhakiki wa vyeti vya watumishi wa Serikali za Mitaa, Taasisi, Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali na taarifa yake kukabidhiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu. Katika mwaka 2016, wakala umeendelea kutoa mafunzo ya uongozi na usimamizi na vile vile imetoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule pamoja na Maafisa Elimu kama ambavyo imeainishwa katika kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania. Bodi ya Huduma za Maktaba imewezesha upatikanaji wa vitabu 68,801, magazeti 10,698 na majarida 461. Vile vile imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa maktaba za shule na vyuo katika shule 88. Aidha, imeimarisha maktaba 43 kwenye mikoa na halmashauri kwa kuanzisha *reading corners,* yaani kunakuwa na *corner* ambazo zinawekwa mahususi kwa ajili ya kuimarisha *study* za kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekusudia kujenga utamaduni kwamba, wazazi wanapokuwa wanakwenda maktaba waende na watoto wao na wakifika huko wakati mzazi anasoma na watoto watakuwa wana *corner* ambayo wanaweza wakajenga maarifa ya kusoma, kuandika na kuhesabu na wajukuu pia ruhusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu tushirikiane katika kuzihimiza Halmashauri ili ziweze kuona umuhimu wa kuanzisha Maktaba na kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kusoma vitabu, vijarida na machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Tume ya Vyuo Vikuu. Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kuhakiki ubora wa elimu ya juu kwa kutoa ithibati.  Katika mwaka 2016/2017 Tume ya Vyuo Vikuu iliratibu udahili wa wanafunzi

69,539 ambao walidahiliwa katika vyuo vikuu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 64,919. Nimewapa kiambatisho ambacho kinaonesha orodha ya wanafunzi waliodahiliwa kwa kila chuo kwa mwaka 2016/2017 na kwa mwaka 2015/ 2016 ambayo inapatikana kama kielelezo namba 11(a) na 11(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu pia imeendelea kusimamia ubora wa elimu ya juu kwa kukagua vyuo vya elimu ya juu 98 ili kubaini kama vimekidhi vigezo. Wembe ni ule ule, vyuo ambavyo vitakuwa vinabainika vina upungufu, Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam. Katika mwaka 2016/2017 imanzisha kozi ya Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara kwenye *Campus* ya Mwanza ili kuongeza idadi ya Mafundi Sanifu ambao tunawahitaji sana katika kujenga uchumi wa viwanda, imefanya ukarabati wa miundombinu ya karakana na kusimika mashine ya kisasa ya utambuzi wa magari na imekamilisha ujenzi wa *teaching tower complex*; yaani kuna jengo ambalo tunalijenga la ghorofa kumi ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 984 kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu tunasonga mbele katika kuhakikisha kwamba tunawaletea Watanzania maendeleo katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie Tume ya Nguvu za *Atomic* ambayo ina jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi na imetekeleza majukumu yafuatayo katika mwaka 2016/2017:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefanya ukaguzi wa vituo 131 vinavyotumia vyanzo vya mionzi na kubaini vituo 102 vilivyokidhi matakwa ya kisheria na vituo 29 vilikutwa na dosari ambapo hatua stahiki zimechukuliwa. Ilifungua Ofisi za Kanda katika Miji ya Songea, Sirali na Mtwara kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mionzi katika mipaka

ya nchi yetu. Vile vile imefanya upembuzi wa awali na michoro ya kiuhandisi kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya kisasa ya upimaji wa mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina mpango wa kujenga maabara kubwa ya kisasa na ya kipekee, ya kupima mionzi ambayo tunaamini kwamba kutakuwa na vifaa vya kipekee ambavyo katika Afrika Tanzania itakuwa inaongoza. Kwa hiyo, tunaendelea na mchakato, michoro imekwishaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandelea Arusha. Taasisi ya Nelson Mandela imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuendeleza ubunifu na ujasiriamali na imeanza utekelezaji wa vituo mahiri vya taaluma *(African Centers of Excellency)* wenye thamani ya takribani dola za kimarekani milioni kumi na mbili. Tayari wanafunzi 29 wa Uzamivu na Uzamili wameshadahiliwa. Vituo hivyo vya umahiri vinalenga katika masuala ya maji, nishati na usafi wa mazingira, kilimo, lishe na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka kuhakikisha kwamba, vyuo vyetu vikuu vinafanya tafiti ambazo moja kwa moja zinakuwa na manufaa kwa jamii. Utaona maeneo tuliyoyachagua, maji, nishati, usafi wa mazingira, kilimo na lishe, usalama wa chakula ni maeneo muhimu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Nelson Mandela kimeanza utekelezaji wa mradi wa kuongeza uwezo wa tafiti za sayansi na teknolojia Afrika, mradi ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika na unathamani ya shilingi bilioni 8.2; na tayari wanafunzi 51 wamedahiliwa kwa ajili ya uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niwaelekeze Waheshimiwa Wabunge katika usimamizi na utekelezaji wa miradi. Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi na *program* mbalimbali katika Sekta ya Elimu, Sayansi

na Teknolojia; nitazungumzia kwa uchache kwa sababu ya muda; lakini nitaomba kwamba hotuba yangu yote kwenye kitabu iingie kwenye *hansard* kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* ya kukuza stadi za kusoma na kuandika na kuhesabu. Katika juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba watoto wanaojiunga elimu ya msingi, pamoja na walio nje ya mfumo rasmi wanamudu vema stadi za kusoma kuandika na kuhesabu Wizara yangu inaendelea na uratibu wa utekelezaji wa *program* ya kukuza stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu; ambayo tunaiita *program* ya *Literacy and Numeracy Education Support (LANES).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Program* hii ambayo tunapata ufadhili kutoka *Global Partnership in Education* imewezesha upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada, nyenzo za kufundishia na uwezeshaji wa Walimu kumudu ufundishaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *program* ya lipa kulingana na matokeo ambayo nina hakika Waheshimiwa Wabunge wote mnaifahamu kwa sababu ama mnapata fedha kwenye halmashauri zenu au mmenufaika na madarasa ambayo tumeweza kuyajenga kupitia kwenye program hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza *program* ya lipa kulingana na matokeo kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ambao ni Benki ya Dunia, Idara ya Maendeleo ya Kitaifa ya Uingereza *(DFID)* na Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa Sweden *(Swedish International Development Agency)* au kwa kifupi *SIDA*. Mradi huu umefanya mambo mengi kama nilivyokwishaeleza kwenye taarifa yangu, ujenzi wa miundombinu, ukarabati wa shule kongwe, upatikanaji wa vifaa vya maabara na mambo mengine ambayo nimeshayaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie mradi wa kuimarisha mafunzo ya ualimu. Nafurahi kulifahamisha Bunge

lako Tukufu kwamba, mnamo tarehe 24 Machi, 2017, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Canada, imeingia mkataba ya kuboresha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu unaojulikana kama *Teacher Education Support Project (TESP).* Mradi huu utafadhiliwa na Serikali ya Canada na una thamani ya dola za Canada milioni hamsini na tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi. Mradi huu wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi, umeandaliwa ili kuwezesha utekeleza wa mkakati wa Taifa wa kukuza na kupanua stadi za kazi na ujuzi nchini. Mkakati huo uliandaliwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utajikita katika kuongeza fursa za upatikanaji wa stadi za kazi na kuongeza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele za kukuza uchumi ambazo ni kilimo uchumi, utalii, uchukuzi, ujenzi, nishati na madini pamoja na TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa uchache kazi ambazo zimefanywa na Wizara yangu ambazo kutokana na muda sijaweza kuzisema taasisi zangu zote, lakini zote zimeainishwa katika kitabu cha hotuba. Sasa naomba nijielekeze kwenye mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu itafanya shughuli zifuatazo katika kuimarisha mazingira ya utoaji elimu. Itafanya mapitio ya sheria ya elimu, kama nilivyoeleza, tulianza na uchambuzi lakini mwaka huu tutafanya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura ya 354 pamoja na sheria za taasisi zilizo chini ya Wizara yangu ili ziendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Itakamilisha taratibu za uanzishwaji wa Bodi ya Kitaalam ya Walimu, ambayo lengo la Bodi hii ni kusimamia taaluma ya Walimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ualimu ni taaluma, na kama ambavyo zilivyo taaluma nyingine kama Madaktari,

Wahandisi wana Bodi zao, tunataka na Walimu nao wawe na Bodi ya Kitaaluma ambayo itasimamia weledi katika Sekta ya Ualimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *Program* ya Lipa Kulingana na Matokeo, Wizara itaendelea kuratibu ujenzi wa vyumba vya madarasa 2,000, ukarabati wa shule kongwe za sekondari 17 na ili kukabiliana na changamoto za uhaba wa madarasa au kupunguza msongamano katika baadhi ya shule zetu za msingi na sekondari. Vile vile itagharamia ujenzi wa ukarabati wa miundombinu ya maji na vyoo katika shule 1,000 za msingi na shule 200 za sekondari kupitia *program* ya huduma ya maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni ambayo kwa kifupi tunaita *SWASH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Utoaji wa Elimu Maalum. Kama nilivyosema, suala la Elimu Maalum ni kipaumbele na litaendelea kuwa kipaumbele mpaka pale ambapo Serikali itajiridhisha kwamba changamoto za msingi kwenye elimu maalum zimetatuliwa. Hivyo basi, katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu itaimarisha utoaji wa elimu maalum na elimu jumuishi katika shule za msingi na sekondari kwa kuhuisha miongozo kuhusu miundombinu. Hapa kwenye miundombinu kuna tatizo kubwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, tunataka hili suala tuliangalie vizuri kuhusiana na miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum vile vile vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itapitia utaratibu wa kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuongeza ushiriki wao na kuimarisha ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Pamoja na hayo hatutawasahau Walimu wanaowafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, tutaendelea kuwapa mafunzo kazini ili waweze kuwatumikia wanafunzi hao kwa weledi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie mipango katika kuimarisha mafunzo ya elimu ya ualimu. Tutaendelea

na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ualimu sita vya Kleruu, Mpwapwa, Dakawa, Tabora, Butimba na Marangu. Vile vile Wizara yangu itaendelea na ukarabati wa miundombinu na maktaba na maabara za TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejizatiti na kupitia huu mradi ambao nimeueleza ambao tumesaini mkataba wake mwezi wa tatu tutaweka maabara za kufundishia somo la *computer* katika vyuo vyetu vya elimu vya umma vyote 35. Tutaendelea na ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Ualimu Mpuguso, Ndala, Shinyanga na Kitangali. Vile vile tutaendelea kuwajengea uwezo Wakuu wa Vyuo vya Ualimu katika uandaaji wa mipango na usimamizi wa shughuli katika vyuo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafanya mapitio ya mtaala wa stashahada ya ualimu ili uendane na mahitaji ya sasa na pia kwa kuzingatia mtaala wa elimu ya msingi ulioboreshwa. Kama tunavyofahamu tumefanya maboresho ya mtaala wa elimu msingi na kwa sababu hawa Walimu wanaoenda kwenye vyuo vya ualimu baadaye ndiyo wanaokwenda kufundisha kwenye hizi shule, basi hatuna budi kuhakikisha kwamba yale wanayoyafundisha yanawiana na kile ambacho kitakuja kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuboresha mazingira ya Wadhibiti Ubora wa Shule. Wizara yangu itajenga ofisi 50 za Wadhibiti Ubora wa Shule za Wilaya. Ujenzi wa ofisi hii utazingatia Wilaya ambazo zipo katika majengo ya kupanga, Wilaya mpya ambazo hazina ofisi kabisa. Sambamba na ujenzi huu Wizara yangu itaendelea na kazi ya kukagua shule kama nilivyoanisha katika kitabu changu na itafungua ofisi za udhibiti ubora katika baadhi ya wilaya mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Program* ya Lipa Kulingana na Matokeo. Katika mwaka 2017/2018 *program* ya Lipa Kulingana na Matokeo itaendelea kutoa motisha kwenye Halmashauri pamoja na kufanya uboreshaji wa mazingira ya shule, kuimarisha utoaji wa elimu nchini kwa kutoa vifaa

vya kufundishia kama vile vifaa vya maabara na vilevile kuendelea kukamilisha ukarabati wa miundombinu katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia changamoto kubwa ya uhaba wa wahadhiri katika vyuo vya ualimu, Wizara yangu imepanga kutoa ufadhili wa Wahadhiri 100 ili waweze kufanya shahada za uzamivu katika fani ambazo zina uhaba mkubwa wa Wahadhiri katika vyuo vikuu vya umma. Vile vile Wizara yangu itajenga shule ya kisasa kabisa hapa Dodoma, Makao Makuu ya Nchi ili kuhakikisha kwamba tunaimarisha miundombinu ya Shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uratibu wa taasisi na wakala zilizo chini ya Wizara yangu. Wizara itaendelea kuratibu shughuli za wakala zilizo chini Wizara yangu na kwa ufupi tu kwa sababu ya muda naomba nizungumzie kuhusiana na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivi ni muhimu na hivyo basi Wizara yangu itaendelea kuhakikisha kwamba inaviimarisha kwa kuvifanyia ukarabati. Miundombinu yake kwa kweli ni michakavu sana na baadhi havina vifaa kabisa, ukienda kwenye karakana havina vifaa, kwa hivyo tutaendelea kuimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi tutaendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika Mikoa ya Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa na tutaanza na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera, ambacho niseme kwamba Chuo cha Kagera kwa kweli kimechelewa kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mimi kama Waziri mwenye dhamana hili jambo halinifurahishi. Hata hivyo kuna changamoto za msingi, ambapo eneo la chuo kuna changamoto ya miundombinu na barabara lakini nimekwishazungumza na Mawaziri wenzangu na tutalipatia ufumbuzi na mara baada ya ufumbuzi kupatikana ujenzi utaanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zilizofanywa na taasisi zangu zimeainishwa katika aya kuanzia 120 mpaka 161, ukurasa 100 mpaka 137 kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe shukrani. Ufanisi na mafanikio yaliyopatikana umetokana na mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika Wizara. Kipekee kabisa, tena sana, napenda nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Stella Martini Manyanya, Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, kwa kweli kwa ushirikiano mkubwa sana ambao ananipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara Dkt. Leonard Akwilapo; Manaibu Makatibu Wakuu Profesa Saimon Samwel Msanjila na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara yangu. Ushirikiano wanaonipa ni mkubwa na naomba Mwenyezi Mungu tuendelee kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumshukuru Bi. Maimuna Tarishi ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu hadi alipohamishiwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge. Pia napenda kuwashukuru Viongozi wote wa Vyama vya Wafanyakazi chini ya Wizara yangu, watumishi wa Wizara, wanataaluma, wanafunzi, Walimu na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika kueneza Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Natambua na kuthamini sana sana michango ambayo wananipa na nimekuwa nikiifanyia kazi, naomba tuendelee kushirikiana tulijenge Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa pia napenda kuishukuru sana familia yangu kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa na kwa kunivumilia, hata wakati mwingine tunaweza tukakaa nyumba moja hata siku tano hatuonani. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, washirika mbalimbali wa maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa si rahisi kutokana na muda kuwataja wote lakini basi naomba niwashukuru angalau wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutambua mchango wa Serikali ya Algeria, Canada, China, Quba, India, Italia, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Sweden, Uingereza, Korea Kusini, Uturuki, Ubelgiji na Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuyashukuru Mashirika ambayo yamechangia maendeleo, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *British Council Campaign for Female Education*, Care *International, DART, DIFD, Ford Foundation, Global Partnership for Education, International Labour Organization, International Reading Association, Irish Aid, Japan International Cooperation Agency, Korea International Cooperation Agency, Peace Corps, Sweden International Cooperation Agency, Site Servers International,* Mtandao wa Elimu Tanzania, Umoja wa Nchi za Ulaya, *UNDP*, *UNESCO, UNICEF, USAID* na *Water Aid* na wengine wote kwa sababu ya muda sitaweza kuwataja wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha. Hapa inabidi nitulie, niwe mnyenyekevu kabisa, niweze kuliomba fedha Bunge lako Tukufu. Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyopangwa katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba kuidhinishiwa jumla ya sh.1,366,685,241,000 ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi hayo mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sh.88,544,393,736.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo sh.70,202,722,328.00 ni kwa ajili ya mishahara na Sh.18,341,671,408.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Sh.331,299,025,264.00 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya wakala na taasisi zilizo chini Wizara ya yangu. Kati ya fedha hizo Sh.318,393,044,000 ni kwa ajili ya mishahara na Sh.12,905,981,264 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha Sh.916,841,822,000 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo Sh.606,769,619,000 ni fedha za ndani na Sh.310,072,206,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliomba pia Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.663,123,262,000 kwa ajili ya Tume ya *UNESCO* na kati ya fedha hizo Sh.330,830,000 ni kwa ajili ya mishahara na Sh.322,292,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kutoa shukrani za dhati kwako wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba yangu inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.moe.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imeungwa mkono.

# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2017/18.

2. **Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu na kwa namna ya pekee napenda kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa ya kulitumikia Taifa letu na kuwatumikia wananchi wenzangu katikanafasi hii. Ninaahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu aniongoze na kunisimamia katika kazi zangu zote.

3. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na wenye mafanikio makubwa kwa maendeleo ya Watanzania. Ninamshukuru sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri Mkuu

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa maelekezo mazuri na miongozo wanayonipa katika kutekeleza kazi zangu za kila siku. Aidha, ninampongeza Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein kwa kuiongoza vema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee ninakushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza Vikao vya Bunge hili kwa weledi wa hali ya juu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao wameungana nasi katika Bunge hili. Wabunge hao ni Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mb), Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb), na Mheshimiwa Abdalla Majura Bulembo (Mb). Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare (Mb) kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuingia kwenye Bunge lako Tukufu katika nafasi ya Viti Maalum pamoja na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge aliyeteuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo kujaza nafasi ya Viti Maalum iliyoachwa wazi na Marehemu Mheshimiwa Elly Macha.

6. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Serikali hii ya awamu ya tano, ya kuleta maendeleo ya kweli kwa Watanzania. Tunaomba Watanzania wote waendelee kutuunga

mkono ili nchi yetu iweze kusonga mbele kwa kasi kubwa zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika,** Natoa pia pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa PeterJoseph Serukamba (Mb) kwa kuichambua Bajeti ya Wizara yangu. Ushauri ambao umekuwa ukitolewa na Kamati hii umeiwezesha na utaendelea kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

8. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17 Bunge lako Tukufu liliwapoteza wabunge wenzetu; Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir (Mb) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani - CCM na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha (Mb) aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum – CHADEMA. Pia, Taifa letu lilimpoteza Mheshimiwa Samwel John Sitta aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa familia zao, marafiki zao na watanzania wote walioguswa na misiba hiyo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi.

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa sana napenda kuungana na watanzania wenzangu katika maombolezo tuliyonayo kutokana na msiba mzito uliolikumba Taifa letu. Vifo vya wanafunzi 32, walimu 2 na dereva wa shule ya Msingi ya St. Lucky Vicent, viliyotokana na ajali ya gari iliyotokea Mkoani Arusha tarehe 06/05/2017 vimeacha simanzi na majonzi makubwa kwa watanzania wote.

10. **Mheshimiwa Spika,** Msiba huu umewagusa pia majirani na marafiki zetu ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee kabisa namshukuru sana Rais wa Kenya Mheshimiwa Uhuru Kenyatta ambaye

alimtuma Waziri wa Elimu wa Kenya, Mheshimiwa Dkt. Fred Okeng'o Matiang'i kushiriki katika mazishi ya watoto wetu wapendwa, walimu na dereva wao. Serikali ilifarijika sana kwa ushirikiano waliotuonesha na kwa faraja kubwa waliyotupatia katika kipindi hiki kigumu cha majonzi makubwa. Tunasema Asante Sana.

11. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mara nyingine natoa pole sana kwa wazazi/walezi, ndugu, jamaa, marafiki, uongozi shule, walimu, wanafunzi wa St. Lucky Vicent na wote waliopoteza wapendwa wao katika ajali hiyo mbaya. Hakika, Taifa limepoteza vijana ambao walikuwa wanajizatiti kielimu ili waweze kulitumikia taifa lao kwa weledi. Tunamuomba Mwenyenzi Mungu azilaze roho zao Mahali Pema Peponi. Aidha, tuendelee kuwakumbuka katika sala zetu, majeruhi watatu waliosalimika katika ajali hiyo na kwa kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka ili waweze kuendelea na masomo yao.

12. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2016/17 na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17

13. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2016/17 ulizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 – 2020/21, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Aidha, utekelezaji wa Mpango ulizingatia pia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996), Sera ya Taifa ya Utafiti

na Maendeleo (2010), Sera ya Taifa ya Baioteknolojia (2010) na Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia (2013), pamoja na ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

## B.1 Bajeti iliyoidhinishwa Mwaka 2016/17

14. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi **1,396,929,798,625.00** ambapo Shilingi **499,272,251,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **897,657,547,625.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

15. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017, jumla ya Shilingi **979,785,341,945.18** zilikuwa zimetolewa kati ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wizara yangu ambapo Shilingi **350,008,368,423.59** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, sawa na asilimia **70.1** ya Bajeti iliyoidhinishwa.

16. **Mheshimiwa Spika,** Fedha za Maendeleo zilizotolewa ni Shilingi **629,776,872,521.59,** sawa na asilimia **70.2** ya Bajetiya Maendeleo. Aidha, fedha zilizotumika hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017 zilikuwa ni Shilingi **924,821,633,369.42,** sawa na asilimia **94.4** ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **345,545773,733.57** zimetumika kwa Matumizi ya kawaida na Shilingi **579,275,859,725.85** zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo.

## KAZI ZILIZOTEKELEZWA MWAKA 2016/17

### B.2 Usimamizi wa Sera na Sheria za Elimu, Sayansi na Teknolojia

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta ya Elimu ili kuhakikisha kuwa

elimu katika ngazi zote inatolewa kulingana na Sheria, Kanuni na Miongozo inayokidhi mahitaji na inayolenga ufanisi katika utoaji wa elimu nchini. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara yangu imefanya uchambuzi wa mahitaji ya Mfumo bora wa kisheria utakaowezesha kuwepo kwa usimamizi na uendeshaji fanisi zaidi wa elimu na mafunzo nchini.

18. **Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanyika, pamoja na mambo mengine, ulibaini kuwepo kwa Sheria mbalimbali zinazosimamia maeneo mahususi ya kielimu kama vile Elimumsingi na Sekondari, Elimu ya Ualimu, Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mitihani ya Taifa na Mitaala. Aidha, katika mfumo huo, imependekezwa kuwepo kwa Sheria moja kuu ya elimu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Taasisi zilizo chini ya Wizara zitaendelea na utekelezaji wa majukumu chini ya Sheria zao mahususi kwa kuzingatia muktadha wa Sheria kuu.

### B.3 Uboreshaji wa Miundombinu Katika Taasisi za Elimu

19. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa kuwa na Rasilimali watu walioelimika na watakaoweza kuleta chachu ya maendeleo yatakayowezesha nchi yetu kujenga uchumi wa viwanda. Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu ilifanya yafuatayo:

***Ukarabati wa Shule Kongwe***

20. **Mheshimiwa Spika** Wizara yangu imegharimia ukarabati wa Shule za Sekondari Kongwe 25 ambao unafanyika kama ifuatavyo:

(i) Ukarabati wa Shule 10 za Jangwani, Azania, Kibaha, Kigoma, Tosamaganga, Songea Wasichana, Malangali, Milambo, Minaki, Ihungo na Nangwa unasimamiwa na

Wakala wa Majengo Tanzania –TBA;

(ii) Shule 9 za Mpwapwa, Musoma Ufundi, Mtwara Ufundi, Ifakara, Kantalamba, Tanga Ufundi, Ifunda Ufundi, Moshi Ufundi na Bwiru Wavulana zinasimamiwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya – MUST; na

(iii) Shule 5 za Iyunga, Zanaki, Kibiti, Ndanda na Tambaza zinakarabatiwa chini ya uongozi wa Shule na Kamati ya Shule.

### *Ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihungo*

21. **Mheshimiwa Spika**, Mwezi Septemba 2016 Taifa letu lilipata pigo kutokana na tetemeko lililotokea katika mkoa wa Kagera. Tetemeko hilo lilisababisha uharibifu wa miundombinu ikiwemo miundombinu ya Elimu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Uingereza kupitia Idara yake ya Kimataifa ya Maendeleo (DfID) iliipatia Serikali yetu kiasi cha £2.23, sawa na takribani shilingi bilioni 6, kwa ajili ya kujenga upya shule ya Sekondari ya Ihungo ambayo majengo yake yaliharibika kabisa kutokana na tetemeko la ardhi. Kazi ya kujenga upya shule hiyo inayofanywa na Wakala wa Majengo Tanzania imefikia hatua ya kuezeka na itakamilika mwezi Agosti 2017.

### *Ukarabati wa Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto*

22. **Mheshimiwa Spika**, Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto ambayo inachukua wanafunzi wenye mahitaji maalum ni miongonimwa shule ambazo majengo yake yaliathirika na tetemeko. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa UNICEF kwa msaada wa $318,000 walioutoa wa kufanya ukarabati wa shule hiyo, kujenga mabweni 4, zahanati 1 na Vyoo 2. Kazi inafanyika chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba na imefikia hatua ya kupaua. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru

wadau wote walioungana na Serikali katika kurejesha miundombinu ya Elimu.

*Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu*

23. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imegharimia ukarabati wa miundombinu ya madarasa, maabara, vyoo, mabweni, mifumo ya maji taka na maji safi katika Vyuo vya Ualimu kumi (10) vya Tabora, Korogwe, Kleruu, Butimba, Morogoro, Tukuyu, Kasulu, Songea, Mpwapwa na Marangu kwa lengo la kuongeza udahili wa wanachuo wanaosomea masomo ya Sayansi, Hisabati, TEHAMA na Ualimu wa Elimu ya Awali. Kazi iliyofanyika imeondoa changamoto zote za miundombinu katika vyuo hivyo na kufanya mazingira ya kujifunzia kuwa ya kuvutia zaidi.

*Ujenzi wa Miundombinu Mipya katika Vyuo vya Ualimu*

24. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imeendelea na ujenzi na ukarabati Vyuo vinne vya Ualimu vya Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga ambao unafadhiliwa na Serikali ya Canada pamoja na mchango wa Serikali. Hatua ya ujenzi iliyofikiwa katika vyuo hivyo ni kama ifuatavyo:

(i) **Chuo cha Kitangali:** ujenzi wa nyumba 3 za Wakufunzi umekamilika kwa asilimia 63, nyumba ya Mkuu wa Chuo imekamilika kwa asilimia54. Ujenzi wa madarasa, maktaba, ukumbi wa mihadhara na majengo mawili ya mabweni yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 388 unaendelea;

(ii) **Chuo cha Mpuguso:** ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 380 umekamilika kwa asilimia 55, Nyumba ya Mwalimu imekamilika kwa asilimia 85. Ujenzi wa maktaba, Maabara, ukumbi wa

mihadhara, ukumbi wa mkutano na ujenzi wa vyoo unaendelea;

(iii) **Chuo cha Ndala:** ujenzi wa nyumba 3 za walimu, nyumba ya Mkuu wa Chuo, majengo 2 ya ghorofa yenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 380 na ujenzi wa vyoo unaendelea;

(iv) **Chuo cha Shinyanga:** ujenzi wa jengo la walimu la ghorofa mbili umekamilika kwa asilimia 80. Ujenzi wa majengo 2 ya bweni, ujenzi wa uzio, jengo la mabweni, majengo 2ya madarasa, ujenzi wa maktaba na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara unaendelea.

***Ujenzi wa Mabweni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam***

**25.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Serikali imewezesha ujenzi wa mabweni mapya 20 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mabweni hayo yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 3,840 yamejengwa na Wakala wa Majengo ya Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ujenzi huo ambao umekamilika ndani ya miezi nane, utasaidia kuondoa adha waliyokuwa wanapata wanafunzi wanapopanga mitaani. Idadi ya wanafunzi watakaolala katika Mabweni haya ni kubwa kuliko idadi ya wanafunzi takriban 2,700 wanaolala katika Mabweni yaliyopo ndani ya Chuo tangu kilipoanza mwaka 1964. Mabweni mapya yalizinduliwa tarehe 15/4/2017 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

***Ujenzi wa Maktaba ya Kisasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam***

**26.** **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Maktaba mpya ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea na utagharimu Dola za Kimarekani **Milioni 41** sawa na **Shilingi bilioni 86.1**

ambazozinafadhiliwa na Serikali ya China. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Machi 2018. Maktaba hii itakuwa na uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja na itakuwa na huduma ya vyumba vya kuendesha Semina, Mikutano pamoja na Mihadhara. Maktaba hii itakuwa ni moja kati ya Maktaba kubwa katika Afrika Mashariki na Kati.

***Ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia ya Mloganzila***

**27.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili ilikamilisha Ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS). Hospitali hii imejengwa katika eneo la Mloganzila lenye ukubwa wa ekari 3,800. Hospitali hii ni ya kisasa kwa miundombinu na vifaa tiba vinavyotumia teknolojia ya kisasa. Hivyo itawezesha utoaji wa mafunzo ya kiwango cha hali ya juu kwa wanafunzi wa Udaktari, Ufamasia na Uuguzi. Lengo la Serikali ni kuwa na wataalamu wabobezi kwenye eneo la Afya na Tiba.

***Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa ya Ukaa - SUA***

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kimekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa ya Ukaa *National Carbon Monitoring Centre.* Jengo hilo lenye ghorofa moja lina ofisi za walimu, vyumba vya mihadhara, vyumba viwili vya semina ambapo chumba kimoja kina uwezo wa kukaa wanafunzi 60 na chumba kingine kina uwezo wa kukaa wanafunzi 72 na ukumbi wa mikutano. Aidha, jengo hili lina vifaa vya kisasa ambavyo vinatumika kwa ajili ya utafiti na kufundishia hivyo kuweka mazingira yenye ubora wa kufanyia tafiti, ufundishaji, na ujifunzaji. Kukamilika kwa ujenzi huu kumeongeza nafasi za kufundishia wanafunzi 464.

***Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Viumbe Hai***

**29.** **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Mazingira na Viumbe Maji katika Ndaki ya Sayansi ya Tiba ya Wanyama na Binadamu, kupitia programu ya *Training and Research in Aquatic and Environmental Health in Eastern and Southern Africa (TRAHESA)* katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo awamu ya kwanza umekamilika. Kituo hiki ni cha kipekee kabisa katika eneo la Afrika na Maziwa Makuu katika umahiri wa Sayansi ya Tiba kwa viumbe vya majini. Kituo kinatoa mafunzo yenye kiwango cha hali ya juu ambayo hunufaisha wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi.

***Ujenzi wa Maabara ya Sayansi - SUA***

**30.** ***M*heshimiwa Spika** ujenzi wa Maabara 4 za Kemia, Baiolojia, Makrobaiolojia na Mimea kwa ajili ya Kitivo cha Sayansi Kampasi ya Solomon Mahlangu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Ujenzi huu utaongeza nafasi za kufundishia kwa vitendo kwa wanafunzi 400 wa masomo ya Sayansi kwa wakati mmoja na kuongeza ofisi 22 za Wahadhiri.

***Ujenzi wa madarasa na miundombinu ya Shule***

**31.** Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuratibu uboreshaji wa miundombinu kwenye Shule za Msingi na Sekondari. Wizara yangu imeratibu ujenzi wa miundombinu katika Shule 274 (Msingi 142 na Sekondari 132) katika Halmashauri 119 ambapo ujenzi wa jumla ya Madarasa 1,081, Vyoo 2,802, Mabweni 200, Mabwalo 9, Majengo ya Utawala 6, na nyumba za walimu 11 pamoja na uchimbaji wa visima vya maji katika Shule 4 umefanyika. Ujenzi huu ulitumia njia ya *Force Account* kupitia Kamati za Shule ambayo imesaidia kupunguza gharama za

ujenzi na kuongeza ufanisi katika ukamilishaji wa ujenzi.

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na vyoo bora, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na utoaji wa Elimu ya Afya na utunzaji wa mazingira shuleni. Katika mwaka 2016/17, Jumla ya Shule 1,116 (Msingi 1,023 na Sekondari 93) zilijengewa miundombinu ya vyoo bora na kusambaziwa maji safi na salama pamoja na kuunda vikundi vya usafi vya wanafunzi ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuongeza mahudhurio.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imechapisha jumla ya Miongozo ya Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira 3500. Miongozo hii imesambazwa kwenye Mikoa ya Katavi, Songwe, Geita, Njombe, na Simiyu. Miongozo hiyo itasaidia kuweka mipango ya muda mfupi na mrefu ya kuondoa tatizo la upungufu wa vyoo na maji shuleni.

## B.4 **Ithibati na Uthibiti wa Elimu na Mafunzo**

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua kwamba Elimu Bora ni muhimu na ina nafasi ya pekee katika kufanikisha maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ikiwemo kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda na kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hivyo, Wizara yangu imeendelea kuboresha na kuimarisha Mfumo wa Ithibati na Uthibiti Ubora wa Elimu. Katika mwaka 2016/17, kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

### *Ithibati ya Shule za Msingi na Sekondari*

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kusimamia Ithibati ya Shule ambapo Shule 83 zikiwemo shule za Awali na Msingi 71 na Sekondari

12 zilizokidhi vigezo zilipata usajili. Aidha, vibali vya ujenzi wa shule 95 zisizo za Serikali vilitolewa, Wamiliki 86 walithibitishwa. Aidha, Wizara ilitoa vibali vya kuongeza Tahasusi za masomo ya Sayansi kwa shule 54 za Sekondari zilizotimiza vigezo kati ya shule 79 zilizowasilisha maombi.

36. **Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Elimu sura Namba 353 ya Mwaka 1978, na rekebisho lake la mwaka 1995 na 2002 pamoja na kifungu cha 1V sehemu (c) Kipengele 29 (a) kikisomwa pamoja na kipengele cha 28 vinampa mamlaka Kamishna wa Elimu kutoa usajili kwa shule na kuzifungia shule zote ambazo hazijafuata taratibu. Katika Mwaka 2016/17, Wizara yangu ilifunga shule 10 za kutwa kwa kutoa huduma ya elimu bila kusajiliwa. Hivyo napenda kutoa wito kwa wamiliki wote wa shule kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu kwani Wizara yangu haitasita kuchukua hatua kwa yeyote anayekiuka taratibu.

***Uthibiti Ubora wa Shule za Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu***

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizarayangu inatambua kwamba Uthibiti Ubora wa Shule ni jambo muhimu katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa nchini. Hadi kufikia Aprili 2017, Wizara yangu ilikuwa imekagua shule 7,727 zikiwemo shule za Msingi 6,413 na Sekondari 1,314 sawa na asilimia 71.4 ya shule 10,818 zilizolengwa kukaguliwa. Aidha, ushauri ulitolewa kwa Walimu wa masomo ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Wamiliki wa Shule nao walipata ushauri wa namna ya kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa Shule.

38. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha Mfumo wa Uthibiti Ubora ndani ya Shule, Wakuu wa Shule za Sekondari 22 na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 312 wamepewa elimu kuhusu Uthibiti Ubora wa ndani

ya shule, ambapo shule za Msingi na Sekondari 334 za Mfano zimewezeshwa kuunda Kamati za Uthibiti Ubora wa ndani ya shule na kuweza kujitathmini zenyewe, kubaini changamoto na kuweza kuchukua hatua za utatuzi zilizo ndani ya uwezo wao. Hatua hizo zitasaidia kupunguza changamoto zinazojitokeza kwa wakati.

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaendelea na uandishi wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule *(Quality Assurance Framework)* pamoja na kuandaa zana za Uthibiti Ubora wa Shule. Mwongozo huo utakamilika Juni 2017 na utasambazwa katika ofisi zote za Uthibiti Ubora wa Shule Kanda na Wilaya pamoja na wadau wote wa Elimu kwa ajili ya utekelezaji. Ni matarajio ya Wizara kuwa kwa kutumia mwongozo huo, uthibiti ubora utafanyika kwa ufanisi zaidi.

***Uboreshaji wa Mazingira ya kufundishia na kujifunzia***

40. **Mheshimiwa Spika,** Mazingira ya kufundisha na kujifunza yana mchango mkubwa katika kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu ilihuisha Mitaala na Mihtasari ya Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi Darasa la I – VI ili izingatie umahiri na kuendana na malengo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Aidha, Wizara yangu inatambua kuwa uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na umahiri wa walimu ni mambo muhimu katika kuboresha elimu nchini.

***Upatikanaji wa Vitabu Shuleni***

41. **Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha upatikanaji wa vitabu shuleni Wizara yangu imechapisha na kusambaza vitabu shuleni kwa ajili ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Jumla ya nakala 6,862,800 za vitabu vya Darasa la II (Awamu ya Pili) na nakala 6,818,181 za vitabu vya Darasa III tayari vimekamilika na kupelekwa shuleni. *Vielelezo Na. 1a na 1b*

vinaonesha mgawanyo wa vitabu vya Darasa la II na III kwa kila Wlaya.

42. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Sekondari, nakala 1,958,628 za vitabu vya Sekondari Kidato cha I-IV (*Kielelezo Na.2 – Vitabu vilivyosambazwa kwa Wilaya*) na nakala 151,055 za vitabu kwa shule za sekondari Kidato cha 5 na 6 vimesambazwa shuleni (*Kielelezo Na. 3 Vitabu Vilivyosambazwa kwa Wilaya*).

43. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio ya kusambaza vitabu shuleni, Wizara imebaini kuwa vipo baadhi ya vitabu ambavyo vina makosa ya kimaudhui. Uchambuzi wa kina unafanyika kwa vitabu vyote vilivyochapishwa mwaka 2016/17 ili kubaini endapo dosari zilizobainika katika baadhi ya vitabu hazijajitokeza kwenye vitabu vingine.

44. **Mheshimiwa Spika,** Mchakato wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu za utumishi umekwishaanza kwa watumishi ambao vitabu walivyoidhinisha kuwa viko sahihi vimebainika kuwa na makosa. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wahusika ili kukomesha tabia ya uzembe kwenye kazi muhimu za taifa. Aidha, baada ya uchambuzi kukamilika kwa vitabu vyote vilivyochapwa, Wizara itafanya pia maamuzi kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya vitabu ambavyo vitabainika kuwa na dosari.

***Vitabu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum***

45. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ili wasome kwa ufanisi. Wizara ilichapisha pia nakala 12,400 za vitabu vya kiada kwa Darasa la I katika maandishi ya Nukta Nundu na kusambazwa katika Shule za Msingi 63 zenye

Wanafunzi wasioona (*Kielelezo Na. 4*). Vitabu vya Darasa la II na III kwa wanafunzi wasioona vinaendelea kuchapishwa. Vitabu vya masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa Kidato cha I – II vimesambazwa shuleni kama inavyooneshwa katika *Kielelezo Na. 5.*

***Kuimarisha Umahiriwa Walimu katika Ufundishaji***

**46.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu imetoa mafunzo kuhusu Mtaala ulioboreshwa kwa Walimu 32,015 wanaofundisha Darasa la III na IV kutoka mikoa yote 26 ya Tanzania Bara; na Walimu 519 wanaofundisha wanafunzi viziwi na wasioona wa Darasa la I & II. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo walimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Walimu walioshiriki katika mafunzo hayo wameonyesha ari kubwa ya kuimarisha ufundishaji katika shule zao. Ni matarajio ya Wizara kuwa ufanisi wa walimu katika ufundishaji utaendelea kuimarika.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imetoa pia mafunzo kwa wawezeshaji wa Kitaifa 260 *Trainers of Trainers* – (ToTs) katika Mikoa 26 kuhusu ufundishaji wa masomo ya Ufundi ambao watatumika kuendesha mafunzo kwa walimu wengine wa masomo ya Ufundi katika ngazi ya Shule za Sekondari. Vilevile Wizara yangu imeandaa Mwongozo wa Mafunzo Kazini kwa walimu wa masomo ya Ufundi wanaofundisha katika Shule za Sekondari.

***Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa vya Maabara***

imenunua vifaa vya maabara vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 16.9** kwa Shule za Sekondari 1,696 na vimeanza kusambazwa shuleni ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Masomo ya Sayansi kwa nadharia na vitendo. Vifaa hivyo vitasambazwa kwa

kuzingatia idadi ya shule ambapo ujenzi wa maabara umekamilika (*Kielelezo Na. 6.)*

### *Ushiriki katika mashindano ya insha*

**49.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendesha mashindano ya uandishi wa Insha kwa wanafunzi wa sekondari 163 kutoka shule 80 na imetunuku zawadi kwa washindi 10 watakaoingia kwenye mashindano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na washindi 3 watakaoingia kwenye Mashindano ya *Southern Africa Development Community* **(SADC).** Lengo la mashindanohayo ni kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri, kuandika kwa ubunifu katika mambo mbalimbali.

### *Madeni ya Walimu yasiyo ya Mishahara na Motisha kwa Halmashauri*

**50.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo imelipa madeni ya walimu yasiyo ya mishahara yenye thamani ya Shilingi kuanzia Julai 2016 hadi Aprili 2017.

**51.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuratibu utoaji motisha kwa Halmashauri 179 zilizohakikiwa mwaka 2015/16 ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 22,360,574,170.60** zilitolewa kufuatana na viwango vya utekelezaji wa viashiria vya utendaji katika sekta ya elimu. Mgawanyo wa matumizi ya fedha hizo ulikuwa asilimia 35 ya fedha hizi zitumike kwa ajili ya kurekebisha Ikama ya walimu wa Shule za Msingi ndani ya Halmashauri, asilimia 30 ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo, asilimia 25 ukamilishaji wa maabara na madarasa na asilimia 10 kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Kiasi cha fedha za motisha kilichotolewa kwa kila Halmashauri kimewekwa kama *Kielelezo Na 7*.

### *Elimu Nje ya Mfumo Rasmi*

**52.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi unaoendana na mazingira ya sasa kwa lengo la kutoa elimu kwa watu walioikosa itakayowasaidia kumudu mazingira yao. Vilevile, imeandaa Mwongozo wa ufundishaji wa KKK kwa watoto wanaosoma nje yawalimu watakaofundisha madarasa ya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa lengo la kuwasaidia walimu watakaofundisha madarasa ya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; Pia, ilihamasisha vijana na watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kutoka mikoa ya Iringa na Singida kujiunga katika madarasa ya kisomo.

### *Mafunzo ya Walimu*

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na walimu wenye sifa, maarifa na weledi katika kuinua viwango na ubora wa elimu. Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu imefanya yafuatayo katika eneo la Mafunzo ya Ualimu:

(i) imetoa mafunzo kwa Walimu wa Masomo ya Sayansi 1,946 kwa lengo la kuboresha ufundishaji wa masomo haya katika shule za sekondari za umma na kununua kompyuta 290 kwa ajili ya vituo 20 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa TEHAMA katika shule za sekondari;

(ii) imeandaa Kiongozi cha Mwalimu wa Masomo ya Sayansi kwa wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu. Uwepo wa kiongozi hiki utasaidia wanafunzi wasioona wa sekondari kusoma masomo ya sayansi.

(iii) imeendelea kutoa Mafunzo kwa walimu

17,307 katika Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali na Kuratibu Mafunzo kazini kwa wakufunzi 194 wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kutumia TEHAMA. Lengo ni kuandaa walimu mahiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kutumia TEHAMA.

(iv) imeendesha Mafunzo kabilishi kwa wakufunzi 344 wanaofundisha Mtaala wa Stashahada Maalum ya masomo ya Sayansi, Hisabati na TEHAMA katika vyuo 7 vya Ualimu vya Mpwapwa, Butimba, Morogoro, Kasulu, Korogwe, Tukuyu na Songea.

(v) imeanza kupitia mtaala wa Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada ili kuendana na mtaala wa Elimumsingi ulioboreshwa na pia kuzingatia mahitaji ya sasa.

(vi) imetoa mafunzo kwa Wakufunzi 22 juu ya uingizwaji wa masuala mtambuka katika ufundishaji. Masuala hayo ni pamoja na: Elimu Jumuishi, Usawa wa Kijinsia, Haki na Usalama wa Mtoto, Afya na Mazingira Salama ya Shule, Stadi za Maisha, Elimu ya Jinsia na Virusi vya UKIMWI, na Elimu ya Mazingira.

(vii) ilitoa mafunzo kwa Wakufunzi 24 kutoka vyuo vya Ualimu Mpuguso, Tandala na Tukuyu juu ya uchopekaji wa stadi za KKK katika masomo ya darasa la III hadi la VI.

(viii) imenunua na kusambaza vifaa na Kemikali kwa ajili ya maabara za Vyuo vya Ualimu vya Kasulu, Korogwe, Tukuyu, Butimba, Songea, Kleruu, Morogoro, Mpwapwa na Tabora ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo;

(ix) imenunua vifaa vya TEHAMA zikiwemo Kompyuta 30, Kompyuta Mpakato 2 na Projekta 2 kwa kila chuo kwa vyuo vyote 10 ili kuimarisha ufundishaji wa walimu tarajali wa masomo yote hasa wanaosomea ufundishaji wa somo la TEHAMA.

***Kuimarisha Utoaji wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum***

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo ya Taifa na kwamba elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Hivyo, Wizara yangu imeendelea kutoa fursa ya elimu kwa wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kwa kununua vifaa mbalimbali vya kielimu na visaidizi kwa wanafunzi wenye baki ya usikivu na wasioona. *Kielelezo Na. 8* kinaonesha vifaa vilivyosambazwa na usambazaji wake kiwilaya.

55. **Mheshimiwa Spika,** Vifaa vilivyonunuliwa vinajumuisha Mashine za kuandikia maandishi ya nukta nundu (Braille) 932; Vivunge (kits) vyenye vifaa vya msingi vya kujifunzia kwa wanafunzi wasioona 1,495; karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu rimu 2,548; Karatasi za kurudufishia maandishi ya nukta nundu rimu 1,150; na Shime sikio - Hearing Aids kwa ajili ya wanafunzi wenye baki ya usikivu (hard of hearing) 1,150.

56. **Mheshimiwa Spika,** Vifaa hivi vitawezesha kuongeza fursa za kushiriki kwa ufanisi katika Elimu kwa Wanafunzi wenye mahitaji maalum. Aidha, Wizara yangu imeendelea kununua vivunge vya upimaji kwa ajili ya kubaini mahitaji ya ujifunzaji kwa watoto wanaoandikishwa shule. Vifaa hivi vimesambazwa katika mikoa yote Tanzania Bara. *Kiambatisho Na. 9* kinaonesha aina ya vivunge na usambazaji wake.

57. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha ufundishaji wa

masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa wanafunzi wasioona, Wizara yangu imeandaa Miongozo mitatu ya kufundishia na vitabu ili kuwawezesha Wanafunzi kujifunza masomo hayo kwa ufanisi zaidi. Aidha, nakala 4,400 za vitabu vikiwemo 1,400 vya Fizikia, 1,400 vya Kemia na 1,600 vya Hisabati vimechapishwa kwa maandishi ya Nukta Nundu na kusambazwa katika Shule zote 25 za Sekondari zenye Wanafunzi Wasioona. *Kiambatisho Na. 10* kinaonesha usambazaji wa vitabu hivyo.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** Vifaa hivi vitawezesha kuongeza fursa za kushiriki kwa ufanisi katika Elimu kwa Wanafunzi wenye mahitaji maalum. Aidha, Wizara yangu imeendelea kununua vivunge vya upimaji kwa ajili ya kubaini mahitaji ya ujifunzaji kwa watoto wanaoandikishwa shule.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa wanafunzi wasioona, Wizara yangu imeandaa Miongozo mitatu ya kufundishia na vitabu ili kuwawezesha Wanafunzi kujifunza masomo hayo kwa ufanisi zaidi. Aidha, vitabu vya Fizikia, Kemia na Hisabati vimechapishwa kwa maandishi ya Nukta Nundu na kusambazwa katika Shulezote 25 za Sekondari zenye Wanafunzi Wasioona.

***Kuimarisha upatikanaji wa Takwimu za Elimu***

**60.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeimarisha Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji wa Takwimu za Elimu *(Education Sector Management Information System - ESMIS)* kwa kutoa mafunzo juu ya matumizi ya mfumo huo kwa Maafisa Elimu Taaluma wa Mikoa yote Tanzania Bara na Maafisa Elimu wa Vifaa na Takwimu wawili kutoka kila Halmashauri. Upatikanaji wa takwimu kwa wakati utawezesha kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera, kuandaa mipango ya elimu na kutoa maamuzi stahiki.

***Kuimarisha Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.***

61. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu ina jukumu la kusimamia na kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na matumizi yake katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa viwanda. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Kutambua Wabunifu na Wagunduzi nchini *National Inventions and Innovations Guidelines* kwa lengo la kuendeleza bunifu na gunduzi zao ili kuchochea maendeleo ya Taifa. Aidha, imefanya mapitio ya Mkataba wa Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uswisi ili kuimarisha ushirikiano na kupanua wigo wa ushirikiano kwa kuzihusisha taasisi nyingine za Tafiti na kuongeza maeneo ya ushirikiano kwenye nyanja za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

**SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA KWA MWAKA 2016/17**

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kuratibu kazi za Taasisi, Wakala na Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma. Shughuli zilizofanyika katika mwaka 2016/17 ni kama ifuatavyo:

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

63. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Elimu Tanzania inalo jukumu la kuandaa Mitaala na Mihtasari, kutoa Miongozo kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kutoa Mafunzo kwa Walimu kazini na kufanya utafiti na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mitaala katika Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu. Katika mwaka 2016/17 Taasisi ya Elimu ilifanya kazi zifuatazo:

(i) Ilipitia Mtaala na mihtasari ya Elimu ya

Awali, Darasa la I –VI kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kuandaa Miongozo ya walimu ya Elimu ya Awali, Darasa la I –VI kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

(ii) ilikamilisha Miswada 18 ya vitabu vya Darasa la IV hadi la VI vinavyokidhi mahitaji ya utekelezaji wa mtaala, pamoja na kuandika Vitabu vya Kiada aina 22 kwa kuzingatia Mtaala ulioboreshwa.

(iii) ilisambaza nakala 60,672 za Mtaala, nakala 303,360 za Mihtasari na nakala 1,840,183 za vitabu vya kiada Darasa la III – VI.

(iv) ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala kwa Darasa la I na II katika mikoa 10 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni: Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Tabora, Geita, Dodoma, Singida, Arusha na Mbeya.

(v) imehuisha Mihtasari ya Masomo ya Mchepuo ya Sayansi Kimu, Ufundi na Kilimo Kidato cha 1- 4 na kuchapisha Vitabu vya kiada aina 30 vya Kidato cha 1 - 4 na aina 15 za vitabu kwa Kidato cha 5-6. Aidha, imeandaa Mihtasari 18 ya Sekondari Kidato cha 1-6 inayoendana na Mtaala wa mwaka 2005; na kusambaza nakala1,531,627 za vitabu vya kiada kwa Kidato cha 1 – 6 katika mikoa 20 ya Tanzania Bara.

(vi) imetoa Mafunzo kwa wawezeshaji 22 wa kitaifa kutoka katika Vyuo vya Ualimu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Agha Khan Foundation, Right to Play na Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, wakufunzi 375 na walimu 16,129 wa Elimu ya Awali katika vituo 19 Tanzania Bara; na mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo 22 kutoka Vyuo vya Serikali na watatu

(3) kutoka Vyuo Visivyo vya Serikali vinavyotoa mafunzo ya Elimu ya Awali kuhusu uendeshaji wa mafunzo ya Walimu wa Elimu ya Awali.

**Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ina majukumu ya kuratibu, kuthibiti, kugharimia, kutoa na kukuza Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Katika Mwaka 2016/17, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ilitekeleza kazi zifuatazo:

(i) Ilidahili Wanafunzi 11,672 wa Mafunzo ya Ufundi Stadi ya muda mrefu katika Vyuo 28 vya Ufundi Stadi vya VETA wakiwemo Wanawake 3,286 na Wanaume 8,386 ikilinganishwa na lengo la udahili wa wanafunzi 10,463.

(ii) Ili kuongeza fursa za kujiunga na Mafunzo ya Ufundi Stadi, iliendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Njombe Wilayani Ludewa umeanza katika ngazi ya uchimbaji msingi.

(b) Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi Namtumbo ambao upo katika hatua ya ujenzi wa misingi ya majengo mbalimbali.

(c) Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Ufundi Stadi Kihonda pamoja na majengo mawili ya karakana za umeme wa magari na ufundi seremala umefikia hatua za kuanza kupauliwa.

(iii) Ujenzi wa Karakana ya kisasa ya Useremala katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa

Dodoma kwa ajili ya ufundishaji na utengenezaji wa samani za kisasa uko katika hatua za mwisho. Karakana hii itatumika pia katika kutengeneza samani kwa ajili ya biashara na hivyo kukiongezea chuo mapato na kupunguza utegemezi kwa Serikali;

(iv) Ukarabati wa awamu ya kwanza wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Busokelo uliohusisha Karakana 3, Jengo la Utawala na Madarasa 2. Kwa sasa wanafunzi 60 wamedahiliwa katika Chuo hicho na kuanza mafunzo mwezi Machi, 2017 katika fani tatu (3) za Ubunifu, Ushonaji na Teknolojia ya Nguo; Useremala na Ufungaji Umeme;

(v) Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Nkowe kilichopo wilayani Ruangwa umefanyika na tayari Chuo kimepokea wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza wapatao 28 katika Fani za Ufundi wa Umeme, Ujenzi, na Ushonaji. Tunatarajia baada ya ukarabati wa bweni la Wasichana kukamilika, idadi ya wanafunzi wa kike hasa katika fani ya Ushonaji itaongezeka; na

(vi) imepata mkadarasi kwa ajili ya kukarabati Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Karagwe ambapo kazi itaanza rasmi mwezi Juni, 2017 baada ya kukamilika kwa taratibu za mkataba.

(vii) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu VETA ilifanya makubaliano ya kurasimisha ujuzi wa mafundi stadi 3,900 waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi wa mafunzo;

(viii) imetoa mafunzo mbalimbali kwa Wakufunzi/Walimu, Watumishi wa VETA na Wajasiriamali wapatao 1,437 kuhusu kuandaa, kufundisha na kupima mitaala inayozingatia umahiri na masuala ya upatikanaji wa taarifa za kazi.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu – (HESLB)**

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina jukumu la kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wahitaji waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa ajili ya masomo ya Shahada. Bodi pia ina jukumu la kukusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu. Katika mwaka 2016/17, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilifanya yafuatayo:

(i) ilitoa mikopo kwa jumla ya wanafunzi **122,374** ambapo wanafunzi **28,785** ni wapya ambao mkopo wao unagharimu **Shs 104,613,516,187** na wanafunzi **93,559** ni wanaoendelea na masomo ambao unagharimu **Shs 379,180,441,499.**

(ii) ilitoaruzuku ya **Shs. 4,627,160,700.00** kwa wanafunzi **1,584** wanaoendelea na masomo ndani ya nchi na **Shs. 811,091,544.00** kwa wanataaluma **44** wanaoendelea na mafunzo ya uzamivu nchini Ujerumani.

(iii) ilitoa mikopo wanafunzi **448** wanaoendelea na masomo katika Vyuo Vikuu mbalimbali nje ya nchi ambapo jumla ya **Shs 5,362,054,708.00** zilitumika hadi kufikia **Aprili, 2017**.

(iv) inaendelea kutekeleza mikakati ya kukusanya madeni ikiwa ni pamoja na utoaji elimu kwa wanufaika na waajiri kuhusu umuhimu na faida kurejesha mikopo kwa wakati.

(v) imeendelea kuimarisha ushirikiano na Mamlaka nyingine hususan Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango,

Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Taasisi za Kifedha, Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa lengo la kuwatambua Waajiri na Wanufaika Waajiriwa. Ushirikiano utawezesha kutumia Kanzi –Data za Taasisi nyingine ili kubaini wanufaika wengi zaidi.

66. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waajiri kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kuhakikisha wanufaika wa mikopo wanafanya marajesho kwa wakati. Aidha, nitumie fursa hii kuwataka wanufaika wote ambao hawajaanza kufanya marejesho kutekeleza wajibu huo mara moja ili kuepuka usumbufu wa kuchukuliwa hatua za kisheria.

**Kituo cha Maendeleo Dakawa**

67. **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Maendeleo Dakawa kina jukumu la kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa, na miundombinu yote iliyokabidhiwa na chama cha ANC kwa ajili ya kulinda historia ya Ukombozi wa Afrika Kusini. Wizara yangu inao mpango wa kukiendeleza kituo hiki na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi, TEHAMA na Ufundi ili kukifanya kuwa Kitovu cha utoaji wa Elimu ya Sayansi na Teknolojia (Centre of Excellence for Science and Technology). Ili kutimiza azma hiyo katika Mwaka 2016/2017, Kituo cha Maendeleo Dakawa kimetekeleza yafuatayo;

i. Kimeanza taratibu za kupata Hati Miliki ya Kituo kilichokabidhiwa kwa Serikali na chama cha ANC cha Afrika Kusini;

ii. Kimefanya ukarabati na matengenezo ya mitambo ya kusukuma maji safi; na

iii. Kimeanza maandalizi ya kuandaa Muundo

wa Kisheria wa Uendeshaji wa Kituo.

## Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs)

68. **Mheshimiwa Spika,** Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) vina jukumu la kusimamia Mafunzo ya Ufundi Stadi na Elimu ya Wananchi kulingana na mahitaji ya jamii husika na kutengeneza Programu za Mafunzo hayo. Katika mwaka 2016/17 Wizara ilifanya yafuatayo:

(i) ukarabati wa miundombinu ya Madarasa, Mabweni, Karakana pamoja na kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) vya Kasulu, Rubondo, Gera, Kisarawe, Karumo, Sengerema na Bariadi ili viweze kuendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

(ii) imesambaza vifaa vya ufundi katika fani za magari, umeme wa magari, umeme, uashi, useremala, uchomeleaji, ushonaji, fotokopia, na kompyuta ili kuimarisha ufundishaji.

(iii) Imefanya kikao na Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hapa Dodoma tarehe 3 Machi, 2017 ambapo changamoto za Vyuo hivi zilijadiliwa zikiwemo uchakavu wa miundombinu, uboreshaji wa mitaala, migogoro ya ardhi, madeni ya wazabuni na madai ya Watumishi. Maazimio 17 yalitolewa na yanafanyiwa kazi ili kutatua changamoto zilizopo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

## Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi

69. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kimefanya ukarabati wa ofisi

11 za Mikoa ili kuboresha usimamizi wa ofisi za Mikoa kwa kupitia mradi wa *Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support (MIVARF)*. Ukarabati uliofanyika na uwekaji wa samani umegharimu Jumla ya **shilingi 230,780,457.00**. Aidha, Chuo kimefanya ukarabati wa vyumba vya mihadhara, mabweni, nyumba za makazi ya wahadhiri na ofisi. Kazi hii imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

## Chuo Kikuu Cha Mzumbe

**70.** **Mheshimiwa Spika,** katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Wizara imefanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwenye Kampasi ya Mbeya wenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.5.** Aidha, uimarishaji wa miundombinu umeendelea kwa kujenga Jengo la Taaluma na Utawala ambalo litagharimu **shilingi bilioni 2.7.** Hadi sasa Serikali imeshatoa **shilingi milioni 800** kwa ajili ya ujenzi huo. Aidha, Chuo kimepokea mkopo wa **shilingi Milioni 500** kutoka TEA kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo. Kazi zilizokwishafanyika ni pamoja na ujenzi wa msingi, nguzo na jamvi ghorofa ya kwanza. Kukamilika kwa kazi hizi kutaongeza fursa za masomo kwa wanafunzi wa fani za uongozi na kuboresha mazingira ya kufundishia na ujifunzaji katika Kampasi ya Mbeya.

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa

**71.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/2017 Wizara yangu kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kimetekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kimeongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 3,682 mwaka 2015/2016 hadi kufikia wanafunzi 4,135 mwaka 2016/2017, wakiwemo wanawake 886 ambao ni sawa

na asilimia 24;

(ii) Kimefanya ukarabati wa maeneo ya kujifunzia kwa kujenga madawati ya kujisomea (*reading platforms*);

(iii) Kimeazisha shahada ya uzamili katika Sayansi na Elimu kwa masomo ya Biolojia na Kemia; na

(iv) Kimefanya ukarabati wa mabweni ya wanafunzi na kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara;

**Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT)**

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Kimekamilisha ukarabati wa Kituo cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania cha Geita kwa kuboresha kumbi za Mihadhara na Ofisi za Wahadhiri, kazi iliyogharimu **Shilingi milioni 31.2.** Aidha, ukarabati wa miundombinu unaendelea katika Kituo cha Mwanza kwa kuongeza kumbi za Mihadhara na Vyumba vya mitihani, ambapo **Shilingi milioni 100** zimetumika. Ukarabati wa Vituo hivi utaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na hivyo kutoa Elimu yenye ubora zaidi.

**Baraza la Mitihani la Tanzania – NECTA**

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kuendesha Mitihani ya Taifa na kutunuku vyeti kwa wahitimu. Katika mwaka 2016/17, limefanya kazi zifuatazo:

(i) limeendesha upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne uliofanyika mwezi Novemba, 2016 ambapo jumla ya watahiniwa 1,017,776 walifanya mtihani kati ya 1,054,191 waliokuwa wamesajiliwa. Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili ambapo, jumla

ya watahiniwa 410,519 walifanya upimaji huo kati ya 435,075 waliokuwa wamesajiliwa;

(ii) limeendesha Mtihani wa Taifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi Mwaka 2016 ambapo jumla ya watahiniwa 789,479 walifanya mtihani huo kati ya 795,739 waliokuwa wamesajiliwa; pamoja na Mitihani ya Kidato cha Nne na Maarifa ambapo jumla ya watahiniwa 414,608 walifanya mitihani hiyo kati ya 429,033 waliokuwa wamesajiliwa.

(iii) limekamilisha usajili wa watahiniwa wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2017 ambapo jumla ya watahiniwa 74,801 wanaendelea kufanya Mtihani huo ulioanza tarehe 2 Mei, 2017.

(iv) limeimarisha usalama wa mitihani na kurahisisha kazi ya ufungaji wa mitihani ya Taifa kwa kununua mashine ya Kielektroniki ya kuhesabu na kufunga karatasi za mitihani (*poly wrapping and Packing machine)*.

(v) Imekamilisha kazi ya kuunda mfumo wa Kompyuta utakaotumika kuwasajili wanafunzi wote wa shule za msingi nchini. Katika mfumo huu, kila mwanafunzi atasajiliwa na kupatiwa namba ya pekee ya utambulisho ambayo itamtambulisha katika hatua zote za mafunzo atakazoendelea nazo.

(vi) Lilifanya uhakiki wa vyeti vya watumishi wa umma wa Serikali za Mitaa, Taasisi/ Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali na taarifa yake kukabidhiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ina jukumu la kutekeleza Sera ya Elimu ya watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Katika mwaka 2016/2017 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imetekeleza kazi zifuatazo;

(i) Imejenga kumbi mbili za mihadhara na ofisi mbili za wafanyakazi katika Kampasi ya Morogoro (WAMO). Ujenzi upo katika hatua ya kupaua;

(ii) Imefanya ukarabati wa Madarasa mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 kila moja, Jengo la utawala, Jengo la Maktaba, Chumba kimoja cha Mgahawa, chumba cha Kompyuta, bweni moja na vyoo vya wanafunzi katika Kampasi ya Luchelele Mwanza;

(iii) Imedahili wanafunzi 855 katika program za muda mrefu za Shahada, Stashahada na Astashahada;

(iv) Imenunua Vitabu 346 kwa ajili ya mafunzo ya Shahada na Stashahada nakuwekwa katika maktaba za TEWW Dar es salaam (120) na Mwanza (226); na

(v) Imesajili vituo vipya 72 vinavyotoa Elimu ya Sekondari nje ya mfumo rasmi na kufanya jumla ya vituo kuwa 420.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maendeleo yamajukumu ya Uongozi wa Elimu unakuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti,

kuandaa na kusambaza makala na vitabu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu.Katika mwaka 2016/17, ADEM ilifanya shughuli zifuatazo:

(i) imekarabati majengo 2 ya mihadhara na mfumo wa umeme, kufunga viti na meza 831 na kununua seti ya Komputa 117 kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo katika Kampasi ya Bagamoyo.

(ii) iliandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu ambapo imetoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi na Usimamizi wa Elimu (CELMA) kwa Walimu Wakuu 706 kutoka Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe.

(iii) imetoa mafunzo ya Usimamizi wa Shule na ujenzi wa miundombinu na majengo kwa Wakuu wa Shule 1,200.

(iv) imetoa mafunzo kuhusu usimamizi wa elimu katika ngazi ya shule kwa wajumbe 129,609 wa Kamati za Shule za Msingi zipatazo 11,647 kwenye Mikoa 19.

(v) imenunua magari 3 kwa ajili ya matumizi ya Wakala na imefadhili watumishi 3 masomo ya Shahada ya Uzamivu ambao wanaendelea na masomo kwenye Vyuo vya hapa nchini.

**Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania**

**76.** **Mheshimiwa Spika**, Huduma bora za Maktaba zinachangia katika utoaji wa Elimu bora katika nchi yoyote ile. Wizara yangu katika mwaka 2016/17 kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imefanya kazi zifuatazo:

(i) imewezesha upatikanaji wa vitabu 68,801, magazeti 10,698 na majarida 461.

(ii) imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za shule na vyuo katika shule 88, (msingi 46 na sekondari 42), katika Jiji la Dar es Salaam na katika Taasisi za *All Together in Dignity to Overcome Poverty* Awali na Msingi (ATD), Mahabusu ya Watoto ya Jiji la Dar es Salaam, Ubalozi wa Marekani, *Tanzania House of Talent (*THT*), Fore Plan Clinic na Alliance Francee Library.*

(iii) imeimarisha maktaba 43 kwenye Mikoa na Halmashauri kwa kuanzisha *reading corners* za kujifunzia stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuhimiza Halmashauri zote nchini pamoja na Wadau kuona umuhimu wa kuanzisha Maktaba na kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kusoma Vitabu, Vijarida na Machapisho mbalimbali. Wizara yangu iko tayari kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa Maktaba.

## Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ina jukumu la kusimamia Mfuko wa Elimu na kuhamasisha uchangiaji ili kuongeza nguvu za Serikali katika kugharamia miradi ya elimu. Katika mwaka 2016/17 Mamlaka ya Elimu Tanzania ilifanya kazi zifuatazo:

(i) ilifuatilia katika shule 40 za Msingi na Sekondari katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Iringa zilizopatiwa vifaa

vya kuboresha mazingira ya elimu vikiwemo madawati, vifaa vya TEHAMA na mabati ili kuhakiki ubora wa vifaa, matumizi na hatua za utekelezaji wa miradi kulingana na kiasi cha fedha kilichotolewa.

(ii) ilifuatilia miradi 15 inayoendelea ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za sekondari za Uleling'ombe - Kilosa, Luegu - Namtumbo, Isanzu - Mkalama, Kinamapula - Ushetu, Ndoloeleji - Itilima, Kandawale - Kilwa zilizopo katika maeneo magumu kufikika ili kuhakiki maendeleo ya kazi za ujenzi.

**Tume ya Taifa ya UNESCO**

79. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya UNESCO ina majukumu ya kuratibu na kutekeleza Programu za UNESCO nchini katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari. Katika mwaka 2016/17, Tume ya Taifa ya UNESCO imeandaa, imechapisha na kusambaza nakala 700 za Jarida la Tanzania na UNESCO Toleo namba 13, imefadhili Walimu 35 wa shule za sekondari waliopata Mafunzo ya juu ya *Competence Based Assessment*, imefanya mikutano kupitia Kamati za kitaifa ili kuboresha mahusiano na utekelezaji wa programu za UNESCO na kuratibu mkutano wa vijana wa kikanda pamoja na mikutano mingine ili kuwajengea uwezo katika masuala ya amani, uongozi na stadi za kimaisha.

**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)**

80. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) lina jukumu la kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Elimu ya Ufundi nchini. Katika mwaka 2016/17, NACTE ilifanya kazi zifuatazo:

(i) Ilidahili wanafunzi 96,694 wa elimu ya ufundi katika Vyuo 551 vilivyosajiliwa na NACTE.

(ii) Ilihakiki Mitaala 15 ya Programu za Mafunzo kutoka Vyuo 4 vya Elimu ya Ufundi;

(iii) iliidhinisha mitaala 9 inayozingatia mahitaji ya soko la ajira na viwango vya Kitaifa na Kimataifa iliyoandaliwa na Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Chuo cha Bahari Dar es Salaam, na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

(iv) ilifanya *post validation* kwa Mitaala 16 kutoka Vyuo 5 vya Elimu ya Ufundi na ilifanya uhakiki wa awali (prevalidation) kwa Mitaala 45 ya Programu mbalimbali za mafunzo.

(v) iliandaa mfumo wa udahili na kuchakata matokeo ya Watahiniwa Kanuni na Miongozo ya Uthibiti wa Ubora wa Rasilimali Watu katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi nazo ziliandaliwa.

(vi) itaendelea kutengeneza na kuboresha mifumo ya kieletroniki itakayosaidia kuhakikisha ubora wa Elimu ya Ufundi ikiwemo Mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za wanafunzi; usimamizi wa rasilimali watu Vyuoni na mfumo wa kutoa vyeti na *transcript* kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi.

(vii) ilikagua Vyuo 88 vya Elimu ya Ufundi na kufanya tathmini juu ya ubora wa utoaji wa mafunzo ambapo baadhi ya vyuo vilifungiwa kwa sababu mbalimbali

(viii) itaendelea kuimarisha Ofisi za Kanda

ikiwemo kuwaongezea Nguvukazi na vitendea kazi ili kuwafikishia walengwa wote huduma bora. Wizara inategemea kufanya utafiti katika maeneo yanayohusu utoaji wa Elimu ya Ufundi na kutoa ushauri stahiki ili kuhakikisha elimu ya ufundi inakidhi haja ya soko la ajira.

## Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

81. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kuhakiki ubora wa Elimu ya Juu kwa kutoa Ithibati. Katika mwaka 2016/17 Tume ya Vyuo Vikuu ilifanya yafuatayo:

(i) iliratibu mfumo wa udahili wa pamoja ambapo jumla ya wanafunzi 69,539 walidahiliwa. Idadi hii iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2015/16 ambapo walidahiliwa wanafunzi 64,919. Aidha, kati ya wanafunzi hao waliodahiliwa mwaka 2016/17 wanafunzi 44,765 wako katika Vyuo vya Serikali na 24,774 katika vyuo binafsi *(Kielelezo 11a na 11b).*

(ii) imeendelea kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa kukagua Vyuo Vikuu 98 ili kuhakiki Ubora wa Mitaala, ufundishaji vyuoni na uwezo wa vyuo katika utoaji wa Elimu ya Juu nchini. Maeneo yaliyozingatiwa katika ukaguzi huo ni pamoja na uwepo wa Wahadhiri wa kutosha na wenye sifa, uwepo wa miundombinu stahiki, uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, uwezo wa maabara na karakana kulingana na mahitaji ya mafunzo husika pamoja na uongozi wa Vyuo. Aidha, Vyuo vilivyobainika kuwa na kasoro vitaendelea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;

(iii) ilishiriki kwenye vikao vya kikanda vinavyohusiana na Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na vikao vya *Inter – University Council for East Africa, Southern Africa Development Community* na Kamati ya Ufundi ya Elimu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kupata uzoefu na kuongeza weledi katika kusimamia ubora wa Elimu ya Juu;

(iv) imeendelea kuratibu utoaji wa ufadhili kwa wahadhiri 44 wanaoendelea na masomo ya ngazi ya uzamivu nchini Ujerumani;

(v) ilifanya ukaguzi wa Chuo Kikuu kinachopendekezwa kuanzishwa cha Greenbird kilichopo Mwanga, Mkoani Kilimanjaro na kubaini kuwa hakijakidhi vigezo vya kuwa Chuo Kikuu.

(vi) ilitambua Tuzo 547 za ngazi mbalimbali zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchi za nje;

(vii) iliandaa Maonesho ya 11 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo Vyuo vya Elimu ya Juu sitini (60) vya ndani na nje ya nchi vilishiriki.

## Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA)

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kina jukumu la kutoa mafunzo katika Fani za Sayansi Jamii, kufanya utafiti; na kutoa ushauri. Katika mwaka 2016/2017 kilitekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kimeandaa mitaala minne ya Ngazi ya Shahada katika fani za Elimu.

(ii) kimeandaa Mitaala na Vifaa vya ufundishaji

wa Stashahada ya Elimu ya Msingi; Stashahada ya Maktaba na Habari na kiliwezesha Wahadhiri 44 kupata mafunzo kwa lengo la kufundisha kwa ufanisi Stashahada ya Elimu ya Msingi na Stashahada ya Maktaba na Habari.

(iii) kimeandaa Mitaala ya Shahada za Uzamili za Miradi na Usimamizi *Master in Project Planning and Management*, *Human Resources Management, Educational Planning and Administration na Gender and Development* pamoja na mafunzo kwa Kozi fupi 6 juu ya maadili na uongozi na

(iv) kimechapisha Tafiti 37 katika Majarida ya Kimataifa ya Tafiti za Kisayansi.

## Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

83. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ina jukumu la kuratibu na kuendeleza utafiti na ubunifu nchini. Aidha, Tume hiyo imepewa jukumu la kisheria la kusimamia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE). Katika kukuza na kuendeleza teknolojia nchini COSTECH imefanya yafuatayo:

(i) Imekamilisha maandalizi ya kufungua kumbi za ubunifu (innovation spaces) na Atamizi/*Virtual Incubator* katika Mikoa ya Mwanza na Iringa. Vyuo Vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na Zanzibar State University (SUZA) vimeelekezwa kuanzisha atamizi ili kukuza ubunifu miongoni mwa vijana. Atamizi hizi zinachochea uendelezaji wa ubunifu katika sekta mbalimbali na kuongeza ajira kwa vijana;

(ii) imeendelea kufadhili Watafiti 27

wanaoendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamili (4) na Uzamivu (23);

(iii) kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Denmark, imetoa elimu juu ya miliki ubunifu na uhawilishaji wa teknolojia (intelectual propert right) kwa watafiti na wanasayansi (30) toka taasisi za utafiti na elimu ya juu. Mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha watafiti kulinda ubunifu wao;

(iv) Imefadhili miradi ya tafiti 18 katika maeneo ya Viwanda, Afya, Kilimo, Mifugo na Maliasili ili matokeo ya utafiti yaweze kuleta majawabu ya changamoto katika jamii;

(v) Kupitia mfuko wa MTUSATE imefadhili wanafunzi (2) wanaoendelea na mafunzo ya uzamili (4) na uzamivu (23). Aidha COSTECH imeanza utaratibu wa kudahili wanafunzi wapya (50) kujiunga na shahada ya uzamili (35) na uzamivu (15);

(vi) Ili kufanikisha usambazaji wa matokeo ya utafiti yaweze kuwafikia wadau wengi, COSTECH imeanza ukarabati wa chumba cha studio maalum kwa ajili ya kuandaa vipindi vya redio, televisheni na machapisho ya kisayansi katika ili viweze kurushwa katika vyombo mbalimbali vya habari. Kwa lengo la kuhimiza utamaduni wa kutumia sayansi, teknolojia na ubunifu katika kutatua matatizo yanayoikabili jamii; na

(vii) imefanyika ukarabati na kununua vifaa vya maabara katika Kituo cha Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI – Sota) kilichopo mkoa wa Mara. Aidha, ukarabati wa Taasisi ya utafiti wa mifugo Tanga (TALIRI) unaendelea. Ukarabati huu utaboresha miundo mbinu ya utafiti na kufanya matokeo ya utafiti yawe na ubora zaidi.

**Chuo cha Ufundi Arusha**

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2016/17, Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza kazi zifuatazo:

(i) Kimeandaa mtaala utakaotumika katika Kituo cha Kikuletwa kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi Ngazi ya Cheti katika fani za *Hydropower Maintenanace*; *Domestic Electrical Installation*; *Plumbing and Pipe fitting*; na *Blockwork and Masonry*;

(ii) Kimetoa mafunzo ya ukarabati wa Miundombinu pamoja na Mitambo ya kuzalisha umeme utokanao na nguvu za maji *Hyropower* kwa Wanataaluma 19 wa Chuo ili kuwajengea uwezo, zaidi katika fani zao;

(iii) Kimekamilisha mchakato wa kuanzisha mafunzo Ufundi Sanifu Ngazi ya Stashahada ambayo yanatarajiwa kuanza Mwezi Oktoba, 2017 katika fani ya *Electrical and Hydropower Maintenance*;

(iv) Kimeanza kufanya Usanifu wa jengol e n y e Madarasa na Maabara za Programu za Madini na Vito, Uhandisi wa Vifaa Tiba, Uhandisi wa Mawasiliano ya Anga na Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari katika Chuo cha Ufundi Arusha ili kuongeza udahili katika fani hizo;

(v) Kimefanya tafiti zinazolenga kuendeleza matumiziya umwagiliaji wa ya teknolojiamatone kwa kutengeneza vifaa ambavyo matundu yake hayazibi kirahisi ili kuimarisha maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yenye ukame;

(vi) kimeendelea kupima uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa

barabara ili kuanisha ubora wake na kutoa ushauri wa matumizi sahihi wakati wa ujenzi wa barabara;

(vii) Kimeendelea kuboresha fimbo inayowasidia walemavu wa macho (electronic blind stick) katika kutambua sehemu za mapitio yao ili kuwaongoza kwa urahisi na kwa gharama nafuu;

(viii) Kimefanya ukarabati wa Jengo la zamani katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa kulibadili matumizi yake ili kiwe kituo cha kufundishia stadi za kazi katika ufundi bomba, ufundi rangi na ufundi uashi. Jengo hilo lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 94 kwa wakati mmoja na litaongeza idadi ya mafundi mahiri;

(ix) Kimeendelea na utekelezaji wa Mradi wa ukarabati wa miundombimu kwa ajili ya kuendeleza Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Nishati Jadidu pamoja na uzalishaji Umeme utokanao na Maji katika kituo cha kikuletwa kilichopo Wilayani Hai;

(x) Kimekamilisha ujenzi wa Majengo mapya 4 na ukarabati wa majengo saba (7) ya zamani;

(xi) Kimekamisha Mpango Kazi wa Biashara (*Business Plan)* wa kuanzisha Kampuni ya Kikuletwa *Power Public Company Limited* (KPPCL) inayomilikiwa na Chuo cha Ufundi Arusha kwa ajili ya kushughulikia uzalishaji umeme katika Kituo cha Kikuletwa umekamilika; na

(xii) Kinaendela kuunda Helikopta ya gharama nafuu na salama kwa safari fupi nchini ili kurahisisha usafiri katika maeneo yasiyofikika kwa magari.

**Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam - (DIT)**

**85.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/2017 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imefanya shughuli zifuatazo:

(ii) imeanzisha kozi ya Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara kwenye Kampasi ya Mwanza; Kozi hii itazalisha wataalam ambao watasa

(i) imeendelea kutoa mafunzo yateknolojia kwa wanafunzi na wafanyakazi wa viwandani ili waweze kuongeza ujuzi mpya katika taaluma mbalimbali;

(ii) imeanzisha kozi ya Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara kwenye Kampasi ya Mwanza; Kozi hii itazalisha wataalam ambao watasaidia kukabiliana na uhaba wa mafundi sanifu wa maabara katika shule za sekondari, hospitali, vituo vya afya na zahanati; pamoja na kuongeza Mafundi Sanifu wanaohitajika katika viwanda vilivyopo na vitakavyoanzishwa hapa nchini;

(iii) imefanya ukarabati wa miundombinu ya karakana ya magari katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam kwa kununua na kusimika mashine ya kisasa ya utambuzi wa matatizo ya magari; na

(iv) imekamilisha ujenzi wa *Teaching Tower Complex.* Jengo hili litakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 984 kwa wakati mmoja hivyo litasaidia kuongeza udahili wa wanafunzi wa kozi mbalimbali za sayansi na teknolojia ambao unahitajika sana kuiwezesha Serikali kufikia azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda.

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya**

**86.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kilitekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kilikamilisha Mtaala wa kufundishia fani mpya ya stashahada ya *Highway Engineering* katika Chuo cha Sayansi Teknolojia Mbeya na mafunzo yameanza kutolewa kwa wanafunzi 14 waliodahiliwa; Utoaji wa mafunzo katika fani hiyo utasaidia kuongezeka upatikanaji wa wataalamu na wahandisi wa miundombinu ya barabara ambapo kwa sasa kuna uhaba mkubwa;

(ii) Kimekamilisha mitaala ya Stashahada, Shahada ya Uzamili na Uzamivu katika maeneo ya *Automotive Engineering*, *Oil and gas safety and reliability Engineering, Renewable Energy Engineering, Structural Engineering, Civil engineering* na *Water Resources Engineering*. Uanzishwaji wa mafunzo haya utasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wapatao 240 kwa mwaka na hivyo kuongeza wataalamu mbalimbali hususani katika fani ya Mafuta na Gesi ambayo ina uhaba wa wataalamu na hivyo inategemea zaidi wataalamu kutoka nje ya nchi;

(iii) Kimeandaa Mitaala ya mafunzo ya Shahada za *Laboratory Science and Technology na Biomedical Equipment Engineering*;

(iv) Kiliimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kufadhili Watumishi 94 katika mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya Kwanza,

Uzamili na Uzamivu ili kuwawezesha watumishi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi;

(v) Kimeanzisha atamizi ya teknolojia kwa ajili ya kuchochea ubunifu na maendeleo ya teknolojia. Atamizi hii inajikita katika maeneo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uundaji wa mitambo na vifaa mbalimbali, Sayansi na Biashara. Atamizi hii ni chachu ya kuleta maendeleo ya viwanda katika sekta ya uchumi na Biashara pamoja na kuongeza ubunifu na ajira kwa vijana.

**Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania**

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Nguvu za Atomiki ina jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi. Katika mwaka 2016/17 imetekeleza majukumu yafuatayo:

(i) imechambua maombi 244 ya uingizaji nchini, usafirishaji na utumiaji wa vyanzo vya mionzi ili kubaini kama maombi hayo yanakidhi matakwa ya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003. Uchambuzi huo unahusisha chanzo cha mionzi, sifa za kitaaluma za msafirishaji na mtumiaji wa chanzo cha mionzi *operator*, mpango wa uhifadhi wa kudumu wa mabaki ya chanzo husika na mpango wa kudhibiti endapo janga linalohusisha chanzo cha mionzi litatokea;

(ii) imekagua vituo 131 vinavyotumia vyanzo vya mionzi kwa kuangalia ubora wa jengo la kuhifadhi au kutumia chanzo cha mionzi, ubora wa chanzo chenyewe cha mionzi, sifa za kitaaluma za mtumiaji wa chanzo cha mionzi (*Operator)* na usahihi wa taarifa za nyaraka za chanzo cha mionzi na kutoa ushauri kwa lengo la kuhakikisha usalama

kwa watumiaji, raia na mazingira. Kati ya vituo 131, vituo 102 vilikidhi matakwa ya sheria, vituo 26 vilikutwa na dosari kadhaa na zikapewa muda kurekebisha kasoro hizo na vituo 2 vilifungiwa baada ya kuona vimekiuka matakwa ya sheria kwa kiasi kikubwa na kituo kimoja (1) kimesitisha chenyewe utoaji huduma ya uchunguzi wa magonjwa.

(iii) imekamilisha Taarifa sita (6) za kituo cha kupima viasili vya mionzi kwenye hewa ya anga kijulikanacho kama *"Radionuclide Monitoring Station- RN64"* kilichopo katika jengo la Idara ya Fizikia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuzituma kwenye Shirika la Kimataifa la Kuzuia Majaribioya Silaha za Kinyuklia lenye Makao Makuu Vienna Austria. Taarifa hizo zilionyesha kuwa katika kipindi hicho kulikuwa hakuna uchafuzi wa mazingira unaotokana na majaribio ya kinyuklia. Vilevile, taarifa hizo zilionyesha viwango vya kawaida vya chembechembe za vyanzo asili vya mionzi ambavyo havina athari yoyote kwa binadamu na mazingira;

(iv) ilifungua ofisi zake katika miji ya Songea, Sirari na Mtwara kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mionzi katika mipaka ya nchi;

(v) imefanya upembuzi wa awali *(Geophysical survey)* na michoro sanifu ya kiuhandisi ya ujenzi wa Maabara ya Kisasa ya upimaji wa viwango vya mionzi kwa binadamu na mazingira katika eneo la Tume ya Nguvu za Atomiki huko Arusha. Ujenzi wa maabara hii ya Tume utaboresha utoaji wa huduma, utafiti, kuongeza mapato na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya TAEC.

**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha – NM-AIST**

**88.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojiaya Nelson Mandela ina jukumu la kutoa Elimu na Mafunzo katika ngazi ya Uzamili na Uzamivu pamoja na kufanya utafiti katika ngazi ya Ubobezi. Katika mwaka 2016/17, NM- AIST ilitekeleza kazi zifuatazo:

(i) Imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuendeleza Ubunifu na Ujasiriamali katika fani ya TEHAMA *ICT Resource Centre* na kuweka mifumo ya TEHAMA kwenye Kituo hiki imemalizika na kitahudumia wanafunzi wasiopungua 30 kila mwaka;

(ii) Imekamilisha michoro na makisio ya gharama ya ujenzi wa jengo la Idara ya Miliki na uwanja wa mahafali; na imekamilisha kazi ya kuweka mipaka ya ardhi eneo la Karangai kwa asilimia 80; na

(iii) Imeanza utekelezaji wa Mradi wa Vituo viwili mahiri vya Taaluma na Utafiti *Afican Centres of Excellence* wenye thamani ya takriban **USD 12,000,000**; ambapo wanafunzi 29 wa Shahada za Uzamili na Uzamivu wamesajiliwa. Kati ya vituo hivyo, kimojawapo ni kwa ajili ya kuwa mahiri kwenye masuala ya maji, nishati na usafi wa mazingira wakati kituo cha pili kinajenga umahiri katika Kilimo lishe na usalama wa chakula. Vile vile, Vituo hivi vitaongeza fursa za kufanya utafiti, kuimarisha ufundishaji na kujenga uhusiano mzuri kati ya Taasisi na sekta binafsi.

(iv) Imeanza utekelezaji wa mradi wa kuongeza uwezo wa tafiti za sayansi na teknolojia Afrika uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wenye thamani ya Shilingi **bilioni 8.2.** Kupitia mradi huu wanafunzi 51 wa Uzamili na Uzamivu wamedahiliwa;

(v) imekamilisha Mtaala wa Shahada ya Uzamili katika utafiti wa Afya ya Jamii (*Masters in Research of Public Health -MRPH)* na tayari umeshafanyiwa ithibati tayari kwa matumizi. Mtaala huu utaanza kutumika kwenye udahili mwaka 2017/18;

(vi) Imefanya tafiti zilizolenga kutambua mambo yafuatayo:

(a) magonjwa ya wanyama ambayo yana uwezekano wa kuambukiza wanadamu ili kudhibiti maambukizi ya maradhi ya wanyama kwenda kwa binadamu;

(b) magonjwa ya wanyama kupitia nyama yanayoweza kuambukiza binadamu ili kudhibiti maambukizi ya magonjwa ya wanyama kupitia nyama;

(c) mapungufu ya teknolojia ya kuchuja maji kwenye maeneo yenye upungufu wa miundombinu ya maji kwa wananchi Mkoani Arusha na kuiboresha ili kupata huduma ya maji safi na salama; na

(d) magonjwa ambayo yana uwezekano wa kuathiri afya za mifugo ili kuboresha afya za mifugo.

## Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**89.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimefanya kazi zifuatazo:

(i) Kimefanya tafiti zilizolenga kutengeneza teknolojia rahisi ya kutenganisha madini ya shaba ili kuwawezesha Mafundi Mchundo na Wachimbaji wadogo wadogo kutenganisha

shaba kwa ufanisi na tija; Kufuatilia mienendo ya Tembo kwa kutumia teknolojia ya *Global Position System* katika maeneo Hifadhi za Mayowosi, Igosi, Ugalla, Uyungu, Gisima, Luganzo na Gombe kwa lengo kudhibiti mauaji ya Tembo yanayotokana na ujangili; Kutengeneza mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za afya vijijini na katika vituo vya afya nchini ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya huduma za afya vijijini; na

(ii) Kimefanya ukarabati wa bweni namba 1, 3, 4, 5, 6 na 7 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kurekebisha mifumo ya maji safi na maji taka. Aidha, uwekaji wa samani na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia kama vile vyumba vya mihadhara, vyumba vya semina na ofisi za walimu umefanyiwa kazi iliyogharimu jumla ya Shilingi **bilioni 1.2**.

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**90.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Dodoma kimefanya tafiti zifuatazo:

(i) Kuainisha matumizi ya mtandao wa simu za mkononi katika ufuatiliaji wa ubora wa dawa katika mnyororo wa usambazaji (Pharmaceutical Supply Chain in Tanzania) ili kuboresha usambazaji wa dawa nchini;

(ii) Kutambua malisho bora ya kuku wa kienyeji katika wilaya za Kongwa na Kiteto ili kuongeza uzalishaji wa kuku walioboreshwa na hivyo kuimarisha hali ya kipato cha kaya kwa wananchi wanaoishi maeneo yenye ukame;

(iii) Kutambua usugu wa vimelea vya

magonjwa katika maeneo yanayozunguka mbuga ya Serengeti ili kudhibiti magonjwa hayo na kuongeza uzalishaji wa wanyama wanaofugwa katika eneo hilo; na

(iv) Kuanza utafiti wa Kuunda Mfumo wa Upimaji wa Stadi za Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK) na kuandaa maudhui ya Kielektroniki ili kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

## Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

**91.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo cha kimefanya tafiti zifuatazo:

(i) Kupunguza madhara yanayotokana na panya waharibifu wa mazao kwa kutumia harufu ya mkojo wa paka *(Felissilvestric atus urine);* kwa lengo la kuboresha uhifadhi wa mazao*;*

(ii) Kuongeza uzalishaji wa zao la maharage kwa kuongeza kinga na ustahimilivu wa maradhi ya virusi (Angular Leaf Spot na Bean Common Masaic Virus) na bakteria (Common Bacterial Blight) kwa lengo kuinua kipato cha kaya za vijijini hasa wanawake;

(iii) Kutambua vyakula vya samaki vinavyotokana na mimea ya asili ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa ajili maendeleo endelevu ya kilimo cha samaki nchini;

(iv) Kutambua vimelea kinga (vaccine) kwa ajili ya magonjwa ya nguruwe ili kuongeza uzalishaji, kuinua kipato na lishe bora katika kaya;

(v) Kuzuia madhara ya magonjwa ya brucellosis na Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley Fever) kwa Wanyama wanaofugwa kwa kubuni madawa ya kinga ili kuimarisha afya za Wanyama hao; na

(vi) Kuzuia magonjwa ya kupumua kwa kuku wa kienyeji (control of respiratory diseases) kwa kubuni chanjo ya magonjwa hayo ili kuongeza uzalishaji na kuinua kipato cha kaya za vijijini hasa wanawake.

**Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi – Muhimbili**

92. **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishikimefanya tafiti zifuatazo:–

**Muhimbili**

(i) Kuainisha matumizi sahihi ya dawa ya mseto katika kudhibiti na kutibu ugonjwa wa malaria na hivyo kuongeza usalama kwa watumiaji wa dawa hizo;

(ii) Kutambua magonjwa ambayo yana uwezekano wa kuathiri afya ya Wanawake wajawazito na Watoto wachanga katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kuanzisha Kanzidata ili kuboresha afya ya mama Wajawazito na huduma ya Watoto wachanga;

(iii) Kupunguza madhara na vifo miongoni mwa wagonjwa walioathirika na Virusi vya UKIMWI kwa kufanya majaribio ya chanjo ya virusi vya UKIMWI na namna ya kuitoa ili iweze kufanya kazi katika kiwango kinachotakiwa;

(iv) Kupunguza vifo vinavyotokana na Kifua Kikuu kwa kubainisha uwezo wa dawa ya

*Isoaniazid* ili kupambana na ugonjwa huo kwa gharama nafuu;

(v) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya majengo ya mihadhara, ofisi, Maabara na Mabweni yanayotumiwa na wanafunzi 4,010 wa fani za Udaktari wa Binadamu, Udaktari wa Magonjwa ya Kinywa na Meno, Ufamasia Uuguzi na Sayansi ya Mazingira katika Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya maji, ofisi na vyumba vya kufundishia umeendelea katika kituo cha kufundishia cha *Satellite* – Bagamoyo. Kituo hiki hupokea wanafunzi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo na utafiti;

## Chuo Kikuu cha Ardhi

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Ardhi kimefanya tafiti zifuatazo:

(i) Kujenga miundombinu kwa kutumia mchanganyiko wa saruji, mchanga na kemikali maalumu pamoja na kingo za plastiki zinazoweza kutumika mara nyingi bila kuharibika ili kupunguza gharama za ujenzi wa majengo yenye ubora na uimara unaokusudiwa;

(ii) Kutambua uwezekano wa kutokea majanga ya Bahari katika Bandari ya Tanga kwa kutumia takwimu na taarifa sahihi ili kuwawezesha watumiaji wa Bandari, Wavuvi, Watalii, Watafiti na Watoa Elimu kutoa maamuzi sahihi ya kuepukana na majanga kutokana mabadiliko ya tabia ya bahari; na

(iii) Kupunguza athari za milipuko ya volcano

ya Mlima Oldonyo Lengai kwa kuweka Vituo vya upimaji vyenye vifaa maalumu vya kuwezesha Watafiti kupata taarifa sahahi ya hali ya msuguano wa miamba kwa wakati wote ili kutoa tahadhari kwa Wananchi kwa wakati kuepusha madhara.

## Chuo Kikuu cha Mzumbe

94. **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Mzumbe kimefanya tafiti zifuatazo:

(i) Kutathmini matokeo chanya ya kilimo cha mkataba cha miwa ili kimarisha matumizi ya ardhi na kuongeza ajira kwa w a n a n c h i wanaopakana na mashamba ya miwa nchini;

(ii) Kutathmini mchango wa kilimo cha katab a wa zao la tumbaku ili kubainisha manufaa ya bei ya tumbaku katika soko la dunia kwa wakulima wadogo nchini;

(iii) Kutambua matumizi bora na endelevu ya nishati ili kuzifanya Kampasi za Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki kuwa ni maabara hai za matumizi bora na endelevu ya nishati; na

(iv) Kubainisha mchango wa mazao ya asali na upasuaji wa mbao ili kuongeza kipato cha Wajasiriamali katika Wilaya ya Mvomero.

## USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI

95. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika Sekta ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Miradi na programu hizi zimeiwezesha Wizara yangu kuongeza fursa na kuinua ubora wa elimu nchini.

## Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)

96. **Mheshimiwa Spika**, Katika juhudi za kuhakikisha kwamba watoto wanaojiunga na Elimu ya Msingi pamoja na walio nje ya mfumo rasmi wanamudu vema stadi zabKusoma, Kuandika na Kuhesabu, Wizara yangu inaendelea na uratibu wa utekelezaji wa Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu- Programu ya *Literacy and Numeracy Education Support* (LANES). Lengo la programu hii ni kuhakikisha kuwa watoto wanaojiunga na Darasa la I-IV na walio nje ya mfumo rasmi wanajua kusoma kuandika na kuhesabu. Aidha programu hii imewezesha upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada pamoja, nyenzo za kufundishia na uwezeshwaji wa walimu kumudu ufundishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

## Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu II (MMES II)

97. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuanzia mwaka 2010 hadi programu hii ilipofungwa rasmi mwezi Desemba 2016. Katika kipindi cha Julai 2016 Wizara kupitia mradi huu ulifanya yafuatayo: kutoa mafunzo kwa walimu wa sayansi na hisabati, kuandaa kiongozi cha mwalimu kwa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wenye uono hafifu na kununua vifaa vya kufundishia TEHAMA. Vilevile, Andiko la Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Tatu (MMES III) lipo katika hatua ya mwisho ya maandalizi.

**Programu Lipa Kulingana na Matokeo (Programme for Results – ( P4R)**

**98.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo *Programme for Results* - P4R kwa kufadhili Sekta ya Elimu ambapo Serikali hushirikiana na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Dunia (World Bank), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (Department for International Development - DfID) na Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa Sweden (Swedish International Development Agency-SIDA).Programu hii inalenga kujenga uwezo wa Serikali wa kutekeleza vipaumbele vyake ilivyojiwekea na Serikali inapatiwa fedha kutokana na utekelezaji wa vipaumbele hivyo kwa kutumia viashiria vya utekelezaji vilivyokubalika kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kupitia programu hii, Wizara yangu imelipa madeni ya walimu yasiyo ya mishahara, imekarabati vyuo kumi vya ualimu, imejenga madarasa na kutoa motisha kwa halmashauri.

**Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu**

**99.** **Mheshimiwa Spika,** tarehe24 Machi, 2017 Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Canada imeingia mkataba wa kuboresha Mafunzo na Elimu ya Ualimu unaojulikana kama *Teacher Education Support Project (TESP)***.** Mkataba huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2016/17 – 2020/2021) ambapo kiasi cha **Dola za Canada 53,000,000** sawa na **shilingi bilioni 83** zitatolewa na Serikali ya Canada. Mradi huu utahusisha Vyuo 35 vya Ualimu vinavyofundisha walimu wa Msingi na Sekondari. Lengo kuu la Mradi wa TESP ni kuboresha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu inayotolewa katika Vyuo 35 vya Ualimu nchini.

**Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi**

100. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na Kupanua Stadi za Kazi na Ujuzi. Mkakati huu uliandaliwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi Vijana na Ajira, na Watu Wenye Ulemavu. Mradi utajikita katika kuongeza fursa za upatikanaji wa stadi za kazi na kuongeza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele za kukuza uchumi ambazo ni kilimo na kilimo uchumi, utalii, uchukuzi, ujenzi, nishati na madini; na TEHAMA. Uchaguzi wa sekta hizi umezingatia mahitaji makubwa ya waajiri katika sekta hizo; mchango wa sekta katika uchumi; upungufu mkubwa wa wataalamu; uwezo wa kuongeza ajira; na mahusiano kati ya sekta hizi na nyingine.

101. **Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la mradi huu wa kukuza ujuzi ni kuimarisha na kupanua upatikanaji na ukuzaji wa stadi za kazi na ujuzi katika ngazi za ufundi na ufundi stadi, Elimu ya Juu na sekta isiyo rasmi kwenye maeneo lengwa. Aidha, mradi unalenga kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia, kuratibu na kugharimia uendelezaji stadi za kazi katika ngazi ya kitaifa na kisekta kwa kushirikiana na sekta binafsi.

## C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18

102. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2017/18 umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2015-2020), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali. Aidha, imezingatia pia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 – 2020/2021,Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Sera

ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996), Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo (2010), Sera ya Taifa ya Baioteknolojia (2010), Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia (2013) na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

**103. Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2017/18 Wizara yangu imepanga kufanya shughuli zifuatazo:

***Kuimarisha Mazingira ya Utoaji wa Elimumsingi na Sekondari***

**104. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya shule ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi ubora unaotakiwa. Katika Mwaka 2017/18 shughuli zifuatazo zitatekelezwa kwa lengo la kuimarisha utoaji elimu:

(i) kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 pamoja na Sheria za Taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziendane na maudhui ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa lengo la kuimarisha mifumo ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi;

(ii) kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ambayo ina lengo la kusimamia taaluma ya Walimu hapa nchini.

(iii) kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo - P4R Wizara itaendelea kuratibu ujenzi wa Vyumba vya Madarasa 2,000 kwa Shule za Msingi na Sekondari na ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari 17, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa Madarasa na kuwafanya Wanafunzi kujifunza kwa ufanisi zaidi;

(iv) itagharimia ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Maji na Vyoo katika Shule za

Msingi 1000 na Sekondari 200 kwenye Mikoa ya Dodoma, Mara, Tabora, Mwanza, Kagera, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Simiyu, na Shinyanga kupitia Program ya Huduma ya Maji Elimu ya afya na Usafi wa Mazingira shuleni (SWASH).

(v) itahakiki shule za sekondari 700 katika mikoa 26 zitakazohusishwa kwenye mradi wa SWASH pamoja na kufanya ufuatiliaji na utoaji ushauri wa ujenzi kwa kutumia miongozo inayotolewa katika ngazi ya halmashauri.

(vi) itaendelea kusajili Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vituo vinavyotoa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kutilia mkazo uanzishwaji wa Shule zenye mwelekeo wa Sayansi, Kilimo, Teknolojia na Ufundi.

(vii) itahuisha Miongozo kuhusu ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi, Sekondari na Vituo vinavyotoa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kufanya ufuatiliaji katika Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ili kuhakiki uzingatiaji wa masharti ya usajili.

***Kuimarisha Utoaji wa Elimu Maalum***

105. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuongeza fursa za Elimu na Mafunzo kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kwa Mwaka 2017/18, Wizara yangu itafanya yafuatayo:

(i) itaimarisha utoaji wa Elimu Maalum na Elimu Jumuishi katika Shule za Msingi na Sekondari kwa kuhuishamiongozo kuhusu miundombinu na vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

(ii) itapitia utaratibu wa kupima na kutathmini maendeleo ya Wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa lengo la kuongeza ushiriki na ujifunzaji kwa Wanafunzi wenye mahitaji maalum.

(iii) itatoa mafunzo kwa Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Darasa la I - IV ambao hawakupata mafunzo katika Mwaka 2016/17. Lengo la mafunzo haya ni kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK na masomo ya Darasa la III hadi la IV kwa kuzingatia Mtaala ulioboreshwa.

***Kuimarisha Mafunzo Elimu ya Ualimu***

**106.** **Mheshimiwa Spika**, Katika kuendeleza na kuimarisha mafunzo ya ualimu, katika mwaka 2017/18 shughuli zifuatazo zitafanyika:

(i) kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Vyuo 6 vya Ualimu vya Kleruu, Mpwapwa, Dakawa, Tabora, Butimba na Marangu. Vilevile, itafanya ukarabati wa miundombinu ya Maktaba na Maabara za TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu 35 ili kuweka mazingira rafiki ya kujisomea kwa Wakufunzi na Wanachuo.

(ii) kuandaa na kuchapisha vitabu na nyenzo muhimu za kujifunzia na kufundishia ili kuwawezesha Wakufunzi na Wanachuo kupata rejea za kutosha na kuwezesha ujifunzaji.

(iii) itahuisha mitaala ya mafunzo ya Walimu Tarajali katika Vyuo vya Ualimu ili kuendana na mahitaji yaMtaala Ulioboreshwa na kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa

yanalenga kuongeza umahiri na weledi kwa wahitimu.

(iv) itatoa mafunzo kazini kwa Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha uwezo wao katika kumwandaa Mwalimu mwenye umahiri na weledi.

(v) kupitia mradi wa *Tutors Education Program* (TEP) unaofadhiliwa na Serikali ya Canada, Wizara yangu itatoa Mafunzo kwa Wakufunzi wa Hisabati, Sayansi na ICT/TEHAMA (In service Training) kwa Vyuo 35 vya Ualimu ili kuwaongezea ufanisi katika Ufundishaji.

(vi) itawajengea uwezo Viongozi wa Vyuo vya Ualimu katika uandaaji wa Mpango wa Maendeleo na Uongozi ili kuweza kusimamia vizuri utekelezaji wa mtaala na majukumu ya uendeshaji wa Vyuo.

(vii) itafanya mapitio ya Mtaala wa Stashahada ya Elimu ya Ualimu ili kupata Mtaala unaokidhi mahitaji ya sasa na kwa kuzingatia pia Mtaala wa Elimu Msingi ulioboreshwa.

***Kuboresha Mazingira ya Wathibiti Ubora wa Shule***

**107.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu pia inatambua kuwa Wathibiti ubora wa shule wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na mazingira wezeshi ya kufanya kazi zao kwa ufanisi. Hivyo, katika mwaka2017/18 Wizara itajenga Ofisi 50 za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya. Ujenzi wa Ofisi hizi utazingatia Wilaya ambazo zipo katika Majengo ya kupanga, Wilaya mpya ambazo hazina Ofisi na Wilaya ambazo tayari zimetenga maeneo ya ujenzi. Ujenzi wa Ofisi hizo utaboresha mazingira ya kufanyia kazi, kupunguza gharama za kulipia

pango na kuelekeza fedha hizo kwenye shughuli nahsusi zinazolenga kuthibiti ubora wa shule.

**108.** **Mheshimiwa Spika,** Sambamba na ujenzi wa ofisi, katika Mwaka 2017/18, Wizara yangu imepanga pia kufanya yafuatayo katika eneo la la Uthibiti Ubora ya Shule:

(i) itakagua Ubora wa Elimu katika Shule 11,021 zikiwemo Shule za Msingi 8,513, Sekondari 2,375, Vyuo vya Ualimu 133 na Vituo vinavyotoa Elimu ya Watu Wazima na Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa Walimu kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

(ii) itaboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuongeza vitendea kazi katika Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule katika wilaya 20 na Kanda 11. Vifaa vitakavyonunuliwa ni pamoja na Kompyuta 100, *Photocopy Machine 31*, *Printer 31* na *Scana* 31 na Samani za Ofisi.

(iii) itafungua ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule katika baadhi Wilaya mpya za Ubungo, Kigamboni, Chalinze, Nanyamba, Uvinza, Kakonko, Butiama, Ushetu, Msalala na Mlele ili kusogeza huduma za Uthibiti Ubora wa Shule karibu na Wadau. Vigezo vilivyotumika kuchagua Wilaya hizo ni kutokana na idadi ya Shule zilizopo katika Wilaya zilizoanzishwa, umbali kutoka ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule ya Wilaya ya jirani (Wilaya mama) na utayari wa Wakurugenzi wa Halmashauri husika katika kusaidia uanzishaji wa ofisi.

(iv) itaendelea kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa Sera, Nyaraka na Miongozo kuhusu uboreshaji wa Elimumsingi na Sekondari,

pamoja na kufanya tafiti kwa lengo la kubaini changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa Elimumsingi naSekondari na kuzipatia ufumbuzi.

(v) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 na kutumia mapendekezo yake katika kuimarisha utendaji kazi katika ngazi mbalimbali.

**Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (ESPJ)**

109. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu kupitia Mradi wa Elimu na kukuza stadi za kazi na ujuzi itatekeleza yafuatayo katika mwaka 2017/18:

(i) Kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji kwa kuhusisha Wadau;

(ii) Kukamilisha uundwaji wa Baraza la Kitaifa la kuendeleza na kusimamia Stadi za Kazi;

(iii) Kutengeneza Mfumo wa namna ya kuunda na kutumia *Student Voucher Scheme* kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na Wadau;

(iv) Kuandaa Mfumo Huishi wa Taarifa (*online information system*) kuhusu Utoaji wa Elimu na Mafunzo katika Vyuo na Taasisi zote za Elimu na Mafunzo kwa kushirikiana na TCU na NACTE, na VETA; na

(v) Kujenga uwezo waTaasisi zinazosimamia na kuratibu Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini.

**Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo**

110. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Wizara

yangu kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo itaendelea kuratibu utoaji wa motisha kwa Halmashauri zote pamoja na kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Uendeshaji wa Shule ili kuimarisha ubora wa utoaji elimu nchini. Vilevile Wizara itanunua Vifaa vya Maabara Awamu ya Pili ambapo awamu ya mwisho inategemewa kukamilika mwaka 2018/19. Wizara pia itasomesha Wahadhiri 100 katika Shahada ya Uzamivu kwenye fani zilizo na uhaba mkubwa wa wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Umma ili kuhakikisha elimu inayotolewa nchini ina ubora unaotakiwa. Aidha, shule ya kisasa ya Sekondari itajengwa katika mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuongeza miundombinu ya elimu katika makao makuu ya nchi.

## URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA

111. **Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Taasisi na Wakala tunazozisimamia. Shughuli zilizopangwa kufanyika mwaka 2017/18 katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kama ifuatavyo:

### Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

112. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2017/18, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itafanya yafuatayo:

(i) itaendeleza na kuboresha huduma za maktaba kwa kujenga maktaba ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka cha Bagamoyo *(SLADS)*,

(ii) itafanya upanuzi na ukarabati wa jengo la Maktaba ya Dodoma pamoja na ukarabati wa majengo ya Maktaba zaMikoa ya Tabora, Rukwa na Mwanza; na

(iii) itaanza ujenzi wa Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa Wananchi wa Mikoa hiyo kupata huduma za Maktaba.

(iv) itaongeza machapisho/vitabu 40,000 kwa ajili ya watu wazima na watoto pamoja na kuboresha upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA ili kuongeza ari ya usomaji katika jamii.

(v) itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini; na

(vi) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa wafanyakazi wa Maktaba katika Ngazi ya cheti na Diploma.

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania (TEWW)**

**113.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo:

(i) Kuandaa mkakati wa kusaidia kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika kwa kuandaa mafunzo ya wawezeshaji wa programu za kisomo na kufanya kampeni ya Kisomo (Literacy Programmes);

(ii) Kuongeza udahili wa wanafunzi katika programu mbalimbali wakiwemo vijana na watu wazima wanaopata Elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka18,675 mpaka 20,000 na wanafunzi1,500 wa programu za astashahada na stashahada;

(iii) Kuboresha programu za mafunzo kwa kudurusu mitaala;

(iv) Kujenga na kukarabati majengo katika mikoa ya Rukwa (uzio), Morogoro WAMO (Maktaba na Vyoo), Kilimanjaro (ukarabati), Kagera ( Ofisi) na Dar es Salaam (Library Extension);

(v) Kuimarisha uwezo wa Maktaba ya TEWW kwa kununua na kuweka vitabu1,000 vya kiada na ziada na kutumia TEHAMA katika usomaji; na

(vi) Kujenga na kuweka mtandao wa TEHAMA (Local Area Network - LAN) ili kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji.

**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

**114.** **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2017/18, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu utafanya shughuli zifuatazo:

(i) Ukarabati wa jengo la zamani na mabweni 3 ya Wanafunzi na kuanza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu Kampasi ya Bagamoyo na kuanza ujenzi katika vituo vya Mwanza na Mbeya;

(ii) Itafanya Tafiti 4 za kielimu kuhusu uendeshaji na Usimamizi bora wa taasisi za kielimu na kutoa Ushauri Elekezi juu ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu nchini. Tafiti 4 zitakazofanyika zitahusu utafiti kuhusu ufanisi wa mafunzo ya KKK yaliyotolewa kwa walimu wanaofundisha madarasa ya awali; athariza mafunzo ya Cheti cha Uongozi na Usimamizi wa Elimu katika kuimarisha utendaji kazi wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi katika Mikoa ya Njombe, Mbeya, Songwe na Iringa; ufanisi wa mrejesho kutoka kwa Wathibiti Ubora, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu Msingi na

tathmini ya maandalizi ya kupambana na majanga katika Taasisi za kielimu.

(iii) Itatoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa viongozi 1,500 wa idara mbalimbali za Elimu; mafunzo ya Stashahada ya Ukaguzi wa Shule kwa Wakaguzi 1,000 kutoka katika Wilaya zote za Tanzania Bara; na mafunzo ya cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 706 kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Njombe;

(iv) Itatoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wajumbe 10,000 wa Bodi za Shule za Sekondari kuhusu mbinu bora za usimamizi wa Elimu ya Sekondari katika Shule; na mafunzo ya awali ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wapya wa Shule za Sekondari 1,500 kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara; na

(v) Itatoa Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu 300 wa Shule za Sekondari zisizo za Serikali, Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu na Stadi za KKK kwa Wathibiti Ubora wa Shule 1,400, mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu na Stadi za KKK kwa Maafisa Elimu 528 na mafunzo kwa Walimu 45,000 wa Darasa la I na II kuhusu Stadi za KKK kwa Mikoa ya Tanzania Bara.

### Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC)

**115. Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2016 usimamizi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

ulihamishiwa katika Wizara yangu. Kwa kuzingatia hali halisi ya vyuo hivyo, Wizara itaboresha hatua kwa hatua mazingira yake ya kujifunzia na kufundishia ili kuhakikisha kuwa vinatoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya sasa.

**116.** Katika mwaka 2017/18 Wizara itafanya yafuatayo:

(i) itaendelea kuchambua hali halisi ya Rasilimali zilizopo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ikiwemo Wakufunzi, Watumishi wasio Wakufunzi, Miundombinu, Vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa lengo la kubaini mahitaji halisi na kuweka mpango wa muda mrefu wa uboreshaji wa vyuo hivyo.

(ii) itakarabati na kuboresha miundombinu ya Vyuo 10 vya Maendeleo ya Wananchi ili kuweka mazingira bora ya kutolea Mafunzo ya Ufundi Stadi na kuongeza udahili.

(iii) itawajengea uwezo Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili waweze kutoa elimu bora ya nadharia na vitendo kwa wanafunzi.

(iv) itaendelea kuvipatia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Vifaa, Mitambo na Mashine za kisasa za kufundishia na kujifunzia ili viweze kutoa elimu na mafunzo bora kwa walengwa.

(v) Itafuatilia upimaji maeneo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuviwezesha kupata Hati Miliki ya Ardhi. Hatua hii inalenga kuondoa changamoto ya uvamizi wa ardhi katika Vyuo hivyo.

**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi**

**117.** **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2017/18, NACTE itafanya yafuatayo:

(i) Itaendesha mafunzo kwa Maofisa Udahili katika Taasisi na Vyuo kuhusu namna ambavyo vinaweza kusaidia wanafunzi kufanya udahili;

(ii) itakagua na kusajili Vyuo 50 vyenye sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, kukagua na kutoa miongozo itakayoviwezesha Vyuo 100 kupata ithibati kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Aidha, itafuatilia na kutathmini Vyuo 350 vya Elimu ya Ufundi ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa ni yenye ubora na yanakidhi mahitaji ya soko la ajira. Vilevile, itaratibu utengenezaji wa Mitaala 45, kuhuisha Mitaala 10 na kuhakiki Mitaala 50 inayozingatia umahiri katika Vyuo vya Elimu na Ufundi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira;

(iii) itaendelea kutengeneza na kuboresha itayosaidia Mifumo ya Kieletroniki kuhakikisha ubora wa Elimu ya Ufundi ikiwemo Mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu za Wanafunzi; usimamizi wa Rasilimali watu Vyuoni na Mfumo wa Kutoa Vyeti na *transcript* kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi.

**Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA**

**118.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Vocational Education and Training Authority) ilianzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Bunge Sura ya 82 kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundi stadi na kusimamia ithibati na uthibiti wa mafunzo ya ufundi stadi nchini.

**119.** Katika mwaka wa fedha wa 2017/18 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imepanga kutimiza malengo yafuayayo:-

(i) itaendelea kufuatilia ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa;

(ii) itaanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera ambao umechelewa kuanza kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu muhimu kama vile umeme na barabara inayofikika kwa urahisi katika eneo lililotengwa. Mamlaka husika zinafanyia kazi suala la miundombinu na ujenzi wa Chuo utaanza mara baada ya ufumbuzi wa changamoto hizo kupatikana;

(iii) itakamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Namtumbo pamoja na ukarabati wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya Karagwe;

(iv) itaanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya za Chato, Chunya, Kilindi, Nyasa na Ukerewe pamoja na ujenzi wa Karakana ya Mitambo ya Kilimo na Vyumba vinne (4) vya Madarasa katika Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Arusha kilichopo Oljoro;

(v) itakamilisha ujenzi wa Karakana za Useremala, Umeme wa Magari na Jengo la Utawala katika Chuo cha Mkoa Morogoro-Kihonda; pamoja na kukamilisha ujenzi wa Karakana kumi na moja (11) za Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Lindi (4), Pwani (3), na Manyara (4);

(vi) itajenga mabweni mawili katika Chuo cha

Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro;

(vii) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro na kununua vitabu vya kiada na ziada kwa Vituo 7 vya Kanda za Vyuo vya Ualimu;

(viii) itasimamia mafunzo ya ufundi stadi nchini na kuendelea na usajili wa Vyuo na kutoa Ithibati na Uthibiti wa Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini;

(ix) itaendesha mafunzo na kusimamia mafunzo ya ufundi stadi ya muda mrefu na muda mfupi katika Vyuo vya Ufundi Stadi 761 nchini vikiwemo 29 vinavyomilikiwa na VETA na kusimamia utoaji wa mafunzo ya Ualimu wa Ufundi Stadi katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi Morogoro (MVTTC) kwa Walimu 700;

(x) itawezesha mafundi 8,320 kutoka sekta isiyo rasmi kutambuliwa na kurasimishwa baada ya kufanyiwa tathmini (Recognition of Prior Learning) katika fani mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu;

(xi) itawajengea uwezo wa kufanya kazi kwa vitendo wahitimu wa ufundi stadi katika vituo atamizi vya wahitimu *(incubators);*

(xii) itaongeza wigo wa waajiri wanaotoa mafunzo ya Uanagenzi *(Apprenticeship)* na kuboresha stadi za kazi/ujuzi kwa Wajasiriamali 3,000 kupitia Programu ya *Integrated Training for Entrepreneurship Promotion – INTEP.*

**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**120.** **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (Tanzania Commission for Universities-TCU) ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa mwaka 2005 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania, kufuatia maboresho yaliyofanywa na Serikali kwa lililokuwa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (HEAC) lililoanzishwa kwa Sheria ya Elimu Sura ya 523 ya Sheria za Tanzania.

**121.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Tume ya Vyuo Vikuu itafanya kazi zifuatazo:

(i) itaendelea kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa Kupitia Mifumo na Miongozo mbalimbali inayotumika kusimamia Uthibiti na Ithibati ya Elimu ya Juu nchini na Kukagua Vyuo 25 vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuhakiki ubora wake.

(ii) itafanya tathmini kwa programu 100 za masomo katika Vyuo Vikuu nchini na Kufanya tathmini na kutambua Tuzo 3,000 za ngazi za Shahada zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchi za nje;

(iii) itaanzisha Mfumo wa kutumia TEHAMA katika ukusanyaji taarifa kutoka vyuo vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji; na

(iv) Itashiriki katika makongamano na mikutano ihusuyo uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa elimu ya juu nchini.

## Chuo cha Ufundi Arusha

**122.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Chuo cha Ufundi Arusha (ATC) kilianzishwa mwaka 1978 kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu katika fani mbalimbali za elimu ya ufundi. Mwaka 2007 Chuo kilianza kujitegemea kiutendaji (Autonomus Institution) kupitia Tamko (Establishment Order) Namba 78 chini ya sheria ya Bunge namba 9 ya mwaka 1997 ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Katika mwaka 2017/2018 Chuo Cha Ufundi Arusha (ATC) kitatekeleza yafuatayo:

(i) Kudahili wanafunzi 1,065 wa mwaka wa kwanza, Astashahada (55), Stashahada (800) na Shahada (210);

(ii) Kuanzisha program mpya za stashahada katika fani mbalimbali za kiufundi na teknolojia kwa kuzingatia sera za kitaifa na mahitaji ya soko ambazo ni pamoja na “Pipe Works, Oil and Gas Engneering” na “Electrical and Hydropower Engineering”;

(iii) Kujenga Jengo la Madarasa na Maabara kwa fani za Madini na Vito, Uhandisi wa Vifaa Tiba, Uhandisi wa Mawasiliano ya Anga na Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari;

(iv) Kukarabati na kununua vifaa vya karakana za Useremala, Uhandisi Magari na Uhandisi Mitambo;

(v) Kuboresha elimu ya ufundi kwa kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi (wanataaluma 15 na waendeshaji 10) na kuajiri wafanyakazi wapya 104 (waendeshaji 22 na wanataaluma 82);

(vi) Kuhuisha mitaala 12 ya programu zilizopo za Ufundi Sanifu (NTA 4-6);

(vii) Kutekeleza Mpango Mkakati wa kuanzisha Mafunzo ya Umeme utokanao na nishati ya maji na uundaji wa mitambo midogo ya kuzalisha umeme utokanao na nishati ya Maji na kufufua kituo cha uzalishaji umeme cha Kikuletwa;

(viii) Kuendeleza shamba la mafunzo ya kilimo na umwagiliaji la Oljoro;

(ix) Kuendeleza ushirikiano na nchi wahisani, mashirika ya kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya kimataifa;

(x) Kuendelea na utafiti wa kupima uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara ili kuanisha ubora wake na kutoa ushauri wa matumizi sahihi wakati wa ujenzi wa barabara na pia kuongeza umahiri wa mafundi sanifu kwenye ujenzi wa barabara;

(xi) Kuendelea kuboresha fimbo inayowasidia walemavu wa macho electronic blind stick katika kutambua sehemu za mapitio yao ili kuwaongoza kwa urahisi. Hii itasaidia upatikanaji nwa fimbo hizo kwa gharama nafuu;

(xii) Kitaendelea kuunda Helikopta ya gharama nafuu na salama kwa safari fupi nchini ili kurahisisha usafiri katika maeneo yasiyofikika kwa usafiri wa gari kwa urahisi; na

(xiii) Kitaboresha Mafunzo kwa kununua mashine na mitamboya kisasa, kwa fedha zilizotolewa na Serikali ya Austria kama mkopo wa

masharti nafuu wa **Euro 6,000** sawa na takriban shs **billioni 14.** Aidha, Chuo kitaimarisha ufundishaji na kutoa mafunzo yenye lengo la kujenga uwezo kwa wanataaluma ili waweze kutumia mitambo ya kisasa itakayonunuliwa.

**Baraza la Mitihani la Tanzania**

**123.** **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2017/18, Wizara yangu kupitia Baraza la Mitihani imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 900,000 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo Septemba, 2017;

(ii) Kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,060,000 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo Novemba, 2017;

(iii) Kuendesha upimaji wa Kitaifa wa kidato cha Pili kwa watahiniwa 450,000 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2017;

(iv) Kuendesha Mtihani wa Kidato cha Nne kwa watahiniwa 440,000 na wa mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,000 wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo Novemba, 2017;

(v) Kuendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 73,000 wanaotarajiwa kufanya Mtihani huo Mei, 2018; na

(vi) Kuendesha Mtihani wa Cheti na Diploma ya Ualimu wa marudio kwa watahiniwa 5,000 wanaotarajiwa kufanya Mtihani huo Mei, 2018.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

124. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuchapa vitabu vya Kiada kwa Darasa la IV na Masomo ya Elimu ya Sekondari kwa Kidato cha I-VI;

(ii) Kutathmini machapisho mbalimbali yaliyoandikwa na makampuni/watu binafsi ikiwemo yale yaliyo katika mfumo wa kielektroni;

(iii) Kuboresha Mtaala wa Elimu ya Ualimu na kuandaa moduli zake;

(iv) Kuratibu na kuendesha programu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA; na

(v) Kuendesha mafunzo kazini kwa Walimu wa Elimumsingi na Sekondari ili kuboresha utendaji kazi wao.

**Tume ya Taifa ya UNESCO**

125. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Tume ya Taifa ya UNESCO imepanga kutekeleza yafuatayo:

(i) Kuratibu mafunzo kwa ufadhili wa UNESCO; na kuandaa Mikutano kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana ili kutekeleza shughuli za UNESCO kwa kujenga uelewa wa Malengo endelevu; na

(ii) Kuandaa maandiko matano ya Miradi ya kuboresha elimu kwa ajili ya ufadhili kutoka UNESCO na Wadau wengine; na kuandaa Jarida la Tanzania na UNESCO Toleo namba 14.

**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**126.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imepanga kutekeleza yafuatayo:

i. Kutoa Mikopo na Ruzuku kwa wanafunzi wanufaika na mikopo.

ii. Kuboresha vigezo vya utambuzi ili kuwawezesha Wanafunzi wasio na uwezo wa kiuchumi kupata Elimu ya Juu kupitia Mikopo na Ruzuku;

iii. Kupunguza utegemezi wa kifedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa asilimia 35%; na

iv. Kutambua vyanzo vingine vya kuchangia Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Juu na Ufundi kwa ajili ya kukopesha wanufaika wengi.

**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia**

**127.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itaendelea kuratibu maandiko yatokanayo na tafiti mbalimbali *Policy Briefs* katika Taasisi za utafiti ili kuwezesha maamuzi kufanyika kwa kutumia ushahidi wa kisayansi.

**128.** Katika mwaka 2017/18 itafanya shughuli zifuatazo:

(i) itafadhili miradi mipya na inayoendelea ya utafiti katika maeneo ya Viwanda, TEHAMA, Kilimo, Afya, Mazingira na Maliasili.

(ii) Wafadhili watafiti kutoka Taasisi za utafiti za umma wataendelea kuwezeshwa kusoma shahada za uzamivu katika vyuo vya ndani

ya nchi.

(iii) itaendelea kuimarisha matumizi ya matokeo ya utafiti na ubunifu kutoka taasisi za ndani ya nchi ili yaweze kuleta manufaa ya kibiashara.

**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

129. **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) ni Chuo Kikuu cha umma ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 1 Julai, 1970 na kupata ithibati ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Namba 005, mnamo tarehe 24 Novemba, 2006.

130. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 kitatekeleza yafuatayo:

(i) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa shahada za awali kutoka 24,182 hadi 25900 (ongezeko la asilimia 7). Wanafunzi wa shahada na stashahada za uzamili wataongezeka kutoka 2092 hadi 2510 (ongezeko la silimia 20) na wa stashahada na astashahada wataongezeka kutoka kutoka 182 hadi 218 (ongezeko la asilimia 20).

(ii) Kuongeza idadi ya miradi ya utafiti, hasa yenye ufadhili wa washirika wetu wa maendeleo ambapo maandiko ya miradi yamewasilishwa na mengine yanaendelea kutayarishwa;

(iii) Kuongeza idadi ya majarida ya kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka 5 kwa sasa hadi 21 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao;

(iv) Kupanua wigo wa “Juma la Utafiti” na kuonyesha matokeo ya tafiti za Chuo Kikuu

cha Dar es Salaam kupitia runinga na redio;

(v) Kutoa mafunzo maalum ya utafiti na uchapishaji kwa wanataaluma 100 na wanafunzi 100 wa shahada za uzamili;

(vi) Kuanzishakituochakuatamiaubunifu mpya (incubator) kitakachojumuisha maeneo mbalimbali ya kitaaluma.

(vii) Kutoa mafunzo maalum ya ushauri wa kitaalam kwa wanataaluma 100 na wafanyakazi 50 wa kada nyinginezo. Pia kutoa mafunzo ya kisasa kwa jamii, ya muda mfupi na wa kati, katika nyanja mbalimbali na teknolojia mpya na za kisasa; na

(viii) Kupanua wigo wa kutangaza huduma za ushauri kwa njia mbalimbali, kama kushiriki maonesho ya kitaifa na kimataifa na/au kutumia runinga, magazeti, machapisho na vipeperushi.

(ix) Kukarabati bweni Na. 5 la Kampasi ya Mwl. J.K. Nyerere Mlimani na kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji safi na maji taka;

(x) Ujenzi wa awamu ya pili ya Kituo cha Buyu (Zanzibar) kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Bahari; Kujenga ofisi mpya ya michezo katika viwanja vya michezo vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kuongeza ghorofa mbili na samani katika mabweni mapya yanayojengwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ufadhili wa Serikali; na sehemu ya gharama za kujenga miundombinu na kununua vifaa kwa ajili ya hospitali maalum ya mafunzo ya udaktari bingwa;

(xi) kununua samani na vifaa vya maabara

kwa ajili ya majengo mapya na kufanya ununuzi wa vitabu na mashubaka kwa ajili ya Maktaba mpya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(xii) Kuongeza Vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kufanyia matengenezo viwanja na kuongeza vifaa vya michezo.

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**131. Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ni Chuo cha umma kilichoanzishwa baada ya kutiwa saini kwa Hati Idhini ya Chuo tarehe 5 Machi, 2007 na kwa kuzingatia sheria ya vyuo vikuu Namba 7 ya mwaka 2005.

**132. Mheshimiwa Spika,** Malengo ya Chuo kwa mwaka 2017/2018 ni haya yafuatayo;

(i) Kudahili wanafunzi wapya 8,412 wa shahada ya kwanza, Kudahili wanafunzi wapya 3,124 wa Stashahada na Astashahada, Kudahili wanafunzi wapya 348 wa shahada za Uzamili na Uzamivu. Chuo kina lengo la kuwa na jumla ya wanafunzi 28,367 kwa mwaka wa masomo 2017/2018;

(ii) Kuanza ujenzi wa Ukumbi mmoja wa Mihadhara katika Chuo cha Sayansi Asilia na Hisabati; Ujenzi wa Ukumbi mmoja wa Mihadhara katika Chuo cha Sayansi za Ardhi; na Ujenzi wa Madarasa na Ofisi katika Chuo cha Sayansi Asilia na Hisabati pamoja na Chuo cha Sayansi za Ardhi;

(iii) Kuanza Ujenzi wa Awamu ya pili Chuo cha Sayansi za Afya; Pamoja na Ujenzi

wa nyumba 100 za Wafanyakazi Awamu ya Kwanza (nyumba nane (8) za ghorofa kwa ajili ya familia nane kila moja – 64 na nyumba 36 kwa ajili ya Viongozi ikiwa ni pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo, Manaibu Makamu Wakuu wa Chuo, Wakuu wa Vyuo, Wakurugenzi na Wakuu wa Skuli;

(iv) Ununuzi wa magari 20; Ununuzi wa kompyuta; Ununuzi wa vifaa vya maabara; na

(v) Ununuzi wa Samani za Ofisi, Makazi, Madarasa, Maabara na Mabweni ya wanafunzi; na Ukarabati wa Mabweni, Madarasa na majengo mengine ya Chuo;

(vi) Kununua vifaa muhimu vya kufundishia pamoja na zana za kufundishia;

(vii) Kuwapeleka masomoni wafanyakazi 268. Kati ya hao 177 ni watakaokwenda kuanza masomo na 91 ni wafanyakazi wanaoendelea na masomo (shahada ya Uzamivu 81, shahada ya Uzamili 86, Shahada za Awali 15, Stashahada 23, Astashahada 14, mafunzo ya muda mfupi 32, na watakaosomeshwa nje ya nchi 17); na

(viii) kuajiri wafanyakazi wapya 445 ili kukidhi ikama ya wafanyakazi.

**Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo**

**133.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilianzishwa tarehe 1 Julai, 1984 chini ya Sheria Na.6 ya mwaka 1984 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Aprili,

1984 na kurekebishwa na Sheria Na.14 ya mwaka 1984. Sheria hiyo ilifutwa kwa Sheria namba 7 ya mwaka 2005 ya Vyuo Vikuu ambayo ilikipa Chuo mamlaka ya kuwa na Hati idhini yake ya mwaka 2007.

**134.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) Kuanzisha shahada mpya za kwanza sita (6) na shahada za uzamili tisa (9) na masomo yasiyo ya shahada katika fani nne (4) ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira; na

(ii) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wakiwemo wanafunzi wa shahada za kwanza kutoka 3,004 hadi 4,456, shahada za juu (Uzamili na Uzamivu) kutoka 166;

(iii) kufanya tafiti mbalimbali zaidi ya150 katika kulenga uboreshaji na uzalishaji wa mzao ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi n.k ili kupunguza umaskini kwa Wananchi.

(iv) Kuongeza utoaji wa Elimu na Ushauri kwa wakulima kwa kutumia mbinu mbalimbali kama semina, kozi fupi, warsha, luninga na radio;

(v) Kuendesha programu 80 za utoaji wa Elimu na Ushauri wa kitaalamu kwa washiriki 350 wakiwemo Wakulima, Maafisa Ugani na Watafiti;

(vi) Kukarabati vyumba 6 vya mihadhara vilivyomo Kampasi ya Solomon Mahlangu pamoja na Kumbi na Hosteli za Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza;

(vii) Kuendelea kuboresha nyumba za wafanyakazi kwa kukarabati nyumba 60;

(viii) Kuendelea kuboresha mabweni ya wanafunzi kwa kukarabati mabweni 4;

(ix) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kusomea ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa vifaa na zana za kufundishia;

(x) Kukamilisha miradi ambayo inaendelea ikiwepo Mradi wa Ujenzi wa Maabara katika Kampasi ya Solomon Mahlangu;

(xi) Kuongeza miundombinu mipya ya kufundishia ambayo ni pamoja na ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara, Ujenzi wa Maabara, Ujenzi wa Viti vya Kusomea na Hosteli moja ya wanafunzi wa Uzamili na Jengo la Ofisi za Wafanyakazi; na (xii) Kuendelea kujenga mahusiano na Taasisi nyingine ndani na nje ya nchi.

## Chuo Kikuu Mzumbe

135. **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Mzumbe kilianzishwa kwa Sheria ya Chuo Kikuu Mzumbe Na. 9 ya mwaka 2001. Kwa sasa, Chuo kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Hati idhini ya Chuo ya mwaka 2007 iliyotolewa chini ya Kifungu cha 25 cha Sheria ya Vyuo Vikuu ya Mwaka 2005.

136. **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Mzumbe kwa mwaka 2017/18 kimepanga kutekeleza yafuatayo;

x) Kukamilisha miradi ambayo inaendelea

(i) Kudahili wanafunzi wapya 5,092 katika

programu mbalimbali (astashahada - 250, stashahada - 200, shahada ya kwanza – 3,463, shahada ya umahiri – 1,174 na shahada ya uzamivu – 5).

(ii) Kukamilisha utafiti katika maeneo 41 na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo 50 ya menejimenti, uongozi, teknolojia na sayansi ya jamii kwa ujumla.

(iii) Kukarabati mabweni nane (8) ya wanafunzi Kampasi Kuu Mzumbe;

(iv) Kukarabati ofisi za watumishi Kampasi ya Dar es Salaam;

(v) Kukarabati na kujenga miundombinu ya Kampasi ya Mbeya;

(vi) Kujenga kumbi mbili (2) za mihadhara Kampasi Kuu Mzumbe;

(vii) Kujenga jengo la kitaaluma kwa ajili ya programu za Sayansi na Teknolojia Kampasi Kuu Mzumbe;

(viii) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Utawala Kampasi Kuu Mzumbe;

(ix) Kujenga miundombinu ya barabara, umeme, maji safi na majitaka Kampasi Kuu Mzumbe;

(x) Kujenga mtambo wa kuchomea taka hatarishi katika Kituo cha Afya Kampasi Kuu Mzumbe;

(xi) Kuboresha mfumo wa uhasibu wa kompyuta (Sage ERP ACCPAC);

(xii) Kuboresha maabara za kompyuta Kampasi Kuu Mzumbe;

(xiii) Kuanzisha maabara ya kompyuta katika Kituo cha Mwanza;

(xiv) Kuboresha Mfumo na usambazaji wa maji Kampasi Kuu Mzumbe;

(xv) Kuendeleza eneo la Tegeta Kampasi ya Dar es Salaam;

(xvi) Kugharimia mafunzo ya watumishi 36 ambapo 18 katika ngazi ya shahada ya umahiri na 18 katika ngazi ya shahada ya uzamivu; na

(xvii) Kuchapisha vitabu kumi na moja (11), makala za kufundishia nane (8) na makala nyingine 59.

**Chuo Kikuu Huria cha Tanzania**

**137.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilianzishwa kwa sheria ya Bunge Na. 17 ya mwaka 1992. Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi kufuatia tangazo katika Gazeti la Serikali Na. 55 la mwezi Machi, 1993. Hata hivyo, kufuatia uanzishwaji wa Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005, Chuo kwa sasa kinaendeshwa kwa kutumia Hati Idhini yake ya mwaka 2007.

**138.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18, shughuli mbalimbali zimepangwa kutekelezwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kama ifuatavyo:

(i) Kudahili jumla ya wanafunzi 11,100 wa fani mbalimbali ambapo 1000 watadahiliwa ngazi ya Cheti, 1500 watadahiliwa ngazi ya

stashahada, 7500 watadahiliwa kwenye Shahada ya kwanza, 1,000 watadahiliwa shahada ya Uzamili na 100 watadahili shahada ya Uzamivu;

(ii) Kufanya utafiti katika maeneo ya Mazingira, TEHAMA, Nishati, Kilimo na Chakula, Uongozi na Biashara, Maendeleo ya Utalii, Sheria, Uthibiti wa Ubora, Utawala na Maendeleo, Watu wenye Ulemavu na Mahitaji Maalumu, Maliasili, Umaskini, Utamaduni, Haki za Binadamu, Maendeleo ya Watu na Mawasiliano;

(iii) Kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Mazingira, TEHAMA, Nishati, Kilimo na Chakula, Uongozi na Biashara, Maendeleo ya Utalii, Sheria, Uthibiti wa Ubora, Utawala na Maendeleo, Watu wenye Ulemavu na Mahitaji Maalumu, Maliasili, Umaskini, Utamaduni, Haki za Binadamu, Maendeleo ya Watu na Mawasiliano;

(iv) Kujenga Maabara ya Sayansi, hosteli za Wanafunzi na Vyumba vya Madarasa Makao Makuu Bungo, Kibaha;

(v) Kujenga ofisi za Wafanyakazi, ukumbi wa Mihadhara na vyumba vya Maabara ya kompyuta katika vituo vya Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mwanza, Lindi na Manyara;

(vi) Kukarabati vituo vya Mikoa vya Morogoro (Awamu ya II), Songwe, Kilimanjaro, Lindi, Zanzibar na Simiyu pamoja na Vituo vya Uratibu vya Chato, Kibondo, Kasulu, Nachingwea na Serengeti;

(vii) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na

wanafunzi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na matumizi ya TEHAMA hasa katika'Learning Management System';

(viii) Kuweka kozi zote kwenye mfumo wa mtandao (Moodle) ili kurahisisha kujifunza na ufundishaji;

(ix) Kununua samani kwa ajili ya vituo vya Mwanza, Songwe, na Geita na vifaa vya ofisi; na

(x) Kufuatilia kwa ukaribu upatikanaji wa hati Miliki za viwanja vya Chuo katika Mikoa mbalimbali na kujenga uzio kwenye viwanja ambavyo havina uzio.

**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**

**139.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) ni muendelezo wa kilichokuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya (MUCHS) ambacho kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Sheria Na. 9 ya 1991, wakati kitivo cha tiba cha Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kilipobadilishwa na kuwa Chuo Kikuu Kishiriki. Mnamo mwaka 2007, MUCHS ilibadilishwa na kuwa MUHAS (Article 1 of the Charter of Incorporation).

**140.** **Mheshimiwa Spika,** Malengo ya Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi kwenye Bajeti kwa Mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo;

(i) Kudahili wanafunzi 1,370 wakiwemo wa Stashahada 340; wa Shahada ya Kwanza 660; wa Uzamili 360 na wa Uzamivu 10;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo tafiti za:-

- Magonjwa yanayoambukiza (infectious

diseases) yakiwemo UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu;

- Magonjwa yasioambukiza (non-communicable diseases) yakiwemo Kisukari, magonjwa ya moyo, ugonjwa wa selimundu (Sickle cell disease);

- Afya ya uzazi na watoto;

- Magonjwa yasiyopewa kipaumbele (neglected tropical diseases); na

- Tafiti za mfumo wa afya nchini (health system);

(iii) Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na afya za binadamu;

(iv) Kuendelea kutoa huduma kwa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Rufaa, Muhimbili. Vilevile wanataaluma wa Chuo watatembelea baadhi ya Mikoa kushiriki katika utoaji huduma kwa jamii;

(v) Kufanya ukarabati wa hosteli, ofisi, maabara na nyumba za wafanyakazi pamoja, ukarabati wa mfumo wa kusambaza maji chuoni (Muhimbili), uwekaji wa 'lifti' kwenye jengo jipya pamoja na ukarabati wa uwanja wa michezo;

(vi) Kuanza Ujenzi wa majengo ya kufundishia, mabweni, maabara na nyumba za wafanyakazi wa hospitali–Kampasi ya Mloganzila;

(vii) Kuanza Ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu;

(viii) Kuongeza na kuboresha miundombinu ya mawasiliano (ICT infrastructure) pamoja na elimu katika nyanja hiyo kwa wanafanyakazi; na

(ix) Kuajiri wafanyakazi kwenye maeneo yenye upungufu na kuwaongezea elimu;

## Chuo Kikuu Ardhi

**141.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Ardhi kilianzishwa tarehe 31/9/2008 kutokana na Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 (Universities Act, 2005) na baada ya kukidhi kanuni za usajili wa vyuo (TCU, Chartering Registration and Accreditation Procedures Regulation, 2006) pamoja na Hati Idhini ya mwaka 2007 (Ardhi University Charter 2007).

**142.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18 Chuo Kikuu Ardhi kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

(i) Kudahili wanafunzi 4,622 katika fani mbalimbali, kati yao wanafunzi 4,372 ni wa Shahada ya kwanza na 250 ni wa Stashahada za Juu, Uzamili na Uzamivu;

(ii) Kufanya tafiti mpya kumi na nne (14) katika maeneo mbalimbali yahusuyo ujenzi, usimamizi wa mazingira na matumizi bora ya ardhi. Chuo pia kitaendelea kufanya tafiti thelathi (30) zilizokwishaanza;

(iii) Kutoa machapisho 200 yanayotokana na tafiti mbalimbali katika majarida ya nchini na nje ya nchi;

(iv) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ujenzi, usimamizi wa mazingira na matumizi bora ya ardhi kwenye miradi nane(8). Chuo

pia kitatoa huduma kwa jamii kupitia 'public outreach programs' tano (5);

(v) Kukarabati majengo yafuatayo: (a) hosteli za wanafunzi awamu ya IX (b) madarasa, (c) karakana ya useremala, (d) tanki la kuhifadhia maji la ujazo wa lita 600,000, (e) jengo la uchapishaji, (f) nyumba za wafanyakazi na (g) barabara na maegesho ya magari;

(vi) Kuhuisha mitaala ya mafunzo na kuandaa mitaala mipya (curicula review);

(vii) Kugharamia mafunzo ya wafanyakazi katika shahada za uzamivu 45, uzamili 54, shahada ya kwanza 12 na diploma na cheti 20;

(viii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la madarasa na ofisi la 'Lands Building' awamu ya tano;

(ix) Kujenga hosteli za wanafunzi 2000 awamu ya I;

(x) Kujenga jengo la maabara (Multipurpose Laboratory);

(xi) Kujenga miundombinu mipya ya TEHAMA; na

(xii) Kujenga mfumo wa maji taka, kuunganisha majengo pamoja na kujenga mfumo wa umeme wa jua katika majengo yaliyoko kwenye matumizi.

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Saalam (DUCE)**

**143.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Dar es salaam kilianzishwa kupitia tangazo la Serikali Na. 202 lililochapishwa tarehe 22 Julai 2005 chini ya kifungu 55(1) cha Sheria Na. 12 ya mwaka 1970 ya

Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Chuo Kilipewa Hati idhini (Charter) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010.

**144.** **Mheshimiwa Spika,** Malengo ya DUCE katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo:

(i) Kudahili jumla ya wanafunzi 2,000 kati yao 700 wa fani ya sayansi;

(ii) Ujenzi wa kituo cha utafiti;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kukarabati miundombinu ya umeme;

(iv) Kupata ardhi nyingine kubwa zaidi kwa ajili ya upanuzi wa Chuo na pia kufanya upanuzi wa maabara za sayansi, vyumba vya madarasa (Awamu ya II) na mfumo mku wa maji taka. Kukarabati majengo na miundombinu ya Chuo;

(v) Kuendelea kushirikiana na Vyuo na Taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususani kwa shahada za uzamili na uzamivu;

(vi) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na Kununua vifaa vya maabara pamoja na madawa (chemicals); na

(vii) Kuajiri jumla ya wafanyakazi 178 kati yao walimu 75 na waendeshaji 103.

## Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

**145.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 6 ya mwaka 2005.

146. **Mheshimiwa Spika,** Malengo ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 5,173 mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka kufikia 5,900 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na pia kuanza kutoa mafunzo ngazi ya uzamili kwa kuanzia na programu angalau mbili katika Kampasi ya Kivukoni Dar es Salaam.

(ii) Kuimarisha miundo na uendeshaji wa idara ya Tafiti na Machapisho na kuimarisha kitengo cha udhibiti ubora ili kuweza kuboresha Elimu inayotolewa kwa kuweka kitengo kwa kila idara na kuboresha mitaala ili iweze kwenda na wakati;

(iii) Kutoa, elimu, usimamizi wa fedha, utunzaji wa kumbukumbu kwa sekta binafsi na sekta ya umma; na

(iv) kukarabati miundombinu ya chuo hasa madarasa,nyumba za wafanyakazi na ununuzi wa samani;

**Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya**

147. **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST) kilianzishwa mwaka 2012 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7 ya mwaka 2005 baada ya kupandishwa hadhi na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa iliyokuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. MUST ilitunukiwa Hati Idhini ya Chuo Kikuu (Mbeya University of Science and Tecknology Charter 2013) mnamo tarehe 20 Agosti 2013.

**148.** **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

(i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 3,982 kwa mwaka wa masomo 2016/2017 hadi kufikia wanafunzi 4,300 kwa mwaka wa masomo 2017/2018,

(ii) Kuandaa na kukarabati miundombinu ya Chuo katika Kampasi ya Rukwa kwa ajili ya kuanza kutoa mafunzo katika ngazi ya stashahada (Ordinary Diploma) kwa mwaka wa masomo 2017/2018; na pia kuendelea na kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba ili kukidhi mahitaji ya huduma bora za maktaba kwa wanafunzi na wahadhiri;

(iii) Kuandaa mpango kabambe wa upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kuwa na miundombinu stahiki kwa maendeleo ya Chuo Kikuu; pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu ya maji, umeme na majengo ya Chuo Kikuu;

(iv) Kufanya tathimini ya mali za wananchi waishio katika eneo la hekta 511 la Chuo Kikuu ili kupisha shughuli za upanuzi wa Chuo Kikuu;

(v) Kuongeza eneo la Kampasi ya Rukwa kutoka hekta 48 hadi kufikia hekta 500 ili kuwezesha upanuzi wa shughuli za Kampasi hapo baadaye; Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanza ujezi wa Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (College of Engineering and Technology);

(vi) Kuanza ujenzi wa kituo cha Atamizi za Teknolojia (Technology Incubation Centre) kwa lengo la kuchochea na kuongeza ubunifu

wa teknolojia mpya kwa maendeleo ya jamii;

(vii) Kuanza kutoa mafunzo ya ualimu wa sayansi na mafunzo ya sayansi na teknolojia ya maabara katika ngazi ya shahada ya kwanza ili kuongeza upatikanaji wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari na vyuo vya ufundi nchini; na

(viii) Kukamilisha uandaaji wa mitaala mipya ya kufundishia katika ngazi ya stashahada, shahada kwanza, stashahada ya uzamili, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu.

**Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – NM-AIST**

**149.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (The Nelson Mandela African Institute of Science and Techology in Arusha-NM-AIST Arusha) ilianzishwa mwaka 2009 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7 ya mwaka 2005. Taasisi hii ina jukumu la kutoa elimu na mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu pamoja na kufanya utafiti katika ngazi ya ubobezi. Malengo ya Taasisi kwa kipindi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza Udahili wa wanafunzi kutoka 213 hadi 350 kufikia Juni 2018;

(ii) Kufanya mapitio ya mitaala na programu za mafunzo kufikia Juni 2018; pamoja na kusambaza maarifa na kubadilishana mitaala/programu za mafunzo kufikia Juni 2018;

(iii) Kufanya Utafiti na uchambuzi yakinifu kwa ajili ya Kampasi ya Tengeru kufikia juni 2018;

(iv) Kuandaa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi Kampasi ya Tengeru kufanyika kufikia Juni, 2018;

(v) Kubuni michoro na ujenzi wa jukwaa, vyoo na barabara kwa ajili ya viwanja cha michezo na mfumo wa maji safi kwa vyanzo vipya vya maji;

(vi) kubuni na kujenga mfumo wa uondoaji maji taka, kujenga mabweni ya Wanafunzi, kujenga majengo ya ofisi kampasi ya Tengeru kwa ajili ya wafanyakazi 200, vyumba vya madarasa 10 na kumbi 6 ya mikutano pamoja na kubuni na kujenga Kituo cha Afya kufikia Juni, 2018; na

(vii) Kuanzisha maabara maalum kwa kununua vifaa vya sayansi ya miamba kufikia Juni, 2018 na kufanya ununuzi wa kompyuta mpakato 9 ifikapo Juni, 2018.

**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam**

150. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kilianzishwa kwa Sheria ua Bunge Na.6 ya mwaka 1997. Taasisi ina jukumu la kutoa mafunzo katika ngazi ya ufundi sanifu na uhandisi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Ufundi, Teknolojia na Uhandisi;

151. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi hii ina malengo yafuatayo katika mwaka wa fedha 2017/2018.

(i) Kudahili wanafunzi wapya 1,500 na kuendelea kuhudumia wanafunzi 2,926 wanaoendelea hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 4,426;

(ii) Kufanya mapitio ya programu za Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili pamoja na

Kuanzisha kozi mpya za Stashahada ya Uhandisi katika Ujenzi na Barabara; Shahada ya Uhandisi katika Madini; na Shahada ya Uzamili ya Uhandisi katika Nishati Endelevu;

(iii) Kuanzisha kozi ya stashahada ya utengenezaji viatu na kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya kitaalam katika teknolojia ya ngozi kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la ngozi kwa wafugaji;

(iv) Kukamilisha ujenzi wa jengo la DIT Teaching Tower awamu ya pili na ya mwisho; na

(v) Kutekeleza miradi 30 ya huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii na Kutekeleza mradi wa TELMS awamu ya pili unaofadhiliwa na Serikali ya Italia.

**Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

**152.** **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kilipata Hati Idhini tarehe 23 Februari, 2015 baada ya kutimiza vigezo vya TCU vya kuwa Chuo Kikuu kamili. Chuo hiki kilianza kama Koleji ya Ushirika mwaka 1963 na baadaye kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuanzia 2004 hadi tarehe 4 Septemba 2014. Hiki ni Chuo pekee nchini kilichobobea katika kuandaa wataalamu wa Elimu ya Ushirika na fani zinazoshabihiana na ushirika.

**153.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 Chuo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

(i) Kusajili wanafunzi 4,000 kwa mwaka wa masomo 2017/2018 na Kuendeleza mafunzo ya wafanyakazi 70, hususani Wahadhiri katika ngazi za Uzamili na Uzamivu;

(ii) Kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2500 kwa wakati mmoja;

(iii) Kukarabati miundombinu ya zamani; kumbi za mihadhara, madarasa, mabweni, barabara za ndani, majengo ya ofisi, mfumo wa mawasiliano wa ndani na nyumba za makazi; na

(iv) Kuendelea kutoa na kueneza elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususani Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO); Shirikisho wa Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na vyama vya ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa**

**154.** **Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Mkwawa kilianzishwa kupitia tangazo la Serikali Na. 202 la tarehe 22 Julai 2005 chini ya Kifungu 55(1) cha Sheria Na. 12 ya mwaka 1970 ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Chuo Kilipewa Hati Idhini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010. Chuo hiki kimejikita kuandaa waalimu wa shahada ya kwanza wa sayansi na sayansi za jamii kwa lengo la kuhudumia shule za sekondari nchini.

**155.** **Mheshimiwa Spika**, Malengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa katika mwaka 2017/18 ni pamoja na:

(i) Kuboresha ufundishaji wa kiugunduzi na kutumia teknolojia katika ufundishaji katika programu zote za elimu kwa kuunga mkono matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji na

ufundishaji wa kiugunduzi, kuongeza udahili wa wanafunzi na kuanzisha Maktaba ya kisasa;

(ii) Kutoa mafunzo ya kina katika programu za elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali, ngazi ya kati mpaka ngazi ya juu ya kada ya ualimu kwamba Taasisi itarekebisha na kuboresha mitaala katika program za elimu na kutekeleza utafiti na uzinduzi wa programu ya elimu ya mazoezi na sayansi ya michezo (PESS);

(iii) Kuboresha na kutoa mafunzo anuai katika programu za kitaaluma na kiweledi katika nyanja tofauti tofauti kwa kuanzisha programu 3 mpya za shahada ya kwanza, shahada ya umahili na programu mpya za astashahada na stashahada ya uzamili;

(iv) Kuimarisha uwezo wa Rasilimali watu katika utendaji na utoaji huduma kwa jamii kwa kuimarisha kitengo cha masomo ya uzamili, utafiti na huduma kwa jamii, kuongeza matokeo yanayotokana na utafiti na ubunifu kutoka machapisho 50 hadi machapisho 250, kukuza na kujenga ushirikiano na mahusiano ya umma;

(v) Kutangaza Programu za mafunzo yanayotolewa na Chuo kwa kuimarisha Uongozi, Usimamizi na Utawala bora, kuhamasisha na kusimamia ipasavyo rasilimali na fedha za Chuo katika kuimarisha programu za elimu zinazotolewa na Taasisi; na

(vi) Kuboresha na kuimarisha vitendea kazi na miundombinu ya kufundishia na ujifunzaji kwa kumalizia ujenzi wa ukumbi wa mihadhara, ujenzi wa maabara 2 za sayansi, ujenzi wa ofisi na ukarabati wa miundo mbinu ya chuo,

uwekaji wa umeme wa jua na uchimbaji wa visima vya maji safi.

## Tume ya Taifa ya UNESCO

**156.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya UNESCO ni chombo kinachosimamia utekelezaji wa programu za UNESCO nchini. Jukumu lake kuu ni kuratibu utekelezaji wa Progamu za UNESCO nchini katika Nyanja zake tano ambazo ni Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Mawasiliano na Habari.

**157.** **Mheshimiwa Spika,** Kazi zilizopangwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuratibu utekelezaji wa sheria/ miongozo ya UNESCO nchini ikiwa na pamoja na ushiriki wa Tume yaTaifa ya UNESCO katika mikutano ya UNESCO, kuratibu utekelezaji wa programu mbalimbali za UNESCO na pia kuratibu/kutekeleza miradi (participation program) kwa kadri inavyowezekana;

(ii) Kutaarifu wadau na Kuratibu ufadhili wa UNESCO kimasomo pamoja na Kuitangaza Tume ya Taifa ya UNESCO kupitia vyombo vya habari;

(iii) Kushiriki katika kuadhimisha siku 5 za UNESCO na Serikali pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali kisekta;

(iv) Ufuatiliaji wa jarida toleo la 13 la Tanzania na UNESCO na kuandaa jarida toleo la 14 la Tanzania na UNESCO;

(v) Kuandika mawazo ya miradi (angalau miradi 5) kwa UNESCO na wadau wengine ili kunufaisha Taifa letu;

(vi) Kuandaa Mikutano kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana ili kuendana na shughuli za UNESCO lakini pia na kumudu kasi ya Malengo ya Dunia Endelevu na kufanya Mkutano na wadau wote ili kuboresha mahusiano; na

(vii) Kuanzisha mahusiano na Tume za Taifa za nchi zilizopo katika kanda za Mashariki ya kati ya Afrika.

**Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)**

**158.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imeundwa kwa sheria ya Bunge Na. 7 ya mwaka 2003 (The Atomic Energy Act No. 7 of 2003). Majukumu ya Tume ni kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya vyanzo vya mionzi, kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu teknolojia hiyo;

**159.** **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Tume itatekeleza mambo yafuatayo:

(i) Kupokea na kutathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya sheria na kanuni za usalama na kinga ya mionzi ya mwaka 2004;

(ii) Kuendelea na ukaguzi wa migodi 6 mikubwa inayofanya kazi na migodi mingine itakayobainika, ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo; pamoja na kuendelea kukagua vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 150 ili kubaini hali ya usalama wa wafanyakazi na jamii inayovizunguka;

(iii) Kusajili vyanzo vya mionzi vipatavyo1,045 ili kuvitambua na kuhifadhi mabaki ya mionzi yasilete madhara katika mazingira na viumbe hai;

(iv) Kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi katika sampuli angalau 4,000 za vyakula na mbolea pamoja na kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi (Personnel Dosimetry Service) kwa Wafanyakazi 1,600;

(v) Kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo vinne na kuyahifadhi katika jengo maalumu (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF) lililopo Arusha;

(vi) Kuendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga(Radionuclide Monitoring Station-TZP-RN64) kilichopo katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) chini ya mkataba wa kimataifa wa Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty of Nuclear Weapons (CTBT);

(vii) Kuendelea kuratibu miradi mipya sita (6) ya kitaifa, na miradi ya kikanda (AFRA) itakayoanza mwaka wa fedha 2017/18 na miradi ambayo bado inaendelea na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2016/17 ambayo inagharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (International Atomic Energy Agency- IAEA); na

(viii) Kufungua vituo vya Kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Nyanda za Juu katika Mkoa wa Mbeya.

## Kituo cha Maendeleo DAKAWA

**160.** **Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Maendeleo Dakawa kina majukumu ya Kutunza na Kuhifadhi majengo, vifaa, na miundombinu yote iliyokabidhiwa na ANC kwa ajili ya kulinda historia ya Ukombozi wa Afrika Kusini. Mipango ya Wizara ni pamoja na kukiendeleza

kituo na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi, TEHAMA na Ufundi.

161. **Mheshimiwa Spika,** Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuhakikisha kuwa Mazingira ya Kituo yamehifadhiwa na kubaki kama ilivyokuwa enzi za ANC;

(ii) Kuendelea kufuatilia Hati Miliki ya Kituo kilichokabidhiwa na Serikali toka ANC ya Afrika Kusini; na

(iii) Kuendelea kufuatilia Uandaaji wa Muundo wa Kisheria wa Uendeshaji wa Kituo.

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**

162. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Elimu Tanzania imepanga kutoa ufadhili katika Taasisi na maeneo yafuatayo;

(i) Ujenzi wa nyumba nane (8) za walimu katika Shule za Sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi;

(ii) Ujenzi wa vyoo 50 katika shule zenye upungufu mkubwa wa vyoo baada ya kufanya tathmini;

(iii) Kutoa mikopo ya elimu kwa Taasisi za Elimu 10 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(iv) Ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika Taasisi 20 za Elimu na Mafunzo; na

(v) Kuendelea na ukarabati kwa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali nchini; na kuendelea na ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike

katika Shule za Sekondari kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi.

## D. SHUKRANI

163. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt Leonard Douglas Akwilapo; Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa Simon Samwel Msanjila na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao wa karibu katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara yetu. Pia namshukuru Bi. Maimuna Kibenga Tarishi aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu hadi alipohamishiwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge).

164. Napenda pia kuwashukuru, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara, Wanataaluma, Wanafunzi na wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninatambua na kuthamini sana mchango wenu mzuri katika kuhakikisha kuwa sekta ya elimu nchini inaendelea kuimarika.

165. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwa- shukuru wadau wote wa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Viongozi mbalimbali na wananchi wote ambao wamechangia sana katika kufanikisha utekelezaji wa Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

166. **Mheshimiwa Spika**, Washirika mbalimbali wa Maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na

Teknolojia. Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara yangu, kuwashukuru na kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali ya Algeria, Canada, China, Cuba, India, Italia, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Uturuki, Ubelgiji na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**167.** **Mheshimiwa Spika**, Napenda pia kuyashukuru yaliyochangia baadhi katika ya mashirikakufanikisha Programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia: AgaKhan Education Services, Airtel, Tigo, Vodacom, Benki Kuu, Benki ya Barclays, Benki ya CRDB, Benki ya Taifa ya Biashara, Benki ya NMB, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Care International, Children International, Children's Book Project, Commonwealth Secretariat, DAAD, DfID, Education Quality Improvement Programme (EQUIP-T), FEMINA, Ford Foundation, GIZ, Global Partnership for Education, International Labour Organisation (ILO), International Reading Association, Irish Aid, Inter University Council of East Africa (IUCEA), Japan International Cooporation Agency (JICA), Korea International Cooporation Agency (KOICA), Peace Corps, Plan International, Rockefeller Foundation, Swedish International Development Agency (Sida), Sight Savers International, Mtandao wa Elimu Tanzania (TENMET), Umoja wa Nchi za Ulaya, United Nations Development Programme (UNDP), UNESCO, UNICEF, USAID na WaterAid.

## E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18

**168.** **Mheshimiwa Spika**, Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyopangwa katika mwaka 2017/18, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **1,366,685,241,000.00** ili kutekeleza majukumu yake.

169. **Mheshimiwa Spika,** Katika maombi haya:

(i) Shilingi **88,544,393,736.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo Shilingi **70,202,722,328.00** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi **18,341,671,408.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(ii) Shilingi **331,299,025,264.00** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi **318,393,044,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, na Shilingi **12,905,981,264.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo;

(iii) Shilingi **916,841,822,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo, Shilingi **606,769,616,000.00**nifedhazandani na Shilingi **310,072,206,000.00** ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo; na

170. **Mheshimiwa Spika**, Ninaliomba pia Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **663,123,262,000.00** kwa ajili ya Tume ya Taifa ya UNESCO. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **330,830,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **332,292,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

171. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya: http://www.moe. go.tz.

## KUTOA HOJA

172. **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati na kwa niaba ya Mwenyekiti naomba hotuba yetu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa fursa ya kushiriki kikao hiki cha leo. Vile vile nitumie nafasi hii kutoa pole za dhati kabisa kwa familia ya marehemu mzee Paul Sozigwa, lakini vile vile kuwapa pole familia na wananchi wa Mkoa wa Arusha kwa msiba mkubwa uliolikumba Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii vile vile kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Nzega kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kipindi ambacho nimekuwa Mbunge wao mpaka sasa. Niwaahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu sitawangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza Nane (7) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia ikiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kutembelea na kukagua

utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha mwaka 2016/2017, pamoja na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilijiwekea malengo mbalimbali yakiwemo ya ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa shughuli zake kulingana na bajeti, lakini pia utekelezaji wa maoni ushauri na mapendekezo ya Kamati**.** Katika mwaka wa fedha 2016/ 2017, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) ilipanga kukusanya jumla ya bilioni 327.8. Hadi kufikia Machi, 2017, Wizara ilifanikiwa kukusanya bilioni 217 sawa na asilimia 66.3 ya malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa bado Idara zilizo chini ya Wizara hazifanyi vizuri kwani makusanyo yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 11.49 lakini kilichokusanywa ni bilioni 6.6 sawa na asilimia 43. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha hadi ifikapo Juni 3 kiasi kilichobaki cha asilimia 33 nacho kinakusanywana. Mkazo uwekwe zaidi katika Idara ambazo makusanyo yao ni chini ya asilimia 50, kielelezo naba moja (Na. 1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara hii iliidhinishiwa trilioni 1.39, kati ya fedha hizo Sh.499,000,000,000 sawa na asilimia 35 ya fedha zote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2017, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha Sh.345,000,000,000 sawa na asilimia 69.2 ya fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, Wizara ilikuwa imeidhinishiwa kiasi cha Sh.897,000,000,000 sawa na asilimia 64 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa matumizi ya Wizara. Hadi kufikia Machi Wizara ilikuwa imepokea bilioni 500.4 sawa na asilimia 55.8 ya fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tarehe 14 mpaka 24 Machi Kamati ilifanya ukaguzi wa jumla ya miradi mitano kati ya Miradi 16 ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017. Miradi mitano hiyo iliyofanyiwa ukaguzi ni Mradi wa Upanuzi wa Chuo cha Kilimo Sokoine (mradi namba 6361).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ukaguzi katika mradi huu mnamo tarehe 14 Machi. Taarifa ya chuo ilionesha kuwa licha ya mradi huu kuidhinishiwa fedha na Bunge lako Tukufu kiasi cha Sh.4,000,000,000 mpaka Kamati inaenda kufanya Ukaguzi hakuna fedha iliyotolewa. Hali hii ilikilazimu Chuo kutumia fedha zake za ndani kiasi cha Sh. 380,000,000 ili kutekeleza baadhi ya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa kwa kipindi cha miaka minne (4) chuo hakijawahi kuletewa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo licha ya ukweli kwamba hata kiasi kinachoidhinishwa kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya chuo kimekuwa hakifiki hata asilimia 10 ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mnamo tarehe 15 Machi, kamati ilitembelea mradi huu uliotengewa na Bunge kiasi cha Shilingi bilioni 9.4. Hadi Kamati inatembelea mradi huu hakuna fedha yoyote iliyotolewa na Serikali, hali iliyokilazimu chuo kutumia mapato yake ya ndani pamoja na fedha za wahisani. Aidha, wakati Kamati ilipokuwa inachambua bajeti ya Wizara hii ilijulishwa kuwa chuo kimepatiwa Sh.5,000,000,000 sawa na asilimia 52.9 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishuhudia hali mbaya ya Jengo namba tano *(Hall number five)* ya bweni la wanafunzi hali iliyolazimu chuo kuhamisha wanafunzi na kuliacha wazi likisubiri ukarabati. Ikumbukwe kuwa majengo mengi ya chuo hiki ni ya zamani. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kuangalia miradi mingine ikiwemo mradi wa ujenzi wa mabweni ambao umegharimu kiasi cha Sh.10,000,000,000 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais. Kamati inampongeza

Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake ya busara ya kuhakikisha wanafunzi wa chuo hiki wanapata malazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kufundisha na Kutoa Huduma ya Afya Mloganzila. Kamati ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 21 Machi. Kamati iliridhishwa na hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa hospitali kwani ulikuwa umekamilika ikiwemo kuwepo na vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ni miongoni mwa miradi mikubwa nchini iliyogharimu Dola za Kimarekani milioni 94 sawa na shilingi na bilioni 210.6 ambazo ni mkopo wa riba nafuu wa kiasi cha Dola za Kimarekani 76.5 ambapo Tanzania imetoa kiasi cha Dola za Kimarekani 18,000,000. Katika mwaka huu wa fedha chuo kiliomba jumla ya Sh.14,000,000,000 kwa utaratibu maalum *(Special Arrangement)* kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vitendanishi na matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetembelea mradi huu; hakuna fedha iliyokuwa imetolewa. Hata hivyo Waziri aliiahidi Kamati kuwa kufikia mwezi Aprili Serikali itakuwa imetoa kiasi cha Sh.5,000,000,000 kwa ajili ya kuanza kununua vifaa tiba. Pamoja na changamoto ya fedha, bado chuo kina upungufu wa rasilimali watu kwani mahitaji ni watumishi 900 na mpaka Kamati inatembelea waliopatikana ni watumishi 381 tu sawa na asilimia 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha watumishi wote 900 wanapatikana ili kuweza kutoa huduma kwa wagonjwa, kinyume na hapo ni kutoutendea haki *(under use)* mradi huu mkubwa na mzuri wenye vigezo vya hospitali. Si tu hivyo pia Kamati inaona uwekezaji huu mkubwa ni vyema uende sambamba na utolewaji wa fedha za kutosha ili uweze kutoa matunda yanayotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *DIT.* Kamati ilifanya ziara ya Ukaguzi wa mradi huu tarehe 22 Machi. Mradi huu ni

wa muda mrefu sana kwani ujenzi ulianza mwaka 2006, lakini kutokana na sababu mbalimbali hususan changamoto ya kupatikana kwa fedha, mradi umekuwa ukisua sua. Mwaka 2013 mradi ulianza tena na mpaka Kamati inafanya ziara hatua ya kwanza ya mradi ilikuwa imekamilika ambayo ni ujenzi wa jengo. Gharama za mradi huu zimeongezeka kutoka Sh.5,000,000,000 kwenda Sh.9,000,000,000 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati inakagua mradi Sh.5,000,000,000 kilikuwa kimetolewa lakini mradi bado hauendi sawa. Kamati iliagiza Serikali kuhakikisha inafanya ukaguzi maalum *(Special Audit)* ili kuweza kubaini ukweli wa ongezeko la gharama, lakini pia kutokana na maelezo ya Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Bodi kuwa na walakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *COSTECH.* Kamati ilitembelea mradi huu mnamo tarehe 22 Machi katika mwaka wa fedha 2016/2017. Mradi ulitengewa kiasi cha Sh.12,000,000,000 kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti na ubunifu. Kati ya fedha hizo Sh.8,000,000,000 zilitarajiwa kutoka katika mfuko wa Hazina, shilingi bilioni 4.6 kutoka *TCRA* kutokana na tozo za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa hata kiasi hiki kinachotengwa ni kidogo kwani kwa mujibu wa malengo ambayo nchi imejiwekea ni kutenga asilimia moja ya *GDP* katika tafiti; lakini mwaka huu wa fedha ambao pato la Taifa lilikuwa ni Sh.103,000,000,000,000 *COSTECH* ilitengewa bilioni 12.8 sawa na asilimia 0.012 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Kamati inatembelea mradi kiasi cha Shilingi bilioni 4.07 sawa na asilimia 31 kilikuwa kimepokelewa. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 1.5 zilitoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 18 za fedha zilizotengwa kutolewa na Hazina na shilingi bilioni 2.7 sawa na asilimia 53 ya fedha ambazo zimetokana na chanzo cha *TCRA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utolewaji huu wa fedha kutoka Serikalini unadhihirisha ni namna gani Serikali haioni

wala kuthamini tafiti nchini kwani kitendo cha kutoa asilimia 18 tu ya fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kitendo hiki kinasikitisha na ni vigumu kufikia malengo ya kujenga uchumi wa viwanda nchini kwani hivi vyote vinategemea utafiti ili kuchochea ubunifu katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Jumla ya Utekelezaji wa Miradi. Kamati imefanikiwa kukagua miradi mitano kati ya miradi 40 iliyoidhinishiwa sawa na asilimia 12.5 tu. Katika uwasilishaji wa utekelezaji wa Wizara imeonekana dhahiri hata asilimia 87.5 ambayo Kamati haijaweza kukagua nayo ina changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kwani upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni asilimia 51.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Kamati imegundua uwepo wa mikataba ambayo inatia mashaka, kama mkataba wa Mlimani *City* kama taarifa ya *GAG* ilivyoonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa ikipanga miradi mingi wakati haina uwezo wa kuitekeleza yote hali inayopelekea miradi mingi kuanza na kutokamilika kwa wakati. Utaratibu huu umekuwa ukiongeza gharama kubwa kwa Serikali. Kamati inaona ni vyema sasa Serikali ikachagua miradi michache ya kipaumbele na kuhakikisha inaikamilisha kabla ya kuanza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefarijika sana na ujenzi wa hospitali ya mafunzo ya Mloganzila, kwani pamoja na lengo la kuwa hospitali ya mafunzo, lakini pia itasaidia kutoa huduma za kitabibu nchini. Kamati ilishuhudia vifaa vya kisasa na vyenye teknolojia ya hali ya juu vilivyofungwa vya utoaji wa huduma katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuiruhusu hospitali hii iwe inatoa huduma kwa gharama za

juu kidogo ikilinganishwa na hospitali nyingine za Serikali ili iweze kujiendesha yenyewe vyema badala ya kusubiri ruzuku ya Serikali ambayo imekuwa haitabiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji na Ushauri wa Kamati kufikia Mwaka 2016/2017. Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekeo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya 2016/2017. Kamati imepokea taarifa hiyo ambayo utekelezaji wake si mbaya ingawa si mzuri sana kutokana na maelezo ya Wizara kuonesha kuwa mambo mengi yako kwenye mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa rai kwa Wizara, kuhakikisha inamalizia michakato ya utekelezaji wa maoni ya Kamati. Aidha, kwa maoni ambayo Kamati inaona utekelezaji wake si wa kuridhisha kabisa itayarudia kwenye sehemu ya maoni ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya mapato ya 2017/2018. Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika tarehe 29 Machi, Kamati pamoja na kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya 2016/2017, Kamati ilipokea taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 46. Wizara ililitaarifu Bunge kwa barua Kumb.Na. PL/AC.193/283/01D ya tarehe 5 Mei, kuwa sasa itatekeleza shughuli zake kupitia mafungu mawili tofauti *(two separate Votes); y*aani Fungu 46 - Wizara na Fungu 18 - UNESCO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko haya yamefanyika kwa kukifanya Kifungu kidogo cha 2001 kilichokuwa kinatambulika kama taasisi iliyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuwa Fungu kamili, yaani Fungu 18 baada ya kupata ridhaa ya Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 19, hivyo maoni na mapendekezo ya Taarifa hii yamezingatia mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya makadirio ya makusanyo ilionesha kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Fungu namba 46 linatarajia kukusanya kiasi cha Sh.366,100,997,547.46 ikilinganishwa na bilioni 327. 887 kilichokadiriwa katika mwaka wa fedha 2016 sawa na ongezeko la asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Fungu 18 linatarajiwa kukusanya kiasi cha Sh.40,000,000.00. Vyanzo vya maduhuli haya ni kutokana na makusanyo ya uchapishaji wa jarida la tume ya michango ya wadau. Makusanyo haya sawa na ongezeko la asilimia 40 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo ilikuwa ni Sh.24,000,000.00. Kamati inaipongeza Wizara kwa ongezeko hili na ina imani kuwa fedha hizi zote zitakusanywa kwa wakati kama ilivyokadiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara kupitia Fungu 46 inaomba jumla ya Sh.1,336,685,241,000 na kupitia Fungu 18 inaomba kiasi cha Sh.663,123,000, ambapo jumla ya fedha zote zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mafungu yote, 46 na 18 inaonesha kuna upungufu wa asilimia 4.2 ikilinganishwa na Sh.1,396,000,000,000 zilizoombwa katika mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida yanayoombwa ni jumla ya Sh. 419,000,000,000.00 sawa na asilimia 31 ya bajeti yote ya Fungu namba 46 na Fungu 16 na kiasi cha Sh.600,000,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, miradi ya maendeleo inaombewa kiasi cha Sh.916,000,000,000 sawa na asilimia 68.6 ya bajeti nzima ya Wizara; rejea kielelezo Na.4. Bajeti hii inayoombwa kwa ajili ya Wizara Fungu namba 46 na 18 ni sawa na asilimia 4.2 ya bajeti kuu ya Serikali ya trilioni 31 ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maendeleo ya Hali ya Elimu Nchini. Katika taarifa inayohusu, maoni na ushauri wa

mapendekezo ya Kamati kuhusu bajeti ya Wizara hii ambayo iliwasilishwa na Waziri, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya elimu nchini. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa kiasi kikubwa unategemea fedha za wahisani kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi imetengewa kiasi cha Sh.160,000,000,000 lakini fedha hizi zote ni fedha za nje. Ikumbukwe kuwa mwaka wa fedha 2016/2017, kiasi kilichoidhinishwa ni bilioni 55.7 ambazo zilikuwa ni fedha kutoka kwa Wahisani. Hadi kufikia Machi, kiasi kilichotolewa ni bilioni 3.6 sawa na asilimia sita tu ya fedha hizo. Kamati inajiuliza kama wahisani hao wasipotoa fedha zao kwa ajili ya elimu ya msingi itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2016/2017 kama Taifa ndiyo tumeanza kutoa elimu bila malipo katika Elimu Msingi kwa maana ya kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua hii. Utoaji wa elimu ya msingi bure kwa wananchi unaungwa mkono na mataifa mengi ulimwenguni kupitia tamko la mwaka 1948 la haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya sita (6) ya tamko hilo, imeeleza bayana kwamba, angalau Sera ya Elimu Bila Malipo ingefikia ngazi ya Shule ya Sekondari. Ibara hiyo inasema kuwa, naomba kununukuu:-

*“Everyone has the right to education. Education shall be free, at least in the elementary and fundamental stages. Elementary education shall be compulsory. Technical and professional education shall be made generally available and higher education shall be equally accessible to all on the basis of merit.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *Center for Global Development* katika kitabu chao cha "*The Rebirth of Education*" kilichochapwa mwaka 2013, wameelezea kwa kina juu ya malengo ya elimu, jambo ambalo hapa nchini hatujalizingatia kwa viwango vinavyoridhisha. Sehemu ya kitabu hicho katika ukurasa wake wa 13 na 14, unasema, nanukuu:

"Lengo la elimu ni kuwawezesha watoto kufanikiwa pindi wakiwa watu wazima. Kipimo cha msingi cha mafanikio ya mfumo wowote wa elimu ni endapo kila kizazi cha watoto katika elimu kinaenda kuwa kizazi cha watu wazima wenye ujuzi na uwezo wa kuikabili dunia." kinaendelea kusema kuwa "Katika nchi zinazoendelea malengo ya kusoma shule yanashindwa hata kutimiza makusudi mema ya elimu. Hivyo kusoma shule haimaanishi ndiyo kujifunza." *Schooling just aren't learning*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubali kama Taifa kuwa tunapaswa sasa kubadilisha mtazamo wetu juu ya mfumo wa elimu kwa sababu kwenda shule pekee siyo kuelimika wala kujifunza. Pamoja na maboresho mengine ambayo Serikali imekuwa ikiyafanya, Kamati inapendekeza kwa Serikali sasa iamue kuupitia upya mfumo wa elimu hapa nchini kwa ujumla wake ili utoe majibu ya changamoto zinazoikabili jamii na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya kwanza ya Mitaala ni yale yaliyofanyika mwaka 1967 ambayo yalilenga kuondoa shina la ubaguzi katika mfumo wetu wa elimu. Taasisi ya Elimu Tanzania katika ripoti yake iliyotolewa mwezi Machi, mwaka 2013 ilisema "Mabadiliko ya mwaka 1967 yalikuwa ya kwanza na yalilenga kubadili mfumo wa elimu kutoka ule wa kikoloni na kuweka mfumo wenye mtazamo wa Kitanzania kwa kuzingatia elimu ya kujitegemea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya pili ya mwaka 1979, ambayo yalitokana na mwelekeo wa kisiasa wakati mwingine, bila kuzingatia hali ya uchumi katika kipindi kile, mabadiliko hayo, yalilenga kuimarisha na kuipa uhai falsafa

ya Ujamaa na Kujitegemea. Hivyo elimu kuanzia hapo ikalenga kuligeuza Taifa kuwa na kada ya watalaamu wenye ujuzi wa juu katika fani mbalimbali zinazoweza kulifanya Taifa lijitegemee. Taarifa ya Taasisi ya Elimu ilielezea kuwa msisitizo uliwekwa katika uanzishwaji wa mitaala ya mafunzo ya ufundi stadi kwa wahitimu wa elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya nne ya mwaka 1997 ni mabadiliko yaliyokuja kujibu changamoto nyingine ya mabadiliko ya mfumo wa kisiasa, kutoka chama kimoja kwenda mfumo vyama vingi. Mabadiliko haya pia hayakuzingatia ujenzi wa uchumi wa Taifa kuanzia Shule za Msingi hadi Chuo Kikuu. Taasisi ya Elimu Tanzania inakiri kuwa mabadiliko hayo ambayo mengi yalitokana na ripoti ya iliyokuwa Tume ya Hayati Jackson Makwetta ya mwaka 1982, ilitoa maoni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya mabadiliko yaliyopendekezwa na Tume ya Makwetta ilikuwa ni kwenye muda ambao watoto wanajifunza kusoma katika Shule za Msingi kwa Darasa la Kwanza na Darasa la Pili. Mapendekezo yalitaka muda uongezeke kama ifuatavyo: Kusoma (22%), Kuandika (24%) na Hisabati (30%). Muda uliobakia ulitumika katika Michezo (6%), Uchoraji (6%), Uraia (3%), Afya (6%) na Dini (3%) (Rejea kielelezo Na. 6). Uwiano huu ulibadilika kwa masomo ya Darasa la Tatu, Nne, Tano na Sita, ikawa Kiswahili 25%, Kiingereza 15% na Hisabati 25% ambayo ni masomo ya msingi na kuchukua asilimia 65 ya muda wa masomo Darasa la Tatu na Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Tume ya Makwetta ndiyo yaliyoleta mageuzi katika Elimu ya Sekondari hasa katika matumizi ya vitabu vya kiada na ziada, ambapo kulikuwa na ngazi mbili kwa elimu ya Sekondari, yaani ngazi ya kwanza Kidato cha Kwanza na Nne na masomo ya sekondari ngazi ya pili Kidato cha Tano na Sita na Mafunzo ya Ualimu kwa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari yalijumuisha masomo ya kitaalam na masomo ya Ualimu. Maboresho haya yote yalikuwa ni matokeo ya Tume ya Kitaalamu ya Hayati Jackson Makwetta ambaye wakati huo

alikuwa ni Waziri wa Elimu katika Awamu ya Kwanza ya Serikali ya Tanganyika na baadaye Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya nne ya mitaala ni yale yaliyofanyika mwaka 2005, ambapo yalihusu ufundishaji na kuzingatia ujuzi *(competence based),* lakini mara baada ya mabadiliko hayo, tumeshuhudia elimu yetu ilishuka kwa kiasi kikubwa sana. Miaka mitano baada ya mabadiliko hayo ripoti ya Shirika Huru la Elimu nchini kuhusu Elimu ya Tanzania kutokana na tafiti zilizofanywa, inabainisha kuwa, Matokeo ya Kidato cha Nne mwaka 2010 yanaonesha watoto wetu 88% wamepata Daraja la Nne na Sifuri. Pia Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, hivi karibuni Bungeni alikiri kuwa Watanzania takribani 31% hawajui kusoma na kuandika. Huu ni ushahidi tosha kuwa bado jitihada za ziada zinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuboresha Mfumo wa Elimu ambao utapelekea kupata Elimu bora. Umefika wakati wa kuangali kama *D by D* kwenye Sekta ya Elimu inatuletea majawabu tunayotaka. Kwa sababu katika elimu kuna mambo mawili; miundombinu kwa maana ya *hardware* na maunzi laini kwa maana ya *software*, kwa maana ya sera, mitaala na kadhalika ya kutoa maarifa kwa wanafunzi ambayo inasimamiwa na Wizara zaidi ya Wizara Mama ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na kauli ya *UNESCO* inayosema, *UNESCO belives that education is human right for all through life and that access must be match by quality.* Kila mtu ana haki ya kupata elimu ambayo inaendana na ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni maoni na ushauri wa Kamati. Tunapoongelea Elimu ina maana ni kuwekeza kwa kutenga fedha za kutosha. Aliyekuwa Gavana wa 26 wa Jimbo la Oklahoma Marekani, alipokuwa anaongelea kuhusu Elimu alisema, "*No other investment yield as great return as the investment in education. An educated workforce is the foundation of every community and the future of every*

*economy."* Kamati ilitarajia kuwa pale Bajeti ya Serikali inapoongezeka, basi kipaumbele kiwe kuongeza Bajeti ya Elimu. Hata hivyo, Bajeti ya Wizara ya Elimu kwa mwaka ujao wa fedha imepungua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali za kuleta mabadiliko katika Sekta ya Elimu nchini, bado matokeo yamekuwa siyo mazuri na siyo sambamba na kasi ya mabadiliko ya ulimwengu kwa kizazi hiki cha teknolojia. Mabadiliko hayo manne ya mitaala yaliyofanywa na Taifa letu hayagusi mabadiliko yoyote katika uendeshaji na usimamiaji wa utoaji wa elimu nchini ambapo huratibiwa na Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Utumishi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ndiyo mwenye dhamana kuu, *custodian* wa elimu hapa nchini, kuona iko haja ya kuuangalia upya mfumo wetu wa elimu kwa kufanya mapitio makubwa ya mfumo mzima kama ulivyo na kuja na matokeo yatakayotusaidia kuweka msingi imara wa kulijenga Taifa linalojitegemea kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano inavyosisitiza; Hayati Makwetta alishawahi kunukuliwa kwamba "Kama Elimu ni ufunguo wa maisha, elimu mbaya ni ufunguo wa maisha mabaya." Kamati inaona kwamba, kama tunaendelea kuwa na mfumo mbovu wa elimu, tusitarajie miujiza katika kupata Elimu bora, ni lazima kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika suala la elimu. Bila kufanya hivyo, tutatoa watu ambao ni wabovu, ambao hawataisaidia jamii inayokusudiwa na hatimaye kuwa na jamii mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeonesha kuwa, Taarifa ya Kamati inayohusu Maendeleo ya Hali ya Elimu nchini, ni dhahiri mmeona kwamba bado kuna changamoto nyingi hususan za miundombinu na hata za kimaslahi zinazochangia kushusha morali ya ufundishaji kwa Walimu

kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi wakati malipo na miundombinu ipo vile vile. Kamati inaishauri Serikali kujitahidi kuongeza miundombinu pamoja na motisha kwa Walimu katika Shule za Elimu ya Msingi na Sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa miundombinu, takwimu zinaonesha kuwa, kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 146,000 katika Shule za Msingi na vyumba 12,000 katika Shule za Sekondari. Aidha, kuna upungufu wa matundu ya vyoo 350,000 katika Shule za Msingi na matundu ya vyoo 27,000 katika Shule za Sekondari. Siyo hivyo tu, pia kuna upungufu wa nyumba za Walimu 182,000 katika Shule za Msingi na nyumba za Walimu 69,000 wa Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna misemo mingi inayoeleza umuhimu wa kumwelimisha Mwanamke. *Dr.* James Aggrey aliyekuwa Mwanafilosofia wa masuala ya Elimu nchini Ghana alipokuwa akieleza umuhimu wa kuvunja utaratibu uliopo wa kutokuwapa watoto wa kike elimu ya msingi, alisema: *"If you educate a man, you educate an individual, but if you educate a woman, you educate a family."* Kwa tafsiri isiyo rasmi, ukimwelimisha mwanaume, umeelimisha mtu mmoja, lakini ukimwelimisha mwanamke, umeelisha familia na hatimaye Taifa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, imekuwa ni kawaida kabisa kwa wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito kutotakiwa kuendelea na masomo, kufukuzwa kutokuendelea na masomo ilhali wanafunzi wa kiume ambao wamewapa ujauzito huo wakiendelea na masomo na hata kama aliyempa ujauzito mwanafunzi huyo kubaki bila kuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria. Ikumbukwe kuwa akina mama ndiyo walezi wa watoto na nguzo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kitabu kinachoitwa *Economic Development,* kilichoandikwa na Michael Todaro na Stephen Smith, hususan chini ya Mada *"Human Capital Education and Health in Economic*

*Development,"* Waandishi hawa wanasema kuwa kiwango cha marejesho *(Rate of Return)* ya mwanamke mwenye elimu ni kubwa kuliko hata ile ya mwanaume mwenye elimu katika nchi nyingi zinazoendelea. Mwanamke mwenye elimu siyo tu anaongeza uzalishaji katika eneo lake la kazi, lakini pia mwanamke mwenye elimu atachelewa kuolewa, atazaa watoto wachache, *Familiy Palnning program*, atahakikisha watoto wake wanakuwa na afya njema na hivyo kuwa na faida kwa kizazi hicho kijacho. Pia mwanamke anapopata elimu anavunja duara la umasikini *(Vicious circle of Poverty)*. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa tamko rasmi kwamba mwongozo huo uanze...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe, muda wako umekwisha. *Wind-up* dakika moja. Waheshimiwa, someni. Bado dakika moja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa namna ya kipekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kujitoa katika utekelezaji wa shughuli za Kamati na utayarishaji wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kushukuru Wizara kwa ushirikiano ambao wametupa katika kipindi chote cha bajeti na mwisho kabisa napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa maamuzi waliyoyafanya ya ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote iingie kwenye kumbukumbu ya Bunge. Nashukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAWIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## 1.1 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Nyongeza ya nane (7)(1) (a) iliyo chini ya Kanuni ya 118 yaKanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia ikiwemo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1-2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kutembelea na kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ambao ni 2016/2017 pamoja na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ili kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata wa 2017/2018.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIWAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA2016/2017

### 2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, Wizara ilijiwekea malengo mbalimbali yakiwemo ya ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa shughuli zake kulingana na bajeti lakini pia utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**.**

#### 2.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **327,887,974,585.87/= (Bilioni 327.8).** Hadi kufikia Mwezi Machi 2017, Wizara ilifanikiwa kukusanya shilingi **217,380,116,240.61/= (Bilioni 217.38)** sawa na **asilimia 66.3** ya malengo.Kamati imebaini kuwa bado Idara zilizo chini ya Wizara hazifanyi vizuri kwani makusanyo yao yalikadiriwa kuwa shilingi **11,491,790,800/= (Bilioni 11.49)** lakini kilichokusanywa ni **6,658,696,761.66/=** (**Bilioni 6.65**) sawa na **asilimia 43.4**.

**Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha hadi ifikapo Juni 3,2017, kiasi kilichobaki cha asilimia 33.7 nacho kinakusanywana mkazo uwekwe zaidi kwenye Idara ambazo makusanyo yakeni chini ya asilimia 50.*(Rejea Kielelezo Na. 1)***

**KIELELEZO NA.1: UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**




**Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

### 2.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa Mwaka 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, Wizara hii iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **1,396,929,798,625/= (Trilioni 1.39).** Kati ya fedha hizo shilingi**499,272,251,000/=(Bilioni 499)** sawa na asilimia **35.7** ya fedha zote ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Mwezi Machi 2017, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **345,731,550,623.59/= (Bilioni 345.7)** sawa na asilimia **69.2** ya fedha za Matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Wizara ilikuwa imeidhinishiwa kiasi cha shilingi **897,657,547,625/= (Bilioni 897.6)** sawa na **asilimia 64.3** ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa matumizi ya Wizara. Hadi kufikia Mwezi Machi 2017, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **500,452,007,426.18/ = (Bilioni 500)** sawa na**asilimia 55.8** ya fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge.***(Rejea Kielelezo Na. 2)***

**KIELELEZO NA. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**




**Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

## 2.2 Matokeo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** kuanzia tarehe 14 – 24 Machi 2017, Kamati ilifanya ukaguzi wa jumla ya **Miradi 5 kati ya Miradi 16**ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017. Ukaguzi wa Miradi hii michache ulitokana na ukosefu wa fedha pamoja na ufinyu wa muda.Kwa ufupi ni kuwa Kamati imekagua **asilimia 12 tu**ya Miradi yote iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi mitano (5) iliyofanyiwa Ukaguzi na Kamati ni pamoja na:-

### 2.1.1 Mradi wa Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine-SUA (Namba ya Mradi – 6361)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ukaguzi wa Mradi huu mnamo tarehe 14 Machi, 2017. Taarifa ya Chuo ilionesha kuwa licha ya Mradi huu kuidhinishiwa fedhana Bunge lako Tukufu kiasi cha shilingi **Bilioni 4** mpaka Kamati inaenda kufanya Ukaguzi, hakuna fedha iliyotolewa.Hali hii ilikilazimu Chuo kutumia fedha zake za ndani kiasi cha **shilingi 380,500,000/=** kutekeleza baadhi ya kazi zake.Chuo hakikuishia

hapo kimeweza kutekeleza miradi mingine kwa kutumia ufadhili wa wadau mbalimbali ambao imekuwa ikifanya nao kazi. Kamati ilielezwakuwa kwa kipindi cha miakamine (4) Chuo hakijawahi kuletewa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo licha ya ukweli kwamba hata kiasi kinachoidhinishwa ni kidogo ikilinganishwa na mahitajihalisi. Kiasi cha fedha kinachotengwakwa ajili ya Chuo kimekuwa hakifiki hata **asilimia 10** ya mahitaji halisi.

### 2.1.2 Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Dar - Es-Salaam (Namba ya Mradi 6350)

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 15 Machi, 2017 Kamati ilitembelea Mradi huu uliotengewa na Bunge kiasi cha **shilingi Bilioni 9.4**. Hadi Kamati inatembelea Mradi huu, hakuna fedha yoyote iliyotolewa na Serikali hali iliyokilazimu Chuo kutumia mapato yake ya ndani pamoja na fedha za wahisani marafiki kufanya upanuzi na ukarabati wa chuo. Aidha, wakati Kamati inachambua Bajeti ya Wizara hii ilijulishwa kuwa Chuo kimepatiwa shilingi **Bilioni 5** sawa na**asilimia 52.9** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mradi huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishuhudia hali mbaya ya Jengo Na. 5 (Hall 5) bweni la wanafunzi hali iliyolazimu chuo kuhamisha wanafunzi na kuliacha wazi likisubiri ukarabati. Ikumbukwe kuwa Majengo mengi ya Chuo hiki ni ya zamani kwani yana zaidi ya miaka 50 toka yamejengwa. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kuangalia Miradi mingine ukiwemo Mradi wa Ujenzi wa Mabweni ambao umegharimu kiasi cha shilingi **Bilioni 10** zilizotolewa na Mhe. Rais, **Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa maamuzi yake ya busara ya kuhakikisha wanafunzi wa Chuo hiki wanapata malazi.**

### 2.1.3 Mradi wa Hospitali ya kufundishia na kutoa huduma za Afya – Mloganzila (Namba ya Mradi-6364)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mradi huu mnamo tarehe 21 Machi, 2017. Kamati iliridhishwana hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa Hospitali kwani ulikuwa umekamilika ikiwemo kuwepo kwa vifaa vya kisasa. Mradi huu ni moja kati ya Miradi mikubwa nchini ukiwa na gharama ya **Dola za Kimarekani 94,540,000sawa na shilingi Bilioni 210.6** ambazo ni mkopo wa riba nafuu wa kiasi cha **Dola za Kimarekani 76,500,000** na mchango wa Serikali ya Tanzania wa **dola za kimarekani 18,040,000**. Katika Mwaka huu wa fedha 2016/ 2017, Chuo kiliomba jumla ya shilingi **14,549,727,933/=**kwa utaratibu maalum (***Special Arrangement)*** kwa ajili ya ununuzi wa Dawa, Vitendanishi na matumizi mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Kamati inatembelea Mradi hakuna fedha iliyokuwa imetolewa. Hata hivyo, Waziri aliiahidi Kamati kuwakufikia mwezi Aprili Serikali itakuwa imetoa kiasi cha **shilingi Bilioni 5** kwa ajili ya kuanza kununua vifaa tiba. Pamoja na changamoto ya fedha, bado chuo kina upungufu wa rasilimali watu kwani mahitaji ni **Watumishi 900** na mpaka Kamati inatembelea waliopatikana ni**Watumishi 381**tu sawa na **asilimia 42.3** ya mahitaji yote**.**

***Kamati inatoa Rai kwa Serikali kuhakikisha Watumishi wote 900 wanapatikana ili kuweza kutoa huduma kwa wagonjwa kinyume na hapo ni kutoutendea haki(Under Use) mradi huu mkubwa na mzuri wenye vigezo vya Hospitali za Kimataifa. Sio hivyo tu, pia Kamati inaona uwekezaji huu mkubwa ni vyema uende sambamba na utolewaji wa fedha za kutosha ili uweze kutoa matunda tarajali.***

### 2.1.4 Mradi wa Ujenzi wa *DIT Teaching Tower* *(Namba ya Mradi-4384)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Mradi huu tarehe 22 Machi, 2017. Mradi huu umekuwa ni wa muda mrefu sana kwani ujenzi ulianza mwaka 2006 lakini kutokana na sababu mbalimbali hususan changamoto ya kupatikana kwa fedha za mradi umekuwa ukisuasua. Mwaka 2013 Mradi ulianza tena na mpaka Kamati inafanya ziara hatua ya kwanza ya mradi ilikuwa imekamilika ambayo ni

ujenzi wa jengo. Gharama za Mradi huu zimeongezeka kutoka shilingi **Bilioni 5** mwaka 2006 hadi kufikia **Bilioni 9** mwaka 2017.Wakati Kamati inakagua Mradi tayari Bajeti iliyotengwa kiasi cha shilingi **Bilioni 5** kilikuwa kimetolewa lakini mradi bado hauendi sawa.

***Kamati iliagiza Serikali kuhakikisha inafanya Ukaguzi Maalum (Special Audit) ili kuweza kubaini ukweli wa ongezeko la gharama lakini pia kutokana na maelezo ya Mkurugenzi na Mwenyekiti wa bodi kuwa na walakini*.**

### 2.1.5 Mradi wa Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH (Namba ya Mradi-6345)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Mradi huu mnamo tarehe 22 Machi, 2017. Katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, Mradi ulitengewa kiasi cha shilingi **12,846,670,343/=** kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti na ubunifu. Kati ya fedha hizo shilingi **Bilioni 8** zilitarajiwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi **Bilioni 4.8** kutoka TCRA kutokana na tozo za simu za nje (***Telecommunication Traffic Monitoring System***). Ikumbukwe kwamba, hata kiasi hiki kinachotengwa ni kidogo kwani kwa mujibu wa malengo ambayo nchi imejiwekea, ni kutenga **asilimia 1 ya Pato la Taifa (GDP)** katika utafiti lakini katika Mwaka huu wa Fedha ambapo Pato la Taifa lilikuwa ni shilingi **Trilioni 103.7**, COSTECH ilitengewa **Bilioni 12.8** sawa na**asilimia 0.012 tu**. Hadi Kamati inatembelea mradi, kiasi cha shilingi **Bilioni 4.07** sawa na **asilimia 31.7** kilikuwa kimepokelewa. Kati ya Fedha hizo, shilingi **Bilioni 1.5** zilitoka Mfuko Mkuu wa Hazina ambazo pia ni sawa na **asilimia 18.7** ya fedha zilizopaswa kutolewa na Hazina na shilingi **Bilioni 2.57** sawa na **asilimia 53.5** zimetoka TCRA.

**Mheshimiwa Spika,** ***utolewaji huu wa Fedha kutoka Serikalini unadhihirisha ni namna gani Serikali haioni wala kuthamini utafiti nchini kwani kitendo cha kutoa asilimia 18.7 tu cha fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/ 2017 ni cha kusikitisha na ni vigumu kufikia malengo ya kujenga uchumi wa viwanda nchini kwani hivi vyote***

***vinategemea utafiti ili kuchochea ubunifu katika maendeleo.***(**Rejea Kielelezo Na.3**)

**KIELELEZO NA.3: UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MIRADI ILIYOKAGULIWA NA KAMATI**




***Chanzo: Taarifa za Taasisiza utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka 2016/2017***

## 2.2 Maoni ya Jumla kuhusu UtekelezajiwaMiradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanikiwa kukagua miradi 5 kati ya Miradi 40 iliyoidhinishiwa fedha na Bunge katika Mwaka huu wa Fedha 2016/2017 sawa na **asilimia 12.5 tu**. Lakini katika uwasilishaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara, imeonekana dhahiri hata **asilimia 87.5** ambayo Kamati haijaweza kuikagua nayo ina changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha kwani upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 51.7** tu.

**Kutokana na Changamoto hii kubwa, Kamati inatoa maoni ya Jumla yafuatayo:-**

i) Kamati imebaini kuwa Serikali imekuwa ikipanga miradi mingi wakati haina uwezo ya kuitekeleza yote hali inayopelekea Miradi mingi kuanza na kutokamilika kwa wakati. Utaratibu huu umekuwa ukiongeza gharama kubwa kwa Serikali. ***Kamati inaona ni vyema sasa Serikali ikachagua Miradi michache ya kipaumbele na kuhakikisha inaikamilisha kabla ya kuanza miradi mingine. Kama ambavyo tumeona Mradi wa Ujenzi wa DIT Tower umechukua muda mrefu kutokana na kusuasua kwa utolewaji wa fedha hali iliyopelekea gharama za Mradi kuongezeka kutoka shilingi Bilioni 5 Mwaka 2006 hadi kufikia Bilioni 9 Mwaka 2013.***

ii) Kamati imefarijika sana na ujenzi wa Hospitali ya Mafunzo ya Mloganzila kwani pamoja na lengo la kuwa hospitali ya mafunzo, lakini pia itasaidia kutoa huduma za kitabibu nchini. Kamati ilishuhudia vifaa vya kisasa na vyenye Teknolojia ya hali ya juu vilivyofungwa vya utoaji wa huduma katika Hospitali hiyo. Vifaa hivyo vinaweza fananishwa na vile vilivyopo kwenye Hospitali za binafsi kama Agha Khan na Regency na hata zaidi.

**Kamati inaishauri Serikali kuiruhusu Hospitali hii iwe inatoa huduma kwa gharama zajuu kidogo ikilinganishwa na Hospitali nyingine za Serikali ili iweze kujiendesha yenyewe vyema badala ya kusubiri ruzuku ya Serikali ambayo imekuwa haitabiriki.**

## 2.3 Mapitio ya UtekelezajiwaUshauri wa Kamati katika Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya utekeleaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekeo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa uwasilishaji wa Taarifa yake katika Mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati imepokea Taarifa hiyo ambayo kwa tathmini ya Kamati, utekelezaji wake siyo mbaya sana ingawa siyo mzuri sana pia kutokana na

maelezo ya Wizara kuonesha kuwa mambo mengi yapo kwenye mchakato. **Kamati inatoa Rai kwa Wizara kuhakikisha inamalizia michakato ya utekelezaji wa Maoni ya Kamati. Aidha, kwa Maoni ambayo Kamati inaona utekelezaji wake siyo wa kuridhisha kabisa itayarudia kwenye sehemu ya Maoni ya Taarifa hii.**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika tarehe 29 Machi, 2017, Kamati pamoja na kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati pia ilipokea Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii (**Fungu 46**) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara iliitaarifu Ofisi ya Bunge kwa Barua yenye **Kumb.Na. PL/AC.193/283/01D/32** ya **tarehe 5 Mei, 2017** kuwa sasa itatekeleza shughuli zake kupitia mafungu mawili tofauti (*Two Separate Votes*) yaani Fungu 46 (Wizara) na Fungu 18 (UNESCO). Mabadiliko haya yamefanyika kwa kukifanya Kifungu kidogo cha 2001 kilichokuwa kinatambulika kama Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuwa Fungu Kamili, yaani Fungu 18 baada ya kupata ridhaa ya Wizara ya Fedha na Mipango **tarehe 19 Aprili, 2017.** Hivyo, maoni na mapendekezo ya Taarifa hii yamezingatia mabadiliko hayo**.**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Makadirio ya Makusanyo ilionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara **Fungu 46** inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi

**366,100,997,547.46/=** ikilinganishwa na shilingi **327,887,974,585.87/=** kilichokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, sawa na ongezeko la **asilimia 10.4**

Aidha, **Fungu 18** (UNESCO) inatarajia kukusanya kiasi cha **shilingi 40,000,000.00,** vyanzo vya maduhuli haya ni kutokana na makusanyo ya Uchapishaji wa Jarida la Tume ya Michango ya wadau. Makusanyo haya sawa na ongezeko la **asilimia 40** ikilinganishwa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo kiasi cha **shilingi 24,000,000.00**. ***Kamati inaipongeza Wizara kwa ongezeko hili na ina imani kuwa fedha hizi zote zitakusanywa kwa wakati kama ilivyokadiriwa.***

## 2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 46 inaomba jumla ya **shilingi 1,336,685,241,000.00** na kupitia Fungu 18 (UNESCO) inaomba kiasi cha shilingi **663,123,000.000**ambapojumla ya fedha zote zinazoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mafungu yote mawili (46 na 18) inaonesha kuna upungufu wa asilimia **4.2** ikilinganishwa na shilingi **1,396,929,798,625/=** zilizoombwa katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Kawaida yanaombewa jumla ya **shilingi 419,843,419,000.00** sawa na **asilimia 31.4** ya Bajeti yote ya Wizara Fungu 46 na Fungu 18 inaomba kiasi cha shilingi **663,123,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Miradi ya Maendeleo inaombewa kiasi cha shilingi **916,841,822,000.00** sawa na **asilimia 68.6** ya Bajeti nzima ya Wizara. ***(Rejea Kielelezo Na.4)***

**KIELELEZO NA.4: ULINGANISHOWA BAJETI 2016/2017 NA 2017/2018**




| | 2016/2017 | 2017/2018 |
|---|---|---|
| MIRADI YA MAENDELEO | 897,657,547,625 | 916,841,822,000 |
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 499,272,251,000 | 419,843,419,000 |

**Chanzo: Randama ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti hii inayoombwa kwa ajili ya Wizara (Fungu 46 na 18) ni sawa na **asilimia 4.2** ya Bajeti kuu ya Serikali ya shilingi **Trilioni 31.699** kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kiasi ambacho ni kidogo sana kwa Maendeleo ya Sekta ya Elimu nchini.

## 4.0 MAENDELEO YA HALI YA ELIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** katika Taarifa inayohusu, Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii ambayo iliwasilishwa Bungeni **tarehe 26 Mei 2016**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Hali ya Elimu nchini kwa kutumia tafiti mbalimbali.Taarifa hizozilionesha hali ya Elimu nchini siyo nzuri sana kwa ujumla wake kiasi kwamba uwezo wa watoto wa kusoma na kuhesabu ni mdogo ingawa kuna mabadiliko kidogo.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa kiasi kikubwa unategemea fedha za wahisani

kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, katika Mwaka huu wa Fedha (2017/2018), Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi imetengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 160.37**, lakini fedha hizi zote ni fedha za nje, ikumbukwe kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, kiasi kilichoidhinishwa ni shilingi **Bilioni 55.75** ambazo pia zilikuwa ni fedha kutoka kwa Wahisani. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2017kiasi kilichotolewa nishilingi **Bilioni 3.6** sawa na **asilimia 6** tu ya fedha hiyo. **Kamati inajiuliza, kama Wahisani hao wasipotoa fedha zao kwa wakati hali ya ElimuMsingi itakuwaje?**

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2016kama Taifa ndiyo tumeanza kutoa elimu bila malipo katika Elimu Msingi kwa maana ya kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne, **Kamati inapongeza sana Serikali kwa hatua hiyo**. Utoaji wa Elimu Msingi bure kwa wananchi unaungwa mkono na mataifa mengine Ulimwengunikupitia tamko la **mwaka 1948** la Haki za Binadamu katika Ibara ya 26 ya Tamko hilo, imeeleza bayana kwamba, angalau Sera ya elimu bila malipoingefikia ngazi ya Shule ya Sekondari, ibara hiyo inasema kuwa, naomba kununukuu;

***"Everyone has the right to education. Education shall be free, at least in the elementary and fundamental stages. Elementary education shall be compulsory. Technical and professional education shall be made generally available and higher education shall be equally accessible to all on the basis of merit."***

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la *Center for Global Development* katika kitabu chao cha "*The Rebirth of Education*" kilichochapwa mwaka 2013, wameelezea kwa kina juu ya malengo ya elimu, jambo ambalo hapa nchini hatujalizingatia kwa viwango vinavyoridhisha. Sehemu ya kitabu hicho katika ukurasa wake wa 13 na 14, unasema, nitanukuu; ***"Lengo la elimu ni kuwawezesha watoto kufanikiwa pindi wakiwa watu wazima. Kipimo cha msingi cha mafanikio ya mfumo wowote wa elimu ni endapo kila kizazi cha watoto katika elimu kinaenda kuwa kizazi cha watu wazima wenye ujuzi na uwezo wa kuikabili dunia"*** **kinaendelea kusema kuwa**

***"Katika nchi zinazoendelea malengo ya kusoma shule yanashindwa hata kutimiza makusudi mema ya elimu. Hivyo kusoma shule haimaanishi ndio kujifunza (Schooling just ain't Learning).***

**Mheshimiwa Spika,** Tukubali kama Taifa kuwa, tunapaswa sasa kubadilisha mtazamo wetu juu ya Mfumo wa elimu kwa sababu kwenda shule pekee sio kuelimika wala kujifunza.Pamoja na maboresho mengine ambayo Serikali imekuwa ikiyafanya, **Kamati inapendekeza kwa Serikali sasa iamue kuupitia upya mfumo wa elimu hapa nchini kwa ujumla wake ili utoe majibu ya changamoto zinazoikabili jamii na Taifa kwa ujumla.**

**Mheshimiwa Spika,** Maboresho ya kwanza ya Mitaala ni yale yaliyofanyika mwaka 1967 ambayo yalilenga kuondoa shina la ubaguzi katika mfumo wetu wa elimu. Taasisi ya Elimu Tanzania katika ripoti yake iliyotolewa mwezi Machi mwaka 2013 ilisema kuwa "***Mabadiliko ya mwaka 1967 yalikuwa ya kwanza na yalilenga kubadili mfumo wa elimu kutoka ule wa kikoloni na kuweka mfumo wenye mtazamo wa Kitanzania kwa kuzingatia elimu ya kujitegemea".***

**Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko ya pili ya Mitaala ni yale yaliyofanyika mwaka 1979, ambayo yalitokana na mwelekeo wa kisiasa wakati mwingine bila kuzingatia hali ya uchumi katika kipindi kile. Mabadiliko hayo, yalilenga kuimarisha na kuipa uhai Falsafa ya **Ujamaa na Kujitegemea.** Hivyo elimu kuanzia hapo ikalenga kuligeuza Taifa kuwa na kada ya watalaamu wenye ujuzi katika fani mbalimbali zinazoweza kulifanya Taifa lijitegemee. Taarifa ya Taasisi ya Elimu ilielezea kuwa msisitizo uliwekwa katika uanzishwaji wa mitaala ya mafunzo ya ufundi stadi kwa wahitimu wa shule za msingi.

**Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko ya nne ya Mitaala ni yale yaliyofanyika mwaka 1997 na mabadiliko haya yalikuja kujibu changamoto nyingine ya mabadiliko ya mfumo wa kisiasa, kutoka chama kimoja kwenda vyama vingi. Mabadiliko haya pia hayakuzingatia ujenzi wa Uchumi wa

Taifa kuanzia shule za msingi hadi chuo kikuu. Taasisi ya Elimu Tanzania inakiri kuwa mabadiliko hayo ambayo mengi yalitokana na ripoti ya iliyokuwa Tume ya Hayati Jackson Makwetta (1982) ambayo ilitoa maoni mazuri.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Mabadiliko yaliyopendekezwa na Tume ya Makwetta ilikuwa ni kwenye muda ambao watoto wanajifunza kusoma katika shule za msingi kwa darasa la kwanza na darasa la pili. Mapendekezo yalitaka muda uongezeke kama ifuatavyo; Kusoma (22%), Kuandika (24%) na Hisabati (30%); muda uliobaki ulitumika katika Michezo (6%) Uchoraji (6%), Uraia (3%), Afya (6%) na Dini (3%) (***Rejea kielelezo Na. 6***). Uwiano huu ulibadilika kwa masomo ya darasa la tatu, nne, tano na sita, (Kiswahili 25%, Kiingereza 15% na Hisabati 25% ambayo ni masomo ya msingi na kuchukua asilimia 65 ya muda wa masomo (darasa 3 na 4).

**Kielelezo Na. 6: Muda wa Watoto kujifunza katika shule za Msingi kwa asilimia**




***Chanzo: Ripoti ya Makwetta***

Sehemu

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Tume ya Makwetta ndio yaliyoleta mageuzi katika elimu ya Sekondari hasa katika matumizi ya vitabu vya kiada na ziada, ambapo

kulikuwa na ngazi mbili kwa elimu ya Sekondari yaani, ngazi ya kwanza (Kidato cha I na 4) na masomo ya sekondari ngazi ya pili (Kidato cha 5 na 6) na Mafunzo ya Ualimu kwa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari yalijumuisha masomo ya kitaaluma na masomo ya Ualimu. Maboresho haya yote yalikuwa ni matokeo ya Tume ya Kitaalamu ya Hayati Jackson Makwetta ambaye wakati huo alikuwa ni Waziri wa Elimu katika awamu ya Kwanza ya Serikali ya Tanganyika na baadaye Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko ya nne ya Mitaala ni yale yaliyofanyika mwaka 2005, ambapo yalihusu ufundishaji unaozingatia ujuzi (*Competence-Based*). Lakini mara baada ya mabadiliko hayo tumeshuhudia elimu yetuikukua kwa kiasi kidgo sana. Miaka mitano baada ya mabadiliko hayo ripoti ya Shirika huru la Elimu nchini kuhusu hali ya Elimu Tanzania kutokana na tafiti zilizofanywa, inabainisha kuwa ***"Matokeo ya kidato cha nne mwaka 2010 yanaonesha watoto wetu 88% wamepata daraja la nne na sifuri. Na pia Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia hivi karibuni Bungeni alikiri kuwa Watanzania takribani 31% hawajui kusoma na kuandika. Huu ni ushahidi tosha kuwa bado jitihada za ziada zinahitajika"***

**Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na kauli ya UNESCO inayosema "*UNESCO believes that education is a human right for all throughout life and that access must be matched by quality*". Kila mtu anahaki ya kupata Elimu ambayo inaendana na ubora.Kamati inaendelea kusisitiza kuboresha Mfumo wa Elimu ambao utapelekea kupata Elimu bora.**

## SEHEMU YA TATU

## 5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**heshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

### 5.1 Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** tunapoongelea Elimu inamaanani kuwekeza kwa kutenga fedha za kutosha. Aliyekuwa Gavana wa 26 wa Jimbo la Oklahoma Marekani alipokuwa anaongelea kuhusu Elimu na ajira Marekani aliwahi kusema"***No other investment yields as great a return as the investment in education. An educated workforce is the foundation of every communityand the future of every economy***."

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaraji kuwa pale Bajeti ya Serikali inapoongezeka basi kipaumbele kiwe kuongeza Bajeti ya Elimu, hata hivyo Bajeti ya Wizara ya Elimu kwa Mwaka ujao wa Fedha 2017/2018 imepungua kwa **asilimia 4.2** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/ 2017(**kutoka shilingi Trilioni 1.396** hadi **shilingi Trilioni 1.337**). Aidha, bajeti hii ya Wizara ya Elimu ni sawa na **asilimia 4.2** ya Bajeti kuu ya Serikali. **Kamati inaiomba Serikali kuongeza Bajeti ya Wizara hii ili angalau ifikie asilimia 10 ya Bajeti Kuu ya Serikali.**

### 5.2 Mapitio ya Uboreshaji Upya wa Mfumo wa Elimu

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali za kuleta mabadiliko katika Sekta ya Elimu nchini, bado matokeo yamekuwa sio mazuri na sio sambamba na kasi ya mabadiliko ya ulimwengu katika kizazi hiki cha teknolojia. Mabadiliko hayo manne ya mitaala yalifanywa katika Taifa letu hayagusi mabadiliko yoyote katika uendeshaji na usimamiaji wa utoaji wa elimu nchini ambao huratibiwa na Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Utumishi kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ndiyo mwenye dhamana kuu (*Custodian*) ya suala la Elimu hapa nchini,kuona iko haja ya kuuangalia upya mfumo wetu wa elimu kwa kufanya mapitio makubwa ya mfumo mzima**

**kama ulivyo na kuja na matokeo yatakayotusaidia kuweka msingi imara wa kulijenga Taifa linalojitegemea lenye Uchumi wa kati na uchumi wa Viwanda kama Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano inavyosisitiza.**"Hayati Makwetta alishawahi kunukuliwa kwamba"**Kama Elimu ni ufunguo wa maisha Elimu mbaya ni ufunguo wa maisha mabaya**".

**Kamati inaona kwamba, kamatunaendelea kuwa na mfumo mbovu wa elimu tusitarajie miujiza katika kupata Elimu bora ni lazima kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika suala la elimu, bila kufanya hivyo tutatoa watu ambao ni wabovu. Ambao hawataisaidia jamii inayokusudiwa na hatimaye kuwa na jamii mbovu.**

### 5.3 Utekelezaji wa Sera ya Elimu bila Malipo (2016)

**Mheshimiwa Spika,** Kama ambavyo imeoneshwa kwenye Taarifa ya Kamati sehemu ya 4.0 inayohusu Maendeleo ya Hali ya Elimu nchini, ni dhahiri mmeona kwamba bado kuna changamoto nyingi hususan za miundombinu na hata za kimaslahizinazochangia kushusha morali ya ufundishaji kwa Walimu kutokana na kuongezeka kwa wanafunzi wakati malipo na miundombinu ipo vilevile. **Kamati inashauri Serikali kujitahidi kuongeza miundombinu pamoja na motisha kwa walimu katika shule za Elimu ya Msingina Sekondari. Katika upande wa miundombinu takwimu zinaonesha kuwa, kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 146,106** katika shule za Msingina **vyumba 12,568 katika** shulezaSekondari. Aidha, kuna upungufu wa **matundu ya vyoo 350,110** katika shule za Msingi na **matundu ya vyoo 27,761** katika Shule za Sekondari. Si hivyo tu, pia kuna upungufu wa **nyumba za Walimu 182,899** wa Shule za Msingi na nyumba za Walimu **69,794** wa Shule za Sekondari.

### 5.4 Wanafunzi wa Kike wanaopata Ujauzito

**Mheshimiwa Spika**, kuna misemo mingi inayoeleza umuhimu wa kumuelimisha Mwanamke. Dr. James Aggrey aliyekuwa Mwanafilosofia wa masuala ya Elimu nchini Ghana

alipokuwa akieleza kuhusu kuvunja utaratibu uliopo wa kutowapa watoto wa kike elimu alisema***"If you educate a man, you educate an individual, but if you educate a woman, you educate a family (Nation)"*** kwa tafsiri isiyo rasmi, Ukimueleimisha mwanaume umeelimisha mtu mmoja lakini ukimueleimisha mwanamke umeelisha familia na hatimaye Taifa. Kwa maana hiyo, imekuwa ni kawaida kabisa kwa wanafunzi wa kike wanaopata ujauzitowakiwa masomoni kufukuzwa ili kutoendelea na masomo ili hali wanafunzi wa kiume ambao wamewapa ujauzito huo wakiendelea na masomo na hata kama aliyempa ujauzito mwanafunzi huyo kubaki bila kuchukuliwa hatua yoyote ya kisheria. Ikumbukwe kuwa akina Mama ndiyo walezi wa watoto na nguzo ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kitabu kinachoitwa *Economic Development* kilichoandikwa na **Michael Todaro na Stephen Smith, na hususan chini ya Mada *Human Capital: Education and Health in Economic Development,***Waandishi hawa wanasema kuwakiwango cha marejesho (*Rate of Return*) ya mwanamke mwenye elimu ni kubwa kuliko hata ile ya mwanaume mwenye elimu katika nchi nyingi zinazoendelea kwani, mwanamke mwenye elimu siyo tu anaongeza uzalishaji katika eneo lake la kazi, lakini pia mwanamke mwenye elimu atachelewa kuolewa, atazaa watoto wachache (*Familiy Palnning program*), atahakikisha watoto wake wanakuwa na afya njema na hivyo kuwa na faida kwa kizazi hicho na kijacho, pia mwanamke anapopata elimu anavunja duara la umaskini (***Vicious circle of Poverty***).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa kuna mwongozo ambao Serikali imeuandaa kwaajili ya kuwarudisha shuleni wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito mara baada ya kujifungua lakini mwongozo huo bado upo kwa wadau kwaajili ya kupata maoni ili Serikali iweze kufanya maamuzi. ***Kamati inashauri Serikali kutoa tamko rasmi kwamba Muongozo huo uanze kutumika iliwanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakifukuzwa shule kutokana na kupata ujauzito kurudishwa shuleni ili kuendelea na masomo yao.Hil itasaidia Taifa liweze kunufaika usomeshaji wa watoto wa kike.***

### 5.5 Ulipaji wa Madeni makubwa ya Walimu

**Mheshimiwa Spika,** Madeni ya Walimu wa shule za Msingi na Sekondari yapatayo kiasi cha shilingi **Trilioni 1.6** yamekuwa ni ya muda mrefu sana hali ambayo imekuwa ikiwakatisha tamaa walimu hao na kuwavunja moyo katika utendaji kazi wao. Kamati imekuwa ikitoa ushauri juu ya jambo hili mara zote ambapo imekuwa ikiwasilisha Taarifa zake Bungeni lakini bado utekelezaji wa suala hili bado hauridhishi. Katika kulisemea hili, madeni haya ya Walimu yameonekana kushughulikiwa na Wizara mbili kwa maana ya Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI ambao umekuwa ukiwachanganya Wadai na hata wadau wa Elimu.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Taarifa iliyotolewa na Wizara kuwa kwa kipindi cha Oktoba 2015 hadi Machi 2017, Serikali imelipa madeni yasiyo ya Mishahara ya Walimu **86,234** yenye thamani ya shilingi **Bilioni 33.1** sawa na **asilimia 2** tu ya deni lotena kwamba madeni mengine yataendelea kulipwa baada ya kufanyiwa uhakiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona suala la uhakiki linachukua muda mrefu sanawakati deni bado ni kubwa takribani **asilimia 98**lilobaki.***Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara mama ya Elimu ishirikiane na Wizara ya TAMISEMI kuharakisha uhakiki wa madeni haya makubwa ili Walimu waweze kupata stahiki zao mapema.*** Aliyekuwa Mtaalam wa Elimu katika Jimbo la Alabama nchini Marekani Dr. Tommy Bice aliwahi kusema"***Someone put it best the other day. What better investment in education can we make than in our Teachers, We can have all the buildings, supplies... but if we don't have Teachers, it wont matteruntil we get salaries up".*** Serikali haina budi kuhakikisha madeni ya walimu yanalipwa kwa wakati.

### 5.6 Tume ya Vyuo Vikuu Nchini (TCU)

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkonoagizo lililotolewa na Mheshimiwa Rais mnamo tarehe 15 April 2017** wakati wa uzinduzi wa Mabweni mapya ya wanafunzi ya

Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam la kuitaka TCU iache kuwachagulia wanafunzi vyuo vya kwenda kusoma badala yake wawaache wanafunzi wachague wenyewe vyuo wanavyopenda. Agizo hili limekuwa faraja kwa Kamati kwani ni kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikishauri TCU iache kufanya kazi ya udalali na badala yake isimamie ubora wa elimu inayotolewa na Vyuo vyote nchini vya Serikali na hata vya binafsi. Ni imani ya Kamati kuwa kwa agizo hili la Rais basi hata ule mchakato ambao Wizara uliokuwa unaendelea nao wa kuunda Tume ya Wataalam kufanya tathmini ya mfumo wa udahili wa pamoja (***Central Admissison System***) utaharakishwa.***Kamati inaonakwa kuwapa uhuru wanafunzi wachague vyuo wanavyotaka kutaisaidia Serikali kuwalipia ada wanafunzi walioko katika vyuo vya Serikali na hatimaye kuupunguzia mzigo Serikali kwani ada za vyuo vya Serikali zinaratibiwa na Serikali tofauti na vyuo binafsi.***

### 5.7 Bodi ya Mikopo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona suala la Elimu ya Juu ni haki ya Msingi kwa watu wenye sifa. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, wanafunzi **48,502** walijaza fomu kwa ukamilifu lakini ni wanafunzi **25,555** tu ndiyo walipata mikopo na hivyo kuacha wengine **22,947** wakiwa hawana mikopo kutokana na Bajeti iliyotengwa ya **shilingi Bilioni 427.5** kutotosheleza mahitaji.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Bodi ya Mikopo inaombewa kiasi cha shilingi **Bilioni 427.55** wakati huo ufaulu wa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita umeongezeka kutoka **asilimia 88 Mwaka 2012** hadi kufikia **asilimia 99** kwa Mwaka huu. Kamati inaona kwamba katika Mwaka huu wa Fedha wanafunzi wengi zaidi watakosa Mikopo licha ya ufaulu wao mzuri. Kuna msemo usemao "***The Main Hope of a Nation lies in the proper Education of its youth".***

**Kamati inashauri Serikali kuongeza Bajeti ya Bodi ya Mikopo ili wanafunzi wengi zaidi wanaostahili waweze kupata mikopo kwa Maendeleo ya Taifa letu.**

### 5.8 Kufuta Kodi ya Ujuzi (SDL) na Uchangiaji kwenye Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi (WCF) katika Vyuo Vikuu Binafsi

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata elimu bora, Serikali iliwapa nafasi wadau wengine kuanzisha utoaji wa elimu ya juu kupitia Vyuo Vikuu binafsi. Ni dhahiri kuwa Vyuo hivyo vimekuwa vikitoa elimu iliyo bora kwamanufaa makubwa katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa huduma ya Elimu katika jamii, Vyuo hivi binafsi vimekuwa vikikumbwa na changamoto ya tozo mbalimbali ikiwemo tozo ya kodi ya Ujuzi (**SDL**) pamoja na mwajiri kuchangia kwenye Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi wake (**WCF**) ambayo ipo kisheria kwa **asilimia 1** na **asilimia 0.5 kwa Vyuo Vikuu vya Umma.** Kuwepo kwa tozo hizi katika Vyuo Vikuu binafsi kunapelekea kuwa na changamoto ya utoaji wa ajira na hata kumsababishia mwanafunzi pamoja na mzazi/mlezi kulipa ada kubwa ili chuo kiweze kulipa tozo hizo kwa Serikali. Ikumbukwe kwamba ulipaji wa tozo wa **asilimia 0.5** wa Vyuo Vikuu vya Ummapiavinapata ruzuku kutoka kwa Serikalini.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuziangalia upya Sheria hizo zinazoelekeza utoaji wa tozo hizo katika Vyuo Vikuu vya Elimu hapa nchini ili wadau hawa wa Elimu waweze kupunguziwa kiasi cha tozo hizo hadi kufikia asilimia 0.5 ili kuweka usawa wa tozo katika Vyuo Vikuu vya Umma na kama ikiwezekana kufutiwa kabisa ili waendelee kutoa huduma ya utoaji wa Elimu bora kwa wananchi kwa maendeleo ya Taifa zima.**

**Aidha, Kamati inaona kwamba, kwakufanya hivyo, kutaongeza nafasi ya Vyuo hivyo kuendelea kupanuka zaidi na hata kuongeza udahili kwa wanafunzi na hata maslahi bora kwa Wafanyakazi wake na hatimaye Serikali kuendelea kupata mapato yake kwa njia ya kodi ya mfanyakazi mwenyewe (PAYE).**

### 5.9 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)

**Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kuwa kwa sasa nchi inajielekeza katika Uchumi wa Viwanda. Uchumi huu unahitaji rasilimali watu wa kada mbalimbali hususan mafundi mchundo ili kuweza kutekeleza azma hii. **Kamati inashauri Serikali ifanye uwekezaji mkubwa kwenye Vyuo vya Ufundi nchini kwa kupitia upya mitaala ya Vyuo vya vya Ufundi hasa VETA ili kuhakikisha vinatoa mafunzo yanayoendana na uchumi wa kisasa na viwanda.**

### 5.10 Utaratibu wa Viwango vya ufaulu katika shule binafsi

**Mheshimiwa Spika,** Utoaji wa elimu ya Sekondari kwa wananchi wetu upo katika shule za umma na shule za binafsi ambapo mzazi anaamua kumpeleka mtoto wake katika shule anayopenda mwanae asome. Ili kuboresha elimu inayotolewa shule binafsi zimejiwekea utaratibu wa kiwango cha mwanafunzi anachotakiwa kufaulu ili aende darasa linalofuata. Utaratibu huu umeonekana kuwa kero kwa baadi ya Wakuu wa Elimu mkoa na wilaya kiasi cha kuingilia utaratibu wa shule hizo kutoutekeleza na kuwaelekeza kwamba mtoto aendelee na darasa linalofuata bila kuangalia kiwango chake cha ufaulu ambao kama shule ilijiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona si sawa kwani mzazi amempeleka mtoto kwa mapenzi yake mwenyewe, **Kamati inashauri Serikali kuhakikisha shule hizo zinatoa taarifa ya utaratibu huo kwa mzazi kabla hajafanya maamuzi ya kumpeleka mtoto wake katika shule husika. Kwa kufanya hivi hakutakuwa na changamoto ya mzazi kulalamikia utaratibu huo.**

### 5.11 Ada ya Mitihani ya Elimu ya Sekondari

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitoa huduma mbalimbali za Elimu kwa wananchi wake ikiwemo utoaji wa huduma za mitihani ya Sekondari kwa maana ya kidato cha pili, cha nne na cha sita. Lakini utoaji wa huduma hii umekuwa ni wa bila malipo kwa shule za sekondari za umma na

kwakutoa malipo ya mitihanikatika shule za binafsi. **Kamati inaishauri Serikali, kuifanya huduma hii ya mitihani ya Sekondari katika vidato vyote kuwa ya Bila Malipo bila kujali mwanafunzi atafanya mtihani wake katika shule ya umma au ya binafsi. Kwa kufanya hivi kutaleta usawa kwa kuona wanafunzi wote wanafanya mtihani huo huo bila malipo yoyote kwani itakuwa ni huduma kama huduma nyingine za ujumla (*Universal Services*)**

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukurusana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kujitoa katika utekelezaji wa shughuli za Kamati na kuhakikisha kwa umoja wetu tunakamilisha Taarifa hii.

Napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Peter Ambrose Lijualikali, Mb | “ |
| 5. | Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | “ |
| 6. | Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb | “ |
| 7. | Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb | “ |
| 8. | Mhe. Lucia Michael Mlowe, Mb | “ |
| 9. | Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb | “ |
| 10. | Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb | “ |
| 11. | Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb | “ |
| 12. | Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | “ |
| 13. | Mhe. Selemani Said Bungara, Mb | “ |
| 14. | Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mb | “ |
| 15. | Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb | “ |
| 16. | Mhe. Bernadetha Kasabango Mushashu, Mb | “ |
| 17. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb | “ |
| 18. | Mhe. Savelina Sylvanus Mwijage, Mb | “ |
| 19. | Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo, Mb | “ |
| 20. | Mhe. Hussein N. Amar, Mb | “ |
| 21. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | “ |
| 22. | Mhe. Juma A. Juma, Mb | “ |

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii. Aidha, napenda kuwashukuru viongozi wote wa Bunge kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Prof. Joyce Ndalichako (Mb), Waziri waElimu, Sayansi na Teknolojia, Eng. Stella Manyanya (Mb), Naibu Waziri pamoja na Dkt.Leonard Akwilapo, Katibu Mkuu, Prof. Simon Msanjila na Dkt. Ave Maria Semakafu Manaibu Katibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipa Kamati katika utendaji kazi wake wa kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee naombakumshukuru Katibu waBunge Dkt. Thomas D. Kashillilah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndg. Dickson M. Bisile, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera pamoja na Msaidiziwao Ndg. Gaitana Chima kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati. Aidha, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanya kazi kila siku bila kuchoka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kumaliziasasa naomba Bunge lako Tukufu, liliridhie kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (**Fungu 46**) kiasi cha shilingi **1,336,685,241,000.00 (Trilioni Moja, Bilioni Mia tatu thelathini na Sita, Milioni Mia Sita Themanini na Tano, laki Mbili Arobaini na Moja Elfu)**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Peter Joseph Serukamba, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**
13 MEI, 201

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakiongoza na Dkt. Leonard Akwilapo, Katibu Mkuu; Profesa Simon Msanjila, Naibu Katibu Mkuu Sayansi; Dkt. Ave Semakafu, Naibu Katibu Mkuu Elimu; Ndugu Nicolas Buretta, Kaimu Kamishna wa Elimu; wameambatana na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo mbalimbali vilivyopo chini ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni mdogo wa Mheshimiwa Waziri ambaye ni Ndugu Dafroza Ndalichako. *(Makofi)*

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea Bungeni kwa ajili ya Mafunzo. Sasa namwita Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU,SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Kabla sijawasilisha maoni haya, napenda kuchukua fursa hii kwa namna ya pekee kabisa kutoa pole, salaam zangu za rambi rambi kwa wazazi, walezi, ndugu na wadau wote wa elimu nchini na nje ya nchi na jamaa wote wa wanafunzi wote wa Shule ya Mtakatifu Vincent waliofariki katika ajali ya basi iliyotokea Wilayani Karatu. Watoto hawa walifikwa na mauti haya wakati wakiisaka ndoto yao kubwa ya Taifa letu ya kuwa na elimu bora kama msingi wa maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Ramsi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa njia pekee ya kuwaenzi watoto hawa ni kuifanya siku waliyofariki tarehe 6 Mei, kuwa siku ya Elimu Kitaifa *(Education Day).* Siku hii ikumbukwe Kitaifa kama kichocheo cha mabadiliko makubwa ya mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri Kivuli katika Wizara yangu Dkt. Ally Suleiman Yussuf kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naipongeza Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu athari za kibajeti za utekelezaji wa Sera ya Elimu bila Malipo, maarufu Kama Elimu Bure; yalikuwa ni matamanio ya siku nyingi ya Watanzania kupata huduma ya elimu bure. Kwa kujali hitajio hilo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa mara ya kwanza kiliweka katika ilani yake ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, kwamba kingetoa elimu bure. Katika ilani yake ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2010 na 2015 pia, CHADEMA na UKAWA iliendelea kuwaahidi Watanzania kuwapatia elimu bure hadi ngazi ya Chuo Kikuu endapo ingepata ridhaa ya wananchi kuongoza dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi CCM ilipora Sera hii ya Upinzani ya Elimu Bure tena bila hata ya kumtambua mwasisi wake *(acknowledgment)* na kuanza kuitekeleza, kwa wigo mdogo kwa maana ya kuondoa ada kwa elimu msingi pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haina wivu na utekelezaji wa Sera ya Elimu Bure inayotekelezwa na Serikali, kwani lengo la upinzani ni kuwaondolea wananchi kero za aina mbalimbali. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakerwa na uamuzi wa kukurupuka wa Serikali kutekeleza sera hii bila kufanya tathmini ya mahitaji *(needs assessment)* na mpango wa utekelezaji *(implementation plan)* jambo ambalo limefanya utekelezaji wa Sera hii ya Elimu Bure kuwa mgumu na hivyo kutokidhi matarajio yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto mbalimbali zinazokabili utekelezaji wa sera hii ya elimu bila malipo. Mojawapo ya changamoto hizo ni uhitaji wa maboresho na ujenzi wa miundombinu mashuleni kutokana

na ongezeko la udahili. Hivi sasa kuna ongezeko la watoto wapya takriban milioni moja katika Shule za Msingi na Shule za Awali kwa wastani wa wanafunzi 45 kila darasa. Tafsiri ya ongezeko hili ni kwamba, vitahitajika vyumba vipya vya madarasa takriban 23,000 ambavyo gharama zake ni takriban shilingi bilioni 276 kwa gharama ya shilingi milioni 12 kwa kila darasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji hayo ni tofauti na upungufu wa miundombinu ya madarasa 95,945 katika shule za umma kwa takwimu za mwaka 2016 za *BEST*, ambazo gharama yake ni takriban shilingi trilioni 1.1. Kwa hiyo, Serikali itahitaji kutenga kiasi cha takriban shilingi trilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya na ukarabati katika Shule za Awali na Msingi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuweza kukabiliana na ongezeko hilo la wanafunzi kutokana na tangazo la elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za *BEST* za mwaka 2016, Elimu Msingi imeendelea kukabiliwa na changamoto za uhaba wa nyumba za Walimu, matatizo ya vyoo, majengo ya utawala na vyumba vya maktaba. Matokeo ya tafiti hizo yanaonesha kwamba, kuna mahitaji ya nyumba za Walimu 186,008 sawa na asilimia 81.1, majengo ya utawala yapatayo 10,941 sawa na asilimia 83, vyumba vya maktaba vipatavyo 15,000 sawa na asilimia 88 na ukosefu wa vyumba 16,290 vya huduma ya kwanza sawa na asilimia 93. Licha ya upungufu huo, umbali wa kuzifikia shule hizo bado umeendelea kuwa changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ndizo athari za kibajeti za Sera ya Elimu Bure. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu, kuhusu mpango mkakati wa utekelezaji wa sera hii na imetenga bajeti kiasi gani kwa mwaka 2016/2017 na 2018 kugharamia mpango huo ili kukabiliana na changamoto za miundombinu elimu msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhaba wa Walimu Shuleni na Hali ya Ufundishaji; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

ilishaeleza bayana katika miaka iliyotangulia kwamba msingi wa elimu ni Mwalimu na kwamba, bila Mwalimu hakuna elimu. Hivyo, iliishauri Serikali kuwapa Walimu motisha ili wapende kazi yao ya ualimu na hivyo kuondokana na uhaba wa Walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo huo, Ripoti ya Benki ya Dunia ya 2016 inayopima viashiria vya utoaji huduma katika Sekta ya Elimu na Afya ilibainisha kwamba ni asilimia 49 tu ya Walimu walioajiriwa ndio wanaohudhuria darasani kufundisha ipasavyo, asilimia 32 wanafika lakini hawafundishi na asilimia 14 hawafiki shuleni kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Chama cha Walimu Tanzania Shule za Msingi peke yake zina upungufu wa takribani Walimu 100,000 wakati Shule za Sekondari zina upungufu wa Walimu 50,000 kwa kuzingatia mgawanyo wa vipindi, masomo na majukumu mengine wakiwamo Walimu 30,000 wa masomo ya Sayansi na Walimu 20,000 wa masomo ya Sanaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili Tukufu, imetenga bajeti kiasi gani kwa ajili ya kuajiri Walimu wa kutosha, wataalam wa maabara ili kukabiliana na uhaba wa nguvu kazi katika Sekta ya Elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu; kama nilivyoeleza hapo awali, ili Walimu waipende kazi yao na Walimu kufika kazini, ni lazima wapatiwe motisha kwa kuwalipa stahili zao kwa wakati; lakini Utafiti wa Haki Elimu wa mwaka 2016 wa *Teachers Motivation* unaonesha kuwa ni Walimu wanne tu kati ya kumi ndiyo wana motisha na kazi ya Ualimu, lakini pia utafiti wa TWAWEZA kupitia KIUFUNZA wa hamasa ya ufundishaji unaonesha kuwa Walimu wakipewa motisha wanafanya kazi zaidi na kuwa na matokeo chanya katika ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa haiichukulii kada hii ya Ualimu kwa uzito unaostahili hasa kurejesha

hamasa kwa Walimu katika kazi yao. Nasema hivi kwa sababu kada hii inaidai Serikali mabilioni ya fedha lakini Serikali mpaka leo haiwalipi zaidi ya hadithi ya uhakiki wa madeni isiyoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kulipa madeni hayo; na lini itayalipa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwapa taarifa ya maandishi Walimu wote wenye madai yaliyokataliwa na sababu za kukataliwa ili waweze kupata nafasi ya kukata rufaa ili wapate haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa ruzuku ya elimu kwa Shule za Msingi na Sekondari umeendelea kudorora siku hadi siku. Kama inavyojulikana, Shule za Msingi zinatakiwa kupewa ya sh. 10,000/= kwa kila mwanafunzi na Shule za Sekondari sh. 25,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Shirika la Haki Elimu mwaka 2016 juu ya utekelezaji wa elimu bure, ni kwamba Shule za Msingi zilipokea wastani wa sh. 500 kwa mwezi kwa kila mwanafunzi sawa na sh.6,000/= kwa mwaka. Takriban 94% ya Wakuu wa Shule waliohojiwa walithibitisha kuwa kiwango cha ruzuku cha sh.6,000/= kwa mwaka kwa kila mtoto hakitoshi kugharamia mahitaji yote na shughuli za utawala, gharama za mitihani na ukarabati wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ruzuku ya elimu kwa Shule za Msingi na Sekondari kuwa ndogo na kutototolewa kwa utoshelevu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuongeza ruzuku hii angalau kwa Sh.25,000/= kwa kila mwanafunzi kwa Shule ya Msingi kwenda Sh.50,000/= na kwa kila Sekondari na pia kutenga fedha hizi na kuhakikisha zitatolewa kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sakata la vyeti vya kughushi. Tarehe 28 Aprili mwaka huu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokea taarifa na orodha ya

watumishi ambao wamekuwa na vyeti feki au vyeti vya kughushi baada ya ukaguzi kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hiyo, umma wa Watanzania ulijulishwa kuwa watumishi 9,932 katika Utumishi wa Umma wameghushi vyeti vyao vya taaluma. Aidha, umma ulijulishwa kuwa takribani watumishi 1,538 vyeti vyao vinatumika zaidi ya mara moja na pia idadi ya watumishi 11,596 wana vyeti vya utaalam bila vyeti vya taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi msimamo wake kuwa haiungi mkono kabisa matumizi ya vyeti vya kughushi yaani vyeti feki katika Utumishi wa Umma na hata katika sekta binafsi nchini. Ni lazima Taifa tukubaliane kuwa matumizi ya vyeti vya kughushi ni jinai na yanarudisha nyuma ufanisi katika utendaji kazi katika sekta zote ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi kuwa zoezi la uhakiki lilikuwa na upungufu kadhaa ambapo inaweza kupelekea baadhi ya watu kutotendewa haki. Mathalan baadhi ya taarifa ambazo Kambi ya Upinzani imeipata, inasema kwamba zoezi hilo halikuzingatia watumishi ambao wakati wa uhakiki unafanyika walikuwa likizo, wagonjwa, Walimu walioajiriwa katika mpango wa *UPE*, waliokuwa masomoni na waliokuwa nje ya vituo vya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa wanafanya uamuzi mapema wa rufaa zilizoombwa na watumishi ambao kwa namna moja ama nyingine wameona kuwa hawajatendewa haki. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa watumishi wa Baraza la Mitihani, yaani *NECTA*, Wizara ya Elimu na Taasisi au watu binafsi ambao wamekuwa wakijihusisha na shughuli haramu za kughushi vyeti kwa watu wasio na sifa kwa ajili ya kujipatia fedha na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Marudio *(re-entry policy)* kwa wanafunzi waliopata mimba shuleni, kumekuwa na ongezeko kubwa la mimba kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na wale wa Sekondari. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kimataifa la Haki za Binadamu *(Human Rights Watch)* mwaka 2016 ni kwamba, takriban wanafunzi 8,000 hapa Tanzania hushindwa kumaliza masomo yao kutokana na kupata ujauzito kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaomba utulivu ndani ya Bunge, vitabu vinaletwa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1995 na mwaka 2002 ilibainisha kuwa mtoto wa kike akipata mimba ni ushahidi tosha kuwa amefanya vitendo vya ngono ambavyo ni kinyume na shule hivyo afukuzwe shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi mbalimbali Barani Afrika zimelichukulia suala hili kwa uzito wake na tayari nchi kama Zambia, Kenya, Rwanda, Malawi na nyinginezo zimekuwa mfano mzuri katika kuwasaidia watoto hawa na matokeo mazuri yameanza kuonekana. Badala ya watoto hawa kuonekana mizigo katika familia na jamii, Serikali hizo zimeweka mfumo mzuri wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa Elimu akijibu swali la Mheshimiwa Margaret Sitta kuhusiana na *Re-Entry Policy,* alisema kuwa, Serikali imeandaa mwongozo utakaofuatwa na wadau mbalimbali ili kuwawezesha wasichana waliopata mimba kuweza

kuendelea na masomo yao. Mheshimiwa Naibu Waziri alilihakikishia Bunge kuwa mpaka mwezi Machi, 2017 mpango huo utakuwa umekamilika na kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mpango huo wa Serikali umetokomea wapi hadi leo Mei? Je, ni lini Serikali itauleta mpango huo ndani ya Bunge hili ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kupata fursa ya kuufahamu na hata kuutungia sheria ili uweze kutekelezwa vizuri na hivyo kuwasaidia maelfu ya mabinti ambao ndoto zao za kufuta ujinga zimezimika kwa sababu ya kupata mimba? Vile vile Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri tuwe na mtaala wa afya ya uzazi, yaani *Reproductive Health Syllabus* ili kuwasaidia watoto hawa na tunashauri ianzie Darasa la Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishi katika dunia ambayo kila hatua ya maendeleo inasukumwa mbele na uvumbuzi na ugunduzi wa sayansi na teknolojia. Hata hivyo, mazingira ya kuchochea uvumbuzi wa ugunduzi huu hapa nchini sio mzuri kutokana na sera na sheria zinazokinzana katika kukuza uvumbuzi na ugunduzi huu, miongoni mwa wanafunzi kuanzia ngazi ya Shule ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchini Marekani, kijana Mark Elliot Zuckerberg mwenye umri wa miaka 32 tu ni bilionea mwenye utajiri wa dola za Marekani bilioni 58.6 kutokana na umahiri wake katika uvumbuzi, ugunduzi na matumizi ya *TEHAMA*, hapa kwetu Tanzania vijana wanaojaribu kuthubutu kutumia teknolojia hiyo wanatungiwa sheria ngumu na mwishowe wanaishia Gerezani. Kijana huyu wa Kimarekani ni *programmer* wa *computer* na mjasiriamali wa wavuti yaani *internet* na mwanzilishi wa mtandao wa kijamii wa *Facebook*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Marekani inajivunia hayo, hapa kwetu *programmer* wa *computer* na mwanzilishi wa mtandao wa kijamii yaani Jamii *Forums,* Maxence Melo amefunguliwa kesi ya makosa ya kimtandao, yaani *Cyber*

*Crime* chini ya Sheria kandamizi inayodumaza uvumbuzi na ugunduzi katika *TEHAMA*, badala ya kusaidiwa ili aendelee kuvumbua zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuipitia upya Sheria ya *Cyber Crime* na sheria zote zinazozuia ubunifu na ujasiriamali katika sayansi na teknolojia, ikiwa ni pamoja na kubaini maeneo yote katika sheria hizo yanayozuia kukua kwa sayansi na teknolojia hasa TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee matamko yasiyoendana na Sera za Teknolojia. Wakati Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 katika ukurasa wa saba inaelekeza Tanzania kutumia washauri wataalam *(Consultants)* wa Sayansi na Teknolojia kutoka ndani na kufanya shughuli za teknolojia, Mkuu wa Nchi alinukuliwa na gazeti la *The Citizen* la tarehe 2 Julai, 2016 kuwa amekubaliana na Rais Paul Kagame wa Rwanda kupewa Wataalam wa TEHAMA kutoka Rwanda ili kusuka mifumo ya kukusanya kodi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa suala la kuazima wataalam wa TEHAMA kutoka nje ya nchi siyo tu linaidhalilisha Tanzania kuwa haizalishi wataalam wa TEHAMA, lakini pia ni ujumbe unaotumwa kwa Serikali ulimwenguni kuwa Tanzania haina wataalam wa TEHAMA wenye uwezo wa kusuka mifumo imara ya kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kuwa suala hilo linaitweza nchi, lakini pia suala hilo linaonesha kuwa matamko ya Serikali yanakwenda kinyume na maelekezo ya Sera ya Taifa ya Sayansi ya Teknolojia inayotaka nchi iwape fursa vijana kutoka ndani katika kazi zote za utaalam ushauri kuhusu sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matatizo ya vitabu vipya vya Taasisi ya Elimu. Vitabu ni nyenzo muhimu sana katika utoaji wa elimu bora hasa katika kipindi hiki chenye

uhaba mkubwa wa Walimu. Vitabu visipotungwa kwa ubora ni sumu mbaya sana kwa elimu hasa kwa watoto wetu wadogo wa Shule za Awali na Shule za Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu Tanzania ilipewa mamlaka ya uchapishaji wa Vitabu vya Kiada nchini na imechapisha vitabu vipya kwa Shule za Msingi kama vilivyoorodheshwa katika hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 18 hadi 27.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivyo vina upungufu mkubwa sana ambapo usiporekebishwa unaweza kusababisha madhara makubwa katika utoaji wa elimu na hivyo kushusha ubora wa elimu yetu. Miongoni mwa upungufu huo ni kama ifuatavyo:-

Kutokuchapishwa Kiongozi cha Mwalimu ambacho ndicho hasa kinachowasaidia Walimu kufundisha, lakini vile vile kuchapisha mambo yasiyostahili kuingizwa kwenye Kiongozi cha Mwalimu. Haya ni makosa makubwa kwa kuwa yanatoa maelekezo wakati mwanafunzi anatakiwa yeye apokee maelekezo. Vilevile kuna usanifu wa vitabu, picha na makosa ya lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kwa dakika moja tu kwa sababu mimi ni Mwalimu nieleze kwa uchache na nadhani hii ndiyo sababu inatupa shida sana hata Wabunge wanapokuja hapa kujieleza wanashindwa kujieleza. Ni kwa sababu vitabu vyenyewe, kama lugha, mtoto mdogo anayeanza Darasa la Kwanza; hiki ni kitabu cha Darasa la Tatu naomba tu nisome vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kitabu kinasema ukurasa wa 61, anamwambia mtoto aandike *which is long between a pen and rubber? Which is long*? Swali lingine linasema *the driver is taken the Police Station; the driver is taken the police station.* Lingine katika ukurasa wa 143 anaandika Dodoma, kwa hiyo, unajaza Dodoma ni nini? Kwa hiyo, Dodoma *is the big city of Tanzania,* badala ya kusema Dodoma *is the Capital city*. Kwa hiyo, ukisoma hiki

kitabu cha Kiingereza kuanzia mwanzo mpaka mwisho, kila *page* ina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo la aibu sana na nimesikitika sana kumsikia Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake anasema kwamba watawachukulia hatua. Hii siyo mara ya kwanza kwa Taasisi hii kutoa vitabu vibovu na inailetea Serikali hasara kubwa. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Waziri anasema watawachukulia hatua, ilitakiwa awe amewachukulia hatua siku nyingi sana kwa sababu wanawaharibu watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, vitabu hivi vimechelewa sana kwa sababu vingine vimeingia mwezi wa Sita mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani Bungeni inasema kutokana na upungufu huo wote, tunaitaka Serikali kuzuia matumizi ya vitabu hivyo vyenye makosa shuleni; na pia kuiagiza Taasisi ya Elimu kufanya marekebisho ya makosa yaliyopo kwenye vitabu hivyo na kuvichapisha upya. Aidha, Kambi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya uhakiki wa taaluma na weledi wa watumishi wa Taasisi ya Elimu Tanzania ili kujiridhisha kama wana sifa stahiki, uwezo, weledi katika kufanya kazi ya utunzi wa vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza hivyo kwa kuwa Serikali inapata hasara kubwa kurudia kuchapisha vitabu, hivyo kutokana na uzembe wa watumishi wanaohusika na kazi hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema kuwa, utaratibu wa zamani urejeshwe ili vitabu hivi ambavyo ni nyenzo muhimu kwa watoto kujifunzia visanifiwe na chombo kingine ili kudhibiti ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na usimamizi duni wa Sekta ya Elimu na hususan maendeleo ya Walimu nchini jambo ambalo limeyumbisha Sekta ya Elimu unaotokana na kukosekana kwa chombo kimoja chenye mamlaka ya kusimamia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba zangu za miaka ya nyuma nilieleza kuwa ili kuondoa mkanganyiko uliopo kutokana na kuwepo kwa taasisi mbalimbali kusimamia elimu, yaani Wizara ya Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kwa wakati huo huo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuanzisha chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza ianzishwe Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Tanzania *Education and Training Regulatory Authority – TETRA)* ili masuala yote ya udhibiti wa utoaji wa elimu nchini yawe yanashughulikia na chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa ushauri huo, Serikali ilianzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teacher's Service Commission)* badala ya Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu. Kimsingi Tume ya Utumishi wa Walimu haijasaidia hata kidogo kutatua kero za Walimu, kwanza muundo wake una matatizo, ukitoka ngazi ya Taifa hakuna ngazi ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili licha ya Tume hii kupewa hadhi ya mwajiri, lakini haifanyi kazi hiyo kwa sababu haiwezi kulipa mishahara. Hivyo basi, kwa sababu hiyo, bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuanzishwa kwa chombo ambacho kitasimamia, yaani *TETRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ufaulu wa Shule za Sekondari; kumekuwa na tatizo la muda mrefu la ufaulu hafifu kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari. Hata hivyo, hivi karibuni wakati Waziri wa TAMISEMI akiahirisha mjadala wa bajeti ya Ofisi ya TAMISEMI, alinukuliwa akisema kwamba, tunaambiwa elimu ya Tanzania inashuka, sijui wanatumia takwimu gani, lakini kinachoweza kutusaidia, tunajua kwamba elimu imepanda au inashuka ni matokeo ya mitihani. Kama kipo kigezo kingine, labda ni baadaye,

mwisho wa kunukuu. Aliendelea kusema kuwa ufaulu umeongezeka kwa 99% Kidato cha Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ufaulu ni matokeo ya mambo mengi kama nilivyoeleza hapo awali; na kwa kuwa kulikuwa na changamoto kadhaa zilizosababisha ufaulu hafifu; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama changamoto hizo zimetatuliwa zote ndiyo maana ufaulu unaongezeka au kuna jambo gani limefanyika kupandisha ufaulu huu, ikizingatiwa kuwa bado shule zina mazingira duni yale yale na vile vile kwa ongezeko la elimu bure wanafunzi wamedahiliwa wengi na Walimu ni wachache. Kwa hiyo, mtuambie kuna maajabu gani ambayo mmeyatumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Elimu ya Juu hasa vile vikongwe vinakabiliwa na tatizo kubwa la uchakavu wa miundombinu, hususan uchakavu wa majengo. Hata hivyo, matengenezo au ukarabati wa miundombinu hiyo, kwa kiwango kikubwa haujafanyika kutokana na ukosefu wa fedha, hali inayopelekea baadhi hata ya mabweni kufungwa mfano bweni la pili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge, ina mpango mkakati gani wa ukarabati wa miundombinu chakavu hasa katika vyuo vikongwe nchini pamoja na Sokoine na Mzumbe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa miundombinu mipya; Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono ujenzi wa mabweni *(hostels)* uliofanywa na Serikali katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuwa ujenzi huo utawasaidia takriban wanafunzi 4,000 kupata malazi ndani chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufafanunzi wa gharama halisi zilizotumika kujenga mabweni hayo. Kwa uzoefu na mtazamo wa kawaida tu, gharama ya shilingi bilioni 10 kujenga majengo 20 ya ghorofa tatu kila moja ni ndogo sana. Hii ina maana kwamba kila *flat* moja ni shilingi

milioni 500 jambo ambalo linazua sintofahamu kwamba pengine gharama hiyo imetajwa kukidhi matakwa ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inatia shaka kwa ujenzi huo ni bajeti ya ujenzi huo. Kama ilivyo ada, fedha zote za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Jamhuri ya Muungano, huidhinishwa na Bunge lako Tukufu; lakini hakuna kumbukumbu yoyote katika fedha zilizotumika kujenga majengo hayo ziliidhinishwa na Bunge hili. Kwa sababu hiyo, Sheria ya Bajeti ilivunjwa. Aidha, hakuna kumbukumbu zozote zinazoonyesha kama zabuni ya ujenzi wa majengo hayo ilitangazwa, kwa maana hiyo, Sheria ya Manunuzi ilivunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum *(special audit)* kuhusu uhalisia wa gharama uliotumika kujenga mabweni hayo. Kwa sababu hata nyumba ya ghorofa moja tu ya mtu binafsi, inazidi shilingi milioni 500; sembuse maghorofa hayo! Kwa hiyo, tunataka maelezo ya kina na tusipojibiwa, tutashika shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu mkopo wa Elimu ya Juu. Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa mwaka 2016 ambapo pamoja na mambo mengine sheria hiyo ilifanya marekebisho ya Kifungu cha 19 na 20 cha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi. Utekelezaji wa matakwa haya ya sheria unaenda kinyume na misingi ya sheria kwa sababu ilitakiwa utekelezaji wake usiwaathiri wale ambao tayari walishaingia mkataba na Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili sababu za kutekeleza mabadiliko hayo ya sheria huku ikijua kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mikataba ambayo

wanufaika wa mikopo hiyo waliingia na Bodi kabla sheria haijabadilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Majukumu ya Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU);* Tume hii pamoja na mambo mengine ilianzishwa kwa madhumuni ya kufanya udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu pamoja na kusimamia ubora wa elimu. Hivi karibuni wakati Mheshimiwa Rais anafungua *hostel* za Chuo Kikuu, alisema kwamba Tume isishughulike tena na masuala la udahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, *TCU* haitaweza kudhibiti ubora wa Elimu ya Juu ikiwa udahili utakuwa unafanywa vyuo vyenyewe. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuwa pamoja na changamoto zilizopo *TCU,* iboreshe upungufu wote na iendelee kufanya udahili na kutekeleza majukumu yake kwa kuwa upungufu ni mdogo kuliko mafanikio ikiwa ni pamoja na wanafunzi kulipa hela nyingi kama wataachiwa kuchagua wenyewe vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya jumla ya elimu yako katika ukurasa wa 41. Utekelezaji wa bajeti ya maendeleo hadi kufikia mwezi Machi Serikali ilikuwa imetoa asilimia 34 tu ya fedha zote, lakini katika Kitengo cha Elimu, mgawanyo wa fedha hizi shilingi milioni 427 sawa na asilimia 48 ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu na shilingi bilioni 470 sawa na asilimia 52 ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Serikali ilikuwa imeshatoa shilingi bilioni 344 sawa na asilimia 80 ya fedha hiyo. Kwa upande wa miradi halisi ya maendeleo hali ni tofauti, fedha zilizoidhinishwa kwa miradi mingine ya maendeleo zilikuwa ni shilingi bilioni 470 hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ambayo ni sawa shilingi bilioni 156.4 pekee sawa na asilimia 30 tu ya fedha hizi zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya shilingi bilioni 186 zilizotengwa kwa ajili ya miradi mikuu ya maendeleo kwa Wizara ya Elimu ni shilingi bilioni 29 tu sawa na asilimia 16 pekee ya fedha zilizoidhinishwa, ndizo zilitolewa hadi kufikia Machi 2017. Kwa mwenendo huu, miradi hii haitakuwa imefikia angalau asilimia 30 ya utekelezaji hadi mwisho wa mwaka. Hali hii ni hatari kwa shughuli za maendeleo ya Sekta ya Elimu na inaturudisha nyuma kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Baba wa Taifa wa Afrika ya Kusini, Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema, "*no country can really develop unless its citizens are educated.*" Ikiwa na maana kwamba hakuna nchi inayoweza kuendelea kama wananchi wake hawajaelimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaamini kuwa elimu ndiyo kila kitu kwenye mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Changamoto karibu zote ambazo nimezieleza kwenye hotuba yangu, zinahusiana moja kwa moja na changamoto za kisera, usimamizi wa elimu na mfumo wa upangaji wa usimamizi wa bajeti ya Sekta ya Elimu.

Tanzania kama Taifa, tunahitaji kuelewa nini falsafa ya elimu yetu, nini malengo makuu ya elimu yetu na tuwe na mikakati ya kuhakikisha mfumo wa elimu yetu unalenga kutoa elimu jumuishi, elimu inayotoa fursa kwa watoto wote wa Tanzania kupata elimu bora na elimu inayolenga kumlinda na kumwendeleza mtoto. Elimu bora kwa kila mtoto wa Tanzania ndiyo itakayosaidia Taifa hili kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na niseme tena elimu ndiyo msingi wa maendeleo na ndiyo kipaumbele namba moja, kipaumbele namba mbili na kipaumbele namba tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI MHESHIMIWA SUSAN ANSELIM JEROME LYIMO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu kwa mwaka wa fedha 2016/17 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijawasilisha maoni hayo, napenda kuchukua fursa hii kwa namna ya pekee kutoa pole na kutuma salamu zangu za rambirambi kwa wazazi, ndugu, wadau wote wa elimu nchini na nje ya nchi na jamaa wote wa watoto 32, walimu 2 na dereva waliofariki wa shule ya Mt. Lucky Vincent katika ajali ya basi iliyotokea wilayani Karatu huko mkoani Arusha. Watoto hawa walifikwa na mauti wakati wakiisaka ndoto kubwa ya taifa letu ya kuwa na elimu bora kama msingi imara wa maendeleo katika Taifa letu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuwa njia sahihi ya kuwaenzi watoto hawa ni kuifanya siku waliofariki tarehe 6 Mei kuwa siku ya Elimu Kitaifa (education day). Siku hii ikumbukwe Kitaifa kama kichocheo cha mabadiliko makubwa ya mfumo wetu wa elimu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri Kivuli katika wizara hii Dkt.Ally Suleima Yusuf kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naipongeza Sekretarieti ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii.

## 2. ATHARI ZA KIBAJETI ZA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU BILA MALIPO (MAARUFU KAMA ELIMU BURE)

**Mheshimiwa Spika,** yalikuwa ni matamanio ya siku nyingi ya watanzania kupata huduma ya elimu bure. Kwa kujali hitajio hilo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa mara ya kwanza kiliweka katika ilani yake ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, kwamba kingetoa elimu bure. Katika ilani yake ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2010 na 2015, CHADEMA iliendelea kuwaahidi watanzania kuwapatia elimu bure hadi ngazi ya Chuo Kikuu endapo ingepata ridhaa ya wananchi kuongoza dola.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mbinu za kisiasa, CCM ilipora sera hii ya upinzani ya elimu bure tena bila hata ya kumtambua mwanzilishi wake *'acknowledgment'* na kuanza kuitekeleza, lakini kwa wigo mdogo - kwa maana ya kuondoa ada kwa elimu msingi, - yaani kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne pekee.

**Mheshiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haina wivu na utekelezaji wa sera ya elimu bure inayotekelezwa na Serikali kwani lengo la upinzani ni kuwaondolea wananchi kero za aina mbalimbali ambazo kwa miaka mingi Serikali imeshindwa kuziondoa na kufanya maisha yao yawe mazuri kwa kiwango cha juu iwezekanavyo. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakerwa na uamuzi wa kukurupuka wa Serikali kutekeleza sera hii bila kufanya tathmini ya mahitaji (assessment of needs) na mpango wa utekelezaji (implementation plan) jambo ambalo limefanya utekelezaji wa sera hii ya elimu bure kuwa mgumu, na hivyo kutokidhi matarajio yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** zipo changamoto mbalimbali zinazokabili utekelezaji wa sera hii ya elimu bila malipo. Mojawapo ya changamoto hizo ni uhitaji wa maboresho na ujenzi wa miundombinu mashuleni kutokana na ongezeko la udhali. Tamko la Serikali la kutoa elimu bure limehamasisha wazazi wengi kupeleka watoto shule na limepata mwitikio mkubwa. Kwa mujibu wa takwimu za elimu (BEST, 2016) udahili kwa madarasa ya awali umeongezeka kwa

wanafunzi 492,947 sawa na asilimia 46. Aidha, udahili wa shule za msingi umeongezeka kwa wanafunzi 552,286 sawa na asilimia 41, ukilinganisha na udahili wa Mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** hivi sasa kuna ongezeka la takribani watoto wapya milioni moja (1,000,000) shuleni katika shule za awali na msingi, kwa wastani wa wanafunzi 45 kila darasa. Tafsiri ya ongezeko hili, ni kwamba, vitahitajika vyumba vipya vya madarasa takriban 23,000 ambavyo gharama zake ni takribani shilingi bilioni 276 kwa gharama ya shilingi milioni 12 kwa darasa.

**Mheshimiwa Spika,** mahitaji hayo, ni tofauti na upungufu wa miundombinu ya madarasa 95,945 katika shule za umma kwa takwimu za mwaka 2016 za BEST, ambazo gharama yake ni takriban shilingi trilioni 1.151. Kwa hivyo Serikali itahitaji kutenga kiasi cha takribani shilingi trilioni 1.427 kwaajili ya ujenzi wa miundombinu mipya na ukarabati katika shule za awali na msingi kwa mwaka wa fedha 2017/18 ili kuweza kukabilina na ongezeko hilo la wanafunzi kutokana na tangazo la elimu bure.

**Mheshimiwa** Spika, ukiachilia mbali uhaba wa vyumba vya madarasa, kuna uhaba wa miundombinu ya vyoo na vifaa vya kufundishia ambao umeendelea kukua. Kwa mfano, uwiano wa mwanafunzi wa kike shule za msingi kwa tundu la choo umeendelea kuwa mbaya kwa wanafunzi 53 kutumia tundu moja la choo (1:53) badala ya wanafunzi 20 (1:20) kwa tundu la choo. Kwa upande wa wanafunzi wa kiume, watoto 56 wanalazimika kuchangia tundu moja la choo kinyume na maagizo ya serikali yanayotaka wanafunzi 25 tu kuchangia tundu moja. Hii inamaana kwamba kuna upungufu wa takriban asilimia 62 na 56 wa matundu ya choo kwa watoto wa kike na wa kiume katika shule za msingi kwa mtiririko huo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa takwimu za BEST za mwaka 2016, ni kwamba, elimu msingi imeendelea kukabiliwa na changamoto za uhaba wa nyumba za walimu, majengo ya utawala na vyumba vya maktaba. Matokeo ya

tafiti hizo yanaonyesha kwamba, kuna mahitaji ya nyumba za walimu 186,008 sawa na asilimia 81.1, majengo ya utawala yapatayo 10,943 sawa na asilimia 83.4; vyumba vya maktaba vipatavyo 15,342 sawa na asilimia 88 na ukosefu wa vyumba 16,290 vya huduma ya kwanza sawa na asilimia 93.9. Licha ya upungufu huo, umbali wa kuzifikia shule bado umeendelea kuwa changamoto. Hadi kufikia November 2016 takribani asilimia 51 ya shule za msingi zilikuwa zinapatikana umbali wa zaidi ya kilometa 50 kutoka makazi ya watu.

**Mheshimiwa Spika,** hizo ndizo athari za kibajeti za sera ya elimu bure. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge hili kuhusu mpango mkakati wa utekelezaji wa sera hii na imetenga bajeti kiasi gani kwa mwaka wa fedha 2017/18 kugharamia mpango huo ili kukabiliana na changamoto za miundombinu elimumsingi.

### 3. UHABA WA WALIMU SHULENI NA HALI YA UFUNDISHAJI

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishaeleza bayana katika miaka iliyotangulia kwamba msingi wa elimu ni mwalimu na kwamba, bila mwalimu hakuna elimu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliishauri Serikali kuwapa walimu motisha ili wapende kazi yao ya ualimu na hivyo kuondokana na uhaba wa walimu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za BEST za mwaka 2016 zinaonyesha kwamba, wastani wa uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa shule za msingi umeimarika hadi kufikia 1:43 (Mwalimu mmoja anafundisha watoto 43) lakini kwa shule moja moja hali sio shwari na hususani kwa upande wa mahudhurio ya walimu darasani.

**Mheshimiwa Spika,** katika muktadha huohuo, Ripoti ya Benki ya Dunia ya 2016 inayopima viashiria vya utoaji huduma katika sekta ya elimu na afya ilibainisha kwamba, ni asilimia 49 tu ya walimu walioajiriwa ndio wanaohudhuria darasani kufundisha ipasavyo, asilimia 32 wanafika lakini hawafundishi na asilimia 14 hawafiki kabisa shuleni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa CWT, shule za msingi peke yake zinaupungufu wa takribani walimu 100,000 wakati shule za sekondari zina upungufu wa walimu 50,000 kwa kuzingatia mgawanyo wa vipindi, masomo na majukumu mengine wakiwamo walimu 30,000 wa masomo ya sayansi na walimu 20,000 wa masomo ya sanaa.

**Mheshimiwa Spika,** tatizo la uhaba wa walimu linakwenda sambamba na upungufu wa watumishi wengine (non teaching staff). Kuna upungufu wa wataalam wa maabara 4,000 ambao husaidia kupunguza mzigo wa kazi kwa walimu.Takribani asilimia 90 ya shule zote za kata ambazo ni zaidi ya 3,500 hazina wataalamu wa maabara, hivyo kuongeza mzigo kwa walimu wa kawida kushughulika na uandaaji wa majaribio na utunzaji wa vifaa vya maabara.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, imetenga bajeti kiasi gani kwa ajili ya kuajiri walimu wa kutosha, wataalamu wa maabara ili kukabiliana na uhaba wa nguvukazi katika sekta ya elimu?

## 4. MADAI YA WALIMU

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali, ili walimu waipende kazi yao na wadumu katika kazi hiyo, ni lazima wapatiwe motisha kwa kuwalipa stahili zao kwa wakati. Utafiti wa HakiElimu wa mwaka 2016 wa ***"Teachers Motivation"*** unaonesha kuwa walimu 4 tu kati ya 10 ndio wana motisha na kazi ya ualimu na moja ya sababu ya hamasa ndogo ni kutolipwa malimbikizo ya madeni, malipo madogo na mazingira ya kufundishia kutoheshimiwa na jamii. Lakini pia utafiti wa Twaweza wa Kiufunza wa hamasa na ufundishaji unaonesha kuwa walimu wakipewa motisha wanafanya kazi zaidi na kuwa na matokeo chanya katika ufundishaji.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti hizi zinatueleza changamoto ya hali ya motisha kwa walimu lakini pia umuhimu wa motisha katika ufanisi wa walimu. Hata hivyo, Serikali imekuwa haiichukulii kada hii ya ualimu kwa uzito unaostahili hasa

kurejesha hamasa kwa walimu katika kazi yao. Nasema hivi kwa sababu kada hii inaidai Serikali mabilioni ya fedha lakini Serikali haioni kama hili ni tatizo nan a kulipa kipaumbele zaidi ya hadithi ya uhakiki wa madeni isiyoisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT); takribani walimu wastaafu 1097 wanaidai serikali kiasi cha shilingi bilioni 138. Madai hayo ni ya mafao ya michango yao katika mfuko wa hifadhi ya jamii wa PSPF pamoja na pensheni. Deni hili ni la serikali kwakuwa PSPF imeshindwa kuwalipa walimu wastaafu kutokana na Serikali kutopeleka fedha za wastaafu hao katika mfuko huu. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenga fedha katika bajeti hii za kulipa mafao haya PSPF ili hatimaye walimu wastaafu waweze kulipwa stahili zao.

**Mheshimiwa Spika,** walimu waliopo kazini wameendelea kuisoma namba kutokana na kutolipwa madeni wanayoidai Serikali. Hali zao zimeendelea kuwa mbaya licha ya kwamba wamekuwa wakiibeba CCM katika chaguzi mbalimbali. Kwa mujibu wa CWT, takribani walimu 80,000 waliopandishwa madaraja kati ya Februari na Machi 2016 bado wanaidai serikali zaidi ya shilingi bilioni 200 ikiwa ni malipo ya malimbikizo ya ongezeko la mshahara kutokana na kupandishwa daraja.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya kulipa madeni hayo, na ni lini itayalipa?. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwapa taarifa ya maandishi walimu wote wenye madai yaliyokataliwa na sababu za kukataliwa ili waweze kupata nafasi ya kukata rufaa ili wapate haki yao.

## 5. UTOAJI HAFIFU WA RUZUKU YA ELIMU SHULENI (CAPITATION GRANTS)

**heshimiwa Spika,** utoaji wa ruzuku ya elimu kwa shule za msingi na Sekondari umeendelea kudorora siku hadi siku. Kama inavyojulikana, shule za msingi zinatakiwa kupewa ruzuku ya shilingi 10,000/= kwa kila mwanafunzi kwa ajili ya

kugharamia gharama za uwekezaji kama ujenzi wa miundombinu na vifaa vya kufundishia. Aidha, shule za sekondari serikali zilipaswa kupewa ruzuku ya shilingi 25,000 kwa ajili hiyo pamoja na kufidia ada ya shilingi 20,000/= kwa shule za kutwa na shilingi 40, 000/= kwa shule za bweni.

**Mheshimiwa Spika,** utafiti uliofanywa na Shirika la HakiElimu mwaka 2016 juu ya utekelezaji wa elimu bure, ni kwamba; shule za msingi zilipokea wastani wa shilingi 500 kwa mwezi kwa kila mwanafunzi ambayo ni sawa na shilingi 6,000/= kwa mwaka kwa kila mwanafunzi. Takriban asilimia 94 ya wakuu wa shule waliohojiwa walithibitisha kuwa kiwango cha ruzuku cha shilingi 6,000/= kwa mwaka kwa kila mtoto hakitoshi kugharamia mahitaji yote ya shughuli za utawala, gharama za mitihani na ukarabati wa miundombinu na manunuzi madogo madogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ruzuku ya elimu kwa shule za msingi na sekondari kuwa ndogo na kutotolewa kwa utoshelevu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya marekebisho ya viwango vya ruzuku ya sasa ambayo haikidhi uwezo wa manunuzi ya mahitaji ya shule. Kimsingi ruzuku ya Tsh 10,000 ilipangwa mwaka 2001 ikimaanisha dola 10 wakati huo dola 1 ilikuwa Tsh 1,000. Hivi sasa dola 1 ni Tsh 2,250 lakini bado serikali imeendelea kupanga Tsh 10,000 tu ilihali gharama za manunuzi zimepanda.

Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuongeza kiwango hiki cha ruzuku kufikia angalau Tsh 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa shue za msingi na Tsh 50,000 kwa shule za sekondari, na pia kutenga fedha hizi na kuhakikisha zitatolewa kwa asilimia 100.

## 6. SAKATA LA VYETI VYA KUGHUSHI

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 28 Aprili 2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokea taarifa na orodha ya watumishi ambao wamekutwa na vyeti vya kughushi baada ya ukaguzi kutoka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Angela Kairuki.

**Mheshimiwa Spika**, siku ya kukabidhiwa kwa taarifa hiyo, umma wa watanzania ulijulishwa kuwa watumishi 9,932 katika utumishi wa umma wameghushi vyeti vyao vya kitaaluma. Aidha umma ulijulishwa kuwa takribani watumishi 1,538 vyeti vyao vinatumika zaidi ya mara moja na pia idadi ya watumishi 11,596 wana vyeti vya utaalamu bila vyeti vya taaluma.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa hiyo Rais aliagiza wote ambao imethibitika kuwa wameghushi vyeti vyao vya taaluma waondolewe katika orodha ya malipo ya watumishi wa umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi msimamo wake kuwa haiungi mkono matumizi ya vyeti vya kughushi katika utumishi wa umma na hata katika sekta binafisi nchini. Ni lazima kama Taifa tukubaliane kuwa matumizi ya vyeti vya kughushi yanarudisha nyuma ufanisi katika utendaji kazi katika sekta zote ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi kuwa zoezi la uhakiki lilikuwa na mapungufu kadhaa ambapo inaweza kupelekea baadhi ya watu kutotendewa haki. Mathalani baadhi ya taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, ni kuwa zoezi halikuzingatia watumishi ambao wakati uhakiki unafanyika walikuwa likizo, wagonjwa, waalim waliajiriwa katika mpango wa UPE, waliokuwa masomoni au waliokuwa nje ya vituo vya kazi. Hivyo, kitendo cha mtumishi kutokuwepo katika kituo chake cha kazi na kuwasilisha nakala halisi ya cheti (original certificate) kulihesabiwa kuwa mtumishi huyo ana cheti cha kughushi jambo ambalo limewaathiri watumishi wengi ambao wana vyeti halisi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa wanafanya uamuzi mapema wa rufaa zilizoombwa na watumishi ambao kwa namna moja ama nyingine wameona kuwa hawajatendewa haki. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kufanya

uchunguzi wa watumishi wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) na Wizara ya Elimu ambao wamekuwa wakijihusisha na shughuli haramu ya kughushi vyeti kwa watu wasio na sifa, kwa ajili ya kujipatia fedha na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa Serikali ina vyombo vya Ulinzi na Usalama, na kimsingi walikuwa wanafahamu uwepo wa vyeti vya kughushi kwenye utumishi wa umma, lakini hatua zilichelewa kuchukuliwa kutokana na uzembe ndani ya serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa matumizi ya cheti cha kughushi ni kosa la jinai na watumishi waliohusika na sakata hili walifanya ubatili toka mwanzo na kwa hiyo hawawezi hata kulipwa shahiki zao hata kama wamefanya kazi kwa muda mrefu. Pamoja na utambuzi wa matakwa ya kisheria ya watumishi walioghushi vyeti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kuwa na jicho la huruma kwa watumishi waliokumbwa na kashfa hiyo kwa kuwalipa watumishi hao angalau michango yao waliyokuwa wamechangia kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ili waweze kuendelea kuishi wakati wakijipanga kutafuta maisha mahali pengine.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kabla ya usaili, waombaji wa ajira hutakiwa kupeleka vyeti vyao vya taaluma kwa mwajiri kama kigezo kimoja wapo cha kukidhi masharti ya usaili. Zaidi ya hapo mwajiriwa mpya hutakiwa tena kupeleka nakala ya vyeti vyake halisi (original certificates) kwa mwajiri kwa ajili ya uhakiki na hatimaye mwajiriwa huyo kuthibitishwa kazini.

**Mheshimiwa Spika,** haiwezekani katika hatua zote hizo, mwajiri asitambue mapungufu ya vyeti vya taaluma ya mwajiriwa wake kwa muda wote huo halafu mapungufu hayo yaje kutambuliwa na uhakiki huu uliofanyika hivi karibuni. Lazima kuna tatizo, ama la uzembe wa waajiri, au rushwa katika zoezi la uajiri. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi

ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwawajibisha waajiri wote ambao wafanyakazi wao wamekutwa na vyeti vya kughushi.

## 7. SERA YA MARUDIO (RE- ENTRY POLICY) KWA WANAFUNZI WALIOPATA MIMBA SHULENI

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko kubwa la mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na wale wa sekondari. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kimataifa la haki za binadamu (Human Rights Watch) ya mwaka 2016 ni kwamba, takribani wanafunzi 8,000 hushindwa kumaliza masomo kutokana na kupata mimba kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa sheria ya elimu ya mwaka 1978 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1995 na mwaka 2002 ilibainisha kuwa mtoto wa kike akipata mimba ni ushahidi tosha kuwa amefanya vitendo vya ngono ambavyo ni kinyume na shule hivyo afukuzwe shule. Pamoja na hayo mwaka 2016, Bunge hili liliridhia marekebisho ya kifungu cha 60 cha Sheria ya elimu (Education Act, Cap 353) na kuongeza kifungu cha 60 (A) kilichoweka katazo la kumpa mimba au kumuoa mwanafunzi wa shule ya msingi au wa sekondari. Kifungu hiki kilikwenda mbali zaidi na kuongeza adhabu hadi kufikia kifungo cha miaka 30 jela kwa mtu yoyote atakayepatikana na hatia ya kutenda kosa chini ya kifungu hiki.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na marekebisho hayo, sheria hii ya elimu haijatoa fursa kwa mwanafunzi kuendelea na masomo.Hii inaonyesha kwamba serikali ya CCM bado haitambui umuhimu wa mtoto wa kike kupata elimu, madhara ya muda mrefu ya kiuchumi na kijamii yanayoweza kutokea endapo mtoto huyu mwenye mtoto ataachwa bila kupata elimu ya kuweza kumsaidia yeye na yule atayemleta duniani.

**Mheshimiwa Spika**, wataalamu pamoja na takwimu mbalimbali zinaonyesha kuwa mwaka mmoja tu wa masomo unaweza kumuongea mtu umri wa kuishi kwa 0.18%, kukosa elimu kunaweza kumpungumzia mtu fursa ya ajira, kunaongeza uwezekano wa kupata maradhi mbalimbali, kunaongeza umaskini kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** nchi mbalimbali Barani Afrika zimelichukulia suala hili kwa uzito, na tayari nchi ya Zambia, Kenya, Rwanda, Malawi na nyinginezo zimekuwa mfano mzuri katika kuwasaidia watoto hawa na matokeo mazuri yameanza kuonekana. Badala ya watoto hawa kuonekana mizigo katika familia na jamii, serikali hizo zimeweka mfumo mzuri wa kuwasaidia kupata elimu huku watoto wao wakiendelea kupata msaada kutoka kwenye familia au jamii kwa muendelezo mzuri wa malezi na makuzi.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo mwezi Februari 2017, Mheshimiwa Mama Magreth Sitta (Mb) aliuliza swali la nyongeza ndani ya Bunge hili, kutaka kujua mpango wa serikali katika kuwasaidia watoto wa kike waliopata mimba wakiwa mashuleni akitolea mfano wa Zanzibar, Zambia na Kenya jambo lililoungwa mkono kwa makofi na wabunge wengi. Katika majibu ya Naibu Waziri wa Elimu alisema kuwa, serikali imeandaa muongozo utakaofuatwa na wadau mbalimbali ili kuwawezesha wasichana waliopata mimba kuweza kuendelea na masomo. Mheshimiwa Naibu Waziri, alilihakikishia Bunge kuwa mpaka Mwezi Machi, 2017 mpango huo utakuwa umekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mpango huo wa serikali umefikia wapi? Na je, ni lini serikali itauleta mpango huo ndani ya Bunge hili ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupata fursa ya kuufahamu na hata kuutungia sheria ili uweze kutekelezwa vizuri na hivyo kuwasaidia maelfu ya mabinti ambao ndoto zao za kufuta ujinga zimezimika kwa sababu ya kupata mimba?.

## 8. UVUMBUZI NA UGUNDUZI KATIKA SAYANSI NA NA TEKNOLOJIA

### 8.1. Uwepo wa Sheria zinazodumaza kukua kwa Teknolojia Nchini

**Mheshimiwa Spika,** tunaishi katika dunia ambayo kila hatua ya maendeleo inasukumwa mbele na uvumbuzi na ugunduzi wa Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo, mazingira ya kuchochea uvumbuzi na ugunduzi nchini sio mazuri kutokana na sera na sheria zinazokinzana katika kukuza uvumbuzi na ugunduzi miongoni mwa wanafunzi kuanzia ngazi ya shule ya msingi, sekondari, vyuo vya ufundi na elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika,** wakati nchini Marekani, Kijana Mark Elliot Zuckerberg mwenye umri wa miaka 32 tu, ni bilionea mwenye utajiri wa dola za Marekani bilioni 58.6 kutokana na umahiri wake katika uvumbuzi, ugunduzi na matumizi ya TEHAMA, hapa kwetu Tanzania vijana wanaojaribu kuthubutu kutumia teknolojia hiyo wanatungiwa sheria ngumu na mwishowe wanaishia gerezani. Kijana huyu wa kimarekani ni programa wa compyuta na mjasiriamali wa wavuti (internet) na mwanzilishi wa mtandao wa kijamii wa Facebook.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Marekani inajivunia kuwa na kijana aliyevumbua teknolojia ya mtandao wa mawasiliano wa Facebook, hapa nchini kwetu Tanzania, programa wa compyuta na mwanzilishi wa mtandao wa Kijamii (JamiiForums) Maxence Melo amefunguliwa kesi ya makosa ya kimtandao (cyber crime) chini ya Sheria kandamizi inayodumaza uvumbuzi na ugunduzi katika TEHAMA, badala ya kusaidiwa ili aendelee kuvumbua zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe maelezo ni kwa nini inatunga sheria kama hii ya Cyber Crime, ambayo inatumika kudumaza uvumbuzi, ubunifu na kurudisha nyuma sekta ya TEHAMA hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka pia Serikali kuipitia upya Sheria ya Cyber Crime na sheria zote zinazuia ubunifu na ujasiriamali katika Sayansi na teknolojia, ikiwa ni pamoja na kubaini maeneo yote katika sheria hizo

yanayozuia kukua kwa sayansi ya teknolojia hasa TEHAMA na kuzileta sheria hizo ndani ya Bunge lako tukufu ili zifanyiwe marekebisho stahiki.

### 8.2. Matamko yasiyoendana na Sera za Teknolojia

**Mheshimiwa Spika,** wakati sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996, katika ukurasa wa 7 inaelekeza Tanzania kutumia washauri wataalamu (Consultants) wa Sayansi na Teknolojia kutoka ndani kufanya shughuli za kiteknolojia, Mkuu wa Nchi, alinukuliwa na gazeti la The Citizen la tarehe 2 Julai, 2016 kuwa amekubaliana na Rais Paul Kagame wa Rwanda kupewa Wataalamu wa TEHAMA kutoka Rwanda ili kusuka mifumo ya kukusanya kodi hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, suala la kuazima wataalamu wa TEHAMA kutoka Rwanda sio tu linaidhalilisha Tanzania kuwa haizalishi wataalamu wa TEHAMA lakini pia ni ujumbe unaotumwa na Serikali ulimwenguni kuwa Tanzania haina wataalamu wa TEHAMA wenye uwezo wa kusuka mifumo imara ya kukusanya kodi jambo ambalo sio sahihi kwa kuwa nchi yetu ina vijana wenye uwezo wa kufanya hizo kazi isipokuwa Serikali haijawapa nafasi kuonesha uwezo wao.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na kuwa suala hilo linaitweza nchi lakini pia, suala hilo linaonesha kuwa matamko ya Serikali yanakwenda kinyume na maelekezo ya Sera ya Taifa ya Sayansi ya Teknolojia inayotaka nchi iwape fursa vijana kutoka ndani katika kazi zote za utaalamu ushauri (consultancy) kuhusu sayansi na teknolojia.

## 9. MATATIZO YA VITABU VIPYA VYA TAASISI YA ELIMU TANZANIA

**Mheshimiwa Spika,** Vitabu ni nyenzo muhimu sana katika utoaji hasa katika kipindi hiki chenye uhaba mkubwa wa walimu. Vitabu visipotungwa kwa ubora ni sumu mbaya sana kwa elimu hasa elimu shule ya msingi (awali hadi darasa la saba).

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya ELimu Tanzania imechapisha vitabu vipya vya kiada kwa shule za msingi kama ifuatavyo:

**A. Vitabu vya Darasa la Kwanza**

i. Najifunza Kuhesabu Darasa la Kwanza
ii. Najifunza Kusoma, Kitabu cha Kwanza
iii. Najifunza Kusoma, Kitabu cha Pili
iv. Najifunza Kuandika
v. Najifunza Afya na Mazingira
vi. Najifunza Michezo na Sanaa

**B. Vitabu vya Darasa la Pili**

vii. Najifunza Kuhesabu, Darasa la Pili

**C. Vitabu vya Darasa la Tatu**

viii. I Learn English Language

**Mheshimiwa Spika,** vitabu hivyo vina mapungufu makubwa ambayo yasiporekebishwa yanaweza kusababisha madhara makubwa katika utoaji wa elimu, na hivyo kushusha ubora wa elimu yetu. Miongoni mwa mapungufu au matatizo ya vitabu hivyo ni kama ifuatavyo:

- **Kutokuchapishwa Kiongozi cha Mwalimu**

**Mheshimiwa Spika,** maelekezo ya Wizara ya Elimu ni kuwa Mchapishaji wa Kitabu cha Kiada kwa shule za Msingi na Sekondari anawajibika kuchapisha Kitabu cha Mwanafunzi na Kiongozi cha Mwalimu kwa pamoja. Vitabu vyote 8, katika orodha niliyoitaja hapo juu, havina viongozi vya walimu. Madhara ya kukosekana kwa viongozi vya walimu yanajulikana (walimu kutokupatiwa maelekezo na ufafanuzi kuhusu njia/mbinu za ufundishaji wa somo).

**Mheshimiwa Spika,** kosa jingine katika uchapishaji wa vitabu hivyo ni kwamba; kwa baadhi ya vitabu hivi vya wanafunzi mchapishaji ameingiza mambo ambayo yalistahili kuingizwa kwenye kiongozi cha mwalimu. Haya ni makosa makubwa.

Mifano ya maelekezo hayo yako katika vitabu vya: *Afya na Mazingira* (Malengo ya Sura). *Michezo na Sanaa* (Malengo ya Sura na mwisho wa kitabu ameandika "Waelekeze watoto waigize maigizo hayo"). Pia katika kitabu cha *Najifunza Kusoma* kurasa za mwanzo zina maelekezo ambayo hayamhusu mtoto kwa kuwa bado hajafundishwa kusoma. Hali kadhalika ufafanuzi uliopo katika *Najifunza Kuhesabu*, Darasa la 2, mfano uk. 19, 27, 33 n.k. ulitakiwa uwe kwenye Kiongozi cha Mwalimu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzanzani Bungeni inaitaka Serikali kuzuia matumizi ya vitabu hivyo shuleni kwa kuwa uchapishaji wake haukuzingatia maelekezo ya Wizara ya Elimu.

- **Usanifu wa Vitabu**

**Mheshimiwa Spika,** usanifu (ubunifu katika kupanga kurasa za kitabu, picha zake na maandishi n.k.) ni wa hali ya chini sana. Kwa mfano, Jina la kitabu, kwa kawaida lina maana maalum ya jinsi ufundishaji unavyotekelezwa katika kitabu hicho pamoja na vingine katika mfululizo wa vitabu vya somo. Mfululizo huu wa jumla kwa vitabu vyote. Najifunza Kusoma/Kuandika/Kuhesabu kwa madarasa yote hauna msukumo au mvuto kwa walimu na wanafunzi na haumshawishi mwalimu kuzingatia mtindo fulani katika ufundishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Kiingereza, ***I Learn English Language***, (kwanza, siyo jina sahihi maana tafsiri yake ni: Huwa Najifunza Lugha ya Kiingereza) na pia haitoi ishara yoyote ya jinsi mwandishi/mchapishaji anavyotaka Kiingereza kifundishwe.

**Mheshimiwa Spika,** upangaji wa kurasa za kitabu ni jambo muhimu sana. Katika vitabu hivi jambo hilo halikuzingatiwa, kwa ujumla. Mfano, kuna picha ziko ndani ya kitabu cha *Najifunza Kusoma*, Darasa la Kwanza ambazo hakuna maelekezo kwa mwanafunzi kuwa afanye nini na hizo picha, kwa mfano kurasa za 71, 79, 83, 87, 95 n.k. Aidha, sehemu mbalimbali za vitabu, mwandishi/mchapishaji amefanya '***highlighting'*** isiyo na sababu maalum kiasi kwamba kitabu kinaonekana hakina mpangilio maalumu k.m. Najifunza Kusoma Darasa la Kwanza.

- **Picha za vitabu hivi**

**Mheshimiwa Spika,** suala la picha lina uhusiano na usanifu. Lakini tunalipa uzito wa pekee kutokana na hali ilivyo ndani ya vitabu hivi.

(a) Majalada ya vitabu kwa kawaida, yanastahili kuwa na picha mojawapo kati ya picha zilizomo ndani ya kitabu. Majalada yote yana matatizo ya picha, kwa mfano:

- *Najifunza Kusoma*, Kitabu cha Kwanza – picha ya jalada ni ya mwalimu na mtoto. Mtoto huyo, ni yule mwenye tabia mbaya ya kutoroka shuleni katika 'hadithi' iliyo katika kitabu cha *Najifunza Kusoma*, Kitabu cha Pili.

- *Najifunza Kuhesabu*, Darasa la 1 kina picha ya jalada ambayo ina namba za awali (zisizokubalika) na alama za kihisabati ambazo mwanafunzi bado hajajifunza.

- *Najifunza Kuandika*, Darasa la Kwanza kina picha ya mtoto anaandika a b c ambayo ni alfabeti ya Kiingereza. (Kumbuka kitabu hiki ni cha kujifunza kuandika Kiswahili).

- Majina ya Vitabu vyote vya Darasa la Kwanza yametumia herufi za Times Roman ambazo haziruhusiwi kwa madarasa ya kwanza, pili na tatu. Pia vitabu vyote vimetumia tarakimu 9 ambayo pia, haikubaliki kwa ngazi hii ya elimu.

- Kwa *Najifunza Kuhesabu* Darasa la 2, jalada lina hesabu iliyoko ukurasa wa 15 wa kitabu hicho badala ya picha ya kuvutia. Jambo hili ni la ajabu na halina mvuto wowote.

- Kwa Kiingereza (Darasa la 3) *I Learn English Language*, neno Language limeandikwa kwa maandishi makubwa zaidi badala ya English ambayo ndio somo

lenyewe. Pia *I Learn English Language* siyo Kiingereza sahihi (au tafsiri sahihi ya *Najifunza Kiingereza*).

(b) Picha za ndani ya vitabu

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla picha ndani ya vitabu hivi siyo nzuri.

- Picha ndani ya vitabu, hasa vya *Afya na Mazingira*, *Sanaa na Michezo* zimerudiwa mara kadhaa ndani ya vitabu hivyohivyo.

- Picha kukosekana hasa kitabu cha *Najifunza Kuandika* – Badala ya picha, mtoto anaelekezwa kuchambua Kiswahili na kujibu maswali magumu. Mwishoni anatakiwa kuandika insha ya kurasa mbili. Kitabu hicho hakifai zaidi ya vingine.

- Picha nyingi si nzuri hasa katika *Najifunza Kusoma* – Picha siyo angavu; zina rangi nyingi nyeusi na zinashindana na herufi zilizokuzwa kupita kiasi na za rangi mbalimbali. Hali hiyohiyo ipo katika *I Learn English Language*.

- **Kutokumjua mtoto**

**Mheshimiwa Spika,** liko tatizo kubwa kuhusu vitabu hivi linaloonyesha kuwa waandishi hawamjui vizuri mtoto (au hawamjali mtoto) wanayemwandikia. Mtoto wa Darasa la kwanza ni yule ambaye ama amesoma shule ya awali kwa mwaka mmoja au hajaenda shule kabisa. Kwa hali hiyo, mtoto huyu, kwa miezi ya mwanzo anatakiwa awe anasoma picha na neno mojamoja. Kusoma kwake kunazingatia sana alichosoma katika somo la Kiswahili, ambalo kwa makosa makubwa limegawanywa vipande viwili, yaani Kusoma na Kuandika.

**Mheshimiwa Spika,** picha anazosoma mtoto katika miezi ya mwanzo hazina budi kuwa nzuri, sahili na zenye mvuto na ziwe ni za vitu ambavyo mtoto anavyo katika mazingira yake. Maneno yanaongezeka taratibu sana hasa baada ya mtoto

kujifunza na kutambua alfabeti ya Kiswahili (kwa herufi ndogo na baadaye herufi kubwa). Masomo mengine, lazima yawe yamezingatia hali hii ya mtoto. Kwa hiyo, vitabu vinavyoanza kwa maelezo marefu vinadhihirisha kuwa mwandishi/ mchapishaji "hamjui mtoto anayemwandikia kitabu". Mifano ni vitabu vya Darasa la Kwanza vya *Najifunza Kusoma, Kuandika, Kuhesabu, Afya na Mazingira na Michezo* na *Sanaa*.

**Mheshimiwa Spika,** mwalimu mzuri wa Darasa la Kwanza atashangaa kuona vitabu hivi vinavyomwanzisha mtoto kwa kuyafanya masomo yawe magumu kuliko uwezo wake. Bila shaka atajaribu kutafuta njia nyingine za kuwasaidia watoto ili waweze kuelewa na kuendelea vizuri na elimu yao ya msingi.

- **Makosa ya lugha**

Mheshimiwa Spika, Vitabu hivi vina makosa mengi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Pia makosa yamekithiri kuhusu matumizi ya herufi kubwa na ndogo na matumizi ya nukta pacha (colon). Matatizo hayo yamo kwenye vitabu vyote hasa *Najifunza Kusoma, Kuandika, Kuhesabu, Afya na Mazingira, Michezo na Sanaa.*

Kwa mfano, Kitabu cha *Najifunza Kusoma*, Darasa la Kwanza uk 99 kinataja "kucha" kikimaanisha **ukucha**. Pia *Najifunza Kuhesabu* uk 19 kujumlisha bila kubadili kwa wima (badala ya kujumlisha kwa wima bila kubadili) uk 93 na 94 – maneno chupa/chupa ya chai (yakichanganywa).

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu kitabu cha *I Learn English Language*, matatizo ya matumizi ya herufi kubwa na ndogo na colon ni mengi mno – karibu kila ukurasa. Inaelekea pia kuwa mwandishi hana uwezo wa kutosha wa lugha yenyewe kwani kuna makosa mengi ya lugha hiyo ya Kiingereza. Ni vigumu kupata ukurasa mmoja wa kitabu hicho ambao hauna makosa. Kwa mfano,

P 16 – These are my parent.

P 35 – .... writing letters of English alphabet.
P 61 – Which is long between a pen and a ruler?
P 127 – Look at the insects: (There are 11 pictures of i nsects which also include a spider, a flower and a millipede)
P 128 – It catches mosquito.
P 129 – He sleeps without mosquito net.
P 130 – It eats grasses
P 138 – The driver is taken the police station.
P 141 – A boy is on bed at hospital.
P 143 – Which is the big city of Tanzania (meaning Capital City).
P 145 – In which class Mainda is?
P 145 – What village do they live?
P 146 – Write down how do you great your teacher in the morning

- **Ucheleweshaji wa vitabu**

**Mheshimiwa Spika,** vitabu vya Darasa la Kwanza vilichelewa sana kuchapishwa na kuwasilishwa shuleni. Hata hivyo, baada ya hekaheka nyingi za kuchoma nakala zilizokuwa na makosa ya mchapishaji, baadhi ya vitabu vya Darasa la Kwanza vilitoka mwezi Juni 2016 na baadhi mwezi Januari 2017. Kitabu kimoja tu cha Darasa la Pili kimetoka mwaka huu wa 2017 na kingine cha Kiingereza, Darasa la Tatu, *I learn English Language*. Kwa hali hiyo ya utoaji wa vitabu vipya na ucheleweshaji, waalimu na wanafunzi watapata shida kubwa kuutumia mtaala mpya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mapungugu hayo yote, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuzuia matumizi ya vitabu hivyo vyenye makosa shuleni, na pia kuiagiza taasisi ya Elimu kufanya marekebisho ya makosa yaliyopo kwenye vitabu hivyo na kuvichapisha upya. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya uhakiki wa taaluma na weledi wa watumishi wa Taasisi ya Elimu Tanzania, ili kujiridhisha kama wana sifa stahiki, uwezo na weledi katika kufanya kazi ya utunzi wa vitabu. Kambi ya Upinzani inapendekeza hivyo kwa kuwa, Serikali inapata hasara

kubwa kurudia kuchapisha vitabu hivyo kutokana na uzembe wa watumishi wanaohusika na kazi hiyo au watumishi wasio na utaalam katika kazi wanayoifanya. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa, utaratibu wa zamani urejewe ili vitabu hivi ambavyo ni nyenzo muhimu kwa watoto kujifunzia usanifiwe na chombo kingine ili kudhibiti ubora.

## 10. USIMAMIZI DUNI WA SEKTA YA ELIMU NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na usimamizi duni wa sekta ya elimu na hususan maendeleo ya walimu nchini jambo ambalo linayumbisha sekta ya elimu. Usimamizi huo duni untokana na kukosekana kwa chombo kimoja chenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala ya elimu yakiwemo maendeleo ya walimu nchini. Matatizo yanayohusu elimu na hususan madai ya walimu yamekuwa yakishindwa kutatuliwa kikamilifu kutokana na kuwepo kwa taasisi kadhaa zinazoshughulika na masuala ya walimu jambo ambalo linaleta mkanganyiko juu ya nani hasa mwenye mamlaka juu ya walimu.

**Mheshimiwa Spika,** katika hotuba zangu za miaka ya nyuma nilieleza kuwa ili kuondoa mkanganyiko uliopo kutokana na kuwepo kwa taasisi mbali mbali kusimamia elimu – yaani Wizara ya Elimu, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kwa wakati huo na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuanzisha chombo kimoja kitakachoshughulikia masuala hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza ianzishwe Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Tanzania Education and Training Regularity Authority – TETRA) ili masuala yote ya udhibiti wa utoaji wa elimu pamoja na kushughulikia masuala ya walimu yaratibiwe na chombo hicho.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa ushauri huo, Serikali ilianzisha Tume ya Utumishi wa Walimu (Teacher's Service Commission) badala ya mamlaka ya udhibiti wa Elimu na Mafunzao ya Ufundi kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani mapema kabisa wakati wa kujadili muswada wa sheria ya kuanzisha tume

hiyo, ilisema kwamba Tume hii iliazishwa kukidhi maslahi ya kisiasa yaliyolenga kupata kura za walimu katika Uchaguzi Mkuu wa 2015, ahadi kwamba, matatizo ya walimu yangekuwa historia kwa kuanzishwa kwa tume hiyo. Leo ni takriban miaka miwili tangu Uchaguzi Mkuu ufanyike, lakini matatizo ya walimu yamebaki pale pale na katika maeneo mengine yameongezeka zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi Tume ya Utumishi wa Walimu haijasaidia hata kidogo kutatua kero za walimu. Kwanza muundo wake una matatizo. Ukitoka ngazi ya Taifa (Makao Makuu) tume hiyo ina matawi Wilayani tu. Hakuna matawi ngazi ya Mkoa. Matokeo yake, hakuna ngazi ya Taifa inazidiwa na kazi kwa kuwa hakuna ngazi ya mkoa ambayo ingeweza kuchambua matatizo ya walimu katika mkoa husika na kuwasilisha taifani.

**Mheshimiwa Spika,** jambo la pili, licha ya tume hii kupewa hadhi ya mwajiri lakini haifanyi kazi za mwajiri. Majukumu ya mwajiri ni pamoja na kuajiri, kulipa mishahara, kupandisha madaraja, kufukuza n.k. Katika majukumu hayo ya mwajiri; Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka ya kuajiri wala kulipa mishahara – mwenye mamlaka hayo ni Mkurugenzi wa Halmashauri (DED); Tume ya Utumishi wa Walimu haina mamlaka ya kupandisha madaraja ya walimu – mwenye mamlaka hayo ni Mkurugezi wa Halmashauri pia.

**Mheshimiwa Spika,** matatizo ya msingi ambayo walimu wamekuwa wakiyalalamikia siku zote ni kuhusu kupandishwa madaraja na kupandishwa mishahara mambo ambayo tume ya utumishi wa walimu haina mamlaka nayo. Kwa hiyo, tume hiyo haitegemewi kuwasaidia walimu kwa namna yoyote ile.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sababu hiyo, bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuanzishwa kwa Mamlaka ya udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (TETRA) ili kuweza kuondoa mkanganyiko huu wa usimamizi wa utumishi wa walimu.

### 11. HALI YA UFAULU KWA SHULE ZA SEKONDARI NA MSINGI ZA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na tatizo la muda mrefu la ufaulu hafifu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za Serikali hapa nchini. Kutokana na hali hiyo, Serikali kwa nyakati tofauti iliunda tume mbalimbali kuchunguza sababu za kushuka kwa ufaulu ingawa mara zote haikuweka hadharani ripoti za uchunguzi huo. Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya elimu walihusisha ufaulu hafifu na sababu mbalimbali yakiwemo mazingira yasiyo rafiki katika kufundisha na kujifunza. Miongoni mwa mifano halisi ikiwa umbali mkubwa kati ya makazi ya watu na zilipo shule, upungufu wa walimu, upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, miundombinu mibovu katika shule, ukosefu wa chakula shuleni, ukosefu wa nishati ya umeme shuleni, morali iliyoshuka kwa upande wa walimu kutokana na madai mbalimbali n.k.

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni, wakati Waziri wa TAMISEMI anahitimisha mjadala wa bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, aliwaambia waheshimiwa wabunge kuwa;

*"Tunaambiwa elimu ya Tanzania inashuka, sijui wanatumia takwimu gani, lakini kinachoweza kutusaidia kujua inapanda au inashuka ni matokeo ya mitihani. Kama kipo kigezo kingine, labda ni baadaye," alisema na kutoa takwimu za ufaulu wa kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha sita. Alisema ufaulu darasa la 4 kwa mwaka 2014 ulikuwa asilimia 64, lakini mwaka 2016 umefikia asilimia 93, upande wa darasa la 7 ufaulu kwa mwaka 2012 ulikuwa asilimia 33 na sasa umefikia asilimia 70 ilhali kwa kidato cha pili, ufaulu umepaa kutoka asilimia 57 mwaka 2012 hadi asilimia 91. Kwa kidato cha nne ufaulu kwa sasa ni asilimia 70 kutoka 45 za mwaka 2012. Na kidato cha sita, ufaulu wake unatisha, karibu wote wanafaulu. Mwaka 2012 ufaulu wao ulikuwa asilimia 88 na sasa ni asilimia 99. Asanteni sana walimu wa Tanzania, tunawashukuru sana".*

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa ufaulu ni matokeo ya mambo mengi kama nilivyoeleza hapo awali, na kwa kuwa kulikuwa

na changamoto kadhaa zilizosababisha ufaulu hafifu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama changamoto hizo zimetatuliwa zote ndio maana ufaulu unaongezeka au kuna jambo gani limefanyika kupandisha ufaulu huu, ukizingatia shule bado zina mazingira duni ya kufundishia na asilimia kubwa ya walimu hawafundishi kama nilivyosema hapo awali.

## 12. MIUNDOMBINU KATIKA VYUO VYA ELIMU YA JUU

### 11.1. Ukarabati wa Miundombinu chakavu

**Mheshimiwa Spika,** vyuo vya elimu ya juu hasa vile vikongwe vinakabiliwa na tatizo la uchakavu wa miundombinu yake hususani uchakavu wa majengo. Hata hivyo, matengenezo au ukarabati wa miundombinu hiyo, kwa kiwango kikubwa haujafanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Kutokana na hali hiyo, kuna baadhi ya mabweni katika baadhi ya vyuo vya elimu ya juu yamechakaa vibaya kiasi cha kutishia usalama wa wananafunzi wanaoishi humo. Aidha, baahi ya mabweni yamefungwa kabisa kutokana na uchakavu uliokithiri. Mojawapo ya bweni lililofungwa kutokana na uchakavu ni Bweni Namba 2 (Hall Two) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge ina mpango mkakati gani wa ukarabati wa miundombinu chakavu katika vyuo vya elimu ya juu, na imetenga bajeti kiasi gani katika mwaka wa fedha 2017/18 kutekeleza mpango huo?

### 11.2. Ujenzi wa Miundombinu Mipya

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaunga mkono ujenzi wa mabweni (hostels) unaofanywa na Serikali katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuwa ujenzi huo utawasaidia takriban wanafunzi 4,000 kupata malazi ndani chuo. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa ufafanunzi wa gharama zilizotumika kujenga mabweni hayo, kwa kuwa kwa uzoefu na mtazamo wa kawaida tu gharama ya shilingi bilioni 10 kujenga majengo 20 ya ghorofa tatu kila moja ni ndogo jambo ambalo linazua

wasiwasi kwamba pengine gharama hiyo imetajwa kukidhi matakwa ya kisiasa.

**Mheshimiwa Spika,** jambo jingine ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani inatilia shaka katika ujenzi wa mabweni hayo, ni bajeti ya ujenzi huo. Kama ilivyo ada, fedha zote za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Jamhuri ya Muungano, huidhinishwa na Bunge. Lakini hakuna hakuna kumbukumbu yoyote kama fedha zilizotumika kujenga majengo hayo ziliidhinishwa na Bunge. Kwa sababu hiyo, sheria ya bajeti ilivunjwa. Aidha, hakuna kumbukumbu zozote zinazoonyesha kama zabuni ya ujenzi wa majengo hayo ilitangazwa. Kwa maana hiyo, sheria ya manunuzi ilivunjwa pia.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mapungufu hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum (special audit) kuhusu uhalali na utaratibu uliotumika kujenga mabweni hayo na gharama halisi iliyotumika.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni kwa nini ilifanya uamuzi wa kukodi majengo ya NSSF (Mabibo Hostel) ambapo inalipa fedha nyingi ambazo zingeweza kutumika kujenga mabweni katika eneo la chuo kikuu ambalo bado ni kubwa? Pia wanafunzi wanapata shida kubwa sana ya usafiri kwani hivi karibuni mabasi yanayowasafirisha wanafunzi kutoka hostel kwenda main campus (shuttles) yalizuiliwa na hivyo kufanya vijana wetu kukosa mihadhara jambo ambalo limewaathiri sana hasa kipindi hiki wanapojiandaa na mitihani ya chuo kikuu (University Exams).

**13. HOSPITALI YA MAFUNZO MLOGANZILA**

**Mheshimiwa Spika,** hospitali hii imejengwa kwa viwango vya hali ya juu sana, na ina vifaa tiba vya kisasa vyenye teknolojia ya juu sana, lakini cha kusikitisha hakuna majengo yoyote ya watumishi, jambo linalopelekea watumishi hao ambao wengi wao wako Muhimbili kusafiri umbali wa takriban kilometa 60 kwenda na kurudi huku tukijua kuna tatizo kubwa la usafiri Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hali hiyo, bado kuna upungufu mkubwa wa watumishi/ wataalam kwa kuwa vibali vya kuajiri bado havijatoka. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafanya kila liwezekanalo, ili hospitali hii ianze kazi kwa kuwa itatatua matatizo makubwa ya afya hapa nchini. Licha ya kutatatua matatizo ya afya, hospitali hii italiingizia taifa mapato kutokana na ubora wake. Tunamshauri Rais, atoe vibali vya ajira ili jengo lile lisibaki kuwa *'White Elephant'*

## 14. MIKOPO YA ELIMU YA JUU

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako tukufu lilipitisha muswada wa mabadiliko ya sheria mbalimbali namba 03 wa mwaka 2016 ambapo pamoja na mambo mengine sheria hiyo ilifanyia marekebisho kifungu cha 19 na 20 cha sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Baada ya marekebisho kifungu cha 19(3) kinaweka sharti kwa wote walionufaika na mkopo wa elimu ya juu kuanza kulipa madeni yao miaka miwili baada ya kumaliza masomo pamoja na kuwa wanufaika hao wanaweza kuanza kulipa madeni yao mapema kadri iwezekanavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 20(1)(c) baada ya marekebisho kimeongeza kiwango cha makato ya kila mwezi kwa wadaiwa wa mikopo kutoka asilimia nane (8) za awali hadi asilimia kumi na tano (15). Ikumbukwe kuwa mara baada ya muswada kuridhiwa na Bunge lako tukufu serikali ilianza mara moja utekelezaji wa masharti haya bila kuchelewa.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa matakwa haya ya sheria unaenda kinyume na misingi ya kisheria, kwa sababu ingetakiwa utekelezaji wake usiwaathiri wale ambao tayari walishaingia mikataba ya Bodi ya mikopo kwa makato ya asilimia nane kila mwezi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kukiuka msingi huo wa kisheria, ifahamike kuwa wengi wa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wako katika utumishi wa umma kwa maana

ya kuwa ni watumishi wa serikali. Serikali na Bunge lako tukufu watakuwa mashahidi kuwa watumishi wengi wa serikali wanakabiliwa na makato kadhaa katika mishahara yao, ikiwemo kodi ya mapato (PAYE), Chama cha wafanyakazi, mikopo kwa ajili ya kufanya shughuli binafsi za maendeleo, bima ya afya, makato kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Pamoja na makato hayo, serikali imekuja na utaratibu wa kukata mishahara hiyo kiduchu kwa asilimia kumi na tano (15) kwa ajili ya kulipa deni la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge hili sababu za kutekeleza mabadiliko hayo ya sheria huku ikijua kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mikataba ambayo wanufaika wa mikopo hiyo waliingia na Bodi kabla sheria husika haijabadilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa kwa sasa Bodi ya Mikopo inatoza riba kwenye mkopo kila mwaka. Kinachofanywa sasa na Bodi ya Mikopo ni kutoza riba kila mwaka kwa jina la gharama za kulea mkopo kila mwaka ambao mnufaika wa mkopo huo anaoshindwa kulipa! Kambi Rasmi Upinzani inahoji – Bodi ya mikopo imegeuka kuwa taasisi ya fedha inayotoza riba au inatoa huduma ya kusaidia kupatikana kwa elimu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali inadai kwamba mikopo ya elimu ya juu ni fedha za maendeleo kwa kigezo kwamba huo ni uwekezaji kwenye maendeleo ya rasilimali watu; na kwa kuwa fedha za maendeleo kwa miradi mbalimbali huwa hazidaiwi na Serikali, na kwa kuwa uwekezaji katika sekta ya elimu ni muhimu sana kwa kuwa uwekezaji huo unafungua fursa nyingine nyingi za kiuchumi kutokana na kuwa na rasilimali watu yenye weledi, Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuishawishi Serikali isiwadai wanafunzi wanaopewa fedha hizo kugharamia elimu ya juu kwa kuwa ni uwekezaji kama uwekezaji mwingine wa miradi ya maendeleo ambayo serikali hugharamia bila kudai kurudishiwa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika hotuba yangu mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni sababu ya Serikali kuwadai wahitimu wa vyuo vikuu kurejesha fedha waliyokopeshwa kugharamia elimu waliyoipata kwa sababu gharama hiyo wataifidia kupitia kodi ya mapato (Pay As You Earn) pindi watakapoajiriwa. Kodi hiyo itakuwa ndio faida (economic returns) ya kuwalipia wanafunzi wa elimu ya juu ambayo inachangia moja kwa moja kwenye pato la taifa na uchumi kwa jumla. Serikali itambue pia kwamba fedha inazowakopesha wanafunzi wa elimu ya juu inatokana pia na kodi waliyolipa wazazi wa wanafunzi hao.

## 15. MAJUKUMU YA TUME YA VYUO VIKUU (TCU)

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Vyuo Vikuu, pamoja na mambo mengine, ilianzishwa kwa madhumuni ya kufanya udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu pamoja na kusimamia ubora wa elimu ya juu. Kwa sababu hiyo, baada ya kuanzishwa kwake, Tume hiyo ilianzisha mfumo wa pamoja wa udahili (Centeral Admission System) ambao uliondoa matatizo yaliyokuwepo awali ya wanafunzi kudiliwa kwenye chuo zaidi ya kimoja ana ambayo yalipelekea wanafunzi kupata mkopo wa elimu ya juu zaidi ya mara moja kutegemeana na idadi ya udahili uliofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni, wakati Mheshimiwa Rais anafungua hostel mpya za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema kwamba Tume ya Vyuo Vikuu isishughulike tena na suala la udahili, ila ibaki tu na jukumu la kusimamia ubora wa elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba, kuiondoa TCU kwenye jukumu la udahili, kutaturudisha nyuma kwenye matatizo yale ya kudahiliwa kwenye chuo zaidi ya kimoja, na hatimaye kupelekea kupata mkopo wa elimu ya juu mara mbili au zaidi kutokana na idadi ya udhahili. Hata hivyo, kuna hatari ya kuporomoka kwa ubora wa elimu ikiwa vyuo vitaruhusiwa kufanya udahili vyenyewe. Hii ni kwa sababu kutokana na vyuo vingi

kujiendesha kibiashara, hasa vyuo binafsi, kuna hatari ya kuwapokea hata wanafunzi wasio na sifa kwa ajili ya kujipatia fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza, TCU haitaweza kudhibiti ubora wa elimu ya juu ikiwa udahili utakuwa unafanywa vyuo vyenywe. Udhibiti wa ubora utaweza kufanyika pale tu kuna chombo kimoja kinachosimamia suala zima la udahili, uandaajiwa mitaala (prospectus) na mwongozo wa namna ya ufundishaji, utahini na utoaji wa vyeti kwa wahitimu. Ukiachia mambo haya yakafanywa na taasisi mbalimbali – kwa manaa ya vyuo vyenyewe udhibiti hauwezi kufanyika kikamilifu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza TCU iendelee kufanya udhahili na kutekeleza majukumu yake mengine, kwa kuwa ziele sababu za kuanzishwa kwake bado zina maana.

## 16. UHABA WA WAHADHIRI KATIKA VYUO VIKUU

**Mheshimiwa Spika,** wanazuoni wa masuala ya elimu wanatoa tafsiri ya Chuo Kikuu kwamba: “***A University is an institution of higher learning where people’s minds are trained for clear thinking, for independent thinking, for analysis and for problem solving at the highest level, is the centre for advancing the frontiers of knowledge”***. Kwamba: Chuo Kikuu ni taasisi ya elimu ya juu inayoandaa watu kuwa na fikra pevu, fikra huru kwaajili ya kuwa na uwezo mkubwa wa kiuchambuzi na kwaajili ya kutatua matatizo kwa kiwango cha hali ya juu, ni kituo cha kuendeleza maarifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa tafsiri hiyo, ni dhahiri kuwa chuo kikuu kinatakiwa kuwa na wahadhiri wabobevu na wa kutosha ili kuweza kuakisi maana hiyo ya chuo kikuu. Jambo la kushangaza ni kwamba kumeanza kutokea tatizo la uhaba wa wahadhiri katika vyuo vikuu hapa nchini. Wachambuzi wanaeleza kwamba sababu ya uchache wa wahadhiri ni ongezeko la vyuo vikuu vipya ambalo limepelekea wahadhiri kuhamakutoaka vyuo vya zamani na kwenda kwenye vyuo vipya ama kwa kuteuliwa kushika nafasi za uongozi katika vyuo hivyo vipya au kutafuta mazingira bora zaidi ya kufanyika kazi ikiwemo kipato kikubwa zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** inaelezwa pia kwamba, teuzi mbalimbali zinazofanywa na Mkuu wa Nchi kwa wahadhiri wa vyuo vikuu kushika nafasi mbalimbali za kisiasa na kiutendaji serikalini kama vile wabunge wa kueuliwa, makatibu wakuuu na maafisa wengine serikalini zimesababisha kupungua kwa wahadhiri katika baadhi ya vyuo vikuu hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** inafahamika kwamba kumsomesha mhadhiri mpaka kufikia ngazi ya kupata shahada ya uzamifu (PhD) huchukua muda mrefu na si watu wengi hupenda kujiendeleza kufikia kiwango hicho. Mathalani, Tanzania kwa sasa ina wastani wa asilimia 25 ya wahadhiri wenye shahada ya uzamifu (PhD). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee kina asilimia 41 ya wahadhiri wenye shahada ya uzamifu. Uhaba wa wahadhiri umeathiri pia vyuo vikuu vingine kusini mwa jangwa la shahara isipokuwa vyuo hivyo vina nafuu zaidi ukilinganisha na chuo kikuu cha Dar es Salaam. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Botswana ni 65%, Chuo Kikuu cha Capetown 63%; Chuo Kikuu cha Ghana 50%; Chuo Kikuu cha Nairobi 46%; Chuo Kikuu cha Mauritius 42. Hivyo, pamoja na kwamba ninawapongeza wahadhiri walioteuliwa lakini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia vyuo vikuu kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kusomesha wahadhiri ili kusiwe na ombwe kunapofanyika uteuzi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa vyuo vikongwe kutoa motisha kwa wahadhiri wao ili wasipate tamaa ya kuhamia vyuo vingine kwa ajili kutafuta maslahi.

## 17. MATATIZO YA JUMLA YA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,** yapo matatizo mengi, yanayoikabili sekta ya elimu nchini. Hata hivyo, siwezi kuyazungumzia yote katika hotuba hii. Kwa hatua ya sasa nitataja tu baadhi ya matatizo au changamoto hizo, ili Serikali iweze kuyatolea maelezo wa namna ya kuyatatua. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

i. Malalamiko ya walimu kukatwa na bodi ya mikopo asilimia 15 ya mishahara yao wakati makubaliano yalikuwa asilimia 8.

ii. Upungufu wa vitabu vya masomo ya sanaa

iii. Ukosefu wa walimu masomo ya hisabati na sayansi

iv. Ukosefu mkubwa wa wataalam wa maabara ( laboratory technician) hasa kwa mkoa wa Dar es Salaam

v. Walimu kudhalilishwa kwa kushushwa vyeo na kupigishwa deki eti kwa sababu wanafunzi wamefeli.

vi. Kushuka kwa alama za ufaulu kuingia kidato cha kwanza (60 – 70 kati ya alama 250.

vii. Kubagua watoto kwa uwezo wao wa kitaaluma: wasiojiweza kitaaluma kukaa shule moja na wenye uwezo kuwa pamoja. Mfano wanaopata A wanapelekwa shule za kitaifa, wenye B shule za Mikoa, na C shule za kata.

viii. Walimu kukatwa asilimia 2 ya mshahara wao na CWT bila makubaliano na hawaoni msaada wa CWT.

ix. Madai ya walimu ya likizo, madaraja, nauli na kazi maalum.

## 18. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAENDELEO 2016/17

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Mwezi Machi 2017 serikali ilikuwa imetoa asilimia 34% tu ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ya bajeti ya Taifa, jambo ambalo limeathiri pia bajeti ya maendeleo ya sekta ya elimu. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Elimu iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 897.6 kama fedha za miradi ya maendeleo, lakini hadi Mwezi Machi 2017 ni shilingi bilioni 500.4 sawa na asilimia 55 ndizo zilikuwa zimetolewa kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mgawanyo wa fedha hizi, shilingi bilioni 427 (asilimia 48) ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na

shilingi bilioni 470 (asilimia 52) ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi halisi ya maendeleo ya sekta ya elimu inayotekelezwa na Wizara kama ujenzi wa miundombinu ya shule na vyuo.

**Mheshimiwa Spika**, hatari iliyopo katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya wizara ya elimu ni kuwa sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa mpaka mwezi Machi 2017 zilikuwa ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na sehemu kidogo kwa ajili ya miradi halisi ya maendeleo. Mathalani, kwa mujibu wa randama ya bajeti ya wizara ya elimu fungu 46 ya mwaka 2017/18, jumla ya fedha zilizokuwa zimeidhinishwa na bunge kwa ajili ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu ni shilingi bilioni 427. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Serikali ilikuwa imeshatoa shilingi bilioni 344 sawa na asilimia 80 ya fedha hizo. Kwa upande wa miradi halisi ya maendeleo hali ni tofauti. Fedha zilizoidhinishwa kwa miradi mingine ya maendeleo zilikuwa ni shilingi bilioni 470. Hadi kufikia mwezi machi, 2017, ni shilingi bilioni 156.4 pekee sawa na asilimia 30 tu ya fedha hizo zilikuwa zimetolewa na Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya randama ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kuanzia Julai 2016 hadi Machi 2017 imeainisha mapungufu makubwa katika utekelezaji wa bajeti ya miradi mtambuka ya Elimu iliyopangwa kutekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/17. Miradi hiyo ambayo utekelezaji wake umeathirika kutokana na kutolewa kwa bajeti pungufu ya maendeleo ni pamoja na Programu za Maji na Usafi shuleni (WASH), Programu za Uimarishaji wa mafunzo ya KKK chini ya LANES, bajeti ya Ukaguzi na kuimarisha ubora wa Shule.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya shilingi bilioni 186 zilizotengwa kwa ajili ya miradi mikuu ya maendeleo kwa wizara ya elimu ni shilingi bilioni 29 tu, sawa na asilimia 16 pekee ya fedha zilizoidhinishwa, ndizo zilitolewa hadi kufikia Machi 2017. Kwa mwenendo huu miradi hii haitakuwa imefikia walau asilimia 30 ya utekelezaji hadi mwisho wa Mwaka wa fedha wa 2016/2017. Hali hii ni hatari kwa shughuli za maendeleo ya sekta ya elimu na inaturudisha nyuma kwa kiwango kikubwa sana.

**19. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** Baba wa Taifa la Afrika ya Kusini; Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema kuwa ***"No country can really develop unless its citizens are educated"*** ikiwa na maana kwamba *"Hakuna nchi inayoweza kuendelea kama wananchi wake hawajaelimika"*

**Mheshimiwa Spika,** hata Kambi Ramsi ya Upinzani Bungeni, inaamini kuwa, elimu ndio kila kitu kwenye mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Changamoto karibu zote ambazo nimezieleza kwenye hotuba yangu zinahusiana moja kwa moja na changamoto za kisera, usimamizi wa elimu na mfumo wa upangaji na usimamizi wa bajeti ya sekta ya elimu. Tanzania kama Taifa tunahitaji kuelewa nini falsafa ya elimu yetu, nini malengo makuu ya elimu yetu na tuwe na mikakati ya kuhakikisha mfumo wa elimu yetu unalenga kutoa elimu jumuishi, elimu inayotoa fursa kwa watoto wote wa Tanzania kupata elimu bora na elimu inayolenga kumlinda n kumuendeleza mtoto. Elimu bora kwa kila mtoto wa Tanzania ndiyo itakayosaidia Taifa hili kupata maendeleo.

**Mheshimiwa spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Susan Anselm Jerome Lyimo (Mb)
**WAZIRI KIVULI NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KATIKA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**
13 Mei, 2017

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo dogo. Naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho saa 4.00 asubuhi kutakuwa na Semina ya *CPA* ndani ya ukumbi huu na taratibu zote za Kibunge pamoja na majedwali na kalamu zitapatikana kwenye mkutano huo. *(Makofi)*

Ziko baadhi ya Kamati, siyo zote, zilizoalikwa kwenye semina itakayofanywa Morena leo baada ya kuahirisha

Bunge saa 8.00 mchana. Kwa hiyo, zile Kamati zinazohusika zisiache kwenda kwenye semina hiyo saa 8.00 mchana. Kamati wanazijua wenyewe, kama hujui ujue wewe haumo.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza mjadala. Leo tutakuwa na wachangiaji 18 kwa muda wa masaa matatu. Tunaanza saa 5.00 hadi saa 8.00 tunamaliza wachangiaji 18. Tunaanza na Mheshimiwa Mussa Sima. Mheshimiwa Philip Mulugo na Ester Mmasi na Mheshimiwa Mbatia Wajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii...

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliniambia nikae kwanza.

**MWENYEKITI:** Unasema!

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Uliniambia nikae kwanza, nikafikiri unamaliza utaniruhusu ninachotaka kukizungumza. Kwa idhini ya kiti chako!

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Jaku, bado. Tukishamaliza utazungumza. Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha leo tuko hapa kujadili Bajeti hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika mchakato mzima wa kazi ambayo tumempatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri; nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Hakuna ubishi kwamba Serikali inafanya kazi kubwa na mchango wake ni mkubwa sana kwenye eneo hili la elimu, hakuna ubishi kwenye hilo. Sina sababu ya kuelezea mafanikio ya elimu ambayo yapo na kila Mtanzania anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu hiki cha Bajeti ya Elimu. Nina Shule kongwe ya Sekondari ya *Advance* ya Mwenge. Katika ukarabati ambao Serikali inaufanya sasa hivi, lakini shule yangu ya Mwenge haipo kwenye ukarabati huo. Nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri, shule hii mwaka 2016 ilifaulisha kwa asilimia 93, licha ya kwamba miundombinu hiyo hiyo tunaendelea nayo lakini Walimu wangu wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Singida, ni Manispaa ya Singida Mjini pekee ambayo haina Shule ya Sekondari ya Kidato cha Tano na sita na ndiyo tunaitegemea Shule ya Sekondari ya Mwenge na ndiyo Shule ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nilieleze hili bayana ili Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa ukarabati wa shule hii kongwe ya Mwenge Sekondari. Kwa mazingira haya haya, sisi Singida Mjini tunalazimika sasa kuanza ujenzi wa shule nyingine za *Advance* ili kuweza kuwapunguzia mzigo wazazi na vijana ambao wanafaulu kwenda shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukipewa fedha hii, ikikarabatiwa Shule hii ya Mwenge Sekondari itatusaidia katika mazingira ya kuanzisha hata *Mwenge Day* kwa sababu tunao uwezo huo. Yataongezwa madarasa, tunaanzisha *advance* ya *Mwenge Day*. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana utupunguzie mzigo wazazi, nasi tuwe na kauli ya kuweza kuzungumza kwa wananchi waone umuhimu wa uwepo wa *Advanced Level* Singida Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hii inao wazabuni mle ndani, wanadai zaidi ya shilingi milioni 500 na hao wazabuni ndio tunawategemea kutuchangia kwenye maabara na kwingine kwenye ujenzi kwa namna yoyote ile. Sasa Serikali lazima ione umuhimu wao, itusaidie na hao wazabuni wakilipwa wataendelea kutusaidia kwa kadri watakavyojaaliwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri na hili nalo aliwekee umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Singida Mjini, Kata ambazo hazina Sekondari, wameanza kujenga na tayari Kata yangu moja ya Unyanga wamejenga Sekondari, inahitaji usajili Mheshimiwa Waziri. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri; tumeshakamilisha majengo ya maabara, naomba sana Shule hii ya Unyanga nayo iweze kupata usajili na tuweze kuwapa *morale* wazazi wa kuweza kuendelea kuchangia elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumzie juu ya elimu bora *(quality education).* Hakuna ubishi kwamba Serikali inafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha tunafikia malengo ya kuwa na elimu bora. Tayari tunayo elimu bila malipo, tayari kuna *Responsibility Allowance* inatolewa kwa ajili ya viongozi wetu, Wakuu wa Shule, Walimu Wakuu na Waratibu; hakuna ubishi kwenye hili. Katika mazingira haya haya, ziko changamoto ambazo hatuwezi kuziepuka ili kufikia malengo hayo. Hii ina-*create gap* kati ya wale viongozi kwa maana ya Walimu Wakuu, Waratibu wa Shule na Walimu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu anayeingia darasani leo hakuna *allowance* yoyote anayoipata, lakini kiongozi anayemwongoza, anayo *allowance.* Serikali lazima ioneshe ni namna gani inam-*promote* na huyu Mwalimu anayeingia darasani ili tuweze kufikia *quality education.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia kulipa madeni ya Walimu yasiyokuwa ya mishahara. Sasa hayo yaliyokuwa na mishahara ni nani aliyasababisha na ni nani

ataenda kuwalipa? Naomba Serikali isibague, tunahitaji kulipa madeni yote na tuondokane na mpango huu wa Walimu kuendelea kudai, inashusha *morale* ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu leo haendi likizo, fedha ya likizo haipo. Mwalimu anahamishwa, hapewi fedha ya uhamisho, haipo. Mwalimu anawezaje kufanya kazi fedha ya matibabu haipo? Naiomba Serikali ilete fedha kwa wakati Walimu waweze kwenda likizo, Mwalimu anayehamishwa apewe fedha, tuondokane na mpango huu wa madai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la madaraja. Habari ya madaraja miaka mitatu, sijui *OPRAS,* kila kitu kimeletwa hapa, lakini hakina msaada kwa Mwalimu. Walimu lazima wapandishwe madaraja kwa wakati. Hii ndiyo motisha yetu sisi Walimu wala hatuna kitu kingine. Serikali inapaswa izingatie. Kama tumeamua kwenye *Open Performance Appraisal System,* basi tuamue. Habari ya kukaa miaka mitatu na yenyewe haitimiii, jambo hili linatupa mzigo mkubwa sana. Naiomba Serikali iliangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa iangalie *teaching allowance,* hatuwezi kuepuka. Huwezi kutoa *allowance* kwa Walimu hawa ambao ni viongozi, *subordinate* wao ukawaacha. Hatuwezi kuepuka hili! Serikali lazima ije na mpango huu, itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Nidhamu; tunazungumzia elimu bora. Tumeunda Tume ya Utumishi ya Walimu hapa kwa Sheria Na. 25 ya Mwaka 2015, wameizungumza Kambi ya Upinzani pale. Ni ukweli usiofichika, tumefuta Mikoa, Halmashauri, tukapeleka Mamlaka ya Nidhamu hii Tume ya Utumishi kwenye Wilaya. Leo watumishi watatu kwenye Wilaya ambayo ina Halmashauri mbili, wameshindwa Walimu 1,200 watawezaje Walimu 3,000? Mamlaka ya Nidhamu haijapewa kipaumbele. Niiombe Serikali iliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo mamlaka, *TSC* kwenye Ofisi zao haina vitendea kazi, haina fedha, haina chochote. Sasa unatarajia inawezaje kusimamia jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tujue umuhimu wa *quality education,* tunahitaji kuwashirikisha wadau wote wakiwemo *TSC.* Kama inashindikana, tuwape semina Waratibu na Walimu Wakuu waweze kuifanya kazi hii kwa pamoja ili tuhakikishe kabisa kama tunazungumzia uadilifu kwenye utumishi uwe ni uadilifu ambao unawagusa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TSC* kama imeshindikana, tuirudishe sheria hapa ili tuweze kuirekebisha. Leo wale maafisa wa *TSC* wanafanya kazi, hawana vyeo. Haieleweki mishahara yao ikoje, wanafanyaje kazi hii? Naomba sana Serikali iliangalie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni *community participation.* Serikali ina kila sababu ya kuwashirikisha wazazi na wananchi kuweza kushiriki kwenye hili. Baada ya kuanzisha elimu bila malipo, wengi wamerudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuanzisha programu maalum ambayo itainua ubora wa elimu. *Training;* kutoa mafunzo maalum kwa ajili ya wazazi. Tutoe mafunzo maalum kwenye Kamati za Shule, tutoe mafunzo maalum kwa Walimu; hii itatusaidia kufikia malengo ambayo tumeyakusudia ya kuwa na elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kuiomba Serikali ione elimu ndiyo kila kitu. Tusipomwangalia Mwalimu huyu kama *stakeholder* namba moja, hatuwezi kufanikiwa malengo ya kufikia elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mulugo na Mheshimiwa Mmasi jiandae.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, angalau nami nimepata nafasi ya kuchangia Wizara ya Elimu na naomba niseme kwamba mimi ni mdau, ni Mwalimu, kwa hiyo, angalau naelewa mambo mengi ya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana; kabla sijaanza kuchangia hoja zangu za msingi, lakini angalau nilalamike kuhusu suala moja la Halmashauri yangu ya Songwe. Nilikuwa napitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa kwenye kitabu hiki, naona Halmashauri yangu ya Wilaya ya Songwe haijapata vitabu kabisa katika huu mgao wa vitabu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wengi wanachanganya ama niseme sijui ni Makatibu Makuu; wanapoandika Mkoa wa Songwe, wanapoanza kuorodhesha zile Wilaya hawaiweki tena Songwe kwamba kuna Wilaya ya Songwe. Naomba watambue, kuna Mkoa wa Songwe halafu kuna Wilaya ya Songwe, Mbozi, Ileje na Halmashauri ya Tunduma na Momba. Kwa hiyo, kuna Halmashauri tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesoma humu nakuta vitabu vyote vimeenda Ileje, vimeenda Momba, vimeenda Tunduma, vimeenda na kule Momba. Sasa huku kwangu sipati. Kwa hiyo, mwaka huu sijapata vitabu, sasa sijui nimwendee nani. Kwa hiyo, nitakwenda pale Wizarani wanipe vitabu nisafirishe mimi mwenyewe nipeleke, maana naona hii sasa ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa nichangie hoja zangu zile za msingi. Nianze na kuunga mkono hotuba ya Kamati ya Huduma za Jamii iliyosomwa na Mheshimiwa Bashe pale kwenye kuishauri Wizara kuhusu mambo fulani na changamoto za Wizara ya Elimu. Tukianza

na utaratibu wa viwango vya ufaulu katika shule binafsi. Mimi ni mdau, naomba ku- *declare interest* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ikifika mwezi wa Kwanza shule za *private* tunakuwa na *joining instruction,* wanaandika; ili uingie katika shule yangu, unatakiwa ufaulu asilimia labda 41 ama 50 kama zilivyo Seminari. Shule za Serikali utaratibu huo hamna, ukishafaulu arasa la saba, unaendelea mpaka ukaukute Mtihani wa Taifa wa *Form Two* na mpaka umalize *Form Four. Form Two* yenyewe ni alama 30 ambayo mimi kama Mwalimu nasema bado ni alama ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafika mwezi wa 12, mtoto yule hajafikisha hata wastani wa alama 33 mpaka 35. Wanaambiwa; sasa bwana inabidi urudie darasa. Anayekuja kulalamika mtoto kurudia darasa ni mzazi mwenyewe aliyelipia ada, lakini ukienda kwa Afisa Elimu wa Wilaya na Afisa Elimu wa Mkoa wanasema Serikali imekataa wanafunzi kukariri, wasirudie, lazima waendelee. Sasa unajiuliza, hela ni zangu, mtoto ni wangu, elimu ni yangu, atakuja kuajiriwa, mimi mwenyewe ndiyo atakuja kunilinda, sasa iweje tena unanikatalia mimi mtoto kurudia shule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 nilizungumza kwa uchungu mkubwa hapa. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamaliza hoja, hebu alitamke hili. Walilizungumza mwaka 2016 lakini hawakulitolea waraka. Tunaomba shule za *private* ziwe huru kukaririsha, hakuna shida pale mbona! Tatizo ni nini? Yeye alishasema kwamba huyu mtoto ni *slow learner* akamwacha; nilizungumza na mwaka 2016 hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale watoto ambao ni *slow learners,* kama hawajifikisha kiwango fulani cha *marks* wasiendelee, warudie mwaka ili wasome vizuri na wazazi ndio wanaotaka wenyewe. Sasa wanawakingia nini? Hilo naomba niliongee kwa uchungu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *conflict of interest*. Sasa hivi wanaoendesha shule Tanzania ni wadau wanne; Wizara ya Elimu ina shule za mazoezi, za msingi na sekondari zile za mazoezi kwenye Vyuo vya Walimu kwa hiyo nao wanamiliki shule, Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI wanamiliki shule chini ya Mkurugenzi na ni shule nyingi sana, nadhani ndiyo ziko huko kwenye Halmashauri, Sekondari na *Primary*. *TAMONGSCO* wanamiliki shule pamoja na *TAPIA* wamiliki wa shule binafsi, wana umoja wao, wanamiliki shule. Sasa wadau hawa wanne wanaomiliki shule, tunataka tuwe na *Regulatory Body* ambayo itakaa pale juu kuzisimamia hizi shule kwa sababu kuna *conflict of interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi huyu ni mtu wa Serikali, ametoka kwa Mkurugenzi pale pale ama ametoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu; anakwenda kukagua shule ya umma, anaona kuna matundu mawili ya vyoo, anaandika ripoti pale inakwenda kwa Mkurugenzi halafu inakaa tu pale na mambo hayaendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye shule za *private,* akikagua akakuta kuna matundu mawili, yaani shule inafungwa siku hiyo hiyo. Ni hapo hapo, hakuna mjadala. Kwa nini wanawanyanyasa hivyo? Kwa nini vile vile na sisi tusiwe na chombo kitakachokuwa kinasimamia hizi shule? Wakaguzi wale wametoka Serikalini, wanaandika ripoti inaenda kwa Katibu Mkuu. Ndivyo hivyo hivyo tupate mtu fulani kama zilivyo mamlaka nyingine, tuwe na mamlaka itakayosimamia hizi shule zote, hao wanaomiliki shule kwa pamoja kuliko hali hii ya kuonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuna mmiliki mmoja wa shule alilalamika akasema Mheshimiwa Mulugo wanataka kunifungia shule. Nikauliza kuna nini? Akasema, wanafunzi walikuwa 48 darasani, maana sheria inasema angalau wanafunzi 40 mpaka 45. Wanafunzi 48 shule moja ya Kigoma, Mkaguzi ameenda pale kama mbogo, anataka kumfungia

shule kwamba kuna wanafunzi 48. Nikamwambia hivi, nyuma geuka! Nenda shule ya Serikali, kuna wanafunzi 120 darasani, fungeni nayo hiyo! Jamani vitu hivi viwe *realistic!* Wanakuwa mpaka 150 na wenyewe wafunge! Tena angalau mambo ya madawati tumeyamaliza, maana walikuwa hata wanakaa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda kwenye shule za *private* na mmetupa miongozi ninyi wenyewe, tunafuata kila kitu, lakini jamani katika neno la ukaguzi angalau hata asilimia 10 inaweza ikapotea. Watu ni kama wana hasira fulani hivi! Naomba Mheshimiwa Waziri, hebu wasimamie jambo hili, kuna kero nyingi sana kenye shule huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene wiki mbili zilizopita, wamiliki wa shule walikuwa Dodoma hapa walikuwa na mkutano wao wa kujadili mambo, tukamualika akawa mgeni rasmi wa kuja kufunga kile kikao. Tukamworodheshea kero zote na kodi zote ambazo tunalipa kule kwenye shule ambapo kero nyingine ni wazazi wenyewe ndiyo wanalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kibao kinaelekeza labda *Mwambao Secondary School* kiko pale njia panda. Halmashauri na Mkurugenzi wanakuja wanasema lazima kilipiwe kodi, kwenye shule. Ni huduma ile! Tunalipia kupata vibao ambapo bado unaposajili shule Wizara ndiyo inakwambia kwamba lazima uwe na kibao, tunalipia kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene, amekaa na wale wadau, ametulia akaona kwamba kweli hii ni kero. Amesema, kuanzia leo nafuta zile kodi za Halmashauri kwa ajili ya vibao. Tulimpigia makofi na kelele za shangwe na hivi tunasubiri waraka tuweze kufuta ile kodi. Kuna kodi nyingi! Kuna *OSHA, property tax;* jamani kuna vitu vingine ni vya ajabu kweli kule kwenye shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu yeye ndiye mdhamimi wa elimu, atusaidie. Naomba tafadhali siku nyingine wawe wanakaa na wadau wa elimu kwenye Halmashauri kule na kwenye Wilaya, waweke watu wa Serikali, watu wa *TAMONGSCO* na *TAPIA* wawe wanajadili mambo ya elimu kwa pamoja. Sio maadui, wote ni watoto wetu wa Tanzania kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ada za mitihani. Mtihani wa Taifa uko Darasa la Nne, Darasa la Saba, *Form Four, Form Two* na *Form Six.* Serikali ya Mheshimiwa Kikwete iliamua toka miaka minne iliyopita kwamba hii iwe ni ruzuku kwa wanafunzi wote kwamba wasilipie mtihani wa Taifa. Baraza la Mitihani litoe mitihani bure, lakini ilipokuja huku kwenye utekelezaji wakabagua kwamba hapana shule za *private* waendelee kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasifikiri wanakomoa shule za *private* pale, wala siyo hela ya mmiliki, ni hela ya mzazi mwenyewe ndiye anayechangia. Ukienda kwenye *joining instruction* tumeandika mzazi alipie ada ya mtihani na Waheshimiwa Wabunge asilimia 90 hapa mna watoto wenu wanasoma kule. Hiyo hela mnailipia ninyi wenyewe. Naomba ile ada ya mtihani wa *Form Two* na *Form Four* ifutwe kama zilivyofutwa kwenye shule za Serikali. Mzazi abakie kulipa ada tu, ahenyeke kwenye ada lakini siyo kwenye masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Wizara ya Afya chanjo wanatoa bure! Mbona hawabagui inapokuja kwenye chanjo za Shule za Serikali za Msingi na Sekondari! Kwa sababu ni afya ya pamoja; hata elimu wale watoto ni wa pamoja. Wale watoto wakisoma katika shule za *private* hawaendi kufanya kazi Uganda, hawaendi Kenya wapo Tanzania hapa hapa, ni huduma ya kawaida hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inaniuma sana. Nashukuru hata kwenye Kamati ukurasa wa maoni Mheshimiwa Bashe, kwa sababu tu muda umekwisha, lakini

wameliandika hili wanapendekeza ada ya mtihani ifutwe *Form Two* na *Form Four* na Darasa la Nne, kwenye shule za *private*, iwe kama ruzuku, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije lingine ambalo naweza nikatoa machozi kuhusu vitabu. Mungu wangu! Mheshimiwa Susan Lyimo alionesha vitabu hapa lakini nami tayari nilikuwa nimeshafanya *search* kama Mwalimu. Ninavyo vitabu hapa, *Geography for Secondary Schools, Form Three*, *English for Secondary; Form Four,* ni hatari; na hii ni maajabu ya dunia. Ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna mambo mengine lazima tuseme. Serikali ni ya kwangu, nchi ni ya kwangu, watoto ni wa kwangu, Chama ni cha kwangu tunaposema mbili ongeza mbili, mtu mwingine akasema ni sita wakati jibu ni nne, hatuwezi kumfumbia macho. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Utachukua muda wa watu wengine. Ahsante. Mheshimiwa Mmasi na Mheshimiwa Mbatia ajiandae.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa muda nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanaoifanya. Mama yangu Mheshimiwa Ndalichako, Profesa wangu mwema, kwangu katika mchango wangu hata siku moja katika Bunge hili, tofauti na ilivyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengine, mimi sitamwomba aache *legacy, legacy* ameiacha tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakumbuka katika Baraza la Mawaziri wote, mtu wa kwanza aliyekuwa na uthubu ni yeye. Alikubali kukana nafsi

yake, akajitwisha msalaba wake, akafuta *GPA* bila kungoja makelele ya Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili alisimama mwenyewe. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, alisimama akaona kero ya wanafunzi wanaohangaika mitaani kutafuta hifadhi, alisimamia hili ndani ya miezi minane alituonesha kwa mfano, mimi pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti tulikuwa mashahidi. Tulikuja kwenye ufunguzi wa *hostels* za Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu. Mimi ni Mbunge wa kwanza katika Bunge hili jipya kulia kwamba naomba miundombinu iliyowekwa pale *UDOM* ijae, tunapoteza pesa nyingi lakini Mheshimiwa Waziri hukunipa nafasi nije kulalamika mara ya pili. Jana nimeona umetoa waraka kwamba *Central System Admission* ifute ile *process* kwamba vyuo visidahili ila *TCU* iweze kudahili wanafunzi kwa maana ya kwamba kwa kufanya vile vyuo vingi vilikuwa vinabaki *empty*, tunaweka *resources* nyingi lakini pia hatuna matumizi nayo. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye mchango moja kwa moja katika Wizara hii muhimu. Nianze tu kumwambia Mama Ndalichako, tunafahamu na Tanzania inafahamu na sisi wadau tunafahamu kwamba changamoto kubwa katika Wizara yake imekuwa ni urejeshaji wa masuala mazima ya mikopo Elimu ya Juu. Mheshimiwa Mwenyekiti tunakiri hilo.

Mheshimiwa Mwenyikiti, pia kama utaangalia, juzi tukiwa Mei Mosi tulipata taarifa kwamba katika mwaka huu wa fedha tunaomaliza, deni ambalo limekuwa halijalipika mpaka leo ni *seven trillion*, deni tulilotakiwa kulirejeshwa Bodi ya Mkopo ni *seven trillion* lakini mpaka leo ni shilingi bilioni 400 tu zimerejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama yangu Mheshimiwa Ndalichako, *legacy* ameiacha tunataka tuilinde. Naomba asikilize yafuatayo, kwamba sisi Tanzania mwaka 1999

tulituma *delegation* yetu kwenda nchi ya Kenya kujifunza wenzetu wanafanya nini, lakini kule tulichokiona, asilimia 40 na ni *practice* ambayo mpaka leo ndivyo ilivyo. Asilimia 40 ya tengeo la fedha ya Bodi ya Mkopo ndiyo Serikali ina-*meet* lakini asilimia 60 ni *other key players,* kwa maana ya kwamba ni *financial sectors* ndiyo ina-*dish-out* pesa katika kusomesha wanafuzi. Mimi siombi tufike huko, lakini angalizo lipo moja; tusipoangalia, tunaweza tukashindwa kufikisha tumaini letu kwa wananchi wetu walio wengi wanaotutegemea sisi kuweza kusaidia vijana wao waweze kwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia leo tatizo kubwa ni ajira. Tulikaa hapa kwenye *Miscellaneous Amendment* tukasema kwamba tukate asilimia 15 ili fedha hii iweze kurejeshwa, lakini Mheshimiwa Mwenyekiti tunasahau kwamba tulisema tukate asilimia 15, wakati tunaangalia *entry qualification, eligibility qualifications* ya mtu ambaye anaweza kupata mkopo, cha kwanza tuliangalia uhitaji. Kama ni uhitaji, ni *obvious* kwamba wanafunzi hawa wametoka kwenye familia maskini. Sasa kama wametoka kwenye familia masikini na ajira hakuna, tunategemea hii asilimia 15 tunam-*task* mwanafunzi au mzazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate muda tutafakari upya. Asilimia 15 ni rahisi sana kuwekwa kwenye majarida yetu, ni rahisi sana kuja kuijengea hoja Bungeni, lakini watakaoteseka ni wananchi wetu wa vijijini wasiokuwa na uwezo. Kama hivi ndivyo tupate muda tutafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nakuomba, unao wenzako hapo, kila siku wanawasilisha ripoti zao na kusema ni kwa namna gani wanaenzi masuala mazima ya Sera ya Ajira, lakini vitu havikutani. Hatuoni *direct linkages.* Wewe ni shahidi, tulikaa hapa juzi, mama huyu Mheshimiwa Mama Kairuki, Waziri wa Utumishi, alituambia kwamba ameahidi kutoa ajira 58,000 nchini Tanzania lakini *absorption capacity* bado haikidhi tija. Wanafunzi wanaomaliza ni 250,000 lakini unaona *absorption capacity,* ajira ni 58,000 kwa mwaka. Hatuwezi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wizara Ardhi, inastawi, inashamiri, ni vema tumempata kiongozi mahiri, ni sawa; lakini pia ukiangalia vijana wanaomaliza Chuo cha Ardhi wanakosa kazi kupitia hata sheria tunazoleta Bungeni. Tulileta hapa *Valuation and Valuer Registration Act* ambayo ni sheria ya masuala mazima ya wapima na wathamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri ni kwamba Wizara yake itasajili makampuni 57 ambayo yataingia kwenye suala zima la kupima ardhi. Tukamwuliza hapa, akasema pia vijana kupitia zile *three categories* ambapo kuna *full valuer* na *temporary registration valuer* walisema kwamba hata vijana *graduate* wanaruhusiwa kuingia na kuweza kufanya kazi za uthamini katika muktadha wa masuala mazima ya ardhi. Katika makampuni 57 yaliyoingia na kusajiliwa hakuna hata kampuni moja ya *graduate* wa nchi hii, mzawa wa nchi hii aliyeweza kuingia na kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, masuala ya ajira bado yamekuwa ni changamoto. Ninyi ni mashahidi kwamba vijana hawa wanahangaika, vijana hawa wanatulilia, tutawapeleka wapi? Mwaka 2020 unafika, tutajibu nini? Ilani imeeleza, Sera ya Ajira inaeleza, lakini vijana wamelia kwa kila sauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, akae na Wizara nyingine wamsaidie tuweze ku-*link* na kuweza kuzalisha ajira. Leo tunavyoongea, ukuaji wa Sekta ya TEHAMA ni mkubwa, lakini wanafunzi wa *DIT* wanatumika wapi? Hawatumiki! Angalieni mifumo inayotumika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *financial sector, 40 percent* ya kazi za *ICT* inafanyika nchi ya India na Kenya. Watanzania hawashiriki katika muktadha mzima na masuala ya ajira. *Legacy* tutailinda pale ambapo tutaweza kufanikiwa kwenye mtihani huu wa urejeshaji wa mkopo wa

Bodi. Sisi kutunga sheria ngumu bado siyo jibu kwa sababu bado tunampelekea mzigo mkulima, fukara na masikini kule kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala mazima ambayo sisi kwetu bado tunahuzunika sana. Sisi kama akinamama, wewe ni shahidi, tumekuwa na kesi nyingi sana kwenye masuala mazima ya ngono katika Vyuo Vikuu vya Tanzania yetu. Leo ngono inatumika kama kipimo na kigezo cha ufaulu katika shule zetu ama vyuo vyetu nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mama Ndalichako ni shahidi, tumekuwa na kesi nyingi. Atakumbuka juzi hapa, Mhadhiri wa Chuo cha *NIT,* huyu anaitwa Bwana Samsom Mahimbo, alidiriki kumshawishi mwanafunzi na TAKUKURU walimkamata kwamba ili afaulu mtihani wake wa *supplementary* ni lazima atoe rushwa ya ngono.

Mheshimiwa mwenyekiti, sisi ni wazazi, matumbo yetu yanatuuma. Hatuwezi kuangalia dhambi hii! Hatuwezi kuangalia udhalilishaji wa wanafunzi wetu. Imesemwa hapa na waliowasilisha kwenye ripoti zao hapo mbele, imesemwa kabisa, ukimsomesha mwanamke umesomesha Taifa. Tumechoka kuona kudhalilishwa kwa watoto wetu mashuleni. Walimu hawa wanachukuliwa hatua gan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akija aniambie Bw. Samson Mahimbo alichukuliwa hatua gani? Asisahau, aniambie Bw. Kelvin Njunwa, ni *Institute of Accounts*, Dar es Salaam alichukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu, kaka yangu mpendwa Mheshimiwa Simbachawene alienda hapa Hombolo kwenye kesi kama tatu alienda na *ku-rule out* za masuala ya ngono. Hawa watu wanachukuliwa hatua gani? Hatuwezi kusema tunatengeneza rasilimali ya nchi hii kwa kutumia vigezo ambavyo havina ushindani. Hatuwezi kutengeneza rasilimali ya nchi kwa kuwa na watu ambao hatujielewi wala hatujithamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kwenye uchumi wa kati, tunaandaaje rasilimali watu ya nchi yetu ya Tanzania? Tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, tumejiandaaje kuingia kwenye uchumi wa viwanda endapo utafaulu mtoto mwanafunzi wa Chuo Kikuu unapimwa kwa utoaji wa ngono? Tutaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni mama, amezaa, Wizara yake inasimamiwa na akinamama, Semakafu ni *activist* mzuri, ananijua na ananisikia. Semakafu Kamishna wake ni *activist* mzuri; namwomba alipo atusaidie. Tutaangalia haya mpaka lini? Tumechoka, macho yetu yanaumia, nafsi zetu zinauma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu. Nilikuja kwenye Bunge lako hili Tukufu, niliongelea sasa wanafunzi wa Chuo cha *NIT*, nikaomba unisaidie kwamba tumejipanga kwenda kwenye uchumi wa kati, tumejipanga ku-*promote Tourism Sector* yetu kwa kufufua usafiri wa anga, *well and good*. Tume-*invest a lot* kununua ndege, *well and good,* lakini tumejipangaje kuandaa rasilimali watu katika muktadha mzima huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu hata maandiko ya dini wanasema atakayeshindwa kushukuru, huyo ni mnyang'anyi. Namshukuru sana, nilikwenda nikamwomba kwamba watoto hawa wa *NIT* waruhusiwe kufanya mitihani. Milioni kumi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia, ajiandae Mheshimiwa Riziki. *(Makofi)*

**MHE: JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa haraka tu nianze kwa kutoa pole kwa wale wanafunzi wetu wa Lucky Vincent na Jimbo Vunjo

tulikuwa na wanafunzi wawili ambao ni Irene pamoja na Marioni walikumbwa kwenye mkasa huu. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la elimu nchi hii au tatizo kubwa la Taifa letu linaanzia Bungeni hapa. Suala la *GPA* unakumbuka mwaka 2013, Serikali ilivyoleta hoja ya kuondoka kwenye madaraja kuja kwenye *GPA,* Bunge hili likashangilia kweli kweli, likapitisha *GPA*. Baada ya miezi michache wakatoka kwenye *GPA* wakaja kwenye madaraja, Bunge hili hili likashangilia kweli kweli. Sasa tusitumie wingi wa itikadi zetu kuua Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na hiyo kwa sababu tangu tumepata uhuru, Serikali hii ni mwendelezo. Nimemsoma Eliufoo, hotuba yake hii hapa ya tarehe 11 Machi, 1967. Ukimsoma Eliufoo akiwa Waziri wa Elimu na akitoa ripoti ya Elimu ya mwaka 1966, zaidi ya miaka 50 iliyopita anazungumzia bodi ya kusimamia viwango vya elimu nchini Tanzania, wakati huo Mwalimu Nyerere alikuwa na Itikadi ya Ujamaa, lengo likiwa ni kujitegemea. Kwa hiyo, elimu ilikuwa inatolewa kwa misingi ya lengo la kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimefanya utafiti, nitampatia na ripoti ya Eliufoo ambayo najua hana, ambayo ina zaidi ya miaka ambayo sijui kama ulikuwa ameshazaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli inaleta uchungu mkubwa sana kwa sababu kila Waziri anayeingia kwenye Wizara, yeye ndio sera, yeye ndio mitaala na yeye ndio kila kitu. Kama Bunge hili tulishangilia *GPA,* akaja Waziri huyu akabadilisha akaja kwenye madaraja tukashangilia; hivi tupo wapi? *Reasoning power* yetu ipo wapi? Kufikiri kwetu yamkini kuko wapi? Ndiyo sababu tunafika mahali kama Bunge haliwezi likasimamia Serikali vizuri hatuwezi tukafikiri vizuri, hatuwezi tukaiongoza Serikali vizuri, tutaendelea kupata matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema *no research, no data, no right to speak.* Mwaka 2013 kwenye Bunge hili, Mheshimiwa Waziri wa Elimu alisema ataleta ripoti ya Sifuni Mchome, alisoma kauli ya Serikali Bungeni na tukashangilia, hii hapa; mpaka leo hii ripoti ya Mchome hatuna na wakati huo wanafunzi zaidi ya asilimia 65 walikuwa wamepata daraja sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wakati Waziri wa Elimu anajibu hoja Bungeni hapa, ninayo majibu yake. Serikali ni hiyo hiyo moja, kwa sababu tangu tumepata uhuru Serikali ni hiyo hiyo moja. Waziri wa Elimu akiwa anajibu tarehe 01 Februari, 2013, siku ya Ijumaa, Mheshimiwa Waziri alitamka Bungeni hapa kwamba yale yote tuliyoyapendekeza yatatekelezwa na akasema Serikali itaunda Tume ya Kudumu ya Elimu nchini ya kupambana na matatizo yote na akaweka neno "*education quality assurance and control.*" Bunge hili hili! Kwa hiyo, hapa tunapoteza muda tu. Tunaongea, tukishafungasha makabrasha kesho kutwa, tumeondoka, hakuna wa kufuatilia, hakuna tathmini inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 tulizungumzia kuhusu vitabu, mwaka 2015 tumezungumza, miaka mitano mfululizo tumezungumza udhaifu wa Sekta ya Elimu na tukaambiwa kuwa vile vilikuwa vya *EMMAC*. Mheshimiwa Mulugo amemaliza kuzungumza, alikuwa Naibu Waziri, waliivunja *EMMAC* hapa tarehe 5 Juni, 2013. Sasa udhibiti wa vitabu ukapelekwa Taasisi ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli leo hii Mheshimiwa Mama Ndalichako, Serikali ya Awamu ya Tano, wanaandika vitabu, kitabu cha Kiingereza Darasa la Tatu, hapa juu penyewe tu pameandikwa *I learn English Language,* ndiyo imekuwa ithibati. Hapa Kazi Tu! Serikali ya Awamu ya Tano "*I learn English Language,*" ndiyo fedha tunazopitisha Bunge hapa ndiyo zinaandika vitabu hivi, "*I learn English Language*." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu katika *chapter one,* mwanafunzi anaanza kusoma sentensi, "*good morning; thank you; good morning dear mother; good morning,* lakini unaenda mpaka *chapter five* ndiyo wanaanza kusoma a, e, i, o, u. Niliwahi kuimba hapa na leo narudia tena. Tuliwahi kusema kwamba mtoto anaanza kusoma a, e, i, o, u hizi ni herufi kuu tamka kwa sauti kuu ndio a, e, i, o, u na kikombe u, u, u kama jicho e, e, e mwenye mpira o, o, o ni kikombe u,u,u! *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge aliimba wimbo wa a,e,i,o,u)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Kiingereza, *chapter five* ndiyo wanaanza kuimba a, e, i, o, u, njoo kwenye kitabu cha Darasa la Kwanza cha Kiswahili, yaani ukienda kitabu cha Darasa la Kwanza cha Kiswahili kilichopitishwa mwaka huu na Serikali hii ya Awamu ya Tano kimeandikwa taja majina ya wanyama, "yawanyama" ni neno moja. Ndiyo maana leo hii Wizara inamdhalilisha Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais yupo kwenye TV kila siku anasema "ka ta umeme," neno moja. Yaani hata silabi haipo, "ka ta umeme," yaani na watoto wetu ndiyo wanayojifunza "ka ta umeme," ambayo ni silabi. Sasa *quality Assurance and control,* iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Education Act* ya 1962 *section (3)* inazungumzia namna ya kuhakikisha bodi inaweka vigezo gani, marupurupu ya Walimu, marupurupu ya Wafanyakazi, namna ya kuweka mishahara, *allowance* na kila kitu. Naomba urejee kwenye *Education Act section (3) State of Education,* inaeleza vizuri kabisa; *"there-is hereby established a body to be known as the Unified Teaching' Service..."* na mengine yanaendelea, sitayasoma kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nitampatia Mheshimiwa Waziri hii ripoti ya Eliufoo sasa ya 1967.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mengi ambayo tunayasema hapa, tunasema kwa nia njema kwa kuwa tunalitakia Taifa hili mema, lakini Serikali ambayo inaingia madarakani hata hamfanyi rejea kukaa ofisini, mwenzako amekukabidhi nini, inakuwa ni matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye vitabu sasa hivi, mbili ni namba shufwa au siyo namba shufwa; au mbili ni namba tasa au siyo namba tasa? Kuna mgogoro wanasema mbili siyo namba tasa; ndio sumu tunayolisha watoto wetu leo. Sifuri gawanya kwa sifuri wanasema ni sifuri, wakati haigawanyiki. Namba yoyote ikigawanywa kwa sifuri haigawanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matatizo tuliyonayo, kwa mfano Jimbo la Vunjo, tuna Shule za Msingi 128 lakini Mwalimu mmoja kwa uwiano wa wanafunzi 61, Mwalimu mmoja kwa uwiano wa mkondo mmoja na nusu mpaka miwili, yaani hata miundombinu yenyewe, Kitaifa *standard* ni Mwalimu mmoja kwa wanafunzi wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Walimu wa Sayansi mliowaajiri tarehe 18 Aprili, 2017 hawajapewa fedha yoyote ya kujikimu na hili wala siyo la Vunjo tu, hata kule Rungwe nimepata taarifa zao, Bunda nimepata taarifa zao, Halmashauri ya Moshi nimepata taarifa zao, kote huko ni matatizo makubwa. Sasa kulikoni? Tufanye nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta binafsi, kwa nini hatuweki mazingira rafiki ya kuvutia kwa sekta binafsi yaweze kuwekeza vizuri elimu? Kuna tozo na kodi zipatazo zaidi ya 15 kwenye elimu, nani alisema elimu ni biashara katika nchi hii? Katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia kodi 15 kwenye Sekta ya Elimu; tozo na kodi, yaani tumekosa vyanzo vingine vya mapato mpaka tunaenda kufanya elimu kwamba ni biashara!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea namna hii, mazingira ya walemavu wetu, tukienda kwenye TEHAMA, elimu ya juu yaani yapo mambo mengi. Wakati huo wa Mwalimu, walipoamua kutengeneza Taifa lenye *skills,* uwezo na ujuzi walijenga ile shule ya Galanos, Ifunda na Kibaha, kwa ajili ya michepuo ya kilimo na ufundi na wakajenga shule ya Wasichana ya Bwiru na shule ya sekondari ya Moshi kwa ajili ya mchepuo wa biashara, yaani unakuwa na elimu unajua unafanya nini lakini lengo lake miaka mitano, kumi, 20 ikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mheshimiwa Waziri na ulikuwa kwenye sekta hii, hata tukisoma ripoti mbalimbali, ripoti hii hapa wakati huo ukiwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na unajua ile ya mwaka 2010 ikatoka Juni, 2011 unaijua vizuri. Sasa haya mambo ya *trial and error* maana yake nini? *Why? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie na nipendekeze tena kwa sababu naona muda wangu imebaki dakika moja, nasema kwamba elimu ndiyo mapigo ya moyo ya Taifa letu, mapigo ya moyo yakienda kinyume na asilia yake uhai huweza kutoweka. Tunao wajibu wa kuokoa uhai huu kwa sababu maendeleo ya Taifa lolote lile na jamii yake ni tunda la mfumo wa elimu. Lazima tujenge mifumo ya elimu inayojali utu wa mwanadamu, inayokuza utu wetu kwenye utamaduni wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Mngwali ajiandae Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na ardhi kwa kutujalia sisi sote uhai, uzima na fursa ya kuwa hapa leo.

Pia nakushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia mada ambayo iko mbele yetu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kwanza kwa kupongeza Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa taarifa yao nzuri kabisa na nipongeze Kambi Rasmi ya Upinzani kwa hotuba yao nzuri kabisa. Waingereza wanasema; *they have said it all.* Ni matarajio yangu kwamba Waziri atafanyia kazi *document* hizo mbili, kwa uadilifu ili Taifa letu lifike litakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala siachi kumshukuru wifi yangu Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayoifanya na Naibu wako na timu yake yote. Pia nikupongeze kwa kuchagua *partner* ndiyo kwa sababu ulikwenda Kusini ungekwenda Kaskazini yale maneno leo usingeyasema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli haya mambo kama alivyosema Mheshimiwa Mbatia yanaturudisha mle mle kila siku. Halafu tunafanya *trial and errors* hata kwenye elimu! Halafu Bunge kama imepanga ratiba vizuri, jana tumezungumzia mambo ya maji hapa, maji ni uhai, leo tunazungumzia elimu, elimu ni ufunguo wa maisha, lakini tunauchezea ufunguo huu, matokeo yake Taifa hili litaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa najitahidi sana nipate fursa ya kuuliza swali la nyongeza wakati swali namba 199 likipatiwa majibu. Mimi muda wote nasema nchi hii tuna tatizo la ukosefu wa uadilifu, hatufanyi mambo kwa uadilifi. Mheshimiwa Mbatia kasema vizuri pale, hizi itikadi zetu za chama zitatupeleka pabaya. Ikisemwa hapa, ndiyoo, waliosema ndiyo wameshinda, waliosema sio wameshindwa halafu matokeo yake tunapitisha mambo mwisho wa yote yanaturudia wenyewe tunaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi lakini nianze na hili la mambo ya vyuo kwa sababu limenigusa mimi binafsi. Hivi Wizara inapokuja kutuambia kuna vyuo visivyo na sifa lakini vilisajiliwa, vilisajiliwa vipi? Mimi nilikuwa Chuo cha Diplomasia, ni chuo cha Serikali, tulizungushwa miaka miwili na *NACTE* kwa sababu tu hatuna *push door* yaani mlango ule tunaambiwa mlemavu hawezi ku-*access* miaka

miwili chuo cha Serikali kilichoanzishwa miaka karibu ishirini iliyopita. Vyuo binafsi hata mlango wenyewe haupo vinapata usajili, halafu hapa wanakuja kutuambia kuna vyuo visivyo na sifa vilisajiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi wanatumbia vitabu vyenye maudhui siyo vipo, hilo ni tatizo la uadilifu. Tunaona kwenye *tv* zetu hapa programu za kijinga kabisa, watoto wanazini pale mbele ya *screen,* lakini *TCRA* kuna Kamati ya Maudhui hawalioni hili? Tatizo ni uadilifu. Tunawaweka watu siyo kwenye taasisi ndizo, tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NECTA* na vyeti *fake.* Kwenye kikao cha mwaka jana hapa nilisema, mimi nimepoteza cheti changu cha *form four* na *form six,* nakwenda *NECTA* naambiwa nenda kule ulikosoma mwalimu wako mkuu akuandikie barua. Nikawaambia mimi nimetoka Kisutu mwaka 1977, huu mwaka 2011 Mwalimu Mkuu gani wa Kisutu ananijua mimi lakini wewe *NECTA* ndiyo uliyenipa mimi namba ya mtihani na ndiye unayejua kituo changu cha mtihani, *you stand a better position and chance* ya kuni-*clear* mimi kuliko huyo mwalimu. Sasa hapa mmeanzisha hili zoezi wenyewe mnaliita uhakiki wa vyeti *fake,* kisiasa kabisa watu wanaathirika, wengine wala hawahusiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwaambie moja tu. Mimi sasa hivi naitwa Riziki Shahari Mngwali lakini hili nimelipata na nimelisajili rasmi kwa sababu nimeenda kutafuta *deed poll.* Watanzania wangapi wanajua hilo? Mimi miaka yangu yote naitwa Riziki Shahari, majina mawili tu. Hata nilipokwenda chuo kikuu kuomba niwe *admitted* kwa ajili ya programu nyingine nikaambiwa hilo jina la tatu hatulikubali kwa sababu ulisoma hapa digrii ya kwanza kwa majina mawili, tutakusajili tena kwa majina hayo hayo mawili. Sasa hivi vyuo vyetu vingesaidia hivi kuliko kuwaadhiri na kuwatesa watu bila sababu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika lile swali nililolisema la jana namba 199 kulikuwa na *issue* ya wenyewe watalaam

wanaitwa *LOI - the Language of Instruction,* imesemewa mpaka na programu maalum ilikuwepo chuo kikuu pale. Profesa Koro wame-*research* na wameandika bado tunali-*discuss* hapa. Jana likaja hapa linasemwa na leo hivyo hivyo ndiyo tunaona vitabu hapa vinakwenda kushoto kulia, kulia kushoto, pembeni kati, tatizo hatujui tunataka nini. Basi hata kuamua tu lugha gani tutumie kufundishia watoto wetu kwenye ngazi zote za elimu yetu lakini pia tuweke msisitizo wa kuwafundisha *foreign languages not only English, French, Spanish, Arabic* na bado watoto watafaulu watatoka na elimu nzuri na bado watakuwa na *qualification* za *foreign languages* tunazozitaka, tujipange tu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la hizi programu maalum kwenye ukurasa 77, 78, *P4R, TESP* na mengine, nitoe tahadhari ile ile ambayo nilishawahi kusema kwingine *this is donor dependence* ya kutisha kabisa. *These are very special programs* (programu maalum) na ni nzuri kwa kutengeneza mfumo wetu wa elimu, lakini zinafadhiliwa kwa sehemu kubwa kabisa kama siyo sehemu yote. Ni kama vile wewe ili umlee mtoto wako mzuri atoke jirani huku aje akuambie mwanao akiwa na afya nitakupa pesa, mwanao akisoma vizuri nitakununulia gauni, mambo gani haya? Hebu haya mambo mengine tujiwekee sisi wenyewe tuone tunakwenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije nikaishiwa muda bila ya kusema suala la motisha kwa walimu na baadaye tutali-*discuss* kwa watumishi wetu wote wa umma. Jamani mwalimu anafanyiwa stihizai, anapandishwa cheo mwezi huu analipwa mshahara, mwezi unaofuata halipwi, kimya, hapelekewi barua wala hajulishwi chochote, hivi tunategemea hawa watu wafanye kazi namna gani? Mwalimu mnamtoa Kigoma mnampeleka akafundishe Mafia, hapewi nauli wala stahiki zake nyingine, mnatarajia atafanyaje kazi, hata kweli atakuwa na moyo wa kufundisha watu huyu? Watu wengine mnazungumzia mazingira magumu, wana *allowance* nyingine hazina hata na majina lakini walimu wanasahaulika. Nani awatetee hawa walimu na siyo kwamba hawana watetezi, watetezi wapo

wanasema hapa lakini nani anajali kushughulikia hayo ambayo yanasemwa kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani Mheshimiwa wifi hebu badilikeni. Kweli tunakuona mfanyaji kazi, mara hii tunazo kweli timu za akina mama, mmekaa kwenye Wizara, Mheshimiwa Ummy yuko pale na wewe na Naibu wako mmewekwa Wizara moja hebu fanyeni kazi tuone kweli wanawake mtaleta mabadiliko ambayo kweli sisi tutakaa tujivunie. Elimu tukiichezea, Taifa tumelichezea na kuliangamiza. Jamani tubadilike na tufanye kazi inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri Kivuli amezungumzia suala la wataalam wa TEHAMA na mimi pia niliseme. Mimi nilishtuka kwamba eti tunaenda kuazima wataalam kwingine waje watutengenezee programu yetu sisi, mimi nikasema *what a shame! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa kwenye Tume ya Warioba, tulipata vijana wa *IT mashallah* walitengeneza programu pale ya kurekodi zile taarifa zote, mikutano tunayofanya, *Hansard* tulichukua wataalam wa hapa Bungeni, kulitokea programu mpaka siku moja Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Salim Ahmed Salim, mwenyewe alikuwa ananiita jirani maana ofisi zetu zilikuwa *floor* moja, akaniambia jirani hawa watoto ni wa Tanzania? Nikamwambia tena mmoja ni Mpemba, walitengeneza programu mpaka mtu unashangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunaenda kuwatafuta watu wa Rwanda, sijui na watu gani. Hivi tutawasifia lini watoto wetu, tuta-*recognize* lini sifa zao na tutawa-*motivate* vipi watoto hawa? Watoto *excellent* kabisa wengine wame-*graduate* hapo *St. Joseph,* hapo hapo mlipopafunga mwaka jana, watoto wazuri, watoto ambao *TTCL* wanawagombea. Ukipeleka mtoto kufanya *field TTCL* wanamuuliza wewe ni wa *St. Joseph* au wa chuo gani, kwa sababu wanajua watoto wale wamefundishwa sio elimu ya

darasani lakini *hands on,* ile *competence base* ni kweli wamejifunza, lakini yote haya hatuyaangalii tunazidi kuwakatisha tamaa watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nilisema hapa tunahitaji *an integrated process, budgeting, planning and even understanding.* Tukiwa na uelewa wa pamoja tunapanga mambo yetu pamoja, migongano gongano hii haitakuwepo tatizo kila kipande kinatengenezwa peke yake halafu kinakuja kulazimishwa kukaa kwenye kipande kingine. Kwa namna hii hatutafika na kila siku tutakuwa tunaanza palepale kwa sababu mambo yetu tunayapanga kipande kipande halafu tunakuja kulazimisha kuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hasunga ajiandae Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata hii nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa pamoja na mambo yote mazuri ambayo yameandikwa katika kitabu hiki cha bajeti. Kwa kweli hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefarijika sana na jinsi ambavyo mmefanya uchambuzi wa masuala mbalimbali katika kitabu hiki, lakini pia nimefarijika na nimefurahishwa na jinsi ambavyo mnajiandaa kwenda kutekeleza Sera ya Elimu ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii inataka kwamba tutakapofika mwaka 2020 watoto wetu wote watakaokuwa wanamaliza darasa la saba wataenda sekondari, kwa hiyo, inahitaji matayarisho ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi naomba nijikite katika kuongelea ubora wa elimu. Ubora wa elimu ni neno pana, ubora wa elimu una mambo mengi, tunaangalia miundombinu, walimu watakaotumika katika kufundisha, maabara, vitendea kazi na vitu vinginevyo, vitabu, mitaala na mambo mengine mengi, hayo yote kwa pamoja ndio yanajumuisha ubora wa elimu. Ni nini kimejitokeza? Sasa hivi mitaala yetu mingi haikidhi mahitaji ya soko, kuanzia shule za awali, shule za msingi mpaka vyuo vikuu katika maeneo mengi haikidhi mahitaji ya wahitaji, haikidhi mahitaji yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko sokoni ni aina gani ya ujuzi unahitajika, ni aina gani ya elimu inahitajika, ni aina gani ya maarifa inahitajika, hiyo mitaala yetu lazima izingatie hayo. Kwa sasa hivi hali iliyopo mitaala mingi haizingatii hayo, mitaala yetu hii haiwaandai vijana wetu katika kupata maarifa ya kuweza kujitegemea, ndio maana watu wengi wanamaliza sasa hivi hawawezi kujitegemea. Hapa tuna kazi ya ziada ya kufanya, kama nchi lazima tufanye kazi ya ziada. Nadhani hili linahitaji *participation* ya wadau wote kushiriki katika kuhakikisha kwamba hii mitaala ambayo inakuwepo inakidhi mahitaji ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwenye upande wa vitabu, mimi naipongeza Serikali, mmetoa vitabu ambavyo bado vina mapungufu mengi, lakini angalau mmetoa, lakini mmetoa kwa ubaguzi. Utoaji wa elimu kwenye nchi hii siyo wa sekta ya umma peke yake, kutoa elimu lazima kujumuishwe sekta binafsi na wadau mbalimbali. Hivi vitabu mlivyotoa mnapeleka kwenye shule za umma peke yake, sasa shule za watu binafsi zinapata wapi vitabu? Shule zote zinatoa mchango mkubwa katika kuandaa wataalam na wanafunzi wetu. Hivi vitabu chapisheni, wekeni huko, hizo shule zinunue zitatusaidia sana katika kutoa elimu kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema kwa uchungu kwa sababu tarehe 5 Mei niliuliza swali hapa kwamba ni Watanzania wangapi ambao hawajui kusoma, kuandika na

kuhesabu. Takwimu zilizoletwa kwenye lile swali zinaonesha asilimia 22.4 ya Watanzania hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Hiyo inatuonesha ni aina gani ya Taifa tunaenda kulijenga kama Watanzania wengi kiasi hicho hawajui kusoma wala kuandika. Tunaingiaje kwenye kujenga uchumi wa viwanda tukiwa na Watanzania wengi hawajui kusoma wala kuandika? Hapa kama nchi lazima tukae chini tutafakari na tuone namna gani tunaweka mikakati ya kuwasaidia Watanzania hawa ambao hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka miaka ya nyuma tulisoma elimu ya watu wazima, ile mikakati iliyokuwepo ilitusaidia. Mimi nafikiri umefika wakati tuweke mikakati kila kijiji lazima kwenye shule zetu zile wale watu wote ambao hawajui kusoma, kuhesabu na kuandika wakafundishwe kwa lazima. Hatuwezi kujenga nchi kwamba eti wataenda wenyewe lazima wakafundishwe kwa lazima, tupate watu wote wanajua kusoma, kuhesabu na kuandika hapo ndiyo tutakwenda kujenga nchi yenye uchumi wa soko la kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa zetu inaonesha asilimia 80 na kuendelea watoto wetu kwenye shule za sekondari wanapata *division four* na *division zero* na hawa baada ya kumaliza wakiwa wamepata matokeo hivyo wanaenda wapi? Wanaenda kuchangiaje katika uchumi wa viwanda? Ndiyo maana tukasema lazima tuimarishe sekta binafsi tujenge vyuo vingi vya *VETA* viwachukue hawa viwafundishe, viwape ujuzi, viwape maarifa wakafanye kazi zitakazosaidia kufuatana na kiwango cha elimu walichonacho lakini hivi sasa ukisoma hotuba unaona mkakati bado haujatosha katika kujenga hivi vyuo vya ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Jimboni kwangu, Jimbo la Vwawa na hasa Mkoa mzima wa Songwe hakuna Chuo cha *VETA*. Nilitegemea hapa useme kwamba Mkoa wa Songwe tunakwenda kujenga Chuo cha *VETA* sijaona na kule kuna Watanzania na shule nyingi. Baadae nitakuja kujenga

hoja ya kushika shilingi kama sijapata majibu nini kinaenda kufanyika katika lile Jimbo la Vwawa na hasa Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hapa na kila siku tunapiga kelele, hivi kwa nini tuendelee tu kupiga kelele? Tumesema mtoto akipata mimba mwache akajifungue, akimaliza arudi kusoma, kuna tatizo gani? Kwani mtu akipata mimba maana yake asisome?

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Maana yake aishie tu hapo? Huyo anaenda kujenga Taifa gani? Lazima huyu mtu akijifungua, akalea mtoto kidogo, arudi kusoma, hakuna haja ya kuweka masharti, kuna tatizo gani? Nadhani tufike mahali tuwe *serious* katika *issues* ambazo ni *serious.* Hawa watoto ambao wanaishia katikati lazima tuchukue hatua, watu wote wapate elimu ya msingi ndipo tutajenga Taifa zuri na lenye maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia motisha kwa walimu. Walimu katika maeneo mengi wamekata tamaa, hawawezi kutekeleza hii mitaala, hawawezi kutoa elimu bora wakiwa na *frustrations.* Mwalimu anaingia darasani anataka kufundisha anasema lakini ana malalamiko, hapana, tujenge mazingira mazuri, mahusiano mazuri katika kuhakikisha walimu wanakuwa na motisha na maslahi na madaraja yao yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Jimboni kwangu kuna walimu wengi madaraja yao yalisimamishwa, hawapati haki yoyote. Hebu liangalieni hilo ili angalau mambo yaende vizuri na tuweze kujenga Taifa ambalo ni zuri lenye manufaa na ambalo litatusaidia sisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka pia nizungumzie suala la ile Idara ya Kudhibiti Ubora wa Elimu. Ile idara, nimeangalia kwenye bajeti, imepewa shilingi bilioni 30 na kitu hivi lakini katika zile fedha ni za mishahara, fedha za

undeshaji ni shilingi bilioni 3.7 lakini kama watapewa, wanaweza wakafanya kazi kidogo. Sasa hivi ile idara haipewi fedha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaenda kwa Mheshimiwa Kakunda wajiandae Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Suala hili linalozungumzwa hapa la sekta ya elimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote ile, siyo Tanzania peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mengi hapa na Waheshimiwa Wabunge na mengine kwa kweli yanahusu masuala ya maadili. Na mimi nitapingana kidogo na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni wanaharakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo sheria nyingi sana hapa nchini nzuri sana, mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa miaka ya 1990 ndipo yalipotokea mapinduzi makubwa sana ya sayansi na teknolojia, tukawa na *tv* na simu na hizi zimeleta matatizo makubwa sana kwenye mmomonyoko wa maadili ya vijana wetu. Kutokana na mmomonyoko wa maadili ulivyokuwa unatishia haki za wanawake na haki za watoto. Mwaka 1998 ilitungwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, Sura ya 101 ya Sheria za Tanzania. Sheria hiyo ni muhimu sana, isipokuwa tatizo letu sisi hapa Tanzania, tuna sera na sheria nzuri lakini zimekuwa hazitekelezwi. Matokeo yake tunakuwa tunapigia kelele jambo ambalo linaweza likadhibitiwa na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ilirekebisha baadhi ya vifungu kwenye *Penal Code* (Sheria ya Kanuni ya Adhabu) na ikaweka utaratibu mzuri wa namna ya kushughulika na masuala ya maadili kwa

ujumla. Makosa yanayofanywa na mwanaume, yanayofanywa na mwanamke, yamewekwa vizuri sana na adhabu zake zimewekwa vizuri sana, lakini utekelezaji hafifu wa sheria hiyo ndiyo maana unakuta baadhi ya Wabunge hapa wanasimama wanaanza kupiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumepitisha sheria hapa ambayo inadhibiti mtu yeyote anayedunga (anayempa) mimba mwanafunzi, anayeozesha mwanafunzi, anayekwenda kwenye harusi ya mtoto mwanafunzi adhabu zake ni kifungo cha miaka 30. Sasa hata hatujasimamia utekelezaji wa sheria hiyo tunasimama hapa tunasema watoto wenye mimba waruhusiwe kusoma, sawa, lakini tukipitisha hapa sheria ikasema kwamba watoto wanaopata mimba shuleni waendelee kusoma maana yake ni kwamba wote watapata mimba...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Na hiyo itakuwa ni hatari, aidha, wote au walio wengi. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifuatilia vizuri hizi sheria zenyewe zinadhibiti. Kwa mfano, kwenye Ilani ya Uchaguzi tumesema kwamba mtoto aanze kusoma darasa la kwanza mpaka amalize *form four.* Huyo mtoto ambaye atamaliza *form four* yuko chini ya miaka 18 ni yupi? Taratibu tukizifuatilia vizuri, anayedunga mimba miaka 30, ambaye anaacha shule naye vilevile atafutiwe adhabu kwa sababu tunapitisha sheria hapa tuwe na utaratibu mtu aanze darasa la kwanza hadi amalize *form four.* Akimaliza *form four* ameshafika miaka 18 basi hapo tutakuwa tumetatua tatizo la mimba mashuleni na kila kitu.

Kwa hiyo, naomba sana iwe tu kwa yule aliyebakwa, kama kuna ushahidi kwamba amebakwa, hapo kwa kweli inabidi tuwe na hatua zile za kuruhusu kwamba aendelee na shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie masuala ya Jimbo langu la Sikonge. Kule kwetu Sikonge, naomba Mheshimiwa Waziri asikie, bado tunahitaji shule mpya, zile shule ambazo zilijengwa kwa mpango wa MMEM zilitusaidia sana lakini bado tuna maeneo mengi yanahitaji shule mpya kabisa na sisi Halmashauri hatuna uwezo wa kujenga shule mpya na Serikali imeondoa utaratibu wa kujenga shule mpya, hapa ametamka shule sijui tatu au nne katika maeneo maalum. Mimi naomba aiweke Sikonge katika utaratibu wa Serikali kusaidiwa kujenga shule mpya, tuna maeneo takribani 30 ambayo yanahitaji shule mpya. Watoto wetu wanatembea kilometa tisa, kumi, kufuata shule na ni wengi. Kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie, iturudishie mpango wa MMEM maalum kwa ajili ya Wilaya yetu ya Sikonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mafunzo ya ufundi. Sisi Sikonge tuna maeneo mazuri mawili, naomba Wizara ya Elimu iwasiliane na Halmashauri yangu ili kusudi tuone *potential* hizo mbili, mojawapo kijengwe Chuo cha Ufundi cha *VETA*. Tayari tumeshawekeza baadhi ya fedha katika maeneo hayo, ni suala la kuendeleza tu, kuna chuo cha *FDC* pamoja na Kituo cha Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo napenda kuongelea ni mgawanyo wa walimu. Baadhi ya maeneo hapa nchini yamekuwa yanaathirika sana katika matokeo kwa sababu ya mgawanyo wa walimu ambao hauko sawa. Kuna baadhi ya maeneo ya nchi hii yana ziada ya walimu na baadhi ya maeneo yana upungufu mkubwa wa walimu. Kwetu sisi Tabora tuna upungufu mkubwa sana wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana katika maeneo ambayo yana ziada ya walimu wapunguzwe waletwe Tabora na maeneo mengine ya nchi ambayo yana upungufu wa walimu yafanyiwe hivyo hivyo kama ambavyo napendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kusema mengi sana, haya yanatosha, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Hongoli wajiandae Mheshimiwa Ndaki na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Elimu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake mzuri kabisa wa kuamua kujenga mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mabweni haya yamejengwa kwa shilingi bilioni 10 na yataweza kutosha kuwa-*accommodate* wanafunzi 3,840. Nimpongeze sana kwa jitihada hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nimpongeze Waziri wa Elimu na Naibu wake na pia Katibu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu na kupitia elimu hiyo tuweze kupata maendeleo katika nchi yetu maana bila elimu hakuna maendeleo. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kama walivyosema wenzangu ni msingi wa kila kitu. Elimu ndiyo msingi wa maisha, bila elimu hakuna maisha. Kwa hiyo, ili tuweze kupata elimu nzuri ni lazima kuwepo na mwalimu, miundombinu mizuri lakini pia ni lazima tuwe na vitabu vya kufundishia na kujifunzia. Mimi nizungumzie juu ya walimu, walimu tunao japo tuna upungufu lakini kuna changamoto nyingi ambazo wanakabiliana nazo na ndiyo maana unakuta sasa inapofika katika kupata ile *outcome* tunakuwa na matatizo kwa sababu hatujawaweka vizuri walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema Waheshimiwa Wabunge hapa juu ya madeni ya walimu. Haya madeni ndiyo kikwazo katika utoaji wa elimu bora. Kwa wale waliowahi kuwa darasani (walimu) wanajua, mwalimu ili aweze kufundisha vizuri ni lazima awe vizuri *psychologically.* Huwezi kutegemea mwalimu akafundisha vizuri na

akawawezesha watoto kupata elimu nzuri kama *psychologically* yupo *disturbed.* Mwalimu anapokuwa na madeni, mwalimu anapokuwa na kero mbalimbali za kwake binafsi ni vigumu kufundisha vizuri. Anaweza akaingia darasani akajipanga kutaka kufundisha vizuri wanafunzi lakini akikumbuka tu deni wakati anaendelea na jukumu la kufundisha, tayari huyu mwalimu hataweza kufundisha vizuri wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuipongeze Serikali mmeanza kulipa lakini bado *speed* ya ulipaji wa haya madeni sio nzuri sana. Tumeambiwa hapa na Kamati imetoa taarifa kwamba madeni ya walimu ambayo wanaidai Serikali mpaka sasa ni shilingi trilioni 1.6 na madeni yaliyolipwa ni shilingi bilioni 33.1 ambayo ni sawa tu na 32%, *speed* hii bado ni ndogo. Tuiombe Serikali iweze kulipa madeni haya. Tunajua madeni yanazidi kuongezeka kwa sababu wanapopandishwa madaraja madeni yanaongezeka na kwa kuwa yanaongezeka ni vizuri yalipwe mapema haya mengine ambayo yapo ili kupunguza sasa walimu wengi ambao wanakuwa *frustrated. (Makofi)*

Mheshimia Mwenyekiti, hali iliyopo sasa hivi na ukizingatia kuna mambo haya ya vyeti *fake* na ukaguzi na walimu wengine wameambiwa kuna baadhi ya vyeti havipo halali na hawajajua hatma yao. Kwa hiyo, hali iliyopo sasa hivi kwenye mashule walimu wengi hawafundishi bali wanahudhuria madarasani wanaofundisha ni wachache. Wengi wao wamekuwa *disturbed* na haya madeni na vyeti *fake.* Kwa hiyo, naomba Serikali yangu Tukufu tujaribu kujipanga kulipa madeni haraka lakini pia na hili zoezi la vyeti *fake* hili liweze kukamilishwa haraka ili walimu waingie darasani wafundishe wasiingie darasani kuhudhuria tu vipindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali na Waziri nafikiri anaelewa vizuri naposema mambo haya. Nafikiri atayashughulikia vizuri ili walimu wetu waweze kuendelea kufundisha na hatimaye tuje kuweza kutoa elimu bora. Tusipofanya hivyo, tutaendelea kuwaweka wanafunzi shuleni

wanashinda wanacheza, wanakula chakula, wazazi wanafikiri watoto wanasoma kumbe hawasomi. Hata walimu wakuu wanafikiri walimu wanaingia darasani kumbe humo darasani hawafundishwi, mwisho wa siku matokeo yake yatakuwa ni mabaya. Kwa hiyo, niombe tukamilishe hili zoezi la vyeti *fake* lakini pia tukamilishe kulipa madai ya walimu ili walimu wetu hawa waweze kufundisha vizuri darasani na watoto wetu waweze kupata elimu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine upande wa walimu pia, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu katika shule zetu za msingi ukilinganisha na sekondari. Shule nyingi hazina walimu wa kutosha, vivyohivyo na hii inaathiri matokeo, inaathiri mwisho wa elimu kwa ujumla. Kwa hiyo, tuombe mamlaka zinazohusika ziajiri walimu. Tumeshaona kwenye hili zoezi la vyeti *fake* nalo limeondoa walimu wengi sana hasa wa shule za msingi. Ukiangalia idadi kubwa ya walimu wenye matatizo ya vyeti *fake* ni wale walimu wanaofundisha shule za msingi, kwa maana hiyo tufanye *replacement* haraka ili ku-*rescue situation* inayoendelea kwenye hizo shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa elimu maalum kwenye shule zetu hasa shule zetu za msingi. Kwa mfano, kwenye Halmashauri yangu mimi tuna shule moja pale ya Matembwe ambayo yenyewe ni shule jumuishi, inachukua wanafunzi ambao wana ulemavu tofauti tofauti, lakini tuna mwalimu mmoja tu anayefundisha kwenye ile shule. Kwa hiyo, tuombe tupeleke walimu wa kutosha na pia vifaa vya kutosha kwenye elimu hii jumuishi ili watoto hawa ambao wana ulemavu tofauti tofauti waweze kupata haki yao ya msingi, haki yao ya kupata elimu kama watoto wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema juu ya *drop outs* hasa hizi kesi za mimba kwenye shule zetu. Ukiangalia shule nyingi ambazo watoto wanapata mimba ni zile shule za kutwa, shule hizi za kata. Kwa nini wanapata mimba? Ni kwa sababu ya ukosefu wa mabweni. Watoto wengi wa kike wanatembea umbali mrefu sana na tunajua watoto

wetu wa siku hizi hawawezi kutembea kama tulivyokuwa tunatembea sisi zamani. Kwa hiyo, kinachotokea ni kwamba wanatumia usafiri wa bodaboda maeneo mengine wanatumia *taxi.* Hawa wanaowapeleka shuleni ili waweze kuwahi vipindi ndio hao wakati mwingine wanawageuka kuwashawishi watoto kuingia kwenye hivyo vitendo vya ngono na mwisho wa siku wanapata mimba na wengine wanapata maambukizi ya UKIMWI na wengine wanaamua kuacha shule kwa sababu tayari wameshapata wapenzi na wanaenda kuolewa. Tunaipongeza Serikali kwa mpango huu wa kujenga mabweni.

Naomba pia katika Jimbo langu na katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Njombe na shule za kata za kutwa ambazo watoto wengi wanatembea umbali mrefu, katika ule mpango wa ujenzi wa mabweni basi na mimi nipate mabweni ili tuwaokoe watoto hawa ambao wanatembea umbali mrefu tuwakinge na mimba ambazo wanaweza wakazipata kutokana na vishawishi wanavyovipata njiani wanapoenda kwenye shule hizi za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia umbali unachangia wanafunzi wetu kufeli. Wanatumia muda mwingi kutembea kwenda shuleni, anapomaliza kipindi anafikiria kuanza kutembea kwenda nyumbani na akifika nyumbani anakutana na shughuli za nyumbani kwa sababu ni watoto wa kike wanapewa shughuli za pale nyumbani za kupika, kutafuta maji, za kutafuta kuni lakini mwisho wa siku utakuta huyu mtoto anapoteza muda mwingi wa kusoma. Kumbe akibaki bwenini anapata muda mwingi wa kusoma na kufanya *discussion* na wenzake jioni mwisho wa siku atakuja kufaulu vizuri. Kwa hiyo, nashauri tujenge mabweni kwenye shule zote hizi za sekondari ili watoto wetu waweze kusoma vizuri na hatimaye waweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitishwa sana kwenye suala la vitabu. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuamua kutoa kitabu kimoja nchi nzima cha kufundishia *(text book)*. Nipongeze kwa jitihada mlizochukua, lakini nisikitike kwa

kutoa vitabu ambavyo vina makosa, ni aibu kubwa sana wakati tuna wataalam wameajiriwa, wanafanya *editing* ya hivi vitabu, inakuwaje vitabu vingi namna hii vinakuwa na makosa mengi ya *spelling,* ya kisarufi na makosa mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe ndugu yangu, dada yangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako, tukae na watu wa *editing* ili tujue nini kimetoea? Maana tumetumia fedha nyingi na itatakiwa tubadilishe tutatumia gharama kubwa, watuambie ni kwa nini wamekubali kutoa vitabu hivi ambavyo vina makosa? Haijawahi kutokea katika miaka yangu yote ya kusoma kwangu na katika maisha yangu yote kupata mwaka ambao vitabu vimetoka na makosa mengi namna hii, zaidi ya vitabu vya masomo karibia matano, sita, vina makosa!

Kwa hiyo, hebu tukae tujue kuna nini kimetokea? Inawezekana hao watu wanaohusika na *editing* walitaka kuhujumu tu Serikali ili kuonesha kwamba Serikali yetu haifanyi kazi vizuri. Nakuamini dada yangu, naomba kakae na hii Kamati au Kitengo kinachohusika na mambo ya *editing* ya vitabu ili tujue ni kwa nini wametoa vitabu vyenye makosa namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaki, ajiandae Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya kwenye Wizara hii, mapinduzi makubwa yamefanyika kwa muda huu wa mwaka mmoja ambao amekaa hapo. Tumeona kwenye hotuba yake hapa vitu vingi

vimefanyika vikubwa vikubwa ambavyo siku za nyuma vingechukua labda miaka mingi sana lakini kwa muda mfupi amejitahidi. Nichukue nafasi hii kwa kweli kumpongeza sana kwa juhudi anazoendelea nazo. Naamini kwa muda atakaokuwepo kwenye Wizara hii mabadiliko makubwa yatakwenda kutokea kwa sababu ni mama anayejitahidi sana; ni mama anayejali na ni mama kwa kuongea anamaanisha, lakini pia vitendo vyake tunaviona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu mwaka jana nilipeleka maombi ili kunisaidia kwenye shule yangu mojawapo ili iweze kupata kibali hatimaye iwe *A-Level.* Alinisaidia akanipa kama shilingi milioni 100 na zaidi, tukajenga bwalo na mabweni ya wanafunzi tayari yamekamilika na mwaka huu tumepata kibali cha kuingiza watoto wa kidato cha tano. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kutoa mchango wangu kuhusiana na ukaguzi wa shule kwenye maeneo yetu. Ukaguzi wa shule ni muhimu sana kwenye nchi yetu na kwenye shule zetu kwa sababu kwa huo ndio tunaelewa ubora wa elimu yetu inayotolewa huko mashuleni. Hata hivyo, Kitengo cha Ukaguzi kuanzia huko Taifa mpaka huku chini Wilayani kina hali sio nzuri sana. Nichukue mfano wa kitengo hiki kwenye Wilaya yangu ya Maswa. Wilaya yangu ya Maswa kitengo hiki hakina miundombinu inayotakiwa ili kiweze kufanya kazi yake vizuri. Kwanza wako kwenye kaofisi kamoja ambapo wamejibana, lakini pia vifaa hawana, wana gari moja ambalo limezeeka sana na ni gharama kubwa kulifanyia *maintenance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua hali iliyoko kwenye kitengo hiki, vifungu au mafungu ya fedha yanayopelekwa kwenye ukaguzi wa elimu ni kidogo sana kiasi kwamba hawawezi kwenda *field* na kukikuta gari bovu kama ilivyo kwenye Wilaya yangu ndiyo hali inakuwa ngumu kabisa. Hawawezi kufanya *maintenance,* hawawezi kununua mafuta, hawana posho ya kujilipa wanapokwenda kukagua

kwa hiyo, ubora wa elimu kwenye maeneo yetu unakuwa ni wa mashaka mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Kitengo cha Ukaguzi kwa shule zetu, shule za msingi hata shule za sekondari kiboreshewe mazingira yake. Wapewe usafiri unaowezekana kusafiri kwenda kwenye shule kukagua, wapewe vifaa vinavyohitajika, wapewe posho yao, wapewe mafuta, kama hawapewi watafanyaje kazi hizi, itakuwa ni ngumu sana. Gari lililopo pale kwenye Wilaya yangu halina matairi, halifanyiwi *maintenance,* hawa watu wapo tu pale ofisini. Pamoja na kwamba wako wachache lakini wangeweza kujitahidi angalau basi kuzitembelea baadhi ya shule ili waangalie ubora wa elimu inayotolewa pale, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nizungumzie ni hii Tume ya Walimu, sijui kama iko sehemu ngapi, kama iko kwenye Wizara yake, Wizara ya Utumishi au Wizara ya TAMISEMI. Hii Tume ya Walimu na yenyewe ina matatizo lukuki. Hawa Tume inatakiwa akituhumiwa mwalimu waende kwenye eneo la kazi la yule mwalimu, lakini hawaendi kwa sababu pia wanapokea pesa kidogo. Wakienda pia wanatakiwa baada ya kubaini mashtaka aliyonayo warudi waje wafanye kikao ofisini (kikao cha Tume), lakini hawawezi kufanya vikao vyao vya Tume kwa sababu pia hawana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake unakuta mwalimu ametuhumiwa, ameandikiwa mashtaka wamemtembelea lakini hawawezi kumwita kuja kufanya naye kikao kwa sababu fedha hazipo kwenye Tume hii ya Walimu na kwa hiyo, mwalimu huyo anakaa analipwa nusu mshahara kwa sababu anapotuhumiwa anasimamishwa analipwa nusu mshahara muda mrefu. Kwenye Wilaya yangu ya Maswa kuna walimu kama wawili, watatu hivi, wamekaa sasa kama mwaka nzima hawajasikilizwa, wanaendelea kulipwa nusu mshahara. Kwa kweli naomba sasa Wizara hii ya Elimu iweke mpango madhubuti ya kuimarisha Tume hii ya Utumishi ya Walimu ili iweze kuwasaidia walimu hasa wale

wanaopata matatizo na kama mtu kesi yake haieleweki basi imalizwe mapema halafu aendelee kufanya kazi yake vinginevyo kwa mafungu wanayopewa hawawezi kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni majibu wanayosubiri walimu ambao Tume imekwishapeleka hoja zao huko Makao Makuu wanasuburi muda mrefu sana. Wengine wanaposubiri hata barua zinaporudi ili aje arudishwe kazini inachukua muda mrefu mno, lakini ana barua ambayo iname-*clear* mashtaka yake lakini bado kurudishwa kazini inakuwa ni ngumu sijui utaratibu huu unakuwaje. Maana inakuwa pale kwa Afisa Utumishi anaambiwa subiri, subiri, subiri. Nashauri utaratibu huu uangaliwe upya ili tuwarahisishie walimu hawa wanapopata matatizo lakini pia matatizo yao yapogundulika hayapo basi warudishwe kazini haraka iwezekanavyo na stahili zao waweze kupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine nataka nizungumzie kuhusiana na *FDC. FDC* kuanzia mwaka jana Mheshimiwa Waziri alituambia zimerudi kwenye Wizara yake. Hivi *FDC* (Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi) huko kwenye maeneo yetu vina hali siyo nzuri sana. Nichukue mfano wa Chuo cha Maendeleo ya Wanachi cha Malampaka kule kwenye jimbo langu kina miundombinu ambayo imezeeka sana. Mheshimiwa Waziri hiki Chuo cha Maendeleo ya Jamii kimetoka kilipokuwa *middle school* kikageuzwa kikawa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Kwa hiyo, majengo yake ni ya zamani sana, yamechakaa lakini haya hajakarabatiwa na samani zilizoko pale na zenyewe ni za zamani sana zingine zimevunjika, hazina thamani kama jina lake lilivyo. Hivi vyuo kwa sababu vimerudishwa kwake Mheshimiwa Waziri basi naomba aviangalie kwa maana ya kuvipatia vitanda na samani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na cha Malya.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mwenzangu ananikumbusha hapa, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi

cha Malya pia kina matatizo yale yale. Hiki chuo nachokizungumza cha Malampaka kina walimu wawili tu na kinatakiwa kiwe na walimu 26; hakuna usafiri na vifaa vya kujifunzia.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri anapojumuisha ajaribu kuviangalia hivi vyuo pia kwa sababu vimerudi kwake basi viweze kuwasaidia wananchi wetu huko tuliko. Maana vyuo hivi ndiyo mkombozi sasa kwa watoto wetu wale wanaomaliza *form four* wale wanaomaliza darasa la saba ili wajifunze elimu ya kiufundi na elimu mbalimbali iweze kuwasaidia kwenye maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimazilie kwa kusema ahsante sana kwa kunipa nafasi lakini pia naendelea kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri kwa sababu amefanya juhudi kubwa sana kwa kweli hasa kwenye shule yangu ya sekondari ya Malampaka, tuna hali nzuri sasa hivi na tunaanza *A-level,* lakini kama alivyomtuma Katibu wake Mkuu alipofika pale aliahidi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara wajiandae Mheshimiwa Anna Gidarya na Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Nianze kwa kutoa pole sana kwa wananchi wangu wa Jimbo la Ukonga kwa mafuriko ambayo yametokea kwenye kata za Msongola, Chanika, Zingizingiwa, Gongo la Mboto, Pugu, Buyuni na Majohe ikiwepo na Kivule. Hali ya usafiri ni mbaya sana lakini wavumilie kwa sababu tumeshachukua hatua kwamba baada ya mvua hizi tutafanya ukarabati ili barabara zirudi katika hali yake ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitoe pole kwa kufariki Mchumi wa Manispaa ya Ilala ambaye alikuwa pia

Katibu wa Mfuko wa Jimbo la Ukonga. Nampa pole sana Mheshimiwa Mkurugenzi na watumishi wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala akiwepo Mstahiki Meya tupo pamoja nao na tunamtakia Mungu ampe pumziko la amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwalimu wa masomo ya hesabu na *chemistry* na leo nimekusudia kuchangia kitaaluma zaidi. Ningeanza kwa kusema huwa napata shida sana, yako mambo Waheshimiwa Wabunge wanachangia humu ndani, wanazungumzia habari ya elimu lakini inabidi urudi kule kwenye TAMISEMI. Kwa nini Wizara isingeitwa Wizara ya Elimu na mambo yote yanaendana na elimu ili tumuulize yeye, ingekuwa ni rahisi sana. Kama tunazungumza habari ya shule, miundombinu, mahitaji maalum iwe yeye Waziri wa Elimu ndiyo unahusika. Kwa sababu tunazungumza habari ya matundu ya vyoo mpaka tukamuulize TAMISEMI, kwa hiyo, kidogo inaleta shida naomba mliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja ya madai ya walimu. Mheshimiwa Waziri kama ana nia ya kutaka kufanya kazi ambapo mimi sina shaka na uwezo wake, yeye siyo mwanasiasa labda aanze kujingiza kwenye siasa ambayo kimsingi siyo fani yake. Kama anataka kufanya kazi vizuri hebu achukue kitabu cha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, achukue kitabu cha Maoni ya Kamati ajifungie avipitie atamaliza matatizo yaliyopo hapa. Wala ahitaji kuzunguka sana humu, achukue Maoni Kambi Rasmi ya Upinzani na Maoni ya Kamati akiyafanyia kazi mwaka ujao ataonekana Waziri bora kabisa wa Elimu katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walimu wanadai shilingi trilioni 1.6 mpaka sasa wamelipwa asilimia mbili tu. Kwa hiyo, unapozungumzia kuboresha elimu lazima uzungumze kuondoa kesho na malalamiko ya walimu katika nchi hii. Kwa kweli imekuwa ni fedhea sana, ni kwa nini wataalam wa kada zingine hawalalamiki sana. Ukienda kwa madaktari wanalipwa, wanasheria wako vizuri sana, kwa nini kuna shida sana kwa walimu? Kwa hiyo, nadhani hili

jambo kwa kweli ingefika mahali mkalimaliza mtamaliza shida ya walimu na walimu watafundisha vizuri kwa kupata stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamesahihisha mtihani wa *form two* tangu mwaka jana mpaka leo hawajalipwa. Kuna walimu wameenda likizo, madaraja wanalalamika sana tumekutana nao Mheshimiwa Waziri na hivi vitu ni vitu *genuine.* Kwa hiyo, ni muhimu mkayafanyia kazi, akija kwa Waziri anarudishwa TAMISEMI, TAMISEMI inaenda kwa Mkurugenzi. Wakati mwingine mwalimu anadai madai yake anafunga safari kutoka sehemu ya mbali anakuja Halmashauri anaambiwa faili limepotea na huyu ni mtumishi wa umma. Nadhani mngepunguza kero kwa walimu hawa mgetusaidia sana sisi ili mambo shule yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna hoja hapa ya Bodi ya Mikopo. Nilikuwa nataka niseme lakini yupo Mheshimiwa Ester Mmasi, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi mna shida, ilipokuja hoja hapa ya Bodi ya Mikopo, Waziri mlipambana na Mheshimiwa Mwenyekiti ulikalia Kiti mkatupa maoni yetu kabisa. Wanafunzi hao ambao wengine wanasoma na wengine wanaendelea kufanya kazi wanatakiwa kulipa fedha ya mikopo walikubaliana na Serikali kulipa asilimia nane, imetungwa sheria hapa ambayo inafanya kazi kisengere nyuma wanakatwa asilimia 15 na wameshaanza kukatwa wanalalamika. Kuna mwalimu ambaye anakatwa mpaka mwisho wa mwezi anaondoka nyumbani na shilingi 80,000 au shilingi 100,000 sasa unamfanyeje? Hakuna usafiri, nyumba za walimu, inabidi akodi wakati mwingine bodaboda au *taxi* aende shuleni. Kwa hiyo, ninyi mmetengeneza mazingira magumu sana kwa kuwahukumu walimu ambao humu Bungeni hawamo na tulipinga mkapitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya bure, juzi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alisema kwamba mpango huu ni nzuri, hatukatai mpango ni mzuri, kweli idadi ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza wameongezeka sana. Sasa shida inakuja nataka mnisaidie,

kuna shule moja ya kule Dar es Salaam katika mtihani wa *form four* waliopata *division one* walikuwa *zero*, d*ivision two* walikuwa watano, *division three* walikuwa 17, *division four* walikuwa 70 na *division zero* walikuwa 105. Kwa hiyo, asilimia 11 ndiyo ilipata daraja la kwanza na la pili, asilimia 88.8 walipata *zero* na *four.* Sasa naomba mnijibu, hawa *division four* na *zero* wako wapi? Wameenda shuleni miaka minne badala ya kwenda kupata uelewa, wameenda kukua kimwili, wako wapi hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya pili, *division one* hakuna, *division two* wanne, *division three* wapo 11, *division four* ni *69* na *zero* 35. Wanafunzi 15 ndiyo waliopata daraja la kwanza na la pili na daraja la tatu na la nne 104, hawa wako wapi? Shule nyingine *division one* wapo wawili, *division two* wapo wawili, *division three* wapo 18, *division four* wapo 57, *division zero* wapo *zero* 97, wanafunzi154 ni *four* na *zero* hawa wako wapi? Ukifanya utafiti taarifa hii inasema asilimia 88 wamepata *division* zero na *division four*. Mtusaidie hawa Watanzania walio wengi wameenda wapi. Kwa hiyo hoja inazungumzwa ni kweli kwamba watu wameongezeka lakini kimsingi ubora wa elimu ambayo wanaipata siyo sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii elimu ya bure, mimi sijui kiswahili labda kwa sababu ni Mkurya, Waziri wa TAMISEMI juzi kasema walichofanya Serikali ni kuleta elimu ya msingi bila malipo. Hivi elimu ya bure na elimu bila malipo kuna tofauti gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitendo hicho kimekwaza wazazi wengi sana, wamekubali hawachangii chochote lakini mashuleni kuna *tuition* zinaendelea, kuna *remidial classes* na kuna mitihani inafanywa. Kwa hiyo, kuna ubaguzi, wale wazazi wanaoweza kuchangia wanachangia wale ambao ni wenzangu na mimi watoto wao hawasomi. Kwa hiyo, tayari mashuleni kuna matabaka. Ni muhimu mkaja na mpango, kama wazazi wanatakiwa kuchangia msizungukezunguke kutafuta lugha ya kudanganya. Waambieni Serikali imeondoa ada, michango mingine ni

halali, mshiriki kuboresha elimu ili watoto wasome vizuri kwa *standard* ambayo inaeleweka. Mtakuwa mmetibu tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu heshima ya walimu, kumekuwa na tabia, sasa hivi kidogo imetulia tuliisemea sana kwenye Kamati ya TAMISEMI, kitendo cha walimu matokeo yakiwa mabaya wanawajibishwa wao. Kitendo hicho kimewakwaza walimu sana tungependa waheshimiwe kama wataalam wengine. Kama kuna makosa wapelekwe kwenye vyombo vinavyohusika ili wachukuliwe hatua ambazo zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtihani wa darasa la saba. Maswali ambayo yanatungwa katika mtihani wa darasa la saba ni ya kuchagua. Nimewauliza walimu kwa nini matokeo ni mabaya, wanasema Serikali imeleta asilimia 20 ya *pass* wakati wa Kikwete, kwa Magufuli wamesema ni asilimia 30, watoto hawa wanapewa maswali ya kuchagua, ana ana doo. Ndiyo maana shuleni kweli kuna watoto ambao ni *form two* hawajui kusoma na kuandika kwa sababu ameandika jibu ni "A" lakini ukimuuliza "A" umeipataje hawezi kukueleza.

Kwa hiyo, walimu wanalalamika wanasema maswali yasiwe ya kuchagua, wapewe maswali ya kuandika, watoto wapimwe uwezo, yule ambaye anaenda sekondari aende ambaye haendi mpeleke *VETA* wasipoteze gharama na muda. Katika jambo hili Mheshimiwa Waziri naomba isifanyike siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nizungumze hapa ni kwamba kuna upungufu wa walimu wengi sana hasa wa masomo ya sayansi na hisabati. Hata kwenye *Lab. Technician* kwa mfano Dar es Salaam, *Lab. Technician* wanaotakiwa ni 67 waliopo ni 7. Kwa hiyo, mwalimu anafundisha *biology, chemistry* au *physics* inabidi aende kwenye *Lab.* Shule ina wanafunzi 640 mwalimu mmoja wa *physics* awafundishe wote maana yake unamwambia kwa wiki atasahihisha madaftari 600 mzigo ni mkubwa kweli kweli.

Mheheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nah ii kazi ya kuhakiki vyeti Mheshimiwa Waziri ambapo mmesema Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawakikiwi siyo sawasawa sana. Mimi siungi mkono kwa sababu hawa ni watu ambao wanaendesha Mikoa na Wilaya ambapo kuna vyuo vikuu, kuna wataalam, wanaenda kwenye mahafali wanapaswa kuhamasisha vijana wasome. Sasa kama wewe ni Bashite namna gani utamhamasisha mtoto asome shule. Kwa hiyo, ni muhimu kila mtumishi wa umma ahakikiwe na vyeti vithibitike na walio-*forge* washughulikiwe, ndiyo tutajenga nidhamu ya taaluma ya nchi hii. Profesa hataweza kukubaliana na vitu vinavyofanyika ambavyo siyo sawa sawa*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumze ambalo mtanisaidia hapa ni uhamisho wa walimu. Ni kweli mnahamasisha mambo ya mahusiano, kuepuka UKIMWI na magonjwa mengine lakini kumekuwa na shida mwalimu kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine aidha mwanamke kumfuata mwanamume au mwanaume kumfuata mwanamke, anapewa masharti kwamba atafute mwalimu mbadilishane. Hiki kitu siyo sawasawa na yenyewe ina-*discourage* walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwanamke anafundisha Kagera, mwanaume yuko Katavi, hayo mahusiano ya hii familia yanajengwa namna gani na tunataka kuwa na malezi bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo mtu kila siku anafanya kazi anamfikiria mwenzake, mke anamfikiria mume na mume anamfikiria mke na matokeo yake hajiandai, hapitii vitabu mbalimbali, hafanyi andalio la somo na kusababisha matokeo kuwa siyo mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ile ya Maoni ya Upinzani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anna ajiandae Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nitoe pole zangu za dhati kwa wananchi wote wa Tanzania na wana wa Arusha kwa msiba mkubwa uliowapata kwa watoto wetu.

Pia naomba nipongeze hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulize maneno haya, kwa macho ya kawaida tunawaona walimu wanayo furaha, lakini katika mioyo yao walimu hawa wanaandamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa elimu ni mfumo ambao hauna tija kwa maslahi ya Taifa hili. Kumekuwa na mitaala mbadala kila Waziri anapokuwa kwenye sekta hiyo. Kila Waziri anayepewa Wizara anakuja na mitaala yake. Sasa sijui Bodi hiyo ya Elimu ina kazi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kupata elimu bora bila kuwa na afya, maji na lishe bora lakini pia na miundombinu bora ya elimu. Ni ukweli usiopingika kwamba tuna uhaba wa walimu, nyumba za walimu, matundu ya vyoo lakini pia shule nyingi za sekondari za kata hazina maabara na mabweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kutaratibu kwa wanafunzi wa shule za kata kwenda kupanga kwenye nyumba za watu binafsi hususan vyumba vinavyoitwa geto. Unawezaje kupata elimu bora kwa kumweka mtoto ambaye ana umri wa miaka chini ya 13 au 18 amepanga, anaishi mwenyewe, anaishi *group* na vijana wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe ni mashahidi watoto hawa ukweli ni kwamba wako kwenye *foolish age,* unatarajia nini? Unatarajia “A” na *zero* ngapi? Mazingira haya yaboreshwe, kama Serikali ilivyoamua kujenga shule za kata wahakikishe mabweni yanakamilishwa ili wanafunzi wetu wapate elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la uhaba wa nyumba za walimu. Kwa macho yangu nilishawahi kushuhudia walimu wanakaa kwenye nyumba za udongo. Nyumba yenye *room* tatu wanakaa walimu sita mpaka tisa, wakike watatu na wanaume sita. Hebu niambieni walimu hawa wakiingia darasani wanafundisha nini kama siyo wanawaza mazingira yale mabovu ya makazi yao na mishahara midogo na kutokulipwa pesa zao za sitahiki zao halali lakini Waziri akija hapa akiulizwa swali anasema wamelipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache kudanganyana, hawa ni Watanzania, tumewapa kazi hii. Sisi zote humu ndani ni kazi ya walimu, lakini leo hii wenzetu wa upande wa pili mnafanya siasa juu ya afya na akili za Watanzania. Kumekuwa na Taifa la vuguvugu si Taifa la watu wasomi kwa sababu kila mtu ana yake kichwani akija ni kubadilisha*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye viwango vya ufaulu. Hebu tuelezane ukweli wa mambo, mwanafunzi kutoka darasa la kwanza mpaka la saba ameshindwa kupata *marks* 100, unampeleka *form one* kufanya nini? Ana tofauti gani na baba yake anayefuga ng'ombe na yeye jioni akirudi anakunya maziwa, maana hata kusoma hajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuanze na *form one* mpaka *form four* mmepandisha daraja la ufaulu mnasema *division four* mpaka *point* 35, mmelenga kufanya nini? Mmeipeleka huko ya nini? Tunafuga watu ambao watatulemea katika Taifa hili. Tunalia na ajira za vijana, mnasema *East African Community* haiajiri vijana wa Tanzania, unaajirije Mtanzania mwenye vyeti kama hivi? Tumebaki kuwa walalamikaji, tumebaki kufanya siasa kwenye maisha ya Watanzania, kila kitu ndiyoooo, mpaka lini, hata kwenye elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa ambalo watu wake hawajali elimu hakuna uchumi, maendeleo na hakuna afya. Madaktari hawa hawa leo mnakuja na uhakiki wa vyeti *fake*

nani kawatengeneza kama sio ninyi? Alikuja Mungai nikiwa darasa la pili alifuta michezo, leo mnalia na michezo? Kwa nini mnakuwa mnakana vivuli vyenu, mnakimbia vivuli, Serikali inakimbia kivuli chake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni niende kwenye elimu ya mtoto wa kike. Tunaomba tuelimishe watoto wa kike, mtoto wa kike ni hazina. Angalieni akina mama ambao hawajasoma, kila mwanaume aliyesimama hapa mbele yake kuna maendeleo ni mwanamke amemshauri vizuri. Je, hawa wanawake wakisoma, natumai asilimia ya maendeleo itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iache utaratibu wa kutuletea elimu ya vuguvugu. Kulikuwa na mpango wa *vodafaster,* mmetuzalishia watoto wengi kupitia hao walimu wa *vodafaster* leo hii mnasema watoto hawa ni mbulula na ni vilaza, ukilaza huu mmetengeneza ninyi Serikali. Nani kautengeneza kama sio ninyi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyeti *fake,* wadau wakubwa wa kuzalisha hivi vyeti feki ni Baraza la Mitihani, hizi namba *fake* ni Baraza linagawa. Anzeni kule msianze na wale ambao siyo wahusika, alipataje namba ya mtihani, nani aliyemuandikia zile *marks* na nani aliyempa kile cheti bandia ambacho hakina alama ya twiga, ni watu wa Baraza. Mheshimiwa Waziri usimung'unye maneno ulikuwa mama mzuri sana lakini wamekuweka kwenye mtego na wamekuweka mtu kati kwenye siasa, acha siasa kwenye elimu ya Watanzania. Tunahitaji Watanzania wenye elimu na afya ya kutosha kwa sababu madaktari wanatokana na elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema hata wale walimu wa *UPE* waliofukuzwa Serikali imewatendea dhambi. Serikali wenyewe ndiyo iliwaajiri wale walimu, leo unasema sio walimu, wameishia ngazi ya diploma, wametumikia Taifa hili na walifundisha vizuri, kuna watu waliotokana na walimu hawa wa *UPE,* leo unasema hawa walimu sio? Muogopeni Mungu mkawalipe wale watu na

wengine wameshastaafu wapate stahiki zao. Msitujengee Taifa linalobeba laana kwa sababu utakapokuwa umejiwekeza kwenye laana na uhakikishe kwamba laana hiyo itakuwa inakutafuna wewe. Hatuhitaji laana ya walimu hao, walipwe pesa zao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Koshumu na wajiandae Mheshimiwa Komanya na Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba nitumie nafasi hii kurekebisha jina langu naitwa Mheshimiwa Koshuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa nafasi ili na mimi niweze kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu hususan katika Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusiana na suala la ubora wa elimu. Nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamekuwa wakichangia kuhusiana na ubora wa elimu kila mtu kwa kadri ambavyo ameweza na ni jambo zuri sana kwani kazi yetu sisi Wabunge ni kuishauri Serikali ili kuona kwamba watoto wetu wanapata elimu iliyo bora na sio bora elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja upande wa vitabu na vitabu hivi vimegaiwa sasa kwa uwiano ambao mimi nauona kabisa kwamba hatuelekei kuzuri. Ukiangalia katika Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Ilemela, kwa mfano, darasa la pili wanafunzi ni 71,000 lakini vitabu ambavyo vimepelekwa katika Wilaya ya Ilemela ni vitabu 10,465. Wilaya ya Magu idadi ya wanafunzi wa darasa la pili ni 100,000 lakini vitabu ambavyo vimepelekwa ni 12,893 na hivyo ni vitabu vya hisabati. Wilaya ya Sengerema wako wanafunzi 151,000 na vitabu ambavyo vimepelekwa ni 13,965 na hivyo hivyo na Wilaya zingine. Waheshimiwa Wabunge kama mtapenda kuendana na mimi ni ukurasa wa 152 na 153.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ugawaji huu wa vitabu siamini kabisa kwamba wanafunzi wataweza kupata elimu iliyo bora. Kwa mfano, kwenye somo hili la hesabu vitabu ambavyo vimepelekwa ukiangalia idadi yake ni vichache ukilinganisha na idadi ya wanafunzi waliopo darasani wa darasa la pili. Hivyo, kwa mahesabu ya haraka haraka utakuta kitabu kimoja wana-*share* wanafunzi hata 30 hadi 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kujaribu kuwaeleza wazazi ukweli. Kutokana na hii Sera ya Elimu Bure ya mwaka 2016 wazazi wengi sasa wamekaa wanasema kwamba Serikali inatoa elimu bure wamesahau kwamba wao pia wanaweza wakachangia katika upatikanaji wa elimu nzuri ya watoto wao. Naomba niwashauri wazazi wote nchini kwamba na wao pia waweze kuisaidia Serikali, lakini pia na Serikali itusaidie sisi Wabunge kwa kupeleka elimu kwa wazazi kupitia Walimu Wakuu na Bodi za Shule wawasaidie kuwaeleza wazazi na wao pia wasaidie kuchangia. Kwani wazazi wakichangia vitabu watasaidia watoto walau kila mmoja kuwa na kitabu chake kama inawezekana au kitabu kimoja kutumiwa na wanafunzi hata watatu hadi watano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia shule nyingi ambazo zinafanya vizuri hapa nchini Tanzania hususan shule za msingi katika elimu ya darasa la kwanza mpaka la saba ni shule za *private* lakini shule za Serikali zimekuwa ziki-*lag behind.* Kuna sababu nyingi tu ambazo zinazosababisha shule za Serikali kutokufanya vizuri zikizidiwa na shule zile za *private.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kabisa wazi kwamba mimi ni mmiliki wa shule za *private,* lakini ukiangalia katika shule za *private* tunaletewa miongozo mingi sana na mnaambiwa kitabu kimoja kitumiwe na wanafunzi watatu. Kwa kweli shule za *private* zimekuwa zikijitahidi sana kuzingatia hilo na ndiyo maana wanaofaulu kwa ufaulu mkubwa wanatoka katika shule za *private.* Naomba Serikali sasa iweke mkazo katika shule zetu, ndio tumetoa elimu bure lakini sasa kama vitabu vinakuwa ni vichache wanafunzi

hawawezi kupata elimu iliyo bora wanatapa bora elimu na kuondoka*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upungufu wa madarasa na miundombinu mingine. Ukiangalia mwaka kwa 2015/2016 uandikishwaji wa wanafunzi mashuleni uliongezeka kwa asilimia kubwa sana. Hiyo ni kutokana na sera nzuri ambayo imetengenezwa na Serikali yetu, Sera ya Elimu Bure. Sasa miundombinu bado ipo ile ile ambapo zamani wazazi walikuwa wanaogopa kupeleka watoto shuleni, madarasa ni machache, wanafunzi hawatoshei kwenye darasa yaani unakuta darasa moja wanakaa wanafunzi zaidi ya 100, mwalimu ni mmoja na wengine bado wanakaa chini. Kuna shule ambazo mpaka leo bado wanafunzi wanakaa chini. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais amesisitiza suala la kuwa na madawati na akasema Wakuu wa Wilaya ambao hawatawajibika katika shule zao kuhakikisha kwamba madawati yanapatikana watafukuzwa kazi lakini bado kuna shule zingine bado wanafunzi wanakaa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote mimi nachosema na mawazo yangu ambayo nafikiria, ni afadhali wanafunzi wakae chini, lakini wale wanafunzi wakapata walimu wa kuwafundisha na madarasa yakatosha. Walau basi tufanye kama ambavyo shule za *private* zinafanya, unakuta darasa moja la kwanza linakuwa na wanafunzi labda 45 kwenye shule za *private* na hiyo yote ni kutokana na kwamba tunafuata vizuri miongozo inayotolewa na Serikali kwa shule za *private* lakini kwenye shule za Serikali unakuta darasa moja wapo wanafunzi 100 hadi 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imejitokeza sehemu nyingi sana kama ningesema nitoe mifano nina mifano mingi hata kwa shule za mjini. Kwa mfano, kuna shule moja ipo pale Mwanza, Wilaya ya Ilemela inaitwa shule ya Isenga, darasa la kwanza mpaka la tatu wanafunzi 120 darasani. Naomba Serikali ijitahidi sana kuweza kuwekeza katika kuongeza madarasa ili wanafunzi wawe wachache na hata kama mwalimu atakuwa mmoja katika darasa ambalo lina wanafunzi wachache tunaamini kabisa wanafunzi hao

wataweza kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Kwa sababu tunaona unapoweka idadi ndogo ya wanafunzi na mwalimu akawa anaweza kumpitia kila mwanafunzi moja mmoja darasani basi wanafunzi hao wataondoka pale wakijua kusoma, kuandika na kuhesabu na hivyo kuelekea kwenye upatikanaji wa elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu bado utaendelea kwenye upatikanaji wa elimu bora na sasa nizungumzie kuhusu motisha za walimu. Walimu wanapokosa motisha kwa kweli inawa-*demoralize.* Unakuta walimu wanakuwa hawana moyo wa kufundisha kwa sababu hawapati motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali ilikuja na mpango mzuri sana wa *Big Results Now* na uliwasaidia walimu wakawa wanafanya kazi kwa kujitoa wakiamini kwamba mwisho wa siku watapewa motisha. Sasa mpango huu umeenda unalegalega tu. Naomba Wizara ya Elimu warudishe mpango huu wa *Big Results Now* na kuuwekea mkazo ili uweze kusaidia walimu kufundisha wanafunzi vizuri na hatimaye kutoa elimu iliyo bora ili waweze kupewa motisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *hardship allowance.* Wameongea Waheshimiwa wengi sana kuhusiana na maslahi ya walimu, unakuta mwalimu anatolewa kituo kimoja kupelekwa kituo kingine na anapelekwa kule ni kijijini, lakini anapofika kule anakuta hakuna nyumba, kama kuna nyumba hakuna umeme, hakuna choo yaani unakuta mazingira ni magumu kiasi kwamba huyu mwalimu hawezi kuwa na moyo hata wa kuingia darasani. Inampasa huyu mwalimu asubuhi akiamka atume wanafunzi kwenda kuteka maji kwa ajili yake. Hivi kweli tunategemea hapo tutapata wanafunzi ambao wanajua kusoma na kuandika, tutawapata wapi wakati wanafunzi hao wanatumika kwenda kuchota maji? Naomba sasa Serikali isaidie kutoa *hardship allowance* kwa walimu ambao wanapelekwa katika mazingira magumu ili waweze kupata moyo wa kufundisha wanafunzi wetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la kubadilika kwa mitaala, hiyo yote pia inapelekea kwenye kupata elimu iliyo bora. Mitaala imekuwa ikibadilika mara kwa mara, anapokuja Waziri huyu anabadilisha mfumo wa elimu na mitaala, anapokuja Waziri mwingine anabadilisha mfumo wa elimu na mitaala, suala hili linawachanganya wanafunzi. Siyo tu kuwachanganya wanafunzi bali wananchi pia wanabaki wamechanganyikiwa hawajielewi hivi wafuate mfumo au mtaala upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mitaala inapokuwa inabadilika vitabu pia inabidi vibadilishwe. Kwa hiyo, naiomba Serikali inapobadilisha mitaala vitabu viende kwa haraka sana. Kwa mfano, mwaka huu vitabu vimechelewa sana kwenda ndio kwanza vimetoka juzi tu vimesambazwa, vimechelewa sana tayari walimu walikuwa wanatumia vitabu vya zamani, wanashindwa jinsi ya wakuwafundisha wanafunzi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Koshuma, anayefuata ni Mheshimiwa Leah Komanya, wajiandae Mheshimiwa Margaret Sitta na Mheshimiwa Janet Mbene.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Elimu.

Kwanza, naunga mkono hotuba ya Wizara ya Elimu na pili naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa namna wanavyojituma kuhakikisha elimu ya Tanzania inainuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie dakika zangu nyingi nijikite katika mpango wa kuinua ubora wa elimu *(Equip Tanzania).* Nitatoa ushauri pamoja na ushauri wangu naomba Serikali nayo itanieleza imejipangaje kutatua yale ambayo mimi nitayaongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni wa miaka minne unaotekelezwa na Serikali ili kuweza kuboresha elimu katika maeneo yaliyokuwa nyuma kielimu. Mpango huu upo katika mikoa saba na Simiyu ni mkoa mmojawapo uliopo katika mpango huu. Naupongeza sana mpango huu kwani umeweza kuinua kiwango cha ufaulu katika Mkoa wa Simiyu kwa kiwango cha asilimia 30.7. kabla ya mpango huu ufaulu katika Mkoa wa Simiyu ulikuwa ni asilimia 36.7 na Mkoa ulikuwa wa 24 kitaifa. Matokeo ya mwaka 2016 kiwango cha ufaulu kimeongezeka mpaka asilimia 67.4 na mkoa umekuwa wa 14 kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Simiyu akisaidiana na Afisa Elimu wa Mkoa kwa namna wanavyoisimamia elimu na kutoa elimu mbalimbali kwa wananchi na wazazi wa Mkoa wa Simiyu. Pamoja na ufaulu huu bado kuna changamoto zilijitokeza ambapo watoto wa kike waliripotiwa kupata mimba na mimi ni mmojawapo niliyeshuhudia mwanafunzi amepata ujauzito akashindwa kuendelea na masomo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mradi huu pia ni kuinua ubora wa elimu inayotolewa hasa kwa mtoto wa kike. Mtoto wa kike katika mpango huu umemtaka amalize elimu ya msingi aendelee na elimu ya sekondari. Nikiangalia mtoto wa kike anazo changamoto nyingi sana ambazo zinaweza zikamsababisha asiweze kufaulu na kuendelea na sekondari ama akatishwe masomo yake na asiendelee na sekondari na kumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niweze kufahamu pamoja na ushauri wangu, je, Serikali imejipangaje kutokomeza yafuatayo katika mpango huu? Serikali imejipangaje kutokomeza mimba na ndoa za utotoni kwa kutoa elimu ya uzazi kwa wanafunzi? Nikiangalia katika shule zetu wataalam wa elimu ya uzazi ni wachache na sehemu zingine hawapo kabisa. Katika ajira hizi zinazotolewa za Serikali sijafahamu wakunga na manesi wataajiriwa wangapi. Naomba hilo pia liangaliwe wakati wa ajira. Tunao watumishi wa idara ya afya wanaofanya *outreach service.*

Nashauri pia waweze kufanya kazi hili kwa kwenda kutoa elimu katika shule za msingi na za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna unyanyasaji wa kijinsia na udhalilishaji wa kingono. Serikali imejipangaje katika mpango huu kutokomeza hayo? Matukio yamekuwa yakiripotiwa kila siku. Juzi tarehe 9, Mkoa wa Mara mtoto wa miaka minne amebakwa, nasikia uchungu sana. Kwa mazingira haya bado itakuwa ni vigumu kwa mtoto wa kike kumaliza shule ya msingi na kuendelea na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la ukeketaji watoto wa kike. Pia napenda kupata majibu ya Serikali imejipangaje kulishughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo ukeketaji wa watoto wa kike napenda kupata majibu, pia kuna tatizo la kutokuwa na usawa wa kijinsia katika elimu. Kwa mfano, shule ya Sekondari ya Itinje iliyopo Jimbo la Kisesa, Wilaya ya Meatu ilikuwa ya kwanza Kiwilaya, ya tatu Kimkoa, lakini shule hii ina tatizo la kutokuwa na matundu ya choo. Je, Serikali inaisaidiaje? Watoto wana hamasa ya kusoma lakini wana mazingira ambayo yanawakwamisha. Ninashauri, katika ule mpango wa *RWSSP* katika kile kipengele cha *sanitation* matenki ya maji yajengwe zaidi shuleni, ambapo matenki hayo yakijengwa lazima pia matundu ya choo yatajengwa. Kwa hiyo, ninaomba matundu hayo yakijengwa yapewe kipaumbele matundu ya watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya adhabu yanayoweza kudhuru mwili au akili ya mtoto, tumeona juzi kuna mahali imeripotiwa watoto wamefungiwa kwenye *safe* mpaka wamefariki, Serikali ina mpango gani wa kumlinda mtoto katika adhabu zenye kudhuru mwili na akili shuleni, viboko visivyo na mpangilio na kufungiwa kwenye vyumba ambavyo havina hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango, umejikita vipi katika kusaidia watoto walio katika mazingira hatari zaidi. Kwa mfano, watoto waliotelekezwa, watoto yatima, watoto

walio katika umaskini wa kupindukia. Je, mpango umejikita vipi kupata mlo mmoja kwa watoto wakati wa mchana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto walio nje ya mfumo rasmi wa elimu ambao wamepitwa na muda kutokana na kwamba wakati ule kabla ya elimu bure walikuwa wanashindwa kwenda shule kwa ajili ya michango na kadhalika. Je, Serikali imejipangaje katika elimu ya MEMKWA na elimu zingine ili kuweza kuwanusuru kuwatoa katika wimbi lile la ujinga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu pia katika kila shule waliambiwa kuandaa *business plan* ili waweze kupata angalau milioni 1.5 kwa ajili ya elimu ya kujitegemea, tayari shule zimeshaweza kupatiwa mchango huu. Naomba kujua, je, katika lile darasa la mtihani la saba, hii elimu ya kujitegemea kuna watoto wa kike ambao watapata changamoto ya kutokwenda shule wakiingia katika siku zao za hedhi na katika darasa la saba naamini bado watoto ni wadogo lakini kuna *one third* ambao tayari wameshaingia kwenye hedhi. Je, katika elimu ya kijitegemea mpango ule umejikitaje hata kununua taulo kwa ajili ya watoto hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma Shule ya Sekondari ya Wasichana Weruweru toka *form one* hadi *form four* kwa kupitia elimu ya kujitegemea, tulikuwa tukipatiwa mataulo shuleni, sikujua gharama ya mataulo toka ninaanza mpaka namaliza. Kwa maana hiyo hata hili linawezekana maana yake katika mipango hii watoto wanaweza wakafanya miradi hata ya ufiatuaji matofali, kulima na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Mbene, jiandae Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Japhary Michael kwa dakika tano, tano.

Mheshimiwa Margaret Sitta, dakika zako kumi kama kawaida.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie, pia namshukuru Mwenyezi Mungu na ninaendelea kuwapa pole wenzetu wa Lucky Vincent, shule ambayo ilipoteza wanafunzi, Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema roho za marehemu. Amen.

Naendelea kuwashukuru wananchi wa Urambo kwa ushirikiano wa wanaonipa. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wizara ya Elimu ni kazi kubwa na tumewaona jinsi ambavyo wanachakarika, ninawapa pongezi sana. Naomba tu yale tunayowapa myapokee ili yale mnayoyafanya yaendelee kuwa mazuri zaidi. Hongera, akina mama wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Kamati ya Huduma za Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Peter Serukamba kwa kweli kwa taarifa yao ambayo inatusaidia wote tunaounga mkono suala la watoto wa shule wanaopata mimba warudi shuleni. Katika taarifa yao kwa ruhusa yako, ukurasa wa 29 unasema hivi; "Kamati inashauri Serikali kutoa tamko rasmi kwamba mwongozo huo unaoruhusu wanafunzi wa kike wanaopata mimba kurudi shuleni utangazwe, uanze kutumika ili wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakifukuzwa shule kutokana na kupata ujauzito kurudishwa shuleni ili kuendelea na masomo yao. Hii itasaidia Taifa liweze kunufaika na usomaji wa watoto wa kike."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono kauli hii ya Kamati. Ninavyofahamu Kamati husika huwa inakaa pamoja na Wizara, kwa hiyo, naamini kabisa kumeshakuwa na mashauriano kati ya Wizara na Kamati kwa hiyo kilichobaki, tuiunge mkono Kamati ambayo inafanya kazi kwa niaba yetu. Tunategemea Waheshimiwa Mawaziri wakati wa kuhitimisha mtoe tamko

kama mlivyoombwa na mlivyoshauriwa na Kamati husika, watoto wetu wa kike warudi shuleni baada ya kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda Kenya, tunapokwenda kwenye nchi nyingine tunajifunza. Unayachukua yale ambayo unaona kwako yatakufaa. Tulipozungumzia wenzetu mnafanyaje kuhusu watoto wa kike wanaopata mimba, walitushangaa, wakasema jamani kwao ni historia, walishaamua zamani, Watanzania na sisi tufanye hivyo kwa sababu ni jambo zuri ambalo na litatusaidia ikikumbukwa kwamba watoto wa wasomi kama sisi tuliopo hapa na viongozi, mtoto akipata mimba tu anarudishwa shule. Wanaopata shida ni watoto wa wakulima na wasiokuwa na uwezo, tuwasaidie. Ndugu zangu, hilo halina ubishi tuunge mkono tu Azimio la Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine labda niongezee kidogo tu kuongelea mazingira wanayopatia mimba hawa watoto sisi tunayajua, ni wenzetu wajanja, wenye hela basi, halafu hao hao wanakataa, watoto lazima warudi shuleni. Kwa msingi huo tuombe, tumesikia changamoto zinazowapata watoto wa kike pamoja na umbali wa shule, tunaomba katika maazimio mengine ambayo tupitishe hapa kwamba kama Serikali ilivyochukua hatua ya kujenga maabara ichukue nguvu ile ile kuhakikisha kwamba shule ziwe na mabweni ya watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka hili suala pia liende vizuri, ndugu zangu tuulize Wizara ya Elimu imejipanga vipi kuimarisha elimu ya kujitambua katika shule. Wazazi wengine wanaogopa kuongea na watoto wao ili wajitambue kwamba ukifikia umri huu utaona haya na haya. Nawapongeza wazazi wanaofanya hivyo, kwa wale ambao hawafanyi hivyo naomba Serikali ijikite katika kuimarisha elimu ya kujitambua katika shule ili waweze kujua. O*f course* elimu hii ikitolewa itazingatia pia umri wa watoto, Serikali imejiandaa vipi kuhusu elimu ya kujitambua katika shule? Je, kuna walimu ambao wameandaliwa? Mimi naelewa,

kuna walimu wengine ukiwaambia wafundishe somo hilo hawawezi, yeye mwenyewe anaona aibu. Je, kuna walimu ambao wameandaliwa kwa somo hilo ili litolewe vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda upande wa walimu; mimi pia ni mwalimu, ndugu zangu ualimu sio mchezo, inahitaji moyo mkubwa sana, changamoto nyingi walizonazo walimu wa nchi hii ninaamini zinaweza zikatatuliwa kama chombo kilichoundwa mwaka 2015, *TSC,* chombo cha kuhudumia walimu kitafanya kazi kama ipasavyo. Najua kipo chini ya Ofisi ya Rais, Waheshimiwa Mawaziri ninyi mnaelewa, ndiyo mnaosimamia mafanikio ya elimu, kwa hiyo mshauriane na TAMISEMI jinsi gani mtaimarisha *TSC* ambayo itasaidia lakini kama *TSC* itakuwa kama ilivyo sasa hivi ndugu zangu *TSC* haijaanza kufanya kazi vizuri. Kesi nyingi za walimu hazifanyiki kwa sababu hazipati fedha za kutosha, ofisi hakuna na wakati mwingine mahali ambapo Halmashauri nyingine zinafanya chini ya Ofisi ya *DC,* tunaomba Halmashauri zote zipewe uwezo na *TSC* ziweze kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mshirikiane na TAMISEMI ili *TSC* ifanyekazi, lakini tukiichukulia kama ilivyo *definition* au maana ya mwajiri, mwajiri wa walimu ni nani? Mpaka sasa hivi ninavyojua waajiri ni 139 kutokana na idadi ya Halmashauri, *TSC* haijawa mwajiri. Sasa tunapokuwa na waajiri 139 hatuwezi kuwasaidia walimu, huwezi kujua changamoto zao kwa pamoja. Hata hii ya walimu *fake,* wangeweza kutambuliwa sana kama kungekuwa na *TSC* ambayo inampima mwalimu kabla haijampa mkataba, naomba *TSC* iimarishwe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulimaliza Wizara ya Maji, nawaomba Wizara ya Elimu nayo kabla haijasajili shule kwanza iitake shule iwe na miundombinu ya kukusanya maji. Watoto wa shule wanapata taabu sana, unakutana nao barabarani wanabeba vidumu kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu shule binafsi nami na-*declare interest,* shule binafsi zinasaidiana na

Serikali kuimarisha watoto wetu, kodi zimezidi. Kodi ni muhimu lakini zimezidi, tunaomba kodi wanazotozwa shule binafsi ziangaliwe ili na wao watoe mchango wao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba labda nisimalize kuzungumza kabla sijasema suala la *VETA. VETA* ni muhimu sana kwa wanafunzi wowote wale wa kidato chochote kile. Urambo ilikuwa na *VETA,* Wilaya ilipogawanywa *VETA* imejikuta ipo Kaliua, kama Urambo tulikobaki hatuna *VETA.* Nawasihi wapenzi wangu, Waheshimiwa Mawaziri mtufikirie Urambo nasi tuwe na *VETA* kwa sababu naamini kwamba watoto wanaomaliza kidato cha nne, wanaomaliza darasa la saba ambao hawakupata nafasi ya kuendelea kwingine, mafunzo ya ufundi yatawasaidia sana kujiajiri na kuajiriwa na hasa kipindi hiki ambacho tunataka uchumi wa viwanda, Mafundi Mchundo na wengineo wote watapatikana kupitia *VETA.* Nawasihi *VETA* ziimarishwe zaidi ya yote mtusaidie na Urambo tupate *VETA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaamini sana Waheshimiwa Mawaziri, najua kabisa mengi mnayafanya mazuri, lakini naomba mpokee yale yote yanayochangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuimarisha yale ambayo mnayafanya. Nawatakia kila la heri, akina Mama wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Janet Mbene, ajiandae Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Japhary Michael dakika tano tano. Mheshimiwa Mbene dakika kumi.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Natoa pole zangu kwa wote wale waliofiwa na watoto na familia ya Mzee Sozigwa, familia ya Mzee Mwambungu na wengine wote ambao wamepata maafa hivi karibuni, Mungu alaze pema roho zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana na kuwapongeza Wizara ya Elimu kwa hotuba nzuri, napongeza Kamati zote mbili kwa maoni yao mazuri waliyoyatoa kwa Serikali, nitashukuru na nitafurahi kuona kuwa Serikali imeyazingatia maoni yote yale ambayo yanafaa katika kuboresha huduma zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumza mambo mengi na nisingependa kuyarudia. Napenda kuzungumzia suala zima la kumuendeleza mtoto anapokuwa mdogo. Wengi tumezungumzia elimu kwa maana ya shule za msingi, shule za sekondari, vyuo na vyuo vya ufundi, lakini nataka turudi katika msingi wa kumlea mtoto ili aje kuwa mwanafunzi mzuri, aje kuwa mfanyakazi mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesahau kabisa suala la kumlea mtoto, kumjengea mtoto uwezo wake tangu akiwa mdogo kwa maana ya shule za awali. Imeonesha kabisa katika tafiti mbalimbali kuwa mtoto akianza kujengewa uwezo mzuri kiafya kwa maana ya lishe, lakini vilevile kiakili kwa maana ya kumpeleka kuanza kuchezacheza shuleni na wenzake, kuanza kujifunza ku-*interact* na wenzake, kuanza kucheza michezo ambayo inamjenga ubongo, kumfundisha utundu wa kutumia ubongo wake, anakuja kuwa mwanafunzi mzuri anapoanza shule ya msingi mpaka kwenda sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kupendekeza kuwa Serikali iwe na mkakati wa kuhakikisha kuwa nchi nzima shule za awali zinatiliwa mkazo kama ambavyo tunatilia mkazo masuala mengine ya afya na maji, vilevile mtoto aanze kujengwa akiwa mdogo. Huwezi kumtoa mtoto aliyekuwa anakaa nyumbani siku zote ukampeleka miaka saba kuanza shule kwa mara ya kwanza, atakuwa hajapata ule msingi wa kumuwezesha. Haya mambo ya *pre-school* siyo mchezo, ni sehemu ambayo inaanza kumjenga mtoto jinsi ya kuelewa vitu lakini kutafakari mambo na vilevile kuzoea ku-*interact* na watoto wa aina nyingine. Kwa hiyo, ningependa sana hili nalo litiliwe mkazo kama ambavyo tunatilia mkazo masuala mengine ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu ya watu wazima; wakati sisi tunakua kulikuwa kuna elimu ya watu wazima na ilikuwa inagusa watu wazima kwa maana ya wazee au watu wazima ambao hawakupitia shule, lakini hata wale vijana ambao kwa bahati mbaya kwa mazingira fulani walishindwa kuendelea na masomo halafu waka-*regress.* Unajua ubongo zoezi lake ni kuutumia, kuusomea, kufanyia vitu ambavyo unau-*challenge* ubongo ndiyo hata ile elimu uliyokuwa umeipata inaendelea kuwepo. Unaweza ukajikuta ulisoma halafu hata kusoma gazeti ukakushindwa kwa sababu umekaa umebweteka hutumii ubongo, kwa hiyo, wale pia walikuwa wanapewa elimu. Sasa hii elimu ya watu wazima sijaiona vizuri hapa, nimesoma imenionesha tu kuwa kuna fedha na mkakati wa kujenga uwezo au kuboresha uwezo wa taasisi yenyewe. Sijaona wapi inaonesha kule chini kwa wananchi elimu ya watu wazima itaendeshwa vipi, ningependa hilo lionekane kwa sababu ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafika mahali ambapo sasa mzazi hajui kusoma chochote, hajui hesabu, atamsimamia vipi mtoto wake kuhakikisha kuwa anafanya kazi zake za shule? Kwa hiyo, inakuwa vigumu kwa mzazi hata kusimamia mtoto masomo kwa sababu yeye mwenyewe hajui na hajiamini kuwa anaweza akamsimamia mtoto. Kwa hiyo, hilo la elimu ya watu wazima naomba lizingatiwe na lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa vya wanafunzi wanaoishi na ulemavu. Watoto wengi bado hawawezi kusoma vizuri kwa sababu wanaishi na ulemavu lakini shule hazitoshelezi kwa mahitaji ya vifaa vyao, vitabu vyao na mambo yote yanayowezesha watoto wanaoishi na ulemavu kusoma vizuri kama watoto wengine wote. Hili naomba nalo lizingatiwe, hasa sisi tunaokaa kwenye Wilaya za pembezoni, kwa kweli hili suala hatulioni kabisa. Kwa hiyo, ni kitu ambacho lazima kiwepo. Kuwachanganya watoto wakati wote siyo vibaya lakini wakati mwingine inabidi wawe *segregated* ili wapate kujifunza vizuri wenyewe kwa *pace* yao. Maana mtoto anayeishi na ulemavu wakati mwingine kwa sababu ya ule ulemavu wake ukimuweka na watoto

wengine inaweza ikawa inam-*challenge* zaidi, kwa hiyo inategemea ni *level* gani unamchanganya na watoto wengine, lakini vifaa havitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *VETA* sijui ni kigezo gani kinatumika kuweka *VETA* kwenye Wilaya zetu, Wilaya yangu ya Ileje nilifanya juhudi zangu binafsi nikapata mfadhili akanijengea *VETA* ambayo Serikali iliahidi kuwa itaichukua, lakini wakanipa masharti kuwa lazima ile ardhi iwe imepimwa na mambo mengine yote. Sasa kutokana na changamoto za kupima ardhi tunazozijua, mpaka leo huu ni mwaka wa pili, hatujaweza kupima ile ardhi na kwa hali hiyo *VETA* imesimama pale haifanyi kazi. Nataka kuwaomba, kama vile ambavyo tuliweza kuijenga bila kuwa tumepima, basi muichukue ianze kufanya kazi wakati taratibu za kupima zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu vitabu; kama ambavyo tumekuwa tukiweka mkazo sana kwenye kujenga madarasa, tukajenga maabara, tukaanza kushughulikia miundombinu ya walimu na mafao yao; shule bila kuwa na vitabu vya kutosha nayo pia ni kazi bure. Imetubidi Wabunge tufanyekazi ya ziada kutafuta vitabu kwa ajili ya shule hasa vitabu vya sekondari, hii inakuwa ngumu. Vitabu ndiyo moja ya kitu ambacho ni ghali sana katika huduma za mwanafunzi. Sasa kuniambia kuwa mimi Mbunge au wazazi peke yao wakasimamie kutafuta vitabu, hasa kwa mfano vya sayansi, vya hesabu, vya lugha, inakuwa vigumu.

Kwa hiyo, naomba sana hili suala la vitabu nalo lizingatiwe, lipewe uzito ule ule tuliotoa kwa masuala ya madarasa, maabara na mambo mengine, kwa sababu bila vitabu pia kufundisha inakuwa vigumu, walimu wanapata shida sana kufundisha bila vitabu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabweni sijui hili nalo litashughulikiwa vipi. Wilaya yangu ya Ileje haina shule ya sekondari ya bweni ya watoto wa kike hata moja. Tunazungumzia miaka 42 tangu Wilaya ianzishwe. Tunajitahidi wenyewe sasa hivi kutafuta namna ya kuanzisha shule ya

bweni ya wasichana lakini mnajua gharama za kujenga shule kwa kutegemea nguvu za wananchi labda na Mbunge wao. Tunaomba sana Wizara kama inaweza kutufikiria, watoto wa kike wengi wa Ileje wanapata mimba za utotoni na tatizo moja ni hilo kuwa wanakwenda mbali sana kusoma, wanakwenda Wilaya nyingine kwenda kusoma au wanasoma pale ndiyo wanapanga kwenye ma-*gheto*. *Gheto* za ya vijijini, *imagine* mjini ma-*gheto* yalivyo, vijijini ni mabaya namna gani. Hakuna umeme, hakuna maji, kwa hiyo wanajikuta wanasoma katika wakati mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika takwimu utakuta wasichana wa Ileje wanapata mimba za utotoni wengi, pengine hata Mkoa mzima wa Songwe sijui, lakini nazungumzia kule ambako nina uzoefu nako. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunahitaji sana Serikali myafanyie kazi, shule za wasichana za mabweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kuna suala zima la hayo Mabweni yenyewe. Mabweni yanajengwa lakini mengi hayajakamilika, mengine zile *certificate contractors* hawajalipwa, kwa hiyo, bado pamoja na kuwa kuna *hostels* chache zimejengwa lakini hazijaanza kutumika kikamilifu kwa sababu hazijkamilika na hiyo pengine ni ukosefu wa fedha au sielewi ni matatizo gani lakini kwa kweli haitusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala zima la tafiti. Tumeona hapa fedha nyingi zinatolewa kwa ajili ya utafiti, tunajiuliza hizi tafiti huwa zinaishia wapi? Kwa sababu tukija kule kwenye Halmashauri zetu bado hatuoni mazao ya zile tafiti zikatusaidia katika kuboresha mazingira ya elimu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tungependa sana hizo tafiti, kwanza hata kule kule kwenye Wilaya zetu tupate hawa watu wanaokuja kufanya utafiti au watu wetu nao wachukuliwe kufanya hizo tafiti yaani wafadhiliwe kufanya hizo tafiti, vilevile matokeo ya utafiti yanapotokea basi yaletwe na kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumezungumzwa jambo la kufundisha watoto hapa masuala ya *study* za maisha. Nataka nitoe angalizo ndugu zangu, tuna miradi mingi ya Kimataifa inayoletwa kwenye nchi zetu ya kutufundishia watoto wetu masuala ya *study* za maisha. Naomba zichunguzwe kabla hazijaanza kupokelewa, watoto wetu wanafundishwa maadili ya ajabu, watoto wetu wanafundishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ruth Mollel dakika tano, Mheshimiwa Japhary Michael dakika tano, ajiandae Mlinga, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Paresso na Mheshimiwa Juma Ali Juma pia ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nichukue pia nafasi hii kuwapa pole watu wa Arusha kwa ajili ya vifo vya Watoto wetu wa shule ya Lucky Vincent na Walimu pamoja na wafanyakazi Mungu awarehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu ina changamoto nyingi sana na mengi yameshazungumzwa. Mimi nitajikita kwenye maeneo kama matatu tu.

Kwanza ni suala la lugha ya kufundishia. Kwa muda mrefu kumekuwa na mjadala mkubwa sana kama tutumie kiswahili au tutumie kiingereza nafikiri baadae, kwa sababu tulishakubali kwamba kiswahili ndiyo lugha ya Taifa nafikiri huo ndiyo msimamo kwamba kiswahili ni lugha ya Taifa bila shaka na lugha ya kufundishia iwe kiswahili. Mpaka sasa hivi hatujachukua hatua. Tunakuwa na wanafunzi wanasoma kiswahili kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba, halafu unamtegemea mwanafunzi huyu aende *form one* akajifunze masomo kwa kiingereza! Kwa kweli huo ni mtihani mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa tumeamua kwamba kiswahili ndiyo tuwe nacho basi kazi ifanyike kubadilisha

mitaala yote ya Sekondari mpaka Chuo Kikuu tujue tuna lugha moja kwa sababu ufanisi wa lugha inamjengea hata mtu *confidence* unakuwa na *confidence* kwamba unaweza ukaizungumza lugha yako vizuri na ukaeleweka na ndiyo maana kila mara tunasema Watanzania hatupati kazi Kenya ni kwa sababu ya *confidence* ya lugha. Tunafundisha watoto kiswahili na tunategemea wafanye mambo mengine kwa kiingereza, kama tumeamua kiswahili basi tuende nacho moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali ya Awamu Tano ni Serikali ya Viwanda, nauliza hatujajua viwanda ni vipi kama ni *textile*, kama ni *agri,* kama ni nini sujui, lakini nilitegemea kwamba Wizara ya Elimu nayo itajipanga kuona kwamba sera ya viwanda ni hii na viwanda gani tunataka kuvianzisha basi Mheshimiwa Waziri aje atuambie katika kutekeleza hii sera ya viwanda ni *skills* zipi ambazo zinakuwa *imparted* kwa ajili ya baadae kutumika kama wataalam katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na hiyo ya viwanda, *labs* (maabara) ni muhimu sana na shule nyingi hazina maabara, tutakuaje sasa na Serikali ya viwanda wakati maabara zetu haziko sawa sawa? Nchi za wengine wanakuwa hata na *mobile* maabara, *mobile kits* za *lab* ambazo zinahamishika kutoka mahali pengine kwenda mahali pengine. Pengine hilo ni jambo muhimu pia la kuweza kujifunza kusudi tuwe na *mobile lab kits* ambazo tunaweza tukatembea nazo katika shule zetu na watoto waweze kafundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi na kwenye kiswahili, kiswahili ni fursa pia Wizara imejipangaje ku-*train* wakalimani kwa sababu tayari *African Union* kiswahili kimekubalika, *East Africa* kiswahili kimekubalika, Wizara imejipangaje kutayarisha wakalimani wa kiswahili kwa sababu ni ajira pia kwa ajili ya Watanzania, vinginevyo tutakuta wakalimani watakuwa ni Wakenya wamejaa kule sisi wenyewe, wenye kiswahili chetu tutabaki nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lako Tukufu lililopita, lilipitisha *bill* hapa kwamba wanafunzi wote wanaochukua *loans* wakatwe asilimia 15, wengine wameshalizungumzia na mimi nakazia hapo pamoja na hotuba ya Upinzani kwamba pamoja na kwamba hili Bunge lilipitisha *15 percent,* lakini haikuwa inatarajiwa kwamba ingerudi nyuma kuhusisha wale wanafunzi wengine wote ambao walikuwa wamesaini mkataba wa asilimia nane.

Kwa hiyo, ni maoni ya Kambi kwamba siyo sahihi kwa sababu unakuwa ume-*change position in the mid of the stream*. Mimi nimesaini nitatoa *eight percent,* tumepitisha *bill* hapa *15 percent,* hiyo isingemu-*affect* mtu ambae ameshasaini mkataba wa *eight percent,* ingehusisha wale ambao ni wapya... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Japhary Michael.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, na mimi naomba kidogo nichangie kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwenye suala la elimu bure ama elimu bila malipo. Sera hii ni sera nzuri kwa maana ya kuwasaidia Watanzania wengi ambao watoto wao walikuwa hawajaandikishwa mashuleni, kama Kambi ya Upinzani ilivyotoa hotuba yake ni hii ni sera inayohitaji tathmini ya hali ya juu ili kuwa na manufaa katika Taifa, vinginevyo inaweza ikawa ni sera yenye matatizo ambayo baadae tutakuja hapa Bungeni kuanza kusutana wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri kwamba ni lazima tuangalie namna gani tunapokea mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuangalia miundombinu ya elimu yetu, kuangalia majengo yetu ya utawala, kuangalia ikama ya walimu wetu katika kuhakikisha kwamba watoto

wanaoandikishwa wanapata elimu bora. Shida ya mfumo huu ni kwamba sasa unasababisha elimu iwe katika ubora wa hali ya chini sana na lengo siyo kuwa na mfumo ambao utaturudisha katika elimu ambayo haina ushindani. Ni lazima kuwe na ushindani kati ya elimu inayotolewa na *private school* na elimu inayotolewa na shule zetu za umma. Sasa ushindani huo haupo kwa sasa. Kwa upande wa shule zetu za umma na shule za *private* bado dhana si kuwasaidia wazazi wapeleke watoto wao katika shule za umma, dhana inawafanya wazazi sasa wapeleke watoto katika shule za *private.* Kwa hiyo, wasio na uwezo bado hawasaidiwi katika huu mfumo tulionao. Ni vizuri sana tuangalie huu mfumo kwa upana wake wa kutosha ili uwe na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu hata huko nyuma kinachoendelea sasa kilikuwa kinafanyika, kwa sababu kilichoondolewa hapa kwa upande shule za msingi ni ada ya kuandikisha wanafunzi shuleni ambayo ndiyo ilikuwa kikwazo. Kwa mfano, sekondari ni ada ya shilingi 20,000 ama 70,000 lakini kwa upande wa *tuition* ilikuwa inabebwa na Serikali mlichokitangaza ni kuondoa michango ambayo wazazi walikuwa tayari wanalipa matokeo, yake wazazi wameamua ku-*relax* hawataki kulipia michango watoto wao. Sasa hivi mmezilazimisha Halmashauri zianze kukamata wazazi na kuwapeleka polisi kuanza kuwafungulia kesi na bahati mbaya kwa sababu hamkuwa na *transitional period*, hamkujiandaa vizuri namna gani baada ya kutangaza huu utaratibu mtahakikisha kwamba ni namna gani Halmashauri zinawabana wazazi, sasa wanatumia Sheria ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kw ahiyo ni rai yangu kwako Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ni sera, zielekezeni Halmashauri zianzishe *by-laws* ambayo itawalazimisha wazazi waweze kulipia watoto wao na kama hawawalipii waweze kuadhibiwa kwa Sheria za Halmashauri zisizozidi shilingi 50,000 kuliko sasa kuwapeleka Polisi *unnecessarily.* Kwa hiyo nilikuwa nafikiri ni jambo la msingi sana kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie habari

ya maslahi ya walimu. Kwanza walimu wana madeni mengi wanaidai Serikali kama Kambi ya Upinzani ilivyoonesha, ambapo bado kuna zaidi ya shilingi bilioni 138 wanadai hawajalipwa. Hiyo inaondoa *moral* yao ya kutimiza wajibu wao wa kuelimisha watoto wetu, hivi hapa katika Serikali ambayo ina miaka zaidi ya 55 bado tunapaswa ku-*debate* habari ya maslahi ya walimu ya madeni yao badala ya kufikiri kwamba ualimu ingetakiwa iwe ni *rear professional* ambayo tunatakiwa watu watu wanaokuwa Walimu tuwalipe vizuri. Leo ualimu umekuwa kama ni ile ajira ambayo inatupiwa watu walioshindwa ndiyo mtu anakuwa mwalimu, haiwezekani! Hatuwezi kulea Taifa ambalo wanaopaswa kuelimisha watoto wetu ndiyo tunaifanya ni *professional* ya mwisho kabisa, mtu akipata *division four* ndiyo anakuwa mwalimu. *Division zero* aliyefeli ndiyo anakuwa mwalimu lazima tubadilishe huu mtazamo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kuwa na elimu bora lazima tutenge maslahi ya kutosha kwa walimu. Kwahiyo nilikuwa nadhani..........

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Paresso dakika tano na Mheshimiwa Juma Ali dakika tano.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mweyekiti, ahsante sana. Kwanza kwa namna ya pekee naomba kutoa pole kwa Mbunge mwenzangu, jirani yangu Mheshimiwa Hadji Mponda kwa kufiwa na mpiga kura wake, Mkuu wa Mkoa wa zamani wa Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Mwambungu. Pili, naomba kutoa shukurani za pekee kwa Baba Askofu Agapitus Ndorobo wa Dayosisi ya Mahenge kwa shule zake za Regina Mundi, *Kasita Seminary, St. Agness* na *St. Joseph* zimekuwa Kinara kwa kuitangaza Ulanga kwa ufaulu. Kwa hiyo, mnaposikia *Kasita Seminary* kuna watu wanaisikia inafaulisha lakini hawajui kama ipo Ulanga kwa Mlinga.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kuipandisha elimu ni pamoja na barabara kwa Majimbo yetu ambayo yana mazingira magumu kama Jimbo la Ulanga. Sasa hivi kuna maeneo hayafikiki kabisa. Kwa mfano, kuna eneo linaitwa Isaka hata baiskeli haiendi na ni zaidi ya kilometa 25, kuna eneo linaitwa Lyandu hakufikiki, kuna eneo linaitwa Majengo kilometa zaidi ya 27 hata baiskeli haifiki, kama Waziri wa barabara upo na unanisikia, naomba uli-*note* hilo kuwa kinachochangia elimu katika Wilaya ya Ulanga kushuka ni pamoja na miundombinu mibovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shukrani na kuwapongeza Maafisa Utumishi wa Wilaya ya Ulanga. Mheshimiwa Spika hapa alilipongeza Bunge kwenye suala la vyeti *fake* kuwa hakuna hata mtu mmoja nami naomba niwapongeze Maafisa Utumishi wa Wilaya ya Ulanga kwani Mtumishi mmoja tu ndiye aliyepatikana kwenye suala la vyeti *fake* na bahati nzuri alilala mbele kabla Rais hajatoa agizo kuwa hawa watu wafukuzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika Jimbo langu la Ulanga wananchi wamejitolea kuna maeneo wamejenga shule, iko shule ya Mikochi, iko shule ya Kipingo na shule ya Mbenja katika kata ya Ilagua lakini suala zito limekuwa kwenye usajili. Wazazi wamejitolea, wajenga majengo, wametafuta walimu, wanawalipa wenyewe Serikali suala la kuisajili wanasema eneo hilo mpaka wapate kibali cha maliasili yaani Serikali hiyo hiyo, Mawaziri hao hao, wameteuliwa na mtu huyo huyo mmoja, lakini kutoka ofisi moja kwenda nyingine inachukua miaka mitatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie unisajilie shule zangu ili tuweze kupata walimu wa Serikali na tuweze kupata vituo vya kufanyia mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ni madai ya walimu, hivi naomba niulize, nilishawahi kumuuliza ofisa mmoja mkubwa Wizara ya Elimu akasema tatizo zinalochelewesha madai ya walimu kwa sababu walimu wapo wengi. Nikamuuliza walimu wengi kwa sababu sisi tunazaa sana? Tungekuwa na watoto wachache walimu

wangekuwepo wengi? Kwa nini tunawanyanyapaa? Wabunge leo hii maslahi yetu yakicheleweshwa macho yanatutoka na tunaibana Serikali na wanawahi kututekelezea, kwa nini kwa walimu iwe tatizo hili na wakati Walimu ndiyo waliotufundisha? Huwezi kuoa bila kuandika barua ya uchumba, lakini walimu ndiyo waliotuwezesha sasa hivi tunawasahau. Humu Wabunge wengine ni maprofesa, wengine madaktari kwa sababu ya hawa walimu, lakini inapofika suala la maslahi yao tunaongea, kwenye kuibana Serikali hatuibani, inaishia kupiga makofi tu yamekwisha. Naomba kwa uchungu kabisa nitajitolea kuwa Balozi wa Walimu katika Bunge hili, yaani sitoki mpaka masuala ya walimu yaeleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano suala la nauli, walimu wanaenda likizo nadhani kwa miaka miwili mara moja na hapewi nauli, lakini Maofisa wengine kila mwaka wanaenda likizo na wanapewa nauli, tena nauli zenyewe ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyeo katika Jimbo la Ulanga kuna walimu miaka 15 kafanya kazi hajapandishwa daraja ukiuliza kwa nini? Wanasema hatujapata bajeti, hivi wakati mnamuajiri mlikuwa hamjui kama atatakiwa apandishwe cheo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ukaguzi; kinachochangia Wilaya ya Ulanga elimu kushuka Wakaguzi hawana gari, kwanza ofisi yenyewe ukiiona huwezi kutamani, hawana usafiri, Jimbo lina mazingira magumu mnategemea wataendaje! Mheshimiwa Waziri naomba unisaidie gari Wakaguzi wa Elimu wa Ulanga ili waweze kwenda kuzikagua shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuna chama kimoja kinaitwa CWT (Chama cha Walimu), naomba nitumie kauli ambayo siyo nzuri, hiki chama kimekuwa kinawakandamiza walimu; kwa sababu mwalimu anapoajiriwa anatakiwa achangie humu kwa lazima, kuna Walimu Ulanga hawajui hata CWT ndiyo nini, anaiona kwenye

*salary slip* kuwa amekatwa hela lakini hajawahi kupata chochote na hajawahi kusaidiwa chochote na hiki chama. Nilitoa pendekezo hapa mwaka jana kuwa walimu wajiunge kwa hiari kwenye huu mfuko ilia one kama una msaada ndiyo ajiunge, kama hauna masaada asijiunge. Wizara mnaliona, mnalifhamu na mnaliachia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI nadhani upo, kuna shule inaitwa Kwiro sekondari nilisoma hapa ndipo nilipoanzia *form one,* hii shule ina wanafunzi 520 wa sayansi lakini haina mwalimu wa hesabu, hawa ni wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita hivi mtu anasomaje sayansi bila kusoma hesabu? Alipangiwa mwalimu mmoja kwenda hapo na mpaka leo hii haja-*report,* kwa hiyo, hawa wanafunzi wanasoma lakini somo la hesabu hawasomi, sasa watafanyaje mtihani wa kidato cha sita hawana mwalimu wa hesabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule ya sekondari hii imechukua jina la Mama yangu Waziri mwenzenu wa zamani, Celina Kombani. Hii shule inatarajia kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita lakini haina bwalo la chakula na haina jiko na nimeshaandika barua kwako, naomba unisaidie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *VETA;* Mheshimiwa mmoja hapa alichangia kuwa wanafunzi wanaofeli waende *VETA,* naomba nimpe taarifa kuwa *VETA* siyo pango la vilaza, wako watu wana akili zao kule. Mheshimiwa Waziri, *VETA* walikuja Ulanga, tuliwapa eneo, walilikagua na walikubali lakini sasa hivi wameingia mitini, naomba tulifuatilie suala hili ili waje kujenga hiki chuo na eneo tulishawapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la mwisho ni suala la mikopo ya elimu ya juu. Tumeongeza asilimia kufikia 15, Mheshimiwa Waziri naomba ufanye *assessment,* nenda kaangalie hiki kilio cha wafanyakazi hii asilimia 15 inavyowaumiza, tuwaonee huruma. Mimi naomba tuleteile sheria hapa Bungeni ili tufanye marekebisho, kwa sababu

wote ni mashahidi mfanyakazi yoyote anapopata ajira cha kwanza kwenda kuchukua mkopo na anachukua mkopo mpaka kwenye *cealing* ya mshahara wake. Mkopo wa Bodi ya Mikopo walikuwa wanachukua asilimia nane sasa hivi asilimia 15, hebu fikirieni maisha yakoje huko uswahilini na sasa hivi hakuna posho zozote sasa hivi ninyi wenyewe mnajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa, Serikali imesema kuwa haitoajiri tena walimu wa masomo ya *arts;* Mheshimiwa Waziri Serikali hii ndiyo ilikuwa inasimamia hawa wanafunzi waende wakasomee ualimu masomo ya *arts* leo hii inasema hawawaajiri, sasa hawa watu watakwenda wapi? Watakwenda kuajiriwa sehemu gani?

Kwa hiyo, naomba mlifikirie upya, ninyi ndiyo muwatafutie *alternative "B"* kuwa watafanyaje. Wataendelea kukaa uswahili hivi na wameshasoma halafu sasa hivi mnawaambia lazima walipe mikopo baada ya muda fulani, hizi hela wanatoa wapi? Wakiwa wakabaji sheria zinakuwa kali mtaani. Huo ndiyo mchango wangu mdogo kwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitoe pole kwa Taifa kwa kupoteza wapiganaji hawa wawili, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma wa zamani Mheshimiwa Said Mwambungu pamoja na Mzee Paul Sozigwa. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu katika Wizara hii na kwa kipekee kabisa naomba nianze na suala la Chuo cha Ufundi Lushoto. Juzi hapa

Mheshimiwa Shekilindi alikuwa na swali linalohusu *VETA*, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati analijibu nadhani hakuwa anaifahamu Lushoto vizuri, sasa naomba kidogo nimpitishe kwenye jiografia aitambue vizuri Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto ni Wilaya ambayo hali ya hewa ni kama hivi tulivyo humu Bungeni, siku zote tupo hivi hakuna joto, kwa hiyo, tunazaana sana. *Population* ya Wilaya ya Lushoto ni karibia watu 700,000, tunazo shule za sekondari 85, ikiwemo Kifungiro, St. Mary's Mazinde Juu, Kongei, hizi ni zile ambazo zinafanya vizuri zaidi. Kwa mazingira hayo tunahitaji kuwa na vyuo vya ufundi. Bahati nzuri huko nyuma tulikuwa na Chuo cha Ufundi cha Kanisa KKKT cha *Magamba Trade*, baada ya wenye chuo kubadilisha matumizi sasa hivi kimekuwa ni Chuo Kikuu cha *SEKOMU* hivyo, hakuna chuo cha ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kata ya Lushoto Mjini pale tulikuwa na karakana ya *RRM - Rural Roads Maintanance* zile za zamani zile, hapa palikuwa na mitambo mpaka sasa hivi ipo na yale majengo yanamilikiwa na Halmashauri na pana mitambo mbalimbali ya kufanya ufundi selemala, kufua vyuma na kadhalika.

Kwa hiyo, tunapozungumza suala la *VETA* Lushoto hatuna maana kwamba tukatafute mapori. Zipo karakana ambazo tayari zipo kimsingi ni namna tu ya kuziboresha. Pia KKKT hawa wana shule ya ufundi ambayo ni kwa watu wenye mahitaji maalum, hata Mheshimiwa Marehemu Dkt. Elly Marco Macha amesoma katika shule hii inaitwa Irente, pale pana chuo cha ufundi cha watu wenye mahitaji maalum.

Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri ama Naibu Waziri, ujipe nafasi ya kuja Lushoto uweze kuona haya mambo, tunapolizunguza *VETA* tuna maana kwamba *population* iliyopo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tukisema tuende mpaka Tanga bado sisi wenyewe katika ndiyo Mkoa wa Tanga tunaongoza kuwa na sekondari nyingi, eneo lile peke yake

linatosha kuwa na Chuo cha *VETA* na maeneo yapo, tupo tayari kukupa majengo ambayo yapo tayari. siyo ya kuanza kujenga.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uchapishaji wa vitabu. Serikali ilipoamua kuifuta Bodi ya *EMAC* tulikosea. Kama kulikuwa na makosa ilipaswa turekebishe, lakini kuifuta na hili jukumu kuipa Taasisi ya Elimu pekee ni suala ambalo kwa kweli linakinzana hata na kauli mbiu hii ya Serikali ya viwanda. Tunavyozungumza sasa yapo makampuni ya sekta binafsi yalikuwa yanafanya kazi hii ya uchapishaji, kampuni za kizalendo wapo kampuni ya Ujuzi, wapo Mkuki na Nyota, Mture, *Education Book Publisher*, *E&D* pamoja na AIDAN ambapo mwanzoni walikuwa wameungana na *Macmillan*. Haya makampuni sasa hivi hayawezi yakafanya biashara kwa sababu Serikali imechukua ili ifanye yenyewe biashara, Serikali imeingia kwenye uchapishaji na matokeo ndiyo tunayoyaona hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa haya kwenye kitabu cha jiografia pekee cha *form four* yapo zaidi ya makosa 15, kwenye kitabu cha *form three* yapo zaidi ya makosa 18, humu kwenye *I Learn English Language* ndiyo usiseme yako mengi, hata neno *below* linaandiwa *double L,* ni jambo la kusikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitaka Serikali kwamba bado hatujakosea sana kwa sababu mambo haya yamefanyika humu Bungeni tuone namna gani tunaweza tukairejesha tena ile bodi ya *EMAC* ambayo inaweza ikaja kufanya hii kazi ya uhakiki wa vitabu. Pia lazima tuangalie kwamba hii sekta binafsi itafanya wapi biashara. Tunazungumza sasa hivi kiswahili kinakua katika Afrika ni lugha ya pili kwa ukubwa, kama kiswahili kinakua tunatarajia kwamba Serikali peke yake ndiyo itachapisha hivi vitabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wakati maufaka kabisa kuwajengea uwezo ili waweze kushindana na hawa akina *Oxford University Press*, washindane na kina *Pearsons*, washindane na kina *Longhorn*, kwa sababu haya

ni makampuni makubwa duniani na yapo hapa Tanzania wanachapa vitabu, tena wao mara nyingi wanachapa nje ndiyo maana hata vitabu vinakuwa bei nafuu. Sisi gharama za uchapishaji kwa hapa ndani peke yake zitakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri hili jambo kama lilifanyika kwa mihemuko ya kisiasa hebu sasa kaa na hawa wadau, hawa ni Watanzania wenzetu, tujaribu kupata mbinu muafaka ambazo zitakuja kutatua tatizo la elimu ya hawa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ukarabati wa shule kongwe. Nimeangalia katika kitabu sijua labda nimeangalia kwa haraka lakini sikuona sekondari kongwe za *Tabora Boys* na *Tabora Girls*. Mheshimiwa Waziri umesoma *Tabora Girls*, na mimi nimesoma *Tabora Boys* ni lazima tukumbuke tulikotoka. Naomba uangalie namna ya kuboresha mazingira ya sekondari hizi. Tulikuja ofisini kwako na timu ya *Elites* ya watu wa *Tabora Boys*, tukionesha kwamba tunaweza kuunga mkono jitihada za Serikali katika hili na ukatuambia kuna nia njema, sasa tunataka nia njema hiyo iende hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isiishie hapo iende na shule ya Malangali, Mimi nilipotoka *Tabora* Boys nilikwenda Malangali nayo sijaiona humu. Mheshimiwa Waziri mimi nimesoma shule za zamani ndiyo maana siyo mtu wa mchezo mchezo, naomba shule hizi tuzifufue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika elimu, Chuo Maalum cha Ualimu cha Patandi pia humu sijakiona. Tanga Galanos sijaiona lakini *Korogwe Girls* pia sijaiona, *Korogwe TTC* sijaiona. naomba sana Mheshimiwa Waziri, hivi pia ziingie katika mfumo huu na ninadhani ulishaniambia kwamba zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nizungumzie vifaa vya maabara. Hapa tumeona kwamba mmesambaza vifaa vya maabara katika maeneo mbalimbali, tunashukuru

kwa hivyo ambavyo tumevipata. Katika Halmashauri ya Lushoto tumepata katika shule tisa pekee. Kama nilivyokuambia tukizungumza Lushoto kama Halmashauri tuna sekondari 65, tukichanganya na Bumbuli ambayo ina Halmashauri yake ndiyo zinafika 85. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba kati ya shule 65 zikipata tisa ina maana bado shule nyingi zimekosa hivi vifaa.

Kwa hiyo, nikusihi sana utuangalie kwa jicho hilo kwamba tumejitahidi katika ujenzi wa hizi shule za sekondari, zipo kata Mheshimiwa Waziri kuna kata moja ina vijiji vinne kila kijiji kina sekondari. Utaona kabisa kwamba huu muitikio ni mkubwa na maabara hizi tumezijenga kwa nguvu za wananchi kwa kiasi kikubwa, tupo tu katika hatua za usafi tunaomba sasa mtuunge mkono katika usafi pamoja na vifaa. Naomba sana utuangalie katika mukhtadha huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala zima la mitaala kwamba mitaala iangaliwe ili iweze kwenda na mahitaji ya Tanzania ya sasa. Tunagundua kwamba sisi angalau tuliobahatika kwenye mitaala ile ya Mwalimu Nyerere ndiyo maana unakuta hata mtu akimaliza darasa la saba anaweza akajiongeza mwenyewe. Lakini tumegundua kwamba sasa hivi, wanafunzi wa sasa anamaliza Chuo Kikuu bado hata kuandika barua au hata yeye mwenyewe kutafuta namna ya kujiwezesha inashindikana. Kwa hiyo, hapa tatizo moja kwa moja inaonekana kwamba ni mitaala yetu haimuandai mwanafunzi ili aje kuwa nani.

Ninaomba sana tuachane na hii dhana ya wanafunzi kumaliza *degree* halafu kutembea na bahasha mitaani. Tutengeneze mitaala ambayo itakuwa ni shirikishi na inaeleweka kwamba atakapomaliza chuo basi anaweza mwenyewe akajiongeza kwa namna yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumeona mlundikano mkubwa huu wa wanafunzi wa masomo ya sanaa, sasa watakuwa hawana ajira, ndiyo anachouliza Mheshimiwa Mlinga waende wapi, kosa lao ni nini, kwa sababu Serikali

yenyewe ndiyo iliyofanya udahili leo haiwezi kuwaajiri, ni lazima tutafute vitu mbadala. Pia ni lazima pia tutumie fursa yakuwepo katika hili Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Paresso dakika tano na Mheshimiwa Juma Ali Juma dakika tano.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwa dakika tano hizo katika Wizara hiyo ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na Watanzania wote kutoa pole nyingi sana kwa wananchi wa Mkoa wa Arusha kufuatia ajali ambayo imechukua maisha ya watoto wetu, walimu pamoja na dereva iliyotokea Wilaya ya Karatu Wilaya ambayo ninatokea, Mkoa wa Arusha ambao ninauwakilisha. Poleni sana na Mwenyezi Mungu azidi kuwapa nguvu familia. Pia nitoe pole kwa wazee wetu hawa ambao wametangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango mfupi kuhusiana na Wizara hii kwa sababu pia ya muda. Taifa lolote ambalo linachezea elimu ni Taifa ambalo linaenda kuangamia na Taifa ambalo linaenda kupotea. Nasema hivi kwa sababu kumekuwa na utamaduni kila Waziri anayekuja kwenye Wizara hii anakuja na *style* yake ambayo ama anafikiri inaenda kuboresha elimu au inaenda kuangamiza elimu kabisa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mama Ndalichako umeingia hapa wewe, wewe ni mtaalam, hujawahi kuwa mwanasiasa, tunaamini utaenda kuweka mifumo thabiti, mifumo itakayoboresha elimu kwa watoto wetu, mifumo ambayo itawaandaa watoto wetu kuwa na Taifa ambalo litaendelea kuwa Taifa kama ambavyo nchi nyingine tumeona. Tunategemea utaenda kuweka mifumo ambayo hata wewe ukiondoka kesho, Waziri yeyote atakayekuja

hataenda tena kucheza na elimu ya watoto na hataweza kwenda kucheza na elimu ya Watanzania. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ndalichako tunategemea utaenda kuweka hiyo mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu mfumo wa mpango wa elimu bure. Serikali imekuwa ikitamba sana kuhusu suala la elimu bure na imesema imefanikiwa. Ukweli sio sahihi. Huwezi kuangalia mafanikio ya elimu bure kwa kuangalia idadi ya watoto waliojiandikisha, ndiyo mmekuwa mkisema hivyo. Idadi ya watoto waliojiandikisha kuanza darasa la kwanza kweli inaongeza, lakini hiyo sababu pekee ya kutamba ya kujigamba na kusema eti elimu bure imekuwa na matokeo chanya kwa Watanzania siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna changamoto nyingi, kuna changamoto nyingi sana katika suala zima la elimu katika nchi hii, ambapo pia taarifa ya Kamati imeonesha. Kwa hiyo, tunategemea ama mje na mfumo mwingine wa kusema kabisa, ama mmeshindwa hiyo elimu bure kutoa, ambayo mnaita elimu bure kwa sababu hizo changamoto au muondoe hilo neno au muwaambie sasa Watanzania kwamba tulisema elimu bure, lakini kuna changamoto, tunahitaji kuwa-*engage* Watanzania na wao katika suala zima la kuondoa changamoto za elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu wanafunzi waliopata mimba na kurudishwa mashuleni. Hatuelewi ni kwa nini kuna kigugumizi kuhusiana na watoto wa kike waliopata mimba wananyimwa kurudi shuleni. Mheshimiwa Kakunda amechangia hapa asubuhi, yeye ni mtaalamu mzuri sana, amekaa kwenye *system* muda mrefu anapinga hili jambo. Hivi, watoto wanapata mimba, hawarudi shuleni, hivi tunazidi kuondoa ujinga au tunazidi kuzalisha ujinga? Kwa sababu hawa watoto wanapata mimba wapo wanaobakwa, wapo ambao kweli inawezekana mazingira yanawalazimisha, wako wengine ambao tu ni watundu wanakuwa kwenye hiyo hali wanapata mimba. Hivi kupata mimba na kuzaa ni dhambi? Wavulana

walowapa mimba wanaendelea, hawa watoto wa kike waliopata mimba wanarudi majumbani. Tunaendelea kuzalisha ujinga kwa Watanzania, na hatujui ni kwa nini Serikali mnapata kigugumizi. Mbona wenzetu wa Zanzibar wanaendelea hawa watoto wakipata mimba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Kumi nilikuwa na Kamati ya Huduma za Jamii tulikuwa tunasimamia Wizara ya Elimu tulienda Zambia, wanarudi mashuleni watoto hawa. Kwa nini kwa Tanzania? Kwa nini mnapata kigugumizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wewe ni mama, wewe ni mwanamke mwenzetu, tuwaonee huruma watoto wetu wa kike ambao wako kule vijijini wanapata mimba, wanarudishwa majumbani, hawawezi kuendelea na shule, halafu watoto wa kiume waliowapa mimba wao wanaendelea na shule.

Waheshimiwa Wabunge wanawake, Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa *TWPG,* Wizara hii bajeti yao isipite mpaka tupate kauli ya Serikali ni lini wataruhusu watoto waliopata mimba waweze kurudi mashuleni. Kwa hiyo, tunategemea Mheshimiwa Waziri utakuja na majibu siku unahitimisha hoja yako na ujiandae kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Juma Ali Juma.

**MHE. JUMA ALI JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Kwanza kabisa naunga mkono hoja na mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hiyo licha ya hali ngumu ya bajeti waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache tu, moja

nilitaka kujua na kupata maelezo juu ya Chuo cha Utafiti wa Sayansi Baharini kilichopo Zanzibar. Chuo hiki kinafanya kazi nzuri na kikiendelezwa vizuri kinaweza kikatoa matumaini ama kufufua uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna jengo Mheshimiwa Waziri la Chuo hicho, jengo hili toka lianzishwe huu ni mwaka wa 13 bado limesimama, jengo limekuwa chaka la uhalifu na vibaka wanajificha pale. Hivyo nakuomba Mheshimiwa Waziri hebu litembelee lile jengo ulione. Tafiti za Chuo hiki zinatumiwa sana na kina mama, akina mama ndiyo wakombozi wa nchi yetu, wamesemaji waliopita hapa, kikiweza kuboreshwa hiki chuo basi tutaweza kuwakomboa akina mama. Kwa mfano, tafiti zilizofanyika kwenye chuo hiki wameweza kugundua mazao yanayopatikana yatokanayo na bahari imegundulika lulu, tunajua lulu thamani yake na faida yake kwenye nchi yetu, pia mwani wameweza kuugundua na mazao mengine mengi kabisa yatokanayo na bahari.

Mheshimiwa Waziri, tukiweza kutumia tafiti hizi vizuri tunaweza tukaendelea vizuri. Bahari ni mkombozi mkubwa kweli, kwenye bahari hakuna mafuriko Mheshimiwa Waziri, kwenye bahari hakuna ukame, sasa hivi wakulima wengi waliolima mazao mengi yamekwenda na mafuriko, lakini tukiwekeza vizuri kwenye tafiti hizi basi tunaweza tukawaomboa wananchi wetu wengi.

Kwa hiyo, mimi naomba ufanye ziara Mheshimiwa Waziri kwenye hicki chuo, pana wataalam wazuri pale, pana maprofesa, lakini ukienda unawaonea huruma ni wanyonge wamejikunja kwa sababu hawana kazi ya kufanya. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri tuelekee huko ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri, nakuomba ukae na Wizara ya Elimu Zanzibar ili muangalie mfumo wa elimu yetu. Kwa sababu mfumo wa elimu ya Zanzibar na Bara hasa ngazi ya msingi uko tofauti, lakini tunapokuja kwenye elimu ya juu tunakutana kwa

pamoja. Kwa hiyo, hebu kaeni na Wizara ya Elimu Zanzibar mpange mkakati ambao utaweza kwenda sambamba kusudi tunapokutana huku juu kwenye elimu ya juu basi wanafunzi wetu wote waendelee kufanya vizuri. Maana kule Zanzibar sasa hivi watoto wanamaliza darasa la sita wadogo mno, lakini ukija huku wanamaliza darasa la saba, pia mitaala haiendani ya msingi wa kule na msingi wa huku mwisho wanakuja kuungana huku juu, wanafanya mitihani ya Taifa, hivyo, naomba mkae ili muweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninarudia tena kuunga mkono hoja mia juu ya mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa niwashukuru wachangiaji wetu wote wamemaliza. Mheshimiwa *Chief Whip*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, napenda kutumia Kanuni ya 68(7) ukisoma pamoja na Kanuni ya 64(1), (g) kuomba muongozo wa kiti chako.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo nimpongeze Mheshimiwa Anna Joram Gidarya wakati anachangia, alichangia vizuri katika mchango wake, lakini naomba Mwongozo wa Kiti chako kuhusiana na baadhi ya maneno ambayo ningependa sana kwa mujibu wa kumbukumbu zikae vizuri kwamba elimu yetu ya Kata ilifananishwa na *VodaFasta.* Ningependa kuomba mwongozo wako kama maneno haya yanafaa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwongozo wako ningependa sana kwa sababu hili Bunge letu lilipitisha sheria nzuri kuanzisha elimu hiyo, sasa tukifananisha pengine elimu hiyo na maneno kama hayo *VodaFasta* ningependa Mwongozo wa Kiti chako ili twende vizuri. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri nimepokea Mwongozo wako nitakujibu baadae. Kwa mujibu wa Kanuni ninaweza kukujibu baadae.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo dogo kwamba *Bunge Sports Club* itakuwa na mechi leo jioni dhidi ya *Iringa Veterans* na timu yetu ya *netball* itakuwa na mechi dhidi ya timu kutoka Hombolo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 8.00 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 15 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*